# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Thelathini na Moja - Tarehe 22 Mei, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELLE):**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Nishati na Madini Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 253

### Mfumo wa Utawala Nchini

**MHE. MOSES J. MACHALI** aliuliza:-

Je, Serikali haioni kuwa kutokana na ukubwa wa nchi yetu ni muhimu kwa sasa kuachana na mfumo wa sasa wa utawala na kuanzisha mfumo wa utawala wa majimbo yatakayoongozwa na Magavana badala ya Wakuu wa Mikoa na watakaochaguliwa na Wananchi?

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimwa Moses Joseph Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Muundo wa Dola *(State),* Tanzania na Mihimili yake, yaani Bunge, Mahakama na Serikali, upo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Aidha, kwa mujibu wa Ibara ya 2(2) ya Katiba hiyo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anayo madaraka ya kuigawa nchi katika Mikoa, Wilaya na maeneo mengine ya utawala kwa kadiri atakavyoona inafaa na kwa kuzingatia taratibu zilizopo kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 61(4) ya Katiba ya Mwaka 1977, inatambua uwepo wa Mikoa na inawapa Wakuu wa

Mikoa, mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa kazi na shughuli za Serikal ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkoa aliokabidhiwa. Mabadiliko ya mfumo wa utawala kutoka katika mfumo wa Mikoa kwenda katika mfumo wa Majimbo, hauwezi kubadilika bila kubadili Katiba iliyopo ambayo inatambua mfumo uliopo. Hivyo, mfumo uliopo utaendelea kutumika kwa sababu ndiyo unaoambuliwa na Katiba iliyopo ya mwaka 1977.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri, maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, swali langu halijajibiwa ipasavyo kwa sababu nimeiuliza iwapo Serikali inaona umuhimu wa kuondokana na mfumo wa sasa, lakini naomba nimwulize maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Mfumo wa sasa umedhihirisha wazi kwamba umefeli kuweza kuhakikisha kwamba maendeleo ambayo yanatakiwa ndani ya nchi yetu tunayafikia na kutokana na hali hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza kukubaliana na mimi kwamba, kwa nyakati tofauti tumekuwa tunasumbuliwa sisi Waheshimiwa Wabunge. Nitatoa mfano wa Wizara yako moja. Unatakiwa Kigoma, unatakiwa Mtwara, unatakiwa Lindi na pia unatakiwa Kilimanjaro, huwezi kujigawa na hii yote ni athari ya mfumo wa sasa. Je, ni sababu gani ambazo zinaifanya Serikali isione umuhimu wa kuweza kuondokana na mfumo wa sasa?

(ii) Imedhihirika wazi kwamba katika Wilaya mbalimbali hapa nchini kuna *contradiction* katika masuala ya utekelezaji wa majukumu baina ya Wabunge pamoja na Wakuu wa Wilaya; ni jambo ambalo lipo wazi, hali ambayo inanishawishi mimi binafsi nione kwamba kuna haja ya kuweza kuvifuta viti vya Wakuu wa Wilaya haraka iwezekanavyo ili kuhakikisha kwamba kama tuna Magavana basi tunahakikisha Wabunge wa Majimbo hata kama kuna Majimbo mawili, watakuwa wana-*rotate either* kwa miaka

miwili kutokana na umri wa uhai wa Bunge wa miaka mitano mitano. Naomba kauli ya Serikali kuhusiana na suala zima la kuondokana na mfumo wa sasa wa kuwa na Wakuu wa Wilaya ili kuweza kuondokana na *contradiction* ambayo inajitokeza baina ya Wabunge pamoja na Wakuu wa Wilaya kwa sababu ...

**SPIKA:** Swali bwana, siyo hotuba!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Naomba kauli ya Serikali kuhusiana na suala la kuvifuta viti vya Wakuu wa Wilaya ili tuhakikishe aidha tunakuwa na Magavana au Wabunge wanaoongoza maeneo yao kwa kuwa ndiyo ambao wanatokana na kura za Wananchi.

**NAIBU WAZIRI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Moses Joseph Machali, kama ifuatavyo:-

Kwanza, hili la kusema kwamba swali halijajibiwa, mimi siwezi kuja na kitu cha kwangu hapa, ninakuja na *constitution* ya nchi. Katiba ya nchi inakuonesha jinsi itakavyotawaliwa na itakavyoongozwa na huu ni mwafaka uliofikiwa na Watanzania wote Tanzania Bara na Visiwani. Kwa hiyo, siwezi kutoka nje ya hapo na nikitoka hapo Waziri ataniuliza hivi Bwana wewe tumesikia umesema Majimbo yamekubalika umeipata wapi hiyo! Chama kinachotawala hapa ni Chama cha Mapinduzi; wapi wali-*discuss* wakasema tutakuwa tunatumia utaratibu wa Majimbo?

Kwa hiyo, ninachofanya hapa, nasema tu *constitution* kwa sasa inachosema ni kwamba, utaratibu huu uliopo unaitwa *Westminster Model,* ambao tuliupata kutoka kwa Waingereza, ambao walituletea hapa; *whereby you have The Judiciary, The Executive and The Legislature,* ndiyo unaotumika hapa. Kwa hiyo, ukibadilika leo, nitakuja niseme umebadilika umekwenda kwenye Majimbo. Hilo la kwanza.

La pili, analosema kwamba sasa tunataka tupeleke

madaraka katika Mikoa na Wilaya *(Decentralisation by Devolution – D by D),* ambayo tunazungumzia, yaani kugatua madaraka kutoka kwenye Serikali Kuu katika Afrika, nchi ya kwanza inayosifiwa kwa utaratibu huo ni Tanzania, mpaka Afrika ya Kusini imekuja hapa kuchukua jambo hili.

Mheshimiwa Spika, rafiki yangu Machali kama utanipa nafasi, hili jambo amekuwa analijadili mara kwa mara, sisi tunasema hivi; tumesema Wananchi wenyewe, yaani wao wenyewe, waamue bila kuitegemea Dodoma na Dar es Salaam. Pelekeni madaraka kule ambako *functions* zipo, yaani kule ambapo majukumu yapo na kule ambapo shule zimejengwa, kule ambapo maji yanapatikana na kule ambapo barabara zinatengenezwa. Peleka madaraka ili waamue wao wenyewe kule, ndicho kinachosemwa hapa. Sisi tunafikiri kwa sasa hiki ndicho tunachokifanya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *contradictions* ambazo anazizungumzia hapa, nazo ni *parallel,* ukitaka kui-*resolve* hapa utasema hivi Rais wa nchi amepewa madaraka akapewa na dhamana, akaambiwa nenda kaitawale nchi hii kwa miaka mitano. Hawezi kwenda na mfumo wowote bali atakwenda na mfumo anaofikiri kwamba huu mfumo ndiyo utakaonipa matokeo ninayoyataka na mfumo ambao Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ameamua kwenda nao ni utaratibu wa Wakuu wa Mikoa na Wilaya. Mkuu wa Mkoa ni msimamizi wa shughuli zote za Serikali katika eneo lililoteuliwa pale, wao ndiyo wamebeba hiyo dhamana kwa niaba yake. Ndani yake, anazungumza habari ya Wabunge na Madiwani, ambapo mfumo huu tulionao una-*provide* pia au unakubali kwa maana ya uwakilishi wa Wananchi. Sisi wote tuliopo hapa, tunatoka katika Majimbo yetu, kwa maana ya kuja kuwawakilisha.

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba, Mheshimiwa Mbunge anaweza kuwa na jambo kubwa hapa. Nasema kwa sauti hii si kwamba nimekasirika, bali ni msisitizo tu wa jambo hili. Ninachotaka kusema, najua Afrika ya Kusini wanafanya hivyo anavyosema Mheshimiwa Machali, nakubaliana naye, Nigeria wanafanya hivyo na wenzetu wa

Kenya wamekuja hapa. Kama kuna mawazo mazuri kama hayo, sasa hivi kuna mchakato unaendelea wa kubadilisha Katiba ya nchi hii, huko ndiko tupeleke mawazo haya ili tukayatetee na ili baadaye itakapokuja Katiba mpya iweze kuchukua hilo. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Naona hii mmeitaka wenyewe na sasa naendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, mmetumia dakika kumi. Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub na badala yake Mheshimiwa Mangungu!

Na. 254

**Kamishna Mkuu wa *TRA***

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU (K.n.y. MHE. JAKU HASHIM AYOUB)** aliuliza:-

Tangu Mamlaka ya Mapato Tanzania iundwe haijawahi kutoa Kamishna kutoka Tanzania Zanzibar:-

(a) Je, kwa kuwa na Kamishna Mkuu wa *TRA* kutoka upande mmoja tu wa Muungano kunaimarisha vipi Muungano wetu?

(b) Kwa sababu Naibu Kamishna anawajibika kwa Kamishna Mkuu; je, ni lini Tanzania Zanzibar itapewa nafasi kutoa Kamishna Mkuu kukiongoza chombo hicho?

(c) Je, kwa kuwa *TRA* ni Chombo cha Muungano, kwa nini tusiweke mfumo wa zamu wa kutoa Kamishna Mkuu wa kuiongoza *TRA* kwa kipindi maalum kitakachokubalika kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako najibu swali la Mheshimiwa Jaku Hasim Ayoub, Mbunge kupitia Baraza la Wawakilishi, lenye vipengele (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* uteuzi wa Kamishna Mkuu wa *TRA* upo kwenye mamlaka ya uteuzi wa nafasi za juu za Viongozi wa Taasisi za Muungano, ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kwa mujibu wa uteuzi wa nafasi hizo, mamlaka ya uteuzi huzingatia sifa za uzoefu wa kazi husika.

(b) Mamlaka ya Mapato Tanzania ni Chombo cha Muungano. Ajira kwenye Taasisi hii vilevile inazingatia ajira kwa Watanzania wote wenye sifa zinazohusika, kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

(c) Kabla ya uteuzi, mamlaka ya uteuzi hushauriwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungao wa Tanzania *(SMT)* na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar *(SMZ),* kwa kupata mapendekezo ya majina na wasifu wa wahusika kwa nafasi za uongozi zilizo wazi na za uteuzi wa kufuata utaratibu uliowekwa.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na ningependa kumwuliza maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Maswali ya nyongeza ni ya kwako!

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Kumekuwa na malalamiko kwamba, nafasi za kazi ambazo zinatolewa kwenye mamlaka hii hazitangazwi kwa uwazi:-

(i) Je, Serikali ipo tayari sasa kuweka uwazi wa utangazaji wa nafasi hizo ambazo zimetamkwa?

(ii) Kumekuwa na matatizo makubwa sana ya wafanyabiashara wa Visiwa vya Zanzibar na wafanyabiashara wanaotoka Bara kwamba bado Serikali haijaweka mfumo ambao unawiana katika ulipaji wa kodi na hii ni moja kati ya kero zinazolalamikiwa. Je, mpaka sasa Serikali imefikia wapi kwenye kutanzua hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mangungu, kama ifuatavyo:-

Kwanza, nafasi za kutangazwa au kutangazwa kwa nafasi za kazi, Serikali ina mfumo wa wazi wa kutangaza nafasi za kazi kwa kutumia vyombo vya habari, *website* za mashirika au taasisi za Serikali pamoja na magazeti. Kwa hiyo, huo ni uwazi tosha kwa Wananchi kuona nafasi hizo.

Swali la pili ni tofauti kidogo, kwani swali la kwanza ni ajira katika *TRA*, sasa Mheshimiwa Mangungu anaulizia kodi za wafanyabiashara. Hata hivyo, nimjibu kwamba, suala hili kuna Kamati sasa hivi ndani ya Wizara ya Fedha, *TRA* na *ZRB*, yaani *Zanzibar Revenue Board* wanafanyia kazi suala hili na wakimaliza watatuletea na *Inshallah* Bunge litajulishwa tumefikia wapi.

**SPIKA:** Ninyi hamkusimama kabla, nilishamwona mtu pale, tunaendelea, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Charles John Mwijage atauliza swali hilo.

Na. 255

**Serikali Kutoa Ruzuku kwa Hospitali za Misheni**

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE** aliuliza:-

Wilaya ya Muleba na Jimbo la Muleba Kaskazini ilichelewa kutekeleza Sera ya Kujenga Zahanati kwa kila Kijiji hivyo kufanya Wananchi wakose fursa ya kupata huduma za afya; na kwa kuwa katika Jimbo hilo kuna Hospitali ya Misheni ya Ndolange, Rwamtenge na Kangondo ambazo zinaweza kuwasaidia Wananchi:-

(a) Je, kwa nini Serikali isitumie Hospitali hizo za Misheni kwa kuzipa ruzuku ya dawa na mishahara ya watumishi ili ziweze kutoa huduma bora na kwa gharama nafuu kwa Wananchi?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kupandisha hadhi Zahanati ya Bumbiile ili ihudumie Wananchi wa maeneo ya Visiwa vya Bumbiile, Kelebe na Makibwa vilivyo mbali na Hospitali hizo za Misheni zilizotajwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles John Paul Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inatoa ruzuku kwa Hospitali 97 za Mashirika ya Dini zilizopo kote nchini. Kati ya hizo, Hospitali 39 ni Teule za Halmashauri, Hospitali mbili za Rufaa ngazi ya Kanda (Bugando na KCMC) na Hospitali kumi zilizopandishwa daraja na kuwa Hospitali za Rufaa ngazi ya Mkoa. Hospitali 56 ni za kujitolea (zikiwemo Ndolage na Kangondo). Ruzuku inayotolewa kwa kila mwaka kwa ajili ya mishahara, dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kwa Hospitali hizo ni shilingi 36,748,288,987. Ruzuku hii ni mbali na ile inayotolewa na Hamashauri zenye Hospitali za Mashirika ya Dini kutoka katika *Basket Fund* na mishahara ya watumishi walioshikizwa katika Hospitali hizo, Vituo vya Afya na Zahanati. Ruzuku hutolewa ili Wananchi wapate huduma katika Hospitali hizo kwa gharama nafuu. Serikali inaendelea kuboresha mazingira yatakayoziwezesha Hospitali hizo zitoe huduma bora kwa Wananchi kwa gharama nafuu.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inasimamia ubora wa huduma na viwango. Katika kutekeleza hili, Wizara imeweka vigezo vya utoaji huduma kwa kila ngazi. Ili Zahanati ya Bumbiile ipandishwe hadhi na kuwa Kituo cha Afya, inahitaji kukidhi vigezo vya ngazi hiyo. Wizara itakapopokea ombi la kuipandisha hadhi zahanati hiyo, itatuma wataalamu kwenda kufanya ukaguzi. Endapo itaonekana kukidhi vigezo, itapandishwa hadhi na kuwa Kituo cha Afya.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nasikitika kwa mtu anayesikiliza katika redio na kuangalia katika televisheni, Waziri anasema shilingi bilioni 36 zimepelekwa kwenye Hospitali za Ndolange na Kangondo, kitu ambacho siyo kweli.

Mheshimiwa Spika, nilichokisema katika swali langu la msingi, naomba nimwongoze Mheshimiwa Waziri ni kwamba, katika Jimbo langu ndiyo naanza kujenga zahanati. Zipo Kata kama Ngenge, Lutoro na Mayondwe, hazina zahanati kabisa, wamishenari ndiyo wanatusaidia. Swali langu ni kwamba, Rwamtege, Kangondo, Ndolange, muwape ruzuku zaidi kusudi watu wapate huduma kama ambavyo wanapata kwenye zahanati za kata na vijiji ambazo zimejengwa.

Mheshimiwa Spika, nimemwambia Waziri ninazo zahanati nane ambazo ninajenga. Swali langu ndiyo hilo.

(i) Je, Waziri yuko tayari sasa kuwapa huduma hawa watu kwenye wigo huo ili waendane na Watanzania wenzao ili nitakapomaliza zahanati zangu wapeleke huduma kule?

(ii) Naishauri Serikali, Mheshimiwa Waziri jibu alilonijibu ni la mezani; je, yuko tayari kuleta wataalam niwaelekeze au kuwaongoza ilipo Bumbiile, Kelebe na Goziba, ili aweze kuelewa mazingira ya watu wa kisiwani na kwamba hawawezi kwenda nchi kavu kupata huduma? *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi; yaani anachosema aende nao wataalam.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwanza, fedha ambazo nimezitaja shilingi bilioni 36 ni kwa ajili ya hospitali zote 97 na siyo hospitali hizo mbili ambazo amezitaja Mheshimiwa Mbunge. Hospitali ya Kangondo inapokea ruzuku ya mishahara pamoja na zile hospitali mbili nyingine. Kama ikiwa kutakuwa na mahitaji ya

nyongeza, basi kuna utaratibu wa kuwasilisha na kujadiliana namna ambavyo Halmashauri ya Wilaya inaamua na Uongozi wa Mkoa unapitia na kuridhia na baadaye upande wetu sisi tutaangalia na kuona uwezekano wa kutaka kufanya kile kitu cha nyongeza, ambacho kinatakiwa kufanywa ilimradi kuhakikisha Wananchi wanapata huduma stahiki kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, suala la kwenda kuona Bumbiile iko wapi na imo katika mazingira yapi, Wizara yangu iko tayari kufanya hivyo. Kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba, Halmashauri ikiwasilisha maombi basi tutakuwa tayari kutuma wataalam ili waweze kuona. Ikionekana zahanati hiyo imekidhi vigezo, hakutakuwa na tatizo lolote la kuifanya kuwa Kituo cha Afya.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, maeneo mbalimbali katika nchi hii wakati mwingine Wananchi, watu binafsi pamoja na Serikali wanajitahidi kujenga hospitali pamoja na zahanati, lakini inachukua muda mrefu sana kupata usajili pale zinapokamilika. Kwa mfano, Jiji la Mwanza tulijenga Zahanati ya Tambukareli, Kata ya Butimba pamoja na Zahanati ya Mbugani, lakini zimechukua muda mrefu sana kupata usajili, kwa sababu ya *bureaucracy* iliyopo Wizara. Pia katika maeneo mengine nchini watu wanalalamika, nataka Waziri atuambie kwa nini kuna *processes* ndefu na *bureaucracy* pale ambapo hospitali na zahanati zinakamilika lakini usajili unaleta shida? *(Makofi)*

**SPIKA:** Yaani inachukua muda gani kusajili? Haya Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama kuna zahanati au kituo cha afya kimeshakamilika na sasa wanawasilisha maombi ili iweze kusajiliwa, haihitaji muda mrefu, isipokuwa utekelezaji wake. Kama ilivyo ni kwamba, inahitaji iingie katika bajeti na

kutengewa fedha. Ikiwa ombi hilo linatekelezwa kabla ya kipindi cha bajeti kufika au wakati bajeti imeshapita, ni lazima kipindi hicho kitapita zaidi ya mwaka mmoja kabla ya kutekelezwa. Kwa hiyo, ni muda tu wa kuwasilisha hayo maombi.

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, hivi sasa Wizara yangu imepitia upya na kuwaandikia Wakurugenzi wote, ikiwataka kuwasilisha majina ya zahanati na vituo vya afya vyote ambavyo vimeshakamilika ili hatua staili ziweze kuchukuliwa kwa haraka. Wizara yangu haipo tayari kuona kituo cha afya ambacho Wananchi na Serikali wamewekeza fedha pale kinakaa bila kutumika kwani ni matumizi mabaya ya fedha.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kama ilivyo kwenye swali la msingi, ni Sera ya Serikali kujenga zahanati katika kila kijiji. Wilaya ya Nanyumbu ina vituo vya afya vitatu na zahanati 15 wakati ina kata 14 na vijiji 89. Hivi ni lini Sera hii ya Serikali ya kujenga Vituo vya Afya katika kila Kata na Zahanati katika kila Kijiji itatekelezwa kikamilifu katika Wilaya ya Nanyumbu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi unaelekeza uwepo wa zahanati katika kila kijiji na kituo cha afya katika kila kata. Ni namna ambavyo Halmashauri na Wananchi wanavyoweza kushirikiana na Serikali katika kujipanga na kutekeleza mpango huo. Kadiri ambavyo Halmashauri itaweza kuwekeza angalau kutenga fedha katika kila mwaka kwa ajili ya kuanza kutekeleza mradi mmoja mmoja au miradi miwili miwili, basi Serikali itakuwa inaendelea kushirikiana nao kuhakikisha mpango huu wa maendeleo ya afya ya msingi na sera hiyo ya kutaka kutekeleza kuwepo na zahanati katika kila kijiji na kituo cha afya katika kila kata unafikiwa. Naamini utekelezaji wa mpango huu utachukua muda, lakini lengo ni kuukamilisha.

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wanywaji, naomba swali langu namba 256 lipatiwe majibu. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**MBUNGE FULANI:** Eeh na wewe mnywaji?

Na. 256

**Madhara ya Pombe kwa Afya ya Binadamu**

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI** aliuliza:-

Tafiti zote Duniani zinaonesha kwamba, pombe si salama kwa afya ya mwanadamu:-

Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya afya ya Wananchi wake hasa wale wanaotumia pombe?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Haji Ali, Mbunge wa Kiwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tafiti zinaonesha kuwa, watu milioni mbili hufariki kila mwaka kutokana na madhara ya matumizi ya pombe na asilimia nne ya matatizo ya kiafya Duniani hutokana na matumizi ya pombe. Hali inazidi kuwa mbaya zaidi katika nchi zinazoendelea hasa kutokana na kukabaliana na hali mbaya ya uchumi na ustawi wa jamii inayochangiwa na magonjwa ya Malaria, Kifua Kikuu na UKIMWI.

Hapa nchini, kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani *(WHO),* umefanyika utafiti kuanzia Februari mpaka Oktoba, 2012 kuhusu viashiria vya magonjwa yasiyo ya kuambukiza (*Step Survey on NCDs Risk Factors*). Utafiti huo umebaini kuwa, asilimia 26.8 hadi asilimia 31.9 ya Wananchi

wanatumia pombe. Kati ya hao asilimia 27.4 ya wanaume ni walevi wa kupindukia na wanawake ni asilimia 13.4.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kwa athari zinazotokana na matumizi ya pombe hasa kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza, Serikali inatekeleza mkakati wa kukabiliana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza, ambao unaelekeza kuhusu kutoa elimu kwa Wananchi kupitia njia mbalimbali. Aidha, Wizara imekamilisha Sera ya Pombe ambayo itahakikisha kuwa na tiba kwa watu walioathirika na matumizi ya pombe na kuhamasisha Wananchi hasa vijana kujizuia na matumizi ya pombe.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utaratibu wa kuziwezesha Hospitali za Rufaa za Mikoa kuanza kutoa huduma kwa waathirika wa matumizi ya dawa za kulevya na pombe. Aidha, Hospitali za Rufaa za Kanda zimejiimarisha katika kutibu magonjwa yasiyo ya kuambukiza, ikiwa ni pamoja na waathirika wa matumizi ya pombe. Kwa hiyo, Serikali inatamka kuwa, matumizi ya pombe kupita kiasi ni mabaya kwa afya yako, familia na taifa kwa ujumla.

**SPIKA:** Eeeh, wote ninyi mnakunywa pombe! (*Kicheko*)

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri kakiri kwamba, pombe ina madhara makubwa kwa afya za binadamu na watu zaidi ya milioni mbili wanapotea kila mwaka kwa kunywa pombe; na si hayo tu kuna matukio mengi yametokea nchini mwetu ambayo yanasababishwa na masuala ya pombe kama ubakaji, UKIMWI, ajali za barabarani na athari zingine. Je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kupiga marufuku pombe? *(Kicheko/Makofi)*

(ii) Kwa kuwa Serikali inafahamu kwamba, pombe ina madhara kwa afya ya binadamu na inawaachia tu Wananchi wake wakaogelea wanavyotaka wenyewe. Je,

kwa wale wanaothibitika kwamba wameathirika kwa pombe Serikali inawaambiaje? *(Makofi)*

**SPIKA:** Inawaambiaje au itawafanyaje? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwanza, matumizi ya vitu vyote ambavyo baadaye vimekuja kujulikana vina madhara, yalienda katika mtiririko wa kihistoria kama vile sigara ilivyoanza na pombe pia. Katika kiwango cha matumizi ya wastani hakikuwa kinajulikana kwamba kina madhara yoyote. Katika tafsiri hiyo, kwenye jamii husika iliendelea kukubalika kwamba, ni kitu sahihi tu kuendelea kukitumia na kwa sababu hiyo, hakukuwa na sheria ya kuzuia au kukifanya kitu hicho kiwe haramu au kiwe na kasoro yoyote ya kukitumia kama ilivyo sigara.

Mheshimiwa Spika, kadiri muda unavyoenda, kama ilivyo chakula na matumizi mengine yoyote, leo chumvi ina madhara kwa binadamu kama ukiitumia kupita kiasi, hatuwezi kupiga marufuku kutumia chumvi. Vivyo hivyo hatuwezi kupiga marufuku kutumia *fast-food*. Vilevile hatuwezi kukulazimisha uwe unafanya mazoezi kila siku kwamba, usipofanya tutakuadhibu. Ni wajibu wa kila mtu kuchukua jukumu la kulinda afya yake na kuwa mwangalizi mzuri wa afya yake, ikiwa ni pamoja na kutotumia pombe kupita kiasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mnawafanyaje wale walioathirika sasa? (*Kicheko*)

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

**SPIKA:** Eeh, uliza halafu Naibu Waziri atajibu yote mawili, ikiwa ni pamoja na alilosahau. Uliza tu.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa madhara ya pombe yanaenda sambamba na madhara ya sigara na tumbaku; na kwa kuwa wanaoathirika sana ni Wananchi wanaoishi vijijini hasa wazee

ambao wanachukua tumbaku jinsi ilivyo na kuweka mdomoni na kutafuna na hivyo madhara kuwa makubwa sana kiasi cha kusababisha Ugonjwa wa Kansa:-

Je, Serikali inasamaje juu ya matumizi haya ya tumbaku ambayo hayafuati viwango hasa vijijini?

**SPIKA:** Kwa sababu wewe ni daktari, pombe na tumbaku ni hao hao ndugu moja. Pia ujibu unawafanyaje walioathirika.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nitoe ufafanuzi juu ya waathirika na kwamba, Serikali inawafanya nini. Kama nilivyoelezea kwenye jibu la msingi, Serikali imeandaa sera ya kuweza kuona ni namna gani watu walioathirika wanapata huduma stahili, ikiwemo kupata ushauri nasaha wa kujizuia au kuacha matumizi ya pombe. Pia kwa wale ambao wameathirika, hupata tiba kwenye vituo vyetu vya tiba wakiwemo wale wa matumizi ya dawa za kulevya.

Suala la kwamba, sasa huyu mtu ameathirika basi Serikali ichukue jukumu la kumlipa au kufanya kitu cha namna hiyo, hilo halipo kwa sasa.

Labda nizungumzie juu ya matumizi ya sigara au tumbaku na kwamba, ikiwa haimo katika mfumo wa kiwango na madhara yake. Hata hii sigara ambayo imekuwa *packed,* inajulikana kabisa kwenye pakiti moja kuna sigara 20 na hata kiwango cha *nicotine* ndani kinajulikana, lakini bado vyote hivi vina madhara. Tunachoweza kusema ni kwamba, ni vyema mtu ukajizuia kutumia sigara au tumbaku kutokana na madhara ambayo tayari watu wengi wameshaanza kuyafahamu. Kwa hiyo, ni maamuzi ya mtu kuchukua jukumu la kulinda afya yake na kuacha kutumia kitu ambacho kina madhara katika mwili wake.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa naona mmesikia hayo maneno. Twende kwenye swali linalofuata; Mheshimiwa Mariam Kisangi!

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Kwa niaba ya Mheshimiwa Mariam Kisangi, naomba swali lake Na. 256 sasa lijibiwe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abia Nyabakari, huwezi kuanza kuuliza mpaka uitwe. Sasa nakuita Mheshimiwa Abia kwa niaba. *(Kicheko)*

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Spika, asante**.** Kwa niaba ya Mheshimiwa Mariam N. Kisangi naomba sasa swali lake Na. 257 lijibiwe.

Na. 257

**Nafasi ya Wategemezi Katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya**

**MHE. ABIA M. NYABAKARI (K.n.y. MHE. MARIAM N. KISANGI)** aliuliza:-

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umefanya mabadiliko yanayozuia wategemezi wasiingizwe katika Mfuko huo:-

Je, Serikali haioni kuwa haiwatendei haki wateja wa Mfuko huu ambao baadhi yao hawana watoto au wazazi na wanakatwa fedha nyingi kwa mwezi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dhana ya Bima ya Afya imejengeka katika misingi ya kuchangiana, ambapo mwenye familia ndogo (wategemezi wachache), anawasaidia wenye familia kubwa. Mwenye mshahara mkubwa, husaidia wenye mishahara midogo. Vijana wanawasaidia wazee. Msingi mkubwa wa Bima za Afya za Jamii ni kuwezesha mwanachama kutibiwa kulingana na tatizo au ugonjwa

wake bila kujali michango yake. Kwa sababu hii, anayechangia ni lazima ndugu zake wa karibu sana *(nuclear family*) na wazazi wake tu ndiyo wanufaike. Katika nchi nyingi ulimwenguni, Bima ya Afya huruhusiwa kwa *nuclear family* tu. Ujazaji wa nafasi zote za mwanachama hata kama hana watoto, ni kukiuka misingi ya Bima za Afya za Kijamii.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kudhibiti eneo la wategemezi, unalenga kuwa na wategemezi halisi wa mwanachama kwa mujibu wa taratibu za Utumishi wa Umma. Sababu zilizofanya Mfuko kuchukua hatua hii ni kudhibiti baadhi ya wanachama walioanza kuandikisha majirani au rafiki kama wategemezi; kudhibiti baadhi ya wanachama walioanza kuuza nafasi zao badala ya kujaza wategemezi wanaostahili kisheria; na kudhibiti watoa huduma wasio waaminifu ambao wamekuwa wakila njama na wanachama wa Mfuko wasio waaminifu, kuwaingiza watu wenye magonjwa sugu au magonjwa yenye gharama kubwa, mfano wenye magonjwa ya Saratani ambapo wastani wa gharama za dawa kwa mwezi ni shilingi 1.2 milioni.

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia suala hili, Mfuko umechukua hatua za kudhibiti kuhakikisha wale wote ambao tayari wameandikishwa kama wategemezi, wanaendelea kupata huduma hadi utaratibu mpya utakapopitishwa rasmi; ushauri wa kisheria toka ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu suala hili; kutoa elimu na kuongeza udhibiti, kuendelea na utekelezaji wa mpango wa kuvibadili vitambulisho vya sasa ili kuwa na aina bora zaidi inayotumia teknolojia mpya ya utambuzi na kuimarisha usimamizi wa huduma katika vituo vilivyosajiliwa na Mfuko hasa vituo vikubwa vilivyoko Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeuagiza Uongozi wa Mfuko wa Bima ya Afya, kubadili mfumo wa vitambulisho ili kuongeza udhibiti na kuendelea kutoa elimu zaidi kuhusu hujuma inazoendelea kukabiliana nazo.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Mariam Kisangi, naomba kuuliza swali la nyongeza.

Wazee wanapokwenda kutibiwa wanakuta hakuna dawa, hakuna vipimo, kwa hiyo, wale wanaowasaidia wanakwenda kununua dawa wenyewe. Si hivyo tu, wazee wanapohitaji vipimo vikubwa wanaambiwa watumie fedha zao wenyewe. Mfuko huu una maana gani kama hiyo siyo kuwahujumu hawa watu ambao hawana familia?

**SPIKA:** Hilo ni swali la kwako na siyo kwa niaba ya Mheshimiwa Kisangi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, Dhana ya Bima ya Afya ya Jamii ni katika suala la kwamba, yule mwenye kiwango kidogo ananufaika kupitia kwa yule mwenye kiwango kikubwa na yule mwenye familia ya watu wachache anamsaidia yule mwenye familia ya watu wengi, ana wategemezi wengi; ni tatizo la riziki ambayo inakuwepo pale kwamba mna-*share* riziki.

Sasa suala la wazee wanasaidiwa vipi wakati wao wanafika na wanaambiwa dawa hakuna. Kwa sasa hivi mzee ambaye yeye mwenyewe amekata Bima ya Afya ya Jamii, anapata huduma kama mwenye Bima yoyote mwingine na dawa zikiwepo pale atapata kwenye kituo husika na kama hazipo pale bado kuna maduka ya dawa ya *HADO*, ambayo yamesajiliwa na Mfuko wa Bima ya Afya, ili aweze kupata dawa kama anavyokuwa anahitaji kwa kutumia Mfuko huo huo wa Bima.

Kwa wale ambao hawana Bima, Serikali imeagiza hospitali kuweka Dirisha Maalum kwa ajili ya kutoa huduma kwa wazee na kuhakikisha kwamba, hao wazee wanapata dawa. Pale ambapo dawa hazipo kwenye hospitali, inakuwa ni suala lingine. Naomba pia usimamizi wa Halmashauri na watendaji wote katika kila Wilaya kuhakikisha kwamba,

wazee wanapata huduma bila ya kulazimika kutoa gharama nyingine.

**SPIKA:** Majibu marefu, sasa nina swali la tano tu, kwa hiyo, inabidi tuendelee mbele huko. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, kwa niaba yake Mheshimiwa Herbert Mntangi!

Na. 258

**Kuondolewa kwa *Crew Tanzania* – Korogwe Mjini**

**MHE. HERBERT J. MTANGI (K.n.y. MHE. YUSUPH A. NASSIR)** aliuliza:-

Mradi wa *CREW Tanzania* ulianzishwa mwaka 1991 – 1995 kwa lengo la kuwasaidia akina mama hususan wa Wilaya ya Korogwe kujiendeleza katika shughuli za uzalishaji mali na mikopo ili kuinua hali ya maisha yao na familia zao:-

(a) Kwa nini Mradi huo uliondolewa na nini hatima ya wafanyakazi wake ya kuwalipa malimbikizo ya mishahara na stahili zao mbalimbali na Serikali ina mpango gani na rasilimali zilizoachwa?

(b) Je, ni lini kiasi cha shilingi milioni 205 zilizochukuliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto mwaka 2000 katika utaratibu usioeleweka zitarejeshwa ili zitumike kusaidia vikundi vingi vya akina mama wajasiriamali?

(c) Je, ni nini hatima ya wote waliohusika kwa makusudi kuhamisha fedha hizo kwa kukiuka utaratibu na kurudisha nyuma maendeleo ya akina mama wa Korogwe?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ningependa kujibu

swali la Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, Mbunge wa Korogwe Mjini, lenye sehemu (a), (b), (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mradi wa *Credit Scheme for Productive Activities of Women in Tanzania (CREW Tanzania),* haukuondolewa katika Wilaya ya Korogwe, bali ulimaliza muda wake kama ulivyopangwa. Mradi huo ulianza mwaka 1991 hadi 1995 na kutekelezwa katika Wilaya za Korogwe, Handeni, Muheza na Lushoto Mkoani Tanga. Aidha, baada ya kukamilika kwa muda wa Mradi huu, mwaka 1995 Serikali ilianzisha chombo kinachojitegemea kilichojulikana kama Chama cha *CREW Tanzania*. Lengo likiwa ni kuendeleza malengo mazuri ya Mradi huo.

Mheshimiwa Spika, watumishi waliokuwa wakifanya kazi katika Mradi huu walikuwa wakilipwa mishahara pamoja na stahili nyingine na Mradi; hawakuwa wakilipwa na Wizara. Aidha, baada ya muda wa Mradi kumalizika, Chama cha *CREW Tanzania* kiliajiri watumishi wake kwa kuzingatia Katiba ya Chama. Serikali haiwajibiki katika kulipa malimbikizo ya mishahara na stahili zingine za watumishi wa Chama hiki. Aidha, kuhusu mali na vifaa vilivyokuwa chini ya Mradi, vilikabidhiwa rasmi kwa Chama cha *CREW Tanzania,* ili vitumike kwa ajili ya kuendeleza shughuli zilizokuwa zinatekelezwa na Mradi.

(b) Mheshimiwa Spika, wakati Mradi wa *CREW Tanzania* ulipomaliza muda wake mwaka 1995, kulikuwepo kiasi cha US$ 70,000, sawa na Sh. 70,000,000 ambazo zilikuwa hazijatumika. Fedha hizo ziliwekwa katika Benki ya NBC, Tawi la Twiga na kuongezeka kutokana na riba na kufikia Tsh. 255,000,000. Wizara iliamua baadhi ya fedha hizo (TSh. 205,000,000) zitumike kwa shughuli zake. Pia Chama cha *CREW - Tanzania* kilipatiwa sehemu ya fedha hizo (TSh. 50,000,000) ili ziweze kutumika kuwakopesha wanawake wajasiriamali. Utekelezaji wa uamuzi huu ulizingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Matumizi ya Fedha za Umma.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia majibu yangu katika sehemu (b), hakuna watumishi waliowajibishwa

kwa kuwa utekelezaji wa uamuzi wa kutumia fedha hizo ulizingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Matumizi ya Fedha za Umma.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ambayo yametolewa. Ninaomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Lengo la mwuliza swali lilikuwa ni kwamba, baada ya *CREW Tanzania* kumaliza muda wake kilianzishwa Chama cha *CREW Tanzania*. Sasa lengo ni kutaka kujua kwa nini Chama cha *CREW Tanzania* bado hawapo Korogwe. Kwa sababu walikuwepo Korogwe, walikuwepo Muheza, Handeni na Lushoto, lakini kwa nini Korogwe hawakuendelea kuwepo?

(ii) Katika maeneo mengi ikiwemo Muheza ambapo tumeanzisha vyama; kwa mfano, *VICOBA*, tuna vikundi zaidi ya 205 vya *VICOBA* vyenye fedha karibu shilingi bilioni moja. Sasa kuna watu wamekuja kwanza wanajiita wao ndiyo waanzilishi wa vikundi vya *VICOBA;* lakini wana lengo la kutaka kukusanya vikundi vyote ili vikae chini yao. Je, Wizara inaweza kwenda kusaidia kuondoa tatizo hilo katika Wilaya ya Muheza?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, Mradi huu ulikuwa chini ya ufadhili wa Denmark, *UNDP* na *ILO* na baada ya kumalizika kulianzishwa Chama chini ya *Societies Act*. Kwa hiyo, ni Chama ambacho kinajitegemea, kina Katiba yake, hakikuwa tena chini ya udhamini wa Serikali.

Tunajua kwamba, bado kuna ofisi Korogwe na kuna ofisi Dar es Salaam, lakini shughuli zao zimekufa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge hilo ni kama jinsi Chama chochote kingine kisicho cha Serikali kinavyofanya kazi. Kama una malalamiko utatuletea tuone ni jinsi gani chama kinaweza kikawa *resolved according to constitution* yake yenyewe.

Mheshimiwa Spika, lakini suala la pili, kuhusu *VICOBA*.

Kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Mntangi, kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuhamasisha wanawake kujiunga katika vikundi ili waweze kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyojua, ukimwezesha mwanamke kiuchumi umeiwezesha familia yake na umeliwezesha Taifa.

Mheshimiwa Spika, tupo tayari kwenda katika Wilaya ya Muheza kwa ajili ya kutazama shughuli mbalimbali za *VICOBA* zinavyofanywa na waanzilishi. Nimjulishe pia Mheshimiwa Mbunge kwamba, vyama hivi vya *SACCOS* vinasimamiwa na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Kwa hiyo, tutashirikiana na wenzetu, kuona ni kiasi gani tutaweza kuvisaidia *VICOBA*. Kama mnavyojua, Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye alikuwa anakaimu katika bajeti yetu, tayari kuna *possibility* ya kupata fedha kwa ajili ya kuongeza fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Tunaamini tutawafikia wanawake wengi zaidi hasa walio vijijini.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Na. 259

**Udhibiti wa Mwendo Kasi wa Magari Barabarani**

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA** aliuliza:-

Askari wa barabarani wamekuwa wakitumia tochi katika kudhibiti mwendo kasi wa magari na kutoza faini papo kwa papo kwa kumwonesha dereva husika mwendo uliozidi:-

Je, kuna uhakika gani kwamba mwendo uliozidi anaooneshwa dereva ndiyo mwendo halali aliokuwa akienda?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kupima mwendo kasi wa magari barabarani unafanywa kwa mujibu wa kifungu cha 51(3) cha Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168, kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2002. Lengo ni kuhakikisha kuwa, magari yanatembea barabarani kwa mwendo unaoruhusiwa kisheria, kwa kuzingatia aina ya magari na mazingira ya barabara husika.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa yapo malalamiko ya madereva juu ya vipimo vya mwendo kasi unaofanywa kwenye kipimio. Mara nyingi madereva wamekuwa wakikana ukweli kwa kuhofia kuadhibiwa na siyo kwa sababu askari ametoa vipimo vya uongo.

Mheshimiwa Spika, mashine inaposoma mwendo kasi, mhusika anaruhusiwa kuangalia; hivyo, atasoma mwendo na kuona muda anaotuhumiwa kuzidisha mwendo kama ulivyopimwa. Pia askari wanaofanya kazi ya kupima mwendo, wamefundishwa jinsi ya kutumia vifaa hivi na hupaswa kumwonesha dereva mwendo aliokuwa nao na hatimaye kumwelimisha madhara ya mwendo huo katika eneo husika. Aidha, ni nia ya Serikali kuhakikisha kuwa, Jeshi la Polisi linapata vifaa vya kisasa zaidi ambavyo vina uwezo wa kupiga picha ya gari, ikionesha mwendo, namba za gari, aina ya gari na hata abiria waliomo ndani ya gari hilo. Aina hii ya kifaa itaondoa wasiwasi anaouonesha Mheshimiwa Mbunge na madereva wengine.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Serikali inafahamu kwamba, kuna vifaa vya kisasa zaidi ambavyo vinaweza vinakaonesha namba ya gari, vikapiga picha, vikaonesha spidi iliyopo na vifaa hivi vimeanza kutumika katika nchi za Afrika kama Zambia, Malawi pamoja na Rwanda kwa muda mrefu:-

(i) Kwa nini Serikali ilikwenda kununua tochi zilizo chini ya kiwango haikununua tochi zinazoweza kukidhi vigezo; je, Serikali haioni kwamba haya ni matumizi mabaya ya kodi za Wananchi?

(ii) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba trafiki wamefundishwa jinsi ya kutumia hizo tochi; na kwa kuwa trafiki hawa hawa wanaweza wakasimamisha magari manne kwa mpigo kwa tochi hizo hizo zilizo chini ya kiwango na kuweza kuwaonesha spidi wote ile ile ambayo ilinasa gari la kwanza. Je, hamwoni kwa matumizi haya ni kuchochea trafiki kuchukua rushwa papo kwa papo na kudidimiza na kuikosesha Serikali mapato?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ujibu kwa kifupi, muda umeshaisha kwa hotuba ndefu ndefu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, kama ifuatavyo:-

Kwanza, hizi tochi ni vyombo vya kiteknolojia na teknolojia hata ungenunua hicho unachosema leo kwamba ni cha kisasa, basi muda mfupi kwa kasi ya teknolojia kitakuwa tayari hakifai. Kwa hiyo, tutaenda kuboresha kufuatana na teknolojia kwa kiwango ambacho bajeti yetu inaruhusu.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nikatae kwamba, haya yalikuwa matumizi mabaya, *then* ilikuwa tochi tulizonunua ndizo za kiwango cha juu au za aina nzuri kuliko zozote zile.

Mheshimiwa Spika, halafu kwamba tochi hizi kwa sababu hazina viwango zinachochea rushwa. Lengo hasa la kutumia tochi ni kutoa ushahidi kwa madereva. Lengo la msingi katika suala la kuwa na trafiki barabarani ni kuwafanya madereva, wakumbuke kwamba wana wajibu wa kutii sheria kwa ridhaa zao na kwamba siyo wale ndiyo watumike katika kuwazuia wasi-*over speed*. Kwa hiyo, suala la rushwa lipo

pengine na tunalifanyia kazi. Jitihada tunazo kubwa kuhakikisha lengo la kuwepo askari barabarani liendelee kuwa ni *deterrents* ya madereva kujisahau na kusababisha madhara ya maisha na mali za watu.

**SPIKA:** Muda hautoshi. Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, atauliza swali hilo.

Na. 260

**Jitihada za Kulinda Usalama wa Raia**

**MHE. ASHA MOHAMED OMARI** aliuliza:-

Matukio ya vurugu yamezidi kuongezeka kwa siku za hivi karibuni na kufanya Polisi kupelekea kufanya kazi ya ziada kudhibiti matukio hayo:-

Je, Serikali inafanya jitihada gani za ziada kudumisha usalama wa raia badala ya kusubiri kudhibiti vurugu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kumekuwa na matukio mengi ya vurugu kwa siku hizi za karibuni na kufanya Jeshi la Polisi kuwa na kazi ya ziada kudhibiti matukio hayo. Matukio mengi kati ya hayo yamekuwa na sura ya kidini, kisiasa na kugombea mali.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti matukio haya yasiendelee kutokea na kudumisha usalama wa raia na mali za Serikali, Jeshi la Polisi limeendelea kutoa elimu kwa Wananchi, juu ya umuhimu wa kuwepo na amani na utulivu kwa Wananchi. Jeshi la Polisi limekuwa likiendelea kutambua migogoro ya Wananchi na kuitafutia utatuzi kabla ya kuleta madhara na kupelekea matumizi ya nguvu. Kwa kutumia

njia mbalimbali na kwa kupitia makundi ya kijamii, Jeshi la Polisi limekuwa likiwataka Wananchi watii sheria bila shuruti, ambayo ni njia pekee ya kuondoa mivutano ndani ya jamii yetu. Aidha, Jeshi la Polisi limekuwa likifanya mazungumzo na makundi mbalimbali ya kijamii, kidini na kisiasa ili kutatua migogoro iliyomo ndani ya jamii yetu na kuongeza kuvumiliana.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kuwasihi Wananchi na Waheshimiwa Wabunge, kutafuta suluhu za tofauti zinazotokea kwa njia ya mazungumzo *(dialogue).*

**MHE. ASHA MOHAMED OMARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Jeshi la Polisi limekubali kwamba vurugu zinazojitokeza mara nyingi zinakuwa na sura za kidini, kisiasa na kugombania mali. Je, kwa nini vurugu hizo huwa mara nyingi zinatawaliwa na vijana?

(ii) Kwa kuwa Askari Polisi huwa wanatumia maji ya kuwasha katika kuondoa vurugu hizo. Je, maji hayo hayana madhara kwa binadamu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ujibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza, kwa nini vijana wanakuwa wengi zaidi katika vurugu hizi. Kwanza, tutambue kwamba, kwa hesabu, Tanzania, vijana ni asilimia 60. Kwa hiyo, kwenye makundi yote ambayo tunayazungumzia, yawe ya kidini, yawe ya kisiasa na yawe ya kugombea mali, watakuwa wengi *proportionally*. Lingine ni kwamba, vijana ambao tunao, bahati mbaya hapa Tanzania sasa hivi wengi wamekosa ajira na kwa sababu hiyo, wanaweza wakapendelea zitokee vurugu ili waweze kupata vitu ambavyo vinaweza vikatokea katika uporaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, vijana pote Duniani wanakuwa hawana cha kupoteza. Akiamua yeye hafikirii familia ipo nyuma au kitu gani; kwa hiyo ni rahisi kushawishiwa kushiriki kwenye masuala kama hayo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, maji ya kuwasha hayana madhara. Katika utafiti ambao ulifanywa katika kutafuta silaha baridi, maji yamethibitishwa kwamba, madhara yake ni ya kushtua ili watu watawanyike, lakini hawapati maradhi ambayo yatawadhuru kwa muda mrefu. Naomba niwahakikishie Wananchi kwamba, lengo hasa ni kuwashtua waondoke na kuwafanya wasiwe *comfort* katika kuendelea na vurugu ili watafute vichochoro wapumzike, lakini baada ya muda mfupi watakuwa vizuri.

**SPIKA:** Ahsante. Naona muda umekwisha, nina maswali mawili kwa dakika tano.

Na. 261

**Matumizi ya Mbolea Isiyo na Viwango**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Wakulima wengi wamepata hasara kutokana na matumizi ya mbolea isiyo na viwango iliyoingizwa nchini na kusambazwa kwa Wananchi:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na changamoto ya uwepo wa mbolea isiyo na kiwango na hivyo kuathiri uzalishaji

na tija katika mazao. Serikali kwa kutambua umuhimu wa udhibiti wa mbolea isiyo na viwango, kupitia Sheria ya Mbolea ya Mwaka 2009, Kifungu cha 7(1) imeunda, Mamlaka ya Usimamizi wa Mbolea *(Tanzania Fertilizer Regulatory Authority – TFRA)*. Kazi za Mamlaka hiyo ni pamoja kudhibiti ubora wa mbolea za viwandani (Chumvi Chumvi) na asilia *(Fertilizer Supplements)*, kutoa leseni za uagizaji na usambazaji wa mbolea hizo, kukagua mbolea zinazoingia nchini kabla ya kusambazwa nchini na kukagua ubora wa maghala ya kutunzia mbolea hizi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kukabiliana na tatizo hilo katika ngazi ya Halmashauri na Wakulima, Serikali imeanza kutoa mafunzo ya Wakaguzi wa Mbolea *(Fertilizer Inspectors)*, ambapo hadi mwezi Mei, 2012, jumla ya Wakaguzi wa Mbolea 44 kutoka Halmashauri mbalimbali walikuwa wamefuzu mafunzo hayo ya awali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2012/2013, Mamlaka ya Usimamizi wa Mbolea ilianza kwa kufanya ukaguzi katika baadhi ya Mikoa hapa nchini ikiwemo Mikoa ya Ruvuma, Rukwa, Mbeya, Iringa na Njombe na kuyafungia baadhi ya makampuni ambayo yalikutwa na mbolea ambazo hazikukidhi viwango.

Katika kuhakikisha kuwa, mamlaka inatekeleza majukumu yake ipasavyo, Serikali imeongeza Bajeti ya Mamlaka hiyo ili iweze kupanua wigo wa utekelezaji wa majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuendelea kutoa mafunzo ya wakaguzi na watathmini wa ubora wa mbolea *(Fertilizer Analysts)* walioko kwenye vituo vya utafiti katika kanda zetu zote.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatarajia kufanya marekebisho ya Sheria ya Mbolea ili kukabiliana na upungufu uliojitokeza baada ya marekebisho ya Sheria ya mwaka 2009. Naomba nitoe wito kwa Halmashauri zote na Viongozi wote wa Mikoa na Wilaya pia hapa nchini kuwapa ushirikiano Wakaguzi wa Mbolea wanapofika kwenye Halmashauri zao ili waweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ni kwa kuwa kwa muda mrefu sasa toka viwanda vyetu vya mbolea vilivyokuwa vinazalisha mbolea nchini vimekufa kabisa na havifanyi kazi hiyo, matatizo ya mbolea isiyokuwa na viwango na yenye ubora yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku; na kwa kuwa sasa hivi Serikali ina utaratibu wa ujenzi wa shughuli za kiuchumi...

**SPIKA:** Waziri wa Mambo ya Nje naomba urudi ukae unakokuwa umekaa. Naomba urudi kule kule. Naomba urudi ulikokaa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa heshima ya Kiti chako naomba nianze tena kuuliza swali langu kwa sababu ya *interruption* iliyotokea. Nadhani muda wangu utabaki vilevile.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la ubora wa mbolea katika nchi yetu limekuwa likiongezeka kutokana na kutokuzalishwa mbolea katika viwanda vyetu nchini ambapo viwanda vilikuwa vinazalisha mbolea nzuri na yenye ubora; na kwa kuwa Serikali ina utaratibu sasa hivi wa *PPP* wa kujenga uchumi wa nchi yetu. Je, ni lini Serikali (na leo nauliza kwa mara ya nne) itaruhusu ama itatengeneza utaratibu wa kutumia hata Mifuko yetu ya Pensheni kujenga viwanda vya mbolea nchini ili kuleta ubora wa mbolea na kupunguza bei ya mbolea kuwaletea tija wakulima katika nchi yetu ya Tanzania? Ni lini? Leo nauliza swali hili kwa mara ya nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini swali langu la pili, kwa kuwa suala la ubora wa mbolea siyo tu viwango vilivyoko katika mbolea yenyewe, hata kucheleweshwa kwa mbolea kuwafikia wakulima kunapunguza thamani ya mbolea kwa matumizi ya wakulima wale. Je, Serikali sasa iko tayari pale mbolea inapochelewa kuwafikia wakulima na kusababisha

hasara kwa wakulima, kuwapa wakulima fidia kama wanavyowapa wazalishaji wengine wa Tanzania wanapopata majanga?

**SPIKA:** Eeh, hilo swali lilikuwa hotuba. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Jenista kwa swal lenyewe, kwa sababu kwanza hili suala la viwanda vya mbolea vya ndani ni jambo ambalo Serikali imekuwa imejielekeza kwa muda mrefu tupate viwanda vya mbolea vya ndani. Sasa hivi na ugunduzi wa mbolea ya gesi asilia Mtwara kule na Lindi tutakuwa na viwanda vya mbolea vya *urea*. Upande wa viwanda vya kaskazini tuna *phosphate* tutakuwa tuna mbolea ya Minjingu.

Mheshimiwa Spika, kuchanganya mbolea hizi *blending* tunapata mbolea ya *NP* ambayo ndiyo mbolea inayotumika katika maeneo mengi ya Tanzania. Sasa tumeona kwa kuchanganya kwake Kiwanda cha Minjingu kimeweza kushusha mbolea hiyo ambayo inafanana na *DAP* kwa asilimia kama 30 hivi. Kwa hiyo, tunaomba kuhimiza na tunaomba kusema kwamba Serikali itaendelea na siyo Mifuko ya Pensheni tu, hata wafanyabiashara binafsi wamekuja, tutawahimiza waende kuzalisha *urea* ili ile *component* ya *urea* inayochanganywa na *phosphate* ipatikane kwa gharama nafuu zaidi. Hilo la upande wa *urea* baina ya sisi na watu wa Nishati na Madini tutahakikisha kwamba hilo linafanyika haraka uwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, hili la ucheleweshaji wa mbolea, naomba niseme kwamba ni kweli kwamba kwa mfumo ule wa zamani ambao bajeti ilikuwa inapita halafu Wizara zinakuja kufanya mambo yake baadaye, Wizara ya Kilimo tulikuwa tunashindwa kupeleka fedha za ruzuku za mbolea kwa wakulima mpaka hadi mwezi wa Septemba au Oktoba, maeneo mengine yanakuta wakati huo yameshaanza kupanda. Kwa hiyo, kwa sasa hivi tulivyojipanga na Wizara ya Fedha imekubali kwamba itatupa fedha hizo ifikapo

tarehe 1 Julai na ile nyongeza ambayo Kamati ya Bajeti imepitisha na Wizara ya Fedha imekubali, itaturuhusu tuwe tuna uwezo wa kuwafikishia wakulima mbolea hiyo ifikapo tarehe 1 Agosti, tuwe tumeshambaza mbolea katika maeneo mengi ambayo yatakuwa yameanza kupanda. Kwa hiyo, tunataraji kwamba kwa mwaka huu kwa mfumo wetu huu mpya hilo tatizo litaondoka.

**SPIKA:** Naomba tuulize swali la mwisho jamani muwe mnaangalia saa ehee!!

Na. 262

**Kunusuru Zao la Muhogo Nchini**

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED (K.N.Y. MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS)** aliuliza:-

Ugonjwa wa Ukoma wa muhogo (Batobato) huenezwa na inzi weupe kwa kasi ya usambazaji ya wastani wa 120 km/saa: Je, Serikali imejipangaje kuutokomeza ugonjwa huu ili kulinusuru zao la muhogo ambalo ni tegemeo kwa zaidi ya nusu ya Watanzania?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis, Mbunge wa Chonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa ukoma wa muhogo (Batobato) au kwa kitaalam *Cassava Mosaic Disease (CMD)* ulienezwa kwa mara ya kwanza hapa nchini kwetu mwaka 1894 miaka 115 iliyopita, kupitia virusi vya mdudu mweupe *(white fly*). Uchunguzi zaidi umegundua virusi vya aina tofauti vya ugonjwa wa Batobato unaosababishwa na virusi vya Africa *(Africa Cassava Mosaic Virus),* Virusi vya Afrika Mashariki *(East Africa Cassava Mosaic Virus)* na virusi vya India *(Indian*

*Cassava Mosaic Virus).* Aidha, kasi ya kusambaa kwa ugonjwa huo inakadiriwa kufikia kilomita 120 kwa mwaka *(120km/year)* kufika hapa leo unafika kilomita 120 baada ya mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, ugonjwa huo huenea na kusambaa haraka kupitia inzi weupe *(whiteflies)* kama nilivyosema, ambao hufyonza majimaji yenye virusi kutoka kwenye mimea iliyoathirika na kuambukiza mimea ambayo haijaathirika pamoja na wakulima kupanda pingili za muhogo zilizotokana na mimea ambayo tayari imeathirika. Athari za ugonjwa huo ni kwamba tija ya muhogo imetoka kutoka tani 10 kwa hekta moja hadi tani sita kwa hekta moja.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Idara ya Utafiti na kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Utafiti za Kitaifa na Kimataifa, kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, *ASARECA*, na kadhalika wamefanyia utafiti zao hilo na kuainisha mbegu tofauti za aina mbalimbali kulingana na mazingira ya kila Kanda nchini zenye ukinzani zinazoweza kupambana na ugonjwa huo.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa aina za mbegu zenye ukinzani dhidi ya magonjwa ya Batobato na michirizi ya kahawia kwenye muhogo kwa kutumia teknolojia ya uhandisi jeni *(Genetic engineering)* unaendelea kupitia kituo cha utafiti cha Mikocheni. Aidha, utafiti huo bado uko katika hatua za awali na unalenga kuainisha vinasaba vyenye ukinzani dhidi ya magonjwa hayo ili kuvipandikiza kwenye aina ya mihogo asilia *(Local Landraces).*

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali ni kuendeleza juhudi za kutafiti mbegu zenye kuvumilia ugonjwa huo, kutoa mafunzo kwa wakulima na Maafisa Ugani kuhusu mbinu za kuzuia kuenea kwa ugonjwa huo pamoja na kuteketeza masalia yote ya muhogo ulioshambuliwa na ugonjwa baada ya kuvuna.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rukia, swali la nyongeza.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Tanzania ni nchi ya tatu kwa uzalishaji wa muhogo barani Afrika baada ya Nigeria na Congo; na kwa kuwa chakula hiki cha muhogo ni chakula kinacholiwa na Watanzania wengi. Je, Serikali ina mpango gani madhubuti ya kulifanya zao hili la muhogo kuwa nambari moja Barani Afrika hasa kwa vile Tanzania ina ardhi kubwa na nzuri kwa ajili ya kilimo hiki?

Pili, Je, Serikali ina mpango gani endelevu wa kuifanyia *processing* muhogo na kuusafirisha nje ya nchi kwa ajili ya kuwapatia mapato wakulima wa kilimo hiki ili kuondokana na umaskini uliokithiri? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri! Wanasema na pombe inaweza kutumika muhogo. Sasa hiyo ni hatari ya pombe.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwanza Tanzania ni nchi ya tatu kwa uzalishaji mihogo Afrika, ina kama tani 7,000,000 za uzalishaji na hata katika uzalishaji huo, uwezo wetu kama nchi bila ya kufanya jitihada ya ziada sana tunaweza kuzalisha mpaka tani 20,000,000.

Kwa hiyo, hiyo ndiyo *strategy* ambayo tunakopelekea sasa hivi na moja ya mambo ambayo tunasema kinatukwaza sasa hivi ni huu ugonjwa Batobato ambao unaenea kwa kasi sana. Watafiti wetu wameshafika hatua nzuri wamepata mbegu ambazo zinakinzana na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, kazi iliyokuwepo sasa hivi ni kusambaza mbegu hiyo nchi nzima na kuhakikisha kwamba wakulima wanatumia mbegu hiyo kwa namna ambayo inazuia kuenea kwa ugonjwa huu na inaongeza uzalishaji. Kwa hiyo, huo ndiyo mkakati wa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, hili suala la pili la *agro processing,* hili la kupata viwanda ambavyo vitaongeza thamani kwenye mihogo; jambo hili linafanyiwa kazi. Kwa sasa hivi tuna mwekezaji ambaye tulikutana naye Afrika Kusini juzi anaitwa Submiller**,** yeye alikuja kutuona *delegation* ya Tanzania. Yeye peke yake anataka kuanza kununua mpaka tani 50,000 za mihogo kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi. Kwa hiyo, tunaamini kwamba yeye atahamasisha uwekezaji mwingine katika *agro processing*. Lakini pia na sisi tunajiweka ili kununua muhogo kama zao la chakula la akiba. Maana kama unavyojua ugali wa muhogo ni ugali mzuri zaidi kuliko karibu ugali mwingine wowote ule.

**SPIKA:** Haya, Waheshimiwa Wabunge, maswali tumezidisha muda, lakini yamekwisha. Jamani tukitaka kipindi chetu kiwe kizuri zaidi tuache kuhutubiana. Maana yule anayeuliza swali la nyongeza anatuhutubia mpaka tunakoma. Lakini na Mawaziri naomba, Waziri anayejibu swali lake kwa kifupi hapa kwa kusoma linakuwa na nguvu zaidi kuliko lile linalonyulumbushwa anajibu mwenyewe mpaka anashindwa kuhema hapa. Sasa nitawataja Mawaziri ambao wana tabia ya kuandika maswali marefu, siwataji hapa nitawaandikia barua. Nawajua na Wabunge wenyewe wanawajua.

Kwa kweli hata wewe mwenyewe unasoma hapa mpaka unasikia kuchoka, halafu huna hakika kama wenzio wanakusikiliza, kwa sababu umesoma kwa muda mrefu mno, *five minutes! We can't do that*.

Kwa hiyo, tunataka Waheshimiwa Wabunge mwulize maswali chapu chapu! Utakuta tunauliza *average* maswali ya nyongeza yanakuwa matatu na kadhalika. Lakini hapa inafika, haiwezekani. Kwa hiyo, tutakuwa tunawaambia mtu anayeuliza swali refu tunamwambia hilo hilo, basi. Kwa hiyo, Mawaziri mjitahidi, nisingependa kuwaweka hapa bayana.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitangaze kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Mazingira - Mheshimiwa James Lembeli, anaomba

niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.15 watakuwa na kikao chao katika ukumbi Na. 231. Halafu Katibu wa Wabunge wa *CUF* - Mheshimiwa Magdalena Sakaya, anasema anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wa *CUF* leo saa 7.00. Nafikiri tufanye saa 7.15 mchana. Kutakuwa na kikao cha Wabunge wa *CUF* katika ukumbi wa *Basement*. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wa *CUF* mnahitajika kuhudhuria hapo *basement* nafikiri saa 7.15 ni vizuri zaidi.

Halafu kuna tangazo lingine linatoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kupitia Naibu Waziri - Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwamba anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote. Mnatangaziwa juu ya uwepo wa matibabu ya bure ya ugonjwa wa fistula yanayotolewa na *CCBRT* na kufadhiliwa na *VODACOM*. Msikilize vizuri. Kwa nini nyie mnasemasema hata vitu hamjaambiwa. Haya, niendele msikilize. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnaombwa kuwahimiza wanawake wote katika Majimbo yenu hasa mnapokuwa katika Mikutano ya Hadhara kuwa fistula inatibika, hivyo wajitokeze kupata matibabu. *(Makofi)*

Mgonjwa anatakiwa kupiga simu bure *VODACOM* na namba imetolewa, nafikiri mtawagawia na watamtumia nauli. Sasa akishapiga hiyo simu, simu yenyewe wanaonakili waandike ni 0800752227. Narudia ni simu ya *Vodacom*, ni 0800752227. Halafu *VODACOM* watamtumia mgonjwa nauli ya kwenda Dar es Salaam. Aidha, atakapofika Dar es Salaam, atapokelewa na kupelekwa moja kwa moja Hospitali ya *CCBRT* na kupatiwa matibabu na malazi bure na kwa gharama za *VODACOM*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, vipeperushi kuhusu huduma hii vimewekwa kwenye *pegion holes* zenu, mnaombwa mpitie mzione. Kwa maelezo zaidi, wasiliana na Waheshimiwa Wabunge, Mabalozi wa kutokomeza fistula ambayo ni Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Naibu Waziri, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Ritta

Kabati na Mheshimiwa Saidi Mtanda. Kwa hiyo, ukitaka zaidi mwende huko. Mimi ni mlezi wa *CCBRT* na hata keshokutwa ni siku ya kukumbuka wagonjwa wa fistula. Ugonjwa huu kwa kawaida unaathiri sana wanawake kisaikolojia. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo!

**SPIKA:** Lakini unapona, tena kwa haraka kabisa. Pale wanatunzwa vizuri na kurudishiwa kujiamini. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tunachokisema, ni kutangaza tu kwa sababu watu wengi wana *tendency* ya kuona aibu. Ndiyo maana tunasema ahaa, sisi! Hata nyie mnaweza kupata matatizo ya namna hiyo. Lakini ugonjwa ni ugonjwa na matibabu yapo, tena matibabu mazuri tu ya heshima. Pale *CCBRT* wanatibu vizuri sana. Kuna mtu pale aliyeachwa na mume wake, ameachwa na ndugu, lakini ametibiwa amekuwa mzima na mmoja pale ndio anayewafundisha wenzake, sasa amekuwa mwalimu wa wenzake. Kwa hiyo, matibabu haya yapo bure, watangazieni na wananchi. *(Makofi)*

Halafu naona mwingine alichelewa kidogo. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala - Mheshimiwa William Ngeleja anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba saa 7.15 kutakuwa na kikao katika ukumbi Na. 133.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali - Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na Taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji ya Mwaka 2012/2013 na

kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, naomba hotuba yangu ya bajeti iingie yote kwenye *Hansard* kama ilivyo kwenye kitabu cha hotuba yangu kwa kuwa ninayoyasoma ni ufupisho wa hotuba hiyo. Hotuba yenyewe ni kurasa 126 na mimi hapa nina kurasa 20 peke yake.

Mheshimiwa Spika, wakati Waheshimiwa Wabunge watakuwa wanapata hotuba yangu, ninawaomba vilevile kwa muda wao waende kwenye *pegion holes* zao wapate vipeperushi na taarifa ambazo ni za msingi kweli kweli katika majadiliano yetu. Taarifa ya kwanza ni hii. "Umeme Ndiyo Uchumi. Hatuwezi kutoa umasikini kama ndugu zetu wa vijijini hawana umeme." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tumewatayarishia ramani kama ilivyokuwa mwaka 2012 na nilitoa hapa ahadi kwamba kila mwaka tutakuwa tunatoa ramani. Tuna ramani ambazo ni tatu za Tanzania zinaonyesha miradi ambayo Wakala wa Umeme Vijijini *(REA)* amekamilisha. Ramani ya kwanza mtaiona na majina ya vijiji.

Ramani ya pili ya Tanzania itakuwa inawaonyesha mahali ambapo miradi sasa hivi inafanyika. Ramani ya tatu ambayo ndiyo ya bajeti hii, hii sasa tumeifanya iwe bora zaidi kuliko mwaka 2012. Tumeweka majina ya Wilaya, vilevile tumeweka idadi ya wakazi kwenye Wilaya hiyo na Mkoa na majina ya vijiji ambavyo vimetengewa fedha kwa bajeti ambayo nitaiwakilisha. Kwa hiyo, hii ni *document* ya kwanza muhimu sana mtaipata kwenye *pegion holes* zenu.

Mheshimiwa Spika, Taarifa nyingine ambayo ni muhimu sana tumeitoa kwenye magazeti, lakini tunadhani Wabunge wengi hamkupata muda wa kuisoma. Tumetengeneza kakijitabu hapa na tutakagawa karibu Tanzania nzima. Hii ni taarifa kwa Watanzania namna Mikoa ya Lindi na Mtwara inavyofaidika na utafutaji na uendelezaji wa gesi asilia. Ni kakijitabu kadogo hapa. Tunaomba

Waheshimiwa Wabunge mkisome kwa ajili ya majadiliano yetu. Mtakavyovikuta kwenye pegion holes zenu vile vile kwa Watanzania wote wakiwemo wa Mtwara na Lindi ni kipeperushi cha matumizi ya gesi asilia, miradi na manufaa yake. Hii ni kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mtakachokikuta kingine ni faida ya matumizi ya gesi badala ya mafuta ya taa na mkaa. Nadhani hii hoja kwamba tunataka ndugu zetu waache kutumia mkaa. Tumewatengenezea kipeperushi vilevile mtakikuta kwenye *pegion halls* zenu na Watanzania wengine tutawagawia huko waliko.

Mheshimiwa Spika, uchimbaji na utafutaji wa mafuta na gesi usituhangaishe kichwa, haukuanza leo. Tumetoa kipeperushi cha historia ya utafutaji wa mafuta ya gesi nchini mwetu toka mwaka 1950 mpaka leo hii. Mtakikuta kwenye *pegion halls* zenu na Watanzania wanaotusikiliza watapata fursa na wao kupewa. Kingine mtakachokikuta kwa mambo ya wazi kabisa, maana wengine wanasema kuna sirisiri huko, uwazi kabisa, kuonyesha leseni ambazo Serikali imezitoa kwa Makampuni yanayotafuta na baadaye yatachimba mafuta na gesi; yapo hapa na majina yao. *(Makofi)*

Ndugu zangu, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wanaonisikiliza, tumeongea sana mambo ya Mtwara, lakini tunasahau kwamba gesi iligunduliwa Songosongo mwaka 1974 na niwashukuru wenyeji wa Songosongo na Lindi ambao toka mwaka huo mpaka leo hii hatujasikia purukushani zozote na bomba hili la Mtwara tunalolijenga siyo bomba la kwanza, bali Songosongo limejengwa bomba ambalo sasa hivi linabeba uchumi wetu kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, historia ya Songosongo iko hapa. Hii ni historia ya nyuma, lakini tuna historia ya hivi karibuni ya Lindi na Mtwara.

Waheshimiwa Wabunge, tunajenga bomba. Niliwapatia mchoro mwaka 2012, lakini huu mchoro unakwenda unabadilika kutegemeana na maendeleo.

Vilevile mtaona mchoro wa bomba tunalolijenga na mahali ambapo tutaweka mitambo ya kufua umeme. Kwa hiyo, mambo ya kusema tutafua umeme siyo mambo ya kusadikika, ni ya kweli. Mchoro wa mwisho mtakaoupata, tumeonyesha eneo la Kinyerezi jinsi ambavyo mitambo mipya isiyokuwa ya *capacity charge* ambayo ni mali ya Tanzania itakapowekwa. Huo mchoro mtaupata kwenye pegion halls zenu na Watanzania wengine watapata fursa ya kugawiwa.

Mheshimiwa Spika, hivi ni vielelezo muhimu sana na Waheshimiwa Wabunge hotuba ninayotaka kuitoa sasa hivi ni ya kihistoria na naomba Waheshimiwa Wabunge muisikilize na Watanzania wote muisikilize kwa makini, kwa sababu katika historia ya Bunge hili, sidhani kama imeshakuja bajeti ambayo asilikia 90 inakwenda kwenye miradi ya maendeleo. Asilimia 90! Kwa hiyo, ndugu zangu zikilizeni kwa makini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii ya kuwasilisha ndani ya Bunge lako Tukufu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2013/2014.

Awali ya yote, napenda kuwashukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal na Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa miongozo na ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, nawashukuru Mheshimiwa George Boniface Simbachawene - Naibu Waziri anayeshughulikia masuala ya Nishati, Mheshimiwa Stephen Julius Masele - Naibu Waziri anayeshughulikia masuala ya Madini kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kuongoza Wizara.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa uongozi wenu mahiri katika kuliongoza Bunge hili na Kamati zake. Kwa namna ya pekee, natoa shukrani zangu za dhati kwa

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini - Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Makamu Mwenyekiti - Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa mchango wao mkubwa katika kuchambua Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2013/2014. Aidha, pamoja na upya wake, Kamati hiyo imekuwa ikitoa ushauri unaolenga kuboresha utendaji wa Wizara kwa maslahi ya Taifa, hasa katika kuhakikisha kwamba umeme wa uhakika unapatikana ili kuwezesha ukuaji wa uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwezi Machi, 2013 Bunge lako Tukufu lilimpoteza Mheshimiwa Salim Hemedi Khamis - Mbunge wa Chambani, Kisiwani Pemba. Naungana na wenzangu kutoa pole kwa Bunge lako, familia ya Marehemu na wote walioguswa na msiba huo. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2012/2013, Wizara iliendelea kutekeleza mipango yake ili kuhakikisha kuwa Sekta za Nishati na Madini zinachangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi na Pato la Taifa. Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika Sekta ya Nishati ni kuongeza miundombinu ya gesi asilia, kuendeleza shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia, kusimamia biashara ya mafuta, kuongeza uwezo wa kufua umeme, kujenga njia za kusafirisha na kusambaza umeme, kuongeza kasi ya kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya na maeneo ya Vijijini, kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu katika ufuaji wa umeme, kuhamasisha matumizi bora ya nishati na kudurusu na kuandaa sera, sheria na mipango kwa ajili ya kusimamia Sekta ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kufanyika katika Sekta ya Madini ni kuboresha utoaji na usimamizi wa leseni za madini; kuendeleza uchimbaji mdogo wa madini; kuhamasisha uongezaji thamani madini; kuimarisha soko la

madini ya vito; kuimarisha usalama, afya na utunzaji wa mazingira migodini; kuwezesha utekelezaji wa shughuli za *Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative (TEITI);* kuongeza fungamanisho la Sekta ya Madini na sekta nyingine za uchumi; ujenzi na uboreshaji wa ofisi za madini; na kuziwezesha Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Ukusanyaji wa Mapato. Katika Mwaka 2012/2013, Wizara yangu ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 193.01. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2013 jumla ya Shilingi bilioni 157.29 zimekusanywa, sawa na asilimia 81.5 ya lengo. Lengo la Wizara ni kufikia asilimia 100 kabla ya mwisho wa mwezi wa Sita. Juhudi za ukusanyaji zinaendelea ili kuhakikisha kuwa Wizara inafikia lengo hilo.

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2012/2013 ilikuwa Shilingi bilioni 641.27. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 110.08, sawa na asilimia 17.2 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi bilioni 531.19, sawa na asilimia 82.8 zilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kwa hiyo, tumetoka kwenye 82.8, tumekwenda 90. Hata hivyo, Bajeti hiyo iliongezeka hadi kufikia Shilingi bilioni 826.27 kutokana na ongezeko la Shilingi bilioni 185.00 katika Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya kuendesha mitambo ya kufua umeme.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2013 jumla ya fedha zilizopokelewa na Wizara kutoka Hazina zilikuwa Shilingi bilioni 740.91, sawa na asilimia 89.7 ya Bajeti yote ya Wizara kwa Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye Sekta ya Nishati, kuhusu hali ya uzalishaji umeme. Katika Mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ili kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme nchini. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2013 uwezo wa mitambo ya kufua umeme *(installed capacity*) ulikuwa MW 1,438.24 (gesi asilia – asilimia

35, maji – asilimia 39 na mafuta – asilimia 26) ikilinganishwa na uwezo wa MW 1,375.75 uliokuwepo Mwezi Juni, 2012. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2012 kiasi cha umeme kilichoingizwa kwenye Gridi ya Taifa kilikuwa MWh 5,759,756 ikilinganishwa na MWh 5,153,400 Mwaka 2011 sawa na ongezeko la asilimia 11.8. Aidha, mahitaji ya juu kabisa ya umeme kwa Mwaka 2012/2013 yalifikia MW 851.35 Mwezi Oktoba, 2012 ikilinganishwa na wastani wa MW 820.35 kwa Mwaka 2011/2012. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 3.8. Sababu ya ongezeko hili ni kutokana na kukamilika kwa miradi mingi ya umeme vijijini.6

Mheshimiwa Spika, lingine linahusu Sekta ndogo ya umeme katika kuongeza uwezo wa kufua umeme. Katika juhudi za kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini, Serikali imechukua hatua mbalimbali ambazo ni pamoja na:-

(i) Ujenzi wa Mtambo wa MW 60 Mwanza;

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kusimamia ujenzi wa mtambo wa kufua umeme wa MW 60 utakaotumia mafuta mazito *(HFO)* katika eneo la Nyakato, Mwanza. Ujenzi wa kituo hicho umekamilika Mwezi Mei, 2013 na unatarajiwa kuzinduliwa rasmi Mwezi Juni, 2013. Kukamilika kwa ujenzi wa kituo hicho kutaboresha upatikanaji wa umeme na kuimarisha Gridi ya Taifa katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa.

(ii) Mradi wa Kinyerezi I - MW 150;

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza utegemezi wa mitambo ya kufua umeme kwa kutumia mafuta ambayo ni ghali, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa Kinyerezi - I (MW 150). Mradi huo utakaotumia gesi asilia na ujenzi wa njia za umeme za msongo wa kV 220 (Kinyerezi - Kimara) na kV 132 (Kinyerezi - Gongolamboto) utagharimu Dola za Marekani milioni 183.30, sawa na Shilingi bilioni 293.28. Mkandarasi wa mradi huo ni *M/S Jacobsen Electro AS* kutoka Norway na Mshauri ni M/S Lahmeyer kutoka Ujerumani. Mkandarasi amelipwa malipo ya awali ya Dola za Marekani milioni 30, sawa na Shilingi bilioni 48 kutoka Hazina zikiwa ni

fedha za Watanzania. Utekelezaji wa Mradi huo umeanza Mwezi Januari, 2013 na umepangwa kukamilika Mwaka 2014/ 2015.

(iii) Mradi wa Kinyerezi II – MW 240;

Mheshimiwa Spika, *Japan Bank for International Corporation (JBIC)* ya Japan ambayo itatoa mkopo wa asilimia 85 ya gharama za mradi wa Kinyerezi – II imewasilisha Serikalini Rasimu ya Mkataba wa Mkopo. Serikali itatoa asilimia 15 ya gharama za mradi. Gharama za mradi huo ni Dola za Marekani milioni 432, sawa na Shilingi bilioni 691.20.

(iv) Mradi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira MW 200;

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2012/2013, Serikali imekamilisha taratibu za kisheria za kuurejesha Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira kutoka Kampuni ya *"TanPower Resources Ltd".* Baada ya hatua hiyo, Serikali kupitia *STAMICO* ilifanya majadiliano na Kampuni ya "China *National Plant Import and Export Corporation Ltd" (COMPLANT)* ili kuharakisha utekelezaji wa mradi huu. Gharama za mradi zinakadiriwa kufikia Dola za Marekani milioni 400, sawa na Shilingi bilioni 640. Mradi huo ukikamilika utakuwa na uwezo wa kufua umeme wa MW 200 kwa hatua ya awali.

(v) Mradi wa Makaa ya Mawe wa Ngaka MW 400;

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ngaka unaendelezwa na Kampuni ya *TANCOAL Energy Limited* ambayo ni Kampuni ya ubia kati ya Serikali kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa – *NDC* (asilimia 30) na Kampuni ya *Intra Energy Limited* ya Australia (asilimia 70). Kampuni hiyo imeendelea na uchimbaji wa makaa ya mawe ambapo kwa kipindi cha kuanzia Agosti, 2011 hadi Aprili, 2013 jumla ya tani 166,775 za makaa ya mawe zilizalishwa, ambapo tani 121,685 ziliuzwa nchini na katika nchi za Kenya, Malawi, Mauritius na Uganda. Mauzo hayo yalikuwa na thamani ya Shilingi bilioni 14.66, sawa na Dola za Marekani milioni 9.16 ambapo Serikali imepata mrabaha wa Shilingi milioni 439.77, sawa na Dola za Marekani 274,856. Kampuni

ya *TANCOAL Energy Limited* inapitia upya Taarifa ya upembuzi yakinifu *(feasibility study)* kwa ajili ya kujenga mitambo ya makaa ya mawe yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa MW 400.

Aidha, majadiliano kati *TANESCO* na *TANCOAL Energy Limited* kuhusu Mkataba wa Kuuziana Umeme *(PPA)* pamoja na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 220 kutoka Ngaka hadi Songea yatakamilika katika Mwaka 2013/ 2014. Mradi huu utagharimu takriban Dola za Marekani milioni 400, sawa na Shilingi bilioni 640.

(vi) Mradi wa Kufua Umeme wa Mchuchuma MW 600;

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Kampuni ya Sichuan Hongda ya China kwa kushirikiana na *NDC* imechoronga mashimo 40 ya utafiti yenye jumla ya kina cha mita 8,800. Mradi huo unaendelezwa kwa ubia kati ya *NDC* (asilimia 20) na Kampuni ya Sichuan Hongda (asilimia 80) unatarajiwa kufua umeme wa MW 300 katika awamu ya kwanza na unatarajiwa kukamilika Mwaka 2015/2016. Mradi mzima utagharimu Dola za Marekani bilioni 1.2, sawa na Shilingi bilioni 1,920.

(vii) Mradi wa Somanga Fungu MW 320;

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANESCO* imekamilisha majadiliano ya mkataba wa kuuziana umeme *(Power Purchase Agreement - PPA*) na Kampuni ya *“Kilwa Energy Ltd”.* Baada ya Mkataba huo kuidhinishwa na *EWURA*, Kampuni hiyo itaanza utekelezaji wa mradi huu kwa awamu ambapo kwa kuanzia itafunga mitambo ya uwezo wa kufua umeme wa MW 230.

Gharama za mradi huu ni Dola za Marekani milioni 365, sawa na Shilingi bilioni 584. Majadiliano kati ya Kampuni ya *Kilwa Energy Ltd* na *TANESCO* kuhusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Somanga Fungu hadi Kinyerezi, Dar es Salaam katika msongo wa kV 220 yatakamilika mwishoni mwa Mwezi Juni, 2013.

(viii) Mradi wa Ufuaji na Usambazaji wa Umeme – Biharamulo, Mpanda na Ngara (ORIO);

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, uchambuzi wa zabuni ya ujenzi wa mradi wa ufuaji na usambazaji wa umeme katika Miji ya Biharamulo, Mpanda na Ngara umekamilika na utekelezaji wake utaanza mwaka 2013/2014 na kukamilika mwaka 2014/2015. Mradi huu unahusisha ukarabati na upanuzi wa mfumo wa usambazaji umeme pamoja na ufungaji wa jenereta tatu zenye uwezo wa kufua umeme wa MW 2.5 kila moja katika maeneo hayo. Gharama za mradi huu ni *Euro* milioni 33, sawa na Shilingi bilioni 66.

(ix) Mradi wa Kufua Umeme, Murongo – Kikagati;

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012/2013, Serikali ilidhamiria kutekeleza mradi wa kufua umeme wa MW 16 kwa kushirikiana na Serikali ya Uganda (MW 8 kwa kila nchi). Hata hivyo, baada ya kupitia kwa kina rasimu ya Mkataba wa mradi huo, imebainika kuwepo kwa upungufu katika rasimu hiyo. Kutokana na hali hiyo, tumeamua kupitia upya vipengele vyote vya Mkataba kabla ya kuanza kwa utekelezaji kwa lengo la kulinda maslahi ya nchi yetu. Gharama za mradi huo ni Dola za Marekani milioni 30.46, sawa na Shilingi bilioni 48.74.

(x) Ukarabati wa Mitambo katika Vituo vya Kufua Umeme;

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa vituo vya kufua umeme kwa kutumia maji vya Kihansi, Kidatu, Nyumba ya Mungu, Mtera na *New Pangani Falls* umeanza, baada ya kupata fedha kiasi cha Krona milioni 63 kutoka Serikali ya Norway, sawa na Shilingi bilioni 18.20. Kampuni ya "Verkis" kutoka nchini Iceland ambayo itasimamia utekelezaji wa mradi imepatikana. Aidha, uchambuzi wa zabuni za kupata Wakandarasi wa kukarabati vituo hivyo unaendelea.

(xi) Mradi wa Aggreko wa MW 100;

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012/2013, Wizara kupitia *TANESCO* ilihuisha Mkataba wa kufua umeme kiasi cha MW 100 na Kampuni ya Aggreko kwa mwaka mmoja zaidi. Uhuishaji wa mkataba huo ulifikiwa baada ya makubaliano ya kupunguza bei za kuuziana umeme pamoja na urejeshaji mtaji *(Energy and Capacity Charges)* kwa takriban asilimia 34.12.

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee kuhusu ruzuku kwa *TANESCO*. Itakumbukwa kuwa Mwezi Agosti, 2011 Serikali iliamua kuidhamini *TANESCO* ili ipate mkopo wa Shilingi bilioni 408, sawa na Dola za Marekani milioni 255. Hata hivyo, kutokana na taratibu za mikopo za kibenki, *TANESCO* imeweza kupata Dola za Marekani milioni 65 tu, sawa na Shilingi bilioni 104. Hivyo, Serikali kulazimika kuingilia kati na kutoa Shilingi bilioni 402.23 kama ruzuku badala ya mkopo. Fedha hizo zimeiwezesha *TANESCO* kuendelea kutoa huduma ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kujenga njia za kusafirisha na kusambaza umeme kwa upande wa uimarishaji njia za kusafirisha na kusambaza umeme; Serikali iliendelea kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo:-

(i) Uboreshaji wa Huduma za Umeme Jijini Dar es Salaam;

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANESCO* imefunga jumla ya transfoma mpya 15 katika vituo vya Buguruni, *City Centre*, Kariakoo, Kipawa, Mbagala, Mbezi, *Oysterbay* na Ubungo. Vilevile, ufungaji wa transfoma mpya katika vituo vya *Bahari Beach,* Gongo la Mboto, Kigamboni na Kunduchi upo katika hatua za mwisho za utekelezaji.

Mradi huu utakamilika mwaka 2014/2015 na utagharimu Dola za Marekani milioni 75, sawa na Shilingi bilioni 120. Ufungaji wa transfoma hizo utaimarisha upatikanaji wa umeme Jijini Dar es Salaam. Zoezi hili linaendelea katika maeneo mengine ya Jiji.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kubadilisha nyaya zenye ukubwa wa milimita 150 na kuweka zenye ukubwa wa milimita 432 pamoja na kubadilisha nguzo zilizooza kwenye njia ya umeme ya kV 33 Ilala – Kurasini imekamilika kwa asilimia 99.

Kazi iliyobaki ni kukarabati maungio yote tangu mwanzo wa njia hadi mwisho. Njia hii ya umeme ilikuwa inakatika mara kwa mara na kusababisha wateja wa maeneo ya Kigamboni, Kurasini, Mbagala na Mkuranga, kukosa umeme wa uhakika. Baada ya ukarabati kukamilika, wateja wa maeneo hayo sasa wanapata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na kumpata Mkandarasi ambaye ni Kampuni ya *M/S ELTEL Group OY* kutoka Finland kwa ajili ya kutekeleza mradi wa huduma za umeme Jijini Dar es Salaam. Mradi huo unafadhiliwa na Serikali ya Finland kwa gharama ya Euro milioni 25, sawa na Shilingi bilioni 57.50 na Serikali itachangia Euro milioni 1.50, sawa na Shilingi bilioni 3.45. Uwekaji wa jiwe la msingi la mradi huo utafanyika tarehe 24 Mei, 2013, Dar es Salaam.

(ii) Mradi wa North - West Grid kV 400;

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kubadilisha msongo wa njia ya kusafirisha umeme kutoka kV 220 hadi kV 400 kwa mradi wa *North - West Grid* ambao utapitia maeneo ya Nyakanazi – Kigoma – Katavi – Rukwa hadi Mbeya ili kukidhi matarajio ya shughuli mbalimbali za kiuchumi katika maeneo hayo. Maombi ya mkopo yamewasilishwa katika Benki ya *Exim* ya China kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Mradi huu utakapokamilika utaimarisha mfumo na upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Mbeya, Rukwa na Shinyanga. Gharama za awamu ya kwanza inakadiriwa kufikia Dola za Marekani milioni 136.25, sawa na Shilingi bilioni 218.

(iii) Mradi wa Makambako – Songea kV 220;

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali ilikamilisha durusu ya kuongeza uwezo wa njia ya umeme *(upgrade)* ya Makambako hadi Songea kutoka msongo wa kV 132 kwenda kV 220 (usafirishaji – kilomita 250 na usambazaji – kilomita 900). Mshauri wa mradi ni Kampuni ya *SWECO International* kutoka Sweden. Vilevile, zabuni ya kupata Mkandarasi wa kusambaza umeme katika maeneo ya mradi imetangazwa na itafunguliwa mwishoni mwa Mwezi Mei, 2013. Utekelezaji wa mradi umepangwa kuanza Mwezi Agosti, 2013. Mradi huu utakapokamilika utawezesha Mkoa wa Ruvuma kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa na kuimarisha juhudi za usambazaji wa umeme katika Miji ya Makambako, Njombe na Songea na katika Wilaya za Ludewa, Mbinga na Namtumbo. *(Makofi)*

(iv) Mradi wa Iringa – Shinyanga kV 400 *(backbone);*

Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilomita 670. Kwa sasa, zabuni za Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa njia kuu na vituo vya kupozea umeme zinachambuliwa. Serikali kupitia *TANESCO* imeanza kulipa fidia katika maeneo ya mradi. Mradi huu ambao gharama yake ni Dola za Marekani milioni 650, sawa na Shilingi bilioni 1,040 utakapokamilika utaimarisha Gridi ya Taifa, kupunguza upotevu wa umeme na kuongeza uwezo wa kusafirisha umeme wa kutosheleza mahitaji ya Kanda ya Kaskazini Magharibi. Mradi huu pia utahusisha usambazaji wa umeme vijijini katika maeneo ya mradi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Mwaka 2015/2016.

(v) Kuimarisha Njia za Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme;

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANESCO* imeendelea kubuni miradi ya kuboresha usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini. Katika kutekeleza miradi hiyo, vifaa vya kisasa vya kulinda mifumo ya Gridi yaani *power system protection relays* vimenunuliwa na kufungwa katika vituo vya Iringa, Kidatu, Mufindi, Mwanza, Shinyanga na

Singida. Aidha, vifaa maalum vya kugundua hitilafu kwenye njia za umeme *(fault locators)* vimenunuliwa na kufungwa katika vituo vya Chalinze, Hale, Kidatu, Msamvu na Ubungo. Gharama za mradi huo ni Dola za Marekani 503,862 sawa na Shilingi milioni 806.18.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara limekuwa kati ya kero kubwa kwa watumiaji wa umeme nchini. Sababu za kuwepo kwa tatizo hili ni pamoja na uchakavu wa miundombinu ya usambazaji umeme na vifaa vyake; kuzidiwa uwezo kwa mifumo ya usambazaji umeme; na wizi wa nyaya za shaba na mafuta ya transfoma, hususan kwenye Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga.

Katika kukabiliana na matatizo hayo, Serikali imechukua hatua zifuatazo: kubadilisha nguzo zilizoharibika katika njia za umeme wa msongo wa kV 0.4 na ule wa kV 11 na 33; kukata miti katika njia za umeme wa msongo wa kV 11 na 33; kubadilisha vikombe *(insulators)* vilivyovunjika; na kubadilisha nyaya chakavu.

Mheshimiwa Spika, wizi na uharibifu wa miundombinu ya umeme nchini, kwa muda mrefu umekuwa tatizo sugu kutokana na wahusika kubuni njia mbalimbali za kufanya uharibifu huo na kusababishia *TANESCO* na nchi kwa ujumla hasara kubwa. Mathalani, kwa kipindi cha Julai, 2012 hadi Aprili, 2013 Shirika limepata hasara ya takriban Shilingi milioni 966.18, sawa na Dola za Marekani 603,862 kutokana na wizi na uharibifu wa miundombinu ya umeme katika Mikoa mbalimbali nchini. Ili kukabiliana na tatizo hili, Wizara kupitia *TANESCO* imefanya juhudi mbalimbali zikiwemo: kuweka transfoma karibu na maeneo ya makazi ili kuimarisha ulinzi; kutumia transfoma zisizohitaji mafuta; kutumia nyaya za aluminium badala ya shaba; na kuchukua hatua kali za kisheria kwa wale wote wanaothibitika kujihusisha na wizi na uharibufu wa miundombinu ya umeme.

Ndugu zangu Watanzania na Waheshimiwa Wabunge, nitoe wito kwa wananchi wote, umeme ni uchumi,

umeme ni maendeleo. Kwa hiyo, ni wajibu wetu na popote tulipo kulinda miundombinu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, Miradi chini ya Ufadhili wa *Millenium Challenge Corporation (MCC)* ya Marekani:-

(i) Mradi wa Kujenga Njia za Kusambaza Umeme;

Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa njia za msongo wa kV 33, kV 11 na kV 0.4 kwa ajili ya kusambaza umeme katika Mikoa ya Dodoma, Iringa, Manyara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Njombe na Tanga. Ujenzi wa njia za usambazaji za msongo wa kV 33 na kV 11 unaendelea na umefikia kiwango cha asilimia 80, ambapo kilomita 1,068 kati ya kilomita 1,335 zimekamilika. Aidha, ujenzi wa njia ndogo za usambazaji za msongo wa kV 0.4 unaendelea na umefikia kiwango cha asilimia 80, ambapo kilomita 1,094.4 kati ya kilomita 1,368 zimekamilika.

Sehemu ya miradi iliyokamilika kwa Mkoa wa Dodoma ilihusisha jumla ya vijiji 46 na ilizunduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 11 Aprili, 2013 katika Kijiji cha Mkoka, Wilayani Kongwa. Gharama za mradi zilizotumika kwa Mkoa huo ni Dola za Marekani milioni 17.80, sawa na Shilingi bilioni 28.5. Sehemu iliyobaki ya mradi huo imepangwa kukamilika mwezi Septemba, 2013. Aidha, ujenzi wa vituo 22 kati ya 24 vya kupozea umeme kV 33/0.4 na kV 11/0.4 unaendelea na utekelezaji wake umefikia asilimia 80. Mradi huu unahusu Mikoa ya Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Njombe na Tanga.

(ii) Ujenzi wa Njia ya Pili ya Umeme kutoka Dar es Salaam kwenda Unguja;

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea na ujenzi wa njia ya pili ya umeme ya kV 132 kutoka Ubungo hadi Ras-Kilomoni na utandazaji wa nyaya za umeme chini ya bahari kutoka Ras-Kilomoni hadi Mtoni – Unguja. Kazi ya kutandaza nyaya

za umeme chini ya bahari ilianza mwezi Julai, 2012 na ilikamilika na kuzinduliwa rasmi tarehe 10 Aprili, 2013 na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein - Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar. Gharama za mradi huo ni Dola za Marekani milioni 50, sawa na Shilingi bilioni 80. Hawa wanapata umeme wa jumla ya megawatt 100 na uwezo wao tunajua ni megawatt 50. Kwa hiyo, tunaomba Zanzibar wawe na viwanda zaidi vya kutumia. Wana umeme wa ziada.

Mheshimiwa Spika, baada ya nchi yetu kukamilisha Awamu ya kwanza ya miradi ya *MCC* ya Marekani kwa ufanisi mkubwa, naomba kulitaarifu Bunge 19 lako Tukufu kuwa Tanzania imechaguliwa tena kuendelea kupata ufadhili kutoka *MCC* katika Awamu ya Pili ambayo itaanza mwaka 2013/2014. Tusijidharau, tunatambulika kwa kufanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, *MCC* inaendelea na uchambuzi wa kina wa miradi itakayofadhiliwa ili kujua kiasi halisi cha fedha kitakachotolewa. Maeneo ya kipaumbele katika awamu hiyo ni pamoja na upelekaji wa nishati jadidifu katika shule, zahanati, na vituo vya afya vijijini; ujenzi wa Kituo cha Malagarasi chenye uwezo wa kufua umeme wa MW 42; na ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kV 132 kati ya Morogoro na Mtibwa.

Mheshimiwa Spika, lingine linahusu Mradi wa kufua umeme Malagarasi MW 42. Moja ya miradi ambayo Serikali iliamua kutekeleza kwa makusudi ili kuondoa kero ya umeme Mkoani Kigoma na Mikoa jirani ni Mradi wa kuzalisha umeme wa Malagarasi. Lengo lilikuwa ni kujenga Kituo cha kufua umeme kwa kutumia nguvu za maji chenye uwezo wa kufua MW 8 *(Stage II)* katika maporomoko ya Igamba kwenye Mto Malagarasi, Mkoani Kigoma na kujenga njia ya umeme ya msongo wa kV 33 kwenda Wilaya za Kasulu, Kigoma na Uvinza.

Mradi huu ni mojawapo ya miradi mikubwa mitatu ya nishati inayofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika la Mfuko wa Changamoto za Milenia *(MCC).*

Mheshimiwa Spika, Maporomoko ya Mto Malagarasi yana maeneo makuu matatu *(potential sites)* ambayo yanaweza kutumika kufua umeme. Maeneo hayo ni Malagarasi *Stage I,* Malagarasi *Stage II* (ambayo ndiyo yenye maporomoko ya Igamba) na Malagarasi *Stage III.*

Hata hivyo, taarifa ya utafiti ya mwaka 2004 ilionesha kuwa kuna konokono na samaki adimu *(rare species)* katika vidimbwi vya maporomoko ya Igamba *(Stage II).* Taarifa hiyo ilitumiwa katika taarifa ya utafiti wa mazingira ya awali *(Preliminary EIA Study)* ilifanywa na Kampuni ya *Norplan* ambayo ilipewa kazi hiyo na *TANESCO* Mwaka 2008. Taarifa hiyo iliwasilishwa *MCC* kama sehemu ya mahitaji ya *MCC* kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Kutokana na taarifa hiyo, Mwezi Agosti, 2009 *MCC* ilituma jopo la Wataalam ili kuthibitisha taarifa za kuwepo viumbe hao adimu kabla ya kuanza kazi ya ujenzi wa mitambo ya kufua umeme.

Taarifa ya jopo la Wataalam toka *MCC* ilithibitisha kuwepo kwa konokono na samaki adimu. Kutokana na taarifa hiyo na kwa kuzingatia kanuni za mazingira za kimataifa, mwezi Novemba, 2009 *MCC* ilisitisha utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mradi huu ni kati ya miradi muhimu iliyokuwa, imeainishwa katika utekelezaji wa *Compact - I, MCC* iliona umuhimu wa kuendelea kuufadhili mradi huu na hivyo kukubali kufanya upembuzi yakinifu mpya katika eneo lingine kwenye Mto Malagarasi *Stage III.* Mbali na kufadhili upembuzi yakinifu katika Malagarasi *Stage III,* miradi mingine ambayo ilikubaliwa na *MCC* kutekelezwa katika Mkoa wa Kigoma ni pamoja na mradi wa ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya kusambazia umeme katika mji mzima wa Kigoma na maeneo yaliyoko jirani na mradi wa umeme utokanao na jua kwa vijiji vya Kasulu, Kigoma na Uvinza.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *ESB International* ya *Ireland* ambayo ni Mshauri na msimamizi wa ujenzi wa miradi ya nishati inayofadhiliwa na *MCC* ilipewa jukumu pia la kufanya uchunguzi upya wa athari za mazingira na jamii na

upembuzi yakinifu wa mradi katika Malagarasi *Stage III*. Katika kutekeleza mradi wa umeme wa Mto Malagarasi, Mshauri vilevile alipewa jukumu la kutayarisha nyaraka za zabuni *(Technical Tender Documents).* Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kazi hizi zilikamilika mwezi Desemba, 2012 na taarifa ya kazi hii inaonesha kuwa, maporomoko hayo yana uwezo wa kuzalisha umeme wa MW 42.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli kwamba muda wa utekelezaji wa miradi ya awamu ya kwanza ya ufadhili wa *MCC (Compact I)* umekwisha na mradi huu hautaweza kutekelezwa, *MCC* imeridhia kuwa mradi wa ufuaji umeme wa MW 42 utekelezwe katika awamu ya pili ya ufadhili wa *MCC (Compact - II).*

Mheshimiwa Spika, Miradi chini ya Ufadhili wa *JICA*, Japan. Serikali kupitia *TANESCO* imekamilisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 66 kutoka Kiyungi hadi Makuyuni Mkoani Kilimanjaro chini ya ufadhili wa Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la *JICA*. Mradi huo umegharimu Dola za Marekani milioni 26.20, sawa na Shilingi bilioni 41.92 na umekamilika Mwezi Februari, 2013. Kazi nyingine zilizofanyika chini ya mradi huu ni ujenzi wa vituo vya kupozea umeme vyenye uwezo wa *MVA 20* katika eneo la *KCMC*, Kiyungi, Lawate na *YMCA* Mkoani Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye upelekaji wa umeme Makao Makuu ya Wilaya na Maeneo ya Vijijini. Serikali kupitia *REA* imeendelea kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya na maeneo ya vijijini. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, upelekaji umeme Makao Makuu ya Wilaya za Namtumbo na Nkasi umekamilika, na uzinduzi utafanywa mwezi Julai, 2013.

Waheshimiwa Wabunge, nawaomba, nimewaagiza Manaibu Waziri mwezi wa Saba, wa Nane na kuendelea wakazindue miradi yote ya umeme vijijini ambayo imekamilishwa. Hii ni muhimu sana kwa sababu kuna watu hawakuchangia senti hata moja, wanasema wao ndio wamekamilisha hiyo miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Namtumbo umegharimu Shilingi bilioni 3.87, sawa na Dola za Marekani milioni 2.42 na mradi wa Nkasi umegharimu Shilingi bilioni 5.58, sawa na Dola za Marekani milioni 3.49.

Aidha, Serikali kupitia *REA* imeendelea kuwezesha utekelezaji wa Mradi Kabambe wa Awamu ya Kwanza wa Kusambaza Umeme Vijijini katika Mikoa 16 ya Tanzania Bara. Gharama za mradi huo ni jumla ya Shilingi bilioni 129, sawa na Dola za Marekani milioni 80.62. Kati ya fedha hizo, takriban Shilingi bilioni 30.0 ni mchango kutoka Serikali ya Sweden. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwaka 2013/2014 badala ya Mwezi Desemba, 2012 kutokana na kuongezwa kwa maeneo mengine kwenye awamu ya kwanza ya mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upelekaji umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Nyang'hwale umefikia asilimia 77. Mradi huo ambao unafadhiliwa na *MCC* utagharimu Shilingi bilioni 4.59, sawa na Dola za Marekani milioni 2.87. Aidha, Mkandarasi wa kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya za Bukombe na Mbogwe ambaye ni Kampuni ya *ELTEL Networks TE AB* ya Sweden amepatikana. Kazi hiyo itaanza Mwezi Juni, 2013 na kukamilisha Mwezi Desemba, 2014. Kazi hii ni sehemu ya Mradi wa *Electricity V.*

Mheshimiwa Spika, tathmini ya zabuni za kuwapata wakandarasi wa kutekeleza Awamu ya Pili ya Mpango Kabambe wa Usambazaji Umeme Vijijini chini ya *REA* itakamilika mwishoni mwa Mwezi Mei, 2013. Gharama za utekelezaji wa mradi wa Awamu ya Pili ya Mpango huo zinakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 881, sawa na Dola za Marekani milioni 550. Aidha, Serikali ya Norway kupitia Shirika lake la Maendeleo *(NORAD)* itachangia Krona za Norway milioni 700, sawa na takriban Shilingi bilioni 192 katika Mfuko wa Nishati Vijijini. Mkataba wa upatikanaji wa fedha za Norway ulisainiwa tarehe 9 Aprili, 2013.

Chini ya mpango huo, umeme utapelekwa katika Makao Makuu ya Wilaya 13 ambazo hazina umeme kwa sasa

na baadhi ya maeneo ya vijijini. Wilaya hizo ni Buhigwe, Busega, Chemba, Itilima, Kakonko, Kalambo, Kyerwa, Mkalama, Mlele, Momba, Nanyumbu, Nyasa na Uvinza. Gharama za upelekaji wa umeme katika Wilaya hizo zinakadiriwa kugharimu Shilingi bilioni 70, sawa na Dola za Marekani milioni 43.75, na kiasi cha fedha kilichobaki cha Shilingi bilioni 122 kitatumika kupeleka umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012/2013, mradi wa kusambaza umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara ulitekelezwa katika maeneo ya Wilaya za Kilwa, Lindi, Masasi, Mtwara Mjini, Nachingwea, Newala, Ruangwa na Tandahimba. Mradi huo unafadhiliwa na Mfuko wa Nishati Vijijini kwa gharama ya Shilingi bilioni 5.0, sawa na Dola za Marekani milioni 3.13. Utekelezaji wa mradi upo katika hatua mbalimbali ambapo katika Mkoa wa Mtwara kilomita 24.78 kati ya 47.53 za njia za usambazaji umeme zimejengwa na transfoma saba kati ya 24 zimefungwa. Jumla ya wateja 277 wameunganishiwa umeme katika Mkoa wa Mtwara na kule Lindi ni 132.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Lindi, jumla ya kilomita 11.28 kati ya 28.20 za njia ya umeme ya msongo wa kV 33 na kV 11 zimejengwa. Aidha, ujenzi wa kilomita 59.5 kati ya 72.3 za njia ya umeme ya msongo wa kV 0.4 umekamilika na transfoma tano kati ya 25 zimefungwa. Jumla ya wateja 132 wameunganishiwa umeme. Aidha, wateja katika Mikoa ya Lindi na Mtwara wataendelea kunufaika kuunganishiwa umeme wa njia moja *(single phase)* hadi mwakani kwa gharama ya Sh. 99,000/= tu ikilinganishwa na Watanzania wengine wanaolipa kiasi cha Sh. 177,000/=, wanazotozwa wateja kwenye maeneo mengine ya vijijini nchini kupata huduma hiyo.

Ndugu zangu, naomba nirudie hapo. Viongozi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara, waliniletea hilo ombi, nikakaa chini na *REA* na *TANESCO* tukakubaliana kwamba watu wa Lindi na Mtwara waendelee kupata bei nafuu mpaka mwakani ya kuunganishiwa kwa Sh. 99,000/= peke yake, ukilinganisha na Watanzania wengine wanaolipa Sh. 177,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, punguzo hili lilikuwa liishe Mwezi Juni, 2013. Kwa kuzingatia usikivu wa Serikali ya CCM na baada ya kupokea maombi kutoka kwa Viongozi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara, Serikali imekubali punguzo hilo liendelee hadi tarehe 30 Juni, 2014. Tunawaomba wananchi wa Mtwara na Lindi wajitahidi kutumia fursa hii kuhakikisha wanaunganishiwa umeme kwa bei hii nafuu.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu mipango ya kupunguza gharama za kuunganisha umeme. Utakumbuka kuwa, katika Hotuba yangu ya mwaka 2012/2013, Serikali iliahidi kupunguza gharama za kuunganisha umeme katika maeneo ya vijijini na mijini ili kuweza kufikisha huduma hiyo kwa wananchi wengi zaidi. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ahadi hiyo imetekelezwa kuanzia mwezi Januari, 2013. Hadi sasa idadi ya Watanzania waliounganishiwa umeme imeongezeka kutoka asilimia 18.4 mwaka 2012 hadi asilimia 21 Aprili, 2013. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa asilimia 30 ya Watanzania wanaunganishiwa umeme ifikapo mwishoni mwa mwaka 2014/2015. Hii inawezekana, ikiwa kwa mwaka mmoja tumetoka asilimia 18.4 mpaka asilimia 21, lazima tutafika asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uendelezaji wa vyanzo vingine vya nishati; mwaka 2012/2013 makaa ya mawe yanayochimbwa Ngaka Wilayani Mbinga tayari yanauzwa nchi za nje, Malawi na Uganda, nasikia na nyingine wameomba kama Mauritius. Ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme wa awali wa Megawatt 200 umeanza na utakamilika mwaka 2016. Ujenzi wa njia za kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220 kutoka Ngaka hadi Songea ambapo ni karibu kilometa 100 ni sehemu ya mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia punguzo hilo la gharama za kuunganisha umeme, maombi yameongezeka na kufikia wastani wa maombi 15,673 kwa mwezi ikilinganishwa na maombi 11,718 kwa mwezi kabla ya punguzo. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 33.8. Kutokana na ongezeko hilo, changamoto kubwa imekuwa ni upatikanaji wa vifaa kama

nguzo na mita kwa wakati ili kukidhi mahitaji. Kati ya Mwezi Januari, 2013 hadi Machi, 2013, wateja 35,405 wameunganishiwa umeme. Ili kuhakikisha wateja wanaunganishiwa umeme kwa wakati, vifaa muhimu vya kuunganishia wateja umeme vilivyoagizwa na *TANESCO* kuanzia Mwezi Januari, 2013 ni kama ifuatavyo: nyaya zenye urefu wa kilomita 22,880, nguzo 133,800, mita 265,000 na transfoma 2,100.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi kuhusu uagizaji wa nguzo za umeme kutoka nje ya nchi, hususan Afrika Kusini, Uganda na Zambia. Hata hivyo, ukweli ni kwamba bei ya nguzo zinazozalishwa na Kampuni za Tanzania ni ghali ikilinganishwa na bei ya nguzo kutoka nchi nyingine. Mfano, bei ya nguzo hapa nchini pamoja na usafiri ni kati ya Sh. 224,000/= hadi Sh. 749,000/= wakati nguzo za Afrika Kusini ni kati ya Dola 138 hadi 420, sawa na kati ya Sh. 219,000/= hadi Sh. 672,000/=. Aidha, baadhi ya wasambazaji wa nguzo wa ndani wamekuwa wakifanya kazi kwa mazoea *(business as usual).* Niwasihi sana wabadilike ili wanapopata kazi, waheshimu mikataba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali imekamilisha utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na ujenzi wa miundombinu ya umeme katika Wilaya za Kilombero (Morogoro) na Mbozi (Mbeya). Kazi hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa Mfano wa Usambazaji Umeme kwa Gharama Nafuu *(Low Cost Design Standards).* Gharama za mradi huo unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia *"Sida Trust Fund"* zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 10, sawa Shilingi bilioni 16, ambapo takriban wateja 20,000 wataunganishiwa umeme. Utekelezaji wa mradi huu unategemewa kupunguza gharama za usambazaji umeme katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa niongee kuhusu Sekta Ndogo ya Nishati Jadidifu *(Renewable Energies),* kuhusu uendelezaji wa umeme wa jua; mwaka 2012/2013, ufungaji wa mifumo ya umeme wa jua katika Shule za Sekondari na Zahanati

uliendelea ambapo mifumo zaidi ya 150 ilifungwa katika Wilaya za Iramba, Kasulu, Kibondo, Mkuranga, Mpanda, Muleba, Nyang'wale, Nzega, Rufiji na Sumbawanga. Sehemu ya Mradi huo *(off grid component)* unagharimiwa na Serikali kwa jumla ya Shilingi bilioni mbili, sawa na Dola za Marekani milioni 1.25 pamoja na ufadhili wa Benki ya Dunia chini ya Mradi wa Tanzania *Energy Development and Access Expansion Project (TEDAP)* kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 22.5, sawa na Shilingi bilioni 36. Mradi huo utakamilika Mwaka 2014/2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine wa umeme wa jua umeanza kutekelezwa na Kampuni ya Solawazi katika Wilaya ya Kigoma. Mradi huo utakaogharimu Dola za Marekani milioni 12, sawa na Shilingi bilioni 19.20 kwa kuanzia utawezesha kufua umeme wa MW 3 utakaoingizwa kwenye Gridi ya Taifa. Kampuni hiyo imeingia Mkataba wa kuuziana umeme na *TANESCO* Mwezi Januari, 2013 chini ya utaratibu wa Mikataba Maalum *(Standardized Small Power Purchase Agreement and Tariff – SSPA/T).*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uendelezaji wa vyanzo vya nishati ya upepo, mwaka 2012/2013, Kampuni ya *Geo-Wind Power (T) Ltd* kupitia Wizara ya Fedha imepeleka maombi ya mkopo Benki ya *Exim* ya China.

Mradi huo unamilikiwa kwa ubia kati ya *Power Pool East Africa Ltd*, *TANESCO* na *NDC*. Mgawanyo wa hisa utajulikana baada ya majadiliano kukamilika mwezi Julai, 2013. Gharama za mradi wenye uwezo wa kufua MW 50 ni Dola za Marekani milioni 136, sawa na Shilingi bilioni 217.60.

Aidha, *TANESCO* imekamilisha taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri *(Technical Advisor)* kwa ajili ya mradi wa kufua MW 100 unaotekelezwa na Kampuni ya *Wind East Africa Limited* kwa gharama za Dola za 29 Marekani milioni 285, sawa na Shilingi bilioni 456. Kampuni hiyo inamilikiwa na *M/S Six Telecoms* (asilimia 40), *M/S Aldwych* (asilimia 40), na *M/S IFC* (asilimia 20). Kampuni hizo zimepatiwa leseni za muda *(provisional licence)* na *EWURA* kwa ajili ya kutekeleza miradi

hiyo. Miradi hiyo miwili itatekelezwa katika eneo la Kititimo, Mkoani Singida.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uendelezaji wa umeme utokanao na maporomoko madogo ya maji; katika jitihada za Serikali kuwezesha sekta binafsi, mradi wa kuzalisha umeme kutokana na maporomoko madogo ya maji ya Mwenga, Mkoani Iringa wa MW 4 umewezeshwa kwa kupatiwa ruzuku ya Dola za Marekani 500, sawa na Sh. 800,000/= kwa kila kaya itakayounganishiwa umeme. Hadi Mwezi Aprili, 2013, jumla ya wateja 465 waliunganishiwa umeme kati ya wateja 2,600 wanaotarajiwa kuunganishiwa. Hivyo kupata ruzuku ya Dola za Marekani 232,500 sawa na Shilingi milioni 372.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012/2013 uhamasishaji wa matumizi bora ya tungamotaka (mkaa wa kuni na biogas) ulifanyika, ambapo mtambo wenye uwezo wa kufua umeme wa kW 24 kwa kutumia biogas ulifungwa katika Kijiji cha Manyata, Wilaya ya Kongwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Kituo cha Uendelezaji wa Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini *(CAMARTEC)* iliendelea na utekelezaji wa Mradi wa *Biogas for Better Life African Initiatives* chini ya mpango ujulikanao kama Tanzania *Domestic Biogas Program*, kwa ajili ya kujenga mitambo ya *biogas* kwa ngazi ya kaya kupitia ufadhili wa *HIVOS* ya Uholanzi. Kwa kipindi cha Mwezi Januari, 2012 mpaka Desemba, 2012 mitambo 2,409 ilijengwa katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Njombe, Pwani, Ruvuma, Shinyanga na Singida. Mitambo mingine 12 imejengwa Zanzibar. Lengo la mradi huu ni kujenga mitambo 12,000 nchini ifikapo Desemba, 2014. Vilevile, kupitia *REA*, mitambo mingine ya *biogas* inajengwa Masasi (Gereza la Namajani) na Songea Vijijini (Kambi ya JKT Mlale).

Mheshimiwa Spika, sambamba na uendelezaji wa *biogas*, mafunzo kwa ajili kuwajengea uwezo Watanzania katika matumizi ya teknolojia hiyo yalitolewa katika maeneo ya Bukombe, Kasulu na Songea. Jumla ya Watanzania

walionufaika na mafunzo hayo katika mwaka 2012/2013 ni 2,400.

Mheshimiwa Spika, mwezi Januari, 2013 *NDC* kwa kushirikiana na Kampuni za "*Geothermal Power Tanzania Limited"* na *"Interstate Mining 31 Company"* za Tanzania zilianza kuchoronga visima vifupi na virefu vya utafiti katika maeneo ya Mbaka na Ziwa Ngozi – Mbeya kwa ajili ya uhakiki wa uwezo wa kufua umeme kutokana na jotoardhi. Serikali pia, kwa kushirikiana na Taasisi ya Jiolojia ya Ujerumani *(BGR)* imeainisha maeneo katika vijiji vya Uyole na Wasanga Mkoa wa Mbeya kwa ajili ya kuchoronga visima vifupi vitatu vyenye kina cha mita 400 kila kimoja. Taarifa za tafiti hizo zitawezesha nchi kuangalia uwezekano wa kufua umeme kutokana na jotoardhi.

Mheshimiwa Spika, gharama za kuchoronga kisima kimoja ni kati ya Dola za Marekani 400,000, sawa na Shilingi milioni 640 hadi Dola za Marekani milioni 1, sawa na Shilingi bilioni 1.6.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maboresho ya gesi asilia, hapa nawaomba Waheshimiwa Wabunge, Wizara tunajitahidi, lakini nawaombeni kwa kuwa ninyi ni Wajumbe wa Halmashauri, tumieni *REA* kuogeza kasi ya Shule na Zahanati kupata umeme. Shule yenye vyumba vinane vinahitaji Shilingi milioni nne peke yake kupata umeme. Kwa nini Halmashauri hii isiwe ni sehemu ya miradi yao? Hasa wakipunguza zile safari, watapata hela hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wilaya 10 zilibainishwa kwa ajili ya kutekeleza mradi wa mfano wa matumizi bora ya nishati chini ya Mradi wa *Low Carbon Energy Efficiency & Climate Change Mitigation.* Wilaya hizo ni Geita, Kasulu, Kahama, Kwimba, Mbinga, Mbulu, Misenyi, Mpanda, Ngorongoro na Urambo.

Lengo la mradi ni kuhamasisha matumizi endelevu ya nishati na kupunguza hewa ukaa *(carbon dioxide).* Mradi huu utagharimiwa na Serikali pamoja na Shirika la Maendeleo la

Umoja wa Mataifa *(UNDP).* Gharama za mradi ni Dola za Marekani milioni 16, sawa na Shilingi bilioni 25.60. 32.

Mheshimiwa Spika, miundombinu na gesi asilia iliyopo kwa sasa; uwezo wa mitambo ya kusafisha gesi asilia iliyopo ni futi za ujazo milioni 70 kwa siku *(mmscfd).* Hata hivyo, kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya gesi asilia, ililazimu kuongezwa *(re-rating)* kwa uwezo wa mitambo hiyo na kufikia futi za ujazo milioni 103. Ikumbukwe kuwa, gesi asilia hivi sasa inasafirishwa na bomba lenye urefu wa kilomita 225 na kipenyo cha inchi 16 kutoka Songo Songo hadi Dar es Salaam ambapo asilimia 80 ya gesi hiyo hutumika kufua umeme na kiasi kinachobaki cha asilimia 20 hutumika kwenye baadhi ya viwanda na Taasisi.

Mheshimiwa Spika, umeme unaozalishwa kwa kutumia gesi asilia unafikia wastani wa MW 330 ikilinganishwa na uwezo wa mitambo iliyopo yenye jumla ya MW 501. Uwezo huo haufikiwi kutokana na kutokuwepo kwa miundombinu ya kutosha ya kusafisha na kusafirisha gesi asilia. Ili kukidhi mahitaji ya umeme, Serikali imelazimika kutumia mafuta kufua umeme ambao ni ghali ikilinganishwa na vyanzo vingine. Mafuta hayo yanaigharimu Serikali takriban Shilingi bilioni tano kwa siku, sawa na Dola za Marekani bilioni moja kwa mwaka. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali inajenga miundombinu mipya ya kusafisha na kusafirisha gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa Bomba la Gesi Asilia kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam ulizinduliwa rasmi tarehe 8 Novemba, 2012 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Mradi huo unahusisha ujenzi wa bomba lenye urefu wa kilomita 532 na kipenyo cha inchi 36.

Pia, bomba hilo lina uwezo wa kusafirisha futi za ujazo za gesi asilia milioni 784 kwa siku. Mradi huo pia utahusisha mitambo miwili ya kusafisha gesi asilia katika maeneo ya *Mnazi Bay* - Madimba (Mtwara) na Kisiwa cha Songo Songo (Lindi). Mradi utagharimu Dola za Marekani milioni 1,225.3, sawa na Shilingi bilioni 1,960. Kazi za usanifu wa mradi na ulipaji

fidia kwa wananchi wapatao 3,092 waliopisha maeneo ya mradi zimekamilika. Aidha, hatua za awali za ujenzi wa mitambo ya kusafisha gesi asilia zimeanza katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Hadi sasa visima viwili vya maji vyenye uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 50 kwa saa kwa kila kimoja vimekamilika. Visima hivyo, ni kwa ajili ya mitambo ya kusafisha gesi asilia katika eneo la Madimba na kwa matumizi ya wananchi. Vifaa mbalimbali vya ujenzi wa 34 nyumba za wafanyakazi wa mradi vimewasili nchini mwishoni mwa Mwezi Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mradi wa kujenga bomba la gesi la Mtwara unaendelea na uko pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miundombinu hii utaleta manufaa makubwa kwa Taifa. Hadi sasa Mikoa ya Lindi na Mtwara imepata manufaa mbalimbali yatokanayo na miradi ya gesi asilia ikiwa ni pamoja na tozo ya asilimia 0.3 ya mauzo ya gesi asilia, huduma za jamii kama zahanati, shule, umeme, maji na ufadhili wa mafunzo katika Vyuo vya Ufundi *(VETA)* na Sekondari. Manufaa mengine yatakayopatikana ni pamoja na ujenzi wa viwanda mbalimbali vikiwemo kiwanda cha Saruji cha Kampuni ya Dangote ambacho ujenzi wake umeanza.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu anakwenda kuweka jiwe la msingi wiki ijayo. Kwa hiyo, haya siyo mambo ya kusadikika, ni ya kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha mbolea, mtambo wa kufua umeme wa MW 400 kupitia Kampuni ya *Symbion* pamoja na ujenzi wa njia ya usafirishaji umeme ya msongo wa kV 220 kutoka Mtwara hadi Songea umeikingiwa makubaliano. Aidha, Kampuni ya *Schlumberger* ya *Houston*, Marekani imejenga karakana kubwa Mtwara ambayo itakuwa inatengeneza vifaa vya uchimbaji, utafutaji na uendelezaji wa rasilimali za mafuta na gesi badala ya kupeleka nje ya nchi.

Waheshimiwa Wabunge, wakati machafuko yamefanyika *Schlumberger* alifuka safari, wafanyakazi wake wote wakaenda Nairobi. Wamerudi tena. Lakini sasa hii ndiyo inataka kuwa *hub. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taratibu za kupata umiliki wa maeneo ya ujenzi wa viwanda *(Industrial Park)* vyenye kutumia gesi asilia zinaendelea katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Ujenzi wa viwanda hivyo utaongeza fursa za ajira kwa Watanzania pamoja na mapato kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika usambazaji wa gesi asilia Jijini Dar es Salaam, ujenzi wa bomba la gesi asilia lenye kipenyo cha inch 12 na urefu wa kilomita 6.3 kutoka Ubungo hadi Mikocheni Jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kusambaza gesi asilia majumbani na viwandani umekamilika. Bomba hili linahudumia wateja wa viwanda waliokuwa wakipata gesi kwa njia ya gesi iliyoshindiliwa ya mitungi *(Compressed Natural Gas – CNG)* pamoja na nyumba 70 zilizopo eneo la Mikocheni. Mradi huu umegharimu Dola za Marekani milioni 3.13, sawa na Shilingi bilioni tano.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa miundombinu iliyopo sasa ya kuleta gesi asilia katika Jiji la Dar es Salaam haitoshelezi, uunganishwaji wa wateja wapya utaanza baada ya kukamilika kwa bomba la gesi asilia linalojengwa na Serikali kutoka Lindi na Mtwara hadi Dar es Salaam. Katika kuendeleza mradi huo, Serikali kupitia *TPDC* imemwajiri Mshauri atakayefanya kazi ya kusanifu michoro ya ujenzi ya mtandao wa kusambaza gesi asilia na vituo vya kujazia gesi hiyo kwenye magari katika Jiji la Dar es Salaam. Vilevile, Mshauri huyo atasimamia upatikanaji wa Mkandarasi atakayejenga mtandao huo. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 80, sawa na Dola za Marekani milioni 50.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Kampuni za utafutaji mafuta ziliendelea kutekeleza mipango kazi kama ilivyoainishwa kwenye mikataba yao. Katika kipindi hicho, Kampuni za *BG/Ophir na Statoil/ExxonMobil* zilifanikiwa kuchoronga visima vinne (Zafarani – 2, Lavani – 2, Tangawizi

na *Jodari North)* kwenye kina kirefu cha maji baharini ili kutathmini kiasi cha gesi asilia kilichopo. Jumla ya futi za ujazo takriban trilioni 18.8 za gezi asilia ziligunduliwa katika visiwa hivyo. Kisima cha Tangawizi kimegundulika kuwa na kiasi cha futi za ujazo kati ya trilioni nne hadi sita wakati kisima cha Jodari kimegundulika kuwa na futi za ujazo trilioni 4.1 badala ya futi za ujazo trilioni 3.4 zilizotangazwa awali. Aidha, kisima cha Zafarani – 2 kimegundulika kuwa na futi za ujazo trilioni sita, wakati kisima cha Lavarani – 2 kimegundulika kuwa na futi za ujazo trilioni 4.7. Hadi sasa kiasi cha gesi asilia kilichogundulika nchini ni takriban futi za ujazo trilioni 41.7 sawa na mapipa ya mafuta bilioni 7.98. Tunawazidi Waganda, mafuta yao ni bilioni nne tu. Sisi tuna karibu bilioni hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie kuhusu upitiaji wa mikataba ya utafutaji na ugawaji wa mapato. Kazi ya kudurusu mikataba ya utafutaji na ugawanaji wa mapato *(Production Sharing Agreements – PSAs)* ilikamilika mwishoni mwa mwezi Novemba, 2012. Kukamilika kwa kazi hiyo kumeiwezesha Serikali kubaini maeneo yanayohitaji kuboreshwa katika mikataba hiyo. Pia, matokeo ya uchambuzi wa mikataba hiyo yatasaidia katika uandaaji wa sera, sheria na kanuni za usimamizi wa sekta ndogo za mafuta na gesi asilia itakayokidhi matakwa ya Watanzania. 37

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *EWURA* iliendelea kusimamia usambazaji wa mafuta ili kuhakikisha kuwa yanapatikana wakati wote na maeneo yote nchini. Hadi mwezi Aprili, 2013 kulikuwa na wafanyabiashara wakubwa *(wholesalers)* 88 na wafanyabiashara wa rejareja 867.

Katika mwaka 2012/2013 hadi kufikia Aprili, 2013, kiasi cha lita za ujazo bilioni 2.30 za nishati ya mafuta ziliingizwa nchini kwa ajili ya soko la ndani yenye thamani ya takriban Dola za Marekani bilioni 1.68, sawa na Shilingi bilioni 2,688. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la lita milioni 303.41, sawa na asilimia 13.20 ikilinganishwa na mafuta yote yaliyoagizwa Mwaka 2011/2012. Kati ya kiasi hicho cha mafuta, lita 1,405,711,203 zilikuwa dizeli, sawa na asilimia 61 ya mafuta yote yaliyoingizwa nchini; petroli lita 562,368,954, sawa na

asilimia 24; na mafuta ya taa lita 230,708,012, sawa na asilimia 10. Bidhaa nyinginezo za mafuta ilikuwa ni asilimia tano ya mafuta yote. Aidha, katika kipindi hicho, lita za ujazo bilioni 1.36 za mafuta yaliagizwa na nchi jirani kupitia Bandari ya Dar es Salaam. Hii ni sawa na asilimia 37.16 ya mafuta yote yaliyoagizwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja Serikali ilikamilisha kudurusu kanuni za uagizaji wa mafuta kwa pamoja yaani *PIC*. Uagizaji wa mafuta kwa pamoja umeendelea kufanyika chini ya Kampuni ya uratibu wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja *(Petroleum Importation Coordinator - PIC).* Aidha, Mwezi Novemba, 2012, Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania *(TPA)* ilizindua boya jipya la kupakulia mafuta, *Single Point Mooring (SPM).* Kuzinduliwa kwa boya hilo kumeongeza uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam wa kupokea meli za mafuta ya dizeli kutoka uzito wa tani 36,000 hadi tani 95,000 kwa wakati mmoja, sawa na ongezeko la asilimia 163.9

Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba, 2012 Kampuni ya *Addax Energy SA* ya Uswisi iliyoshinda zabuni ya kuagiza mafuta kwa pamoja. Iliagiza mafuta kiasi cha tani laki moja za dizeli. Hata hivyo, mafuta hayo yaligundulika kuwa chini ya viwango vinavyotakiwa kwa nchini mwetu, Tanzania. Mafuta hayo yalikuwa na thamani ya takribani Dola za Marekani milioni 96.7, sawa na Shilingi bilioni 154.72. Serikali kupitia Shirika la Viwango la Tanzania *(TBS)* na Kampuni ya Uagizaji Mafuta kwa Pamoja *(PIC)* ilifanikiwa kuzuia mafuta hayo kuingia nchini. Kufuatia tukio hilo, Kampuni hiyo ililipa faini ya takribani Dola za Marekani milioni 1.24, sawa na Shilingi bilioni 1.98 na kufungiwa kushiriki katika shughuli za uagizaji mafuta nchini kwa kipindi cha miezi minne. Naamini hatua hii itakuwa ni fundisho kwa Kampuni yoyote isiyofuata taratibu na inayofikiria kuleta mafuta yasiyokidhi viwango nchini mwetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Tanzania siyo *damp* la mafuta machafu wala siyo *damp* la mafuta yasiyo na viwango. Nawahakikishia Wizara yangu imesimamia hili

jambo kwa umakini na kwa uhakika kweli kweli. Sisi ndiyo tunafukuza hizo meli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kuanza kutafuta mbia kwa ajili ya uanzishwaji wa Hifadhi ya Mafuta ya Taifa *(National Strategic Petroleum Reserve),* kampuni nyingi za nje na ndani ya nchi 39 zilionesha nia ya kushiriki. Ili kupata mshiriki kwa njia ya ushindani na atakayeleta tija kwa Taifa, Serikali ilitangaza zabuni mwezi Machi, 2013 ambapo Kampuni 23 zilijitokeza kuomba kushirikiana na *TPDC*.

Pamoja na Kampuni hizo kujitokeza, Kampuni zilizorudisha zabuni zilikuwa 10. Ufunguzi wa zabuni hii ulikuwa tarehe 29 Aprili, 2013 na Timu ya Uchambuzi inaendelea na kazi yake ili kupata Kampuni inayofaa kushirikiana na *TPDC*. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wakiwemo Wizara ya Fedha, *EWURA, PIC, TPDC* na *TRA* inaandaa kanuni za kusimamia mfumo huo kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *EWURA* imeendelea kudhibiti ubora wa mafuta nchini. Katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Machi, 2013, jumla ya vituo vya mafuta 146 kati ya vituo 900 vilivyopo nchini vimekaguliwa. Vituo 18 kati ya hivyo havikukidhi viwango vya ubora na vilichukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria. Hatua za kisheria zilizochukuliwa ni pamoja na kufungiwa kuendesha biashara hiyo kwa kipindi maalum na kutozwa faini.

Mheshimiwa Spika, *EWURA* pia imeendelea kupanga na kusimamia bei kikomo kwa bidhaa za mafuta kwa mujibu wa Sheria ya *EWURA* ya mwaka 2001 na Sheria ya Mafuta ya mwaka 2008. Kutokana na udhibiti huo, jumla ya vituo 20 vya mafuta vilitozwa faini kwa kukiuka Taratibu za Upangaji Bei *(Price Setting Rules, 2009).* Vituo 40 kati ya hivyo vilikuwa vikiuza mafuta zaidi ya bei kikomo na vituo vinne havikuwa na matangazo ya bei.

Mheshimiwa Spika, bei za mafuta katika Soko la Dunia kwa mwaka 2012 zilikuwa zikipanda na kushuka. Kiwango cha juu cha bei kilikuwa katika Mwezi Machi, 2012 ambapo

mafuta ya dizeli yaliuzwa kwa Dola za Marekani 1,010 kwa tani na mafuta ya taa na ndege yaliuzwa kwa Dola za Marekani 1,071 kwa tani.

Aidha, kiwango cha juu cha bei ya mafuta ya petroli kilikuwa Dola za Marekani 1,150 kwa tani katika Mwezi Aprili, 2012. Kwa wastani, katika mwaka 2012, bei za mafuta katika Soko la Dunia zilikuwa juu kwa asilimia 3.9 kwa mafuta ya petroli; asilimia 0.2 kwa mafuta ya dizeli na asilimia 2.7 kwa mafuta ya taa na mafuta ya ndege ikilinganishwa na bei za mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali kupitia Wizara imeendelea kushiriki katika shughuli za uendeshaji wa Kampuni za *"Puma Energy Limited"* ambapo Serikali ina hisa asilimia 50; *Tanzania - Zambia Pipeline Limited (TAZAMA)* ambapo Serikali pia ina hisa asilimia 30; na *Tanzania International Petroleum Reserve (TIPER)* ambapo ina hisa asilimia 50. Kampuni hizo zinaendelea kufanya vizuri kifedha na Serikali inategemea kupata gawio wakati wowote kazi za uhakiki wa hesabu za fedha zitakapokamilika Julai, 2013.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuandaa Sera na Mipango kwa ajili ya kusimamia Sekta ya Nishati; katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu imekamilisha Rasimu ya Sera ya Gesi Asilia.

Maandalizi ya Rasimu hiyo yalishirikisha wadau mbalimbali wakiwemo Wizara na Taasisi za Serikali; Waheshimiwa Wabunge kupitia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini; Kampuni za utafutaji wa mafuta na gesi asilia, Washirika wa Maendeleo, Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola, Wanataaluma wa Vyuo Vikuu nchini, *Community Based Organization (CBOs),* Mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGO's),* vyombo vya habari na wananchi katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kigoma, Lindi, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Pwani, Rukwa na Tanga. Rasimu ya Sera ya Gesi Asilia imewasilishwa katika ngazi husika za Serikali. Sambamba na Sera hiyo, Mkakati wa Utekelezaji wake *(Natural Gas Implementation Strategy)* uliandaliwa.

Kwa hiyo, ndugu zangu siyo kweli kwamba wananchi hawakuhusishwa, anayesema hivyo, hana uhakika huo. Aidha, durusu ya mipango kabambe ya kuendeleza Sekta ndogo ya Umeme ilikamilika mwezi Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Sekta ya Umeme *(PSMP)* ulipitiwa upya kwa kushirikisha wadau, hususan Wizara na Taasisi za Serikali, Washirika wa Maendeleo na Sekta Binafsi. Aidha, Kanuni za Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja - *The Petroleum (Bulk Procurement) Regulations,* 2013 ziliandaliwa na kutangazwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 59072013 la tarehe 15 Machi, 2013. 42.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza kazi zilizopangwa kwa mwaka 2012/2013, mafaniko yaliyopatikana katika Sekta ya Nishati ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya Watanzania waliunganishiwa umeme kutoka asilimia 18.4 (mwaka 2012) hadi asilimia 21 (Aprili, 2013) ambapo kwa upande wa vijijini idadi ya Watanzania waliounganishiwa umeme imefikia asilimia saba; kuzinduliwa na kuanza kutekelezwa kwa mradi wa ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka *Mnazi Bay* (Mtwara) na Songo Songo (Lindi) hadi Dar es Salaam; kukamilika kwa ulipaji fidia kwa wananchi waliopisha mkuza wa bomba la gesi; kukamilika kwa Mradi wa Ujenzi wa Bomba dogo la Gesi Asilia kutoka Ubungo hadi Mikocheni Jijini Dar es Salaam; kukamilika kwa Rasimu ya Sera ya Gesi Asilia; na kuondoa makali ya upungufu wa umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine katika Sekta ya Nishati ni yafuatayo: kutekelezwa kwa ahadi ya kupunguza gharama za kuunganisha umeme kwa wateja; kukamilika kwa Mradi wa Mwenga MW 4 (Iringa) wa ufuaji umeme kutokana na maporomoko madogo ya maji; kukamilika kwa upelekaji umeme katika Makao Makuu ya Wilaya za Namtumbo na Nkasi; kupatiwa mafunzo kwa wajasiriamali 178 kuhusu nishati jadidifu; kukamilika kwa ufungaji wa mifumo ya umeme wa jua katika maeneo mbalimbali nchini; na kukamilika kwa shindano la *Lighting Rural Tanzania 2012*

ambapo jumla ya Shilingi bilioni 2.17, sawa na Dola za Marekani milioni 1.36 zilitolewa kwa miradi 15 iliyoshinda katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kigoma, Manyara, Morogoro, Mtwara, Njombe, Pwani na Shinyanga ambapo miradi saba ipo katika Mkoa wa Dar es Salaam na mradi mmoja mmoja kwa kila Mkoa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Wizara katika Mwaka 2012/2013 imekabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo kudhibiti upotevu wa umeme; kuwa na mbadala wa kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia majumbani; kufikisha umeme vijijini; kukidhi ongezeko la mahitaji ya nishati nchini, hususan umeme; kuongeza wigo wa rasilimali au vyanzo vya kuzalisha umeme; kukidhi matarajio ya wananchi kuhusu manufaa yatokanayo na gesi asilia; kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Nishati; mabadiliko ya hali ya hewa ambayo yameathiri ufuaji wa umeme kutokana na maji; na uzalishaji wa umeme wa uhakika na wa kutosheleza ambao kwa kiasi kikubwa umetegemea zaidi mafuta mazito na dizeli ambayo ni ghali.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kuwa mnamo mwezi Desemba, 2012 kulifanyika maandamano ya wananchi wa Mtwara wakitaka kujua faida ya kugunduliwa gesi asilia katika Mikoa ya Kusini; ambayo tumeieleza na viongozi wao tumewapeleka mpaka nje ya nchi wakajifunze. Kama hawajaelewa, nimetoa tena kakijitabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utashi wa wananchi ndiyo wa Serikali. Kama nilivyoelezea kwenye hotuba yangu, manufaa yatokanayo na uvunaji wa gesi asilia ni mengi. Hivyo, Serikali makini na sikivu imesikia, imeelewa na sasa inaendelea kutoa elimu kwa wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara na kwa Watanzania kwa ujumla wetu kuhusu manufaa hayo ya gesi asilia. Hata hivyo, ni muhimu ikaeleweka kuwa maandamano ya aina hiyo yanarudisha nyuma utekelezaji wa mipango ya Serikali inayolenga kuleta maendeleo ya kiuchumi kwa wananchi wote na Taifa letu kwa ujumla kwa kutumia raslimali ya gesi asilia ambayo ni mali halali ya Watanzania wote bila ubaguzi wa aina yoyote. Hivyo, yakiendelea yanaweza

kuwafukuza wawekezaji kwa kuhofia maisha yao, mali zao na mitaji yao. Umeme wa uhakika ni uchumi wa uhakika. Ndugu zetu wa Mtwara wasizuie ndugu zao wa Tanzania kupata umeme wa uhakika kwa uchumi wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mchango wa Sekta ya Madini kwenye pato la Taifa; katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kutekeleza mipango mbalimbali ya kukuza shughuli za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini nchini. Pia, Wizara iliimarisha usimamizi wa Sekta ya Madini ili kuongeza mchango wake kwenye pato la Taifa. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi za uchimbaji madini kilifikia asilimia 7.8 katika mwaka 2012 ikilinganishwa na asilimia 2.2 mwaka 2011. Aidha, mchango katika pato la Taifa ulifikia asilimia 3.5 ikilinganishwa na asilimia 3.3 kwa mwaka 2011 kwa bei ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi iliongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 1.98, sawa na Shilingi bilioni 3,168.32 mwaka 2011 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 2.30, sawa na Shilingi bilioni 3,684.05 mwaka 2012. Ongezeko hili la asilimia 16.3, lilitokana na kupanda kwa bei ya dhahabu katika Soko la Dunia kutoka wastani wa Dola za Marekani 1,571.28 kwa wakia mwaka 2011 hadi kufikia wastani wa Dola za Marekani 1,668.63 kwa wakia mwaka 2012. Thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi imeendelea kuchangiwa kwa kiwango kikubwa na madini ya dhahabu ambapo mchango wake kwa mwaka 2012 ni takriban asilimia 94.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, maeneo yaliyopewa kipaumbele katika Sekta ya Madini ni kuboresha utoaji na usimamizi wa leseni za madini; kuendeleza uchimbaji mdogo wa madini; kuhamasisha uongezaji thamani madini; kuimarisha soko la madini ya vito; kuimarisha usalama, afya na utunzaji wa mazingira migodini; kukamilisha maandalizi ya kudurusu Sheria ya Baruti; kuwezesha utekelezaji wa shughuli za *Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative (TEITI);* kuongeza fungamanisho la Sekta ya Madini na sekta nyingine za uchumi; ujenzi na uboreshaji wa ofisi za

madini; na kuziwezesha Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za kuboresha utoaji na usimamizi wa leseni, Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini uliendelea kuimarishwa ikiwa ni pamoja na kuunganisha ofisi za madini za Kanda zilizoko Mikoani katika Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa. Maboresho ya mfumo huo yamewezesha leseni 4,996 kutolewa na maombi 21,390 kukataliwa katika kipindi cha Julai, 2012 hadi mwishoni mwa Mwezi Aprili, 2013, na hivyo kufanya maombi yaliyoshughulikiwa kufikia 26,386.

Aidha, maombi ya zamani yaliyokuwepo *(backlogs)* ilipofika tarehe 01 Julai, 2012 yalikuwa ni 28,333 na maombi mapya yaliyopokelewa hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2013 ni 9,889 na hivyo kufanya maombi yaliyobaki kufikia 11,836 ikilinganishwa na maombi 28,333 yaliyokuwepo mwisho wa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiweka juhudi za kutoa leseni kwa wachimbaji wadogo ambapo hadi sasa kuna jumla ya leseni hai za wachimbaji wadogo 17,040. Hata hivyo, leseni 8,570 zinazomilikiwa na wachimbaji hao hazijalipiwa ada ya mwaka ya jumla ya Shilingi bilioni 2.66 tangu mwaka 2010 hadi 2012. Kwa ujumla deni la ada za mwaka wanalodaiwa wachimbaji wadogo limefikia Shilingi bilioni 4.17 hadi kufikia Aprili, 2013.

Aidha, mrabaha uliolipwa na wachimbaji wadogo katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2010 hadi 2012 ni Shilingi bilioni 2.11, kiwango ambacho ni kidogo sana kwa kuwa wengi wao hawawasilishi takwimu na wanaowasilisha hawaoneshi takwimu sahihi kwa nia ya kukwepa kulipa mrabaha na kodi nyingine za Serikali. Nitoe agizo kwa wachimbaji wadogo wote kuhakikisha kwamba wanalipa madeni ya ada ya mwaka ya leseni zao na wanawasilisha taarifa sahihi za uzalishaji na mauzo ya madini kwa ajili ya malipo ya mrabaha. Watakaoshindwa kutekeleza agizo hili, Wizara yangu haitasita kufuta leseni zao.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoahidi katika hotuba yangu ya mwaka 2012/2013, kwamba tutafuta leseni za madini ambazo zimekuwa hazifanyiwi kazi kwa muda mrefu, nachukua fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba hadi mwezi Aprili, 2013 jumla ya leseni 160 za utafutaji, moja ya uchimbaji wa kati na 268 za uchimbaji mdogo zimefutwa. Maeneo ya leseni hizo yatatolewa kwa waombaji wapya, hususan wachimbaji wadogo kwa mujibu wa Sheria. Zoezi hili ni endelevu ili kuhakikisha kuwa leseni zote zinafanyiwa kazi kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa kuna usalama wa nyaraka muhimu za leseni za madini, Mfumo wa *Data Recovery System (back up)* ulianzishwa. Mfumo huu utatumika endapo patatokea hitilafu katika mfumo mama *(main system)* uliopo Makao Makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza uchimbaji mdogo wa madini kwa Mwaka 2012/2013, Wizara yangu iliahidi kutenga jumla ya maeneo 10 yenye ukubwa wa hekta 105,163 kwa ajili ya uchimbaji mdogo.

Maeneo yaliyotengwa rasmi hadi sasa ni 16 yenye jumla ya hekta 265,396, ikiwa ni asilimia 160 ya lengo, zinazoweza kutolewa leseni takribani 26,539 za uchimbaji mdogo zenye ukubwa wa hekta 10 kila moja. Maeneo hayo na Wilaya husika ni Kakonko (Nyamwironge – Nyamtukuza); Kibaha (Kwamfipa na Viziwaziwa); Misungwi (Mihama); Mkuranga (Langweni - Mwanadilatu na Vianzi - Mindevu); Morogoro (Dete – Mwalazi); Mpwapwa (Winza); Mvomero (Melela); Same (Makanya); Simanjiro (Mwajanga); Singida (Mpambaa); Tarime (Nyakunguru na Nyamwaga); Tunduru (Mbesa); na Uvinza (Ilagala). Tunawajali wachimbaji wadogo. Leseni za uchimbaji mdogo zinaendelea kutolewa kwenye maeneo hayo kwa mujibu wa Sheria.

Aidha, taratibu za kisheria zinatarajia kukamilishwa kabla ya Julai, 2013 za kuwezesha kutengwa maeneo mengine ya Ibaga (Mkalama), Isenyela (Chunya), Kapalamsenga (Mpanda) na Songwe (Mbeya Vijijini).

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012/2013, Serikali ilitenga jumla ya Shilingi bilioni 8.9 kwa ajili ya kutoa mikopo ya kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata vifaa na mitaji kwa ajili ya kufanya kazi zao kwa ufanisi. Ili kuhakikisha mikopo hiyo inanufaisha walengwa na inarejeshwa kwa wakati na wakopaji, Wizara iliamua kutoa mikopo hiyo kupitia mfumo wa kibenki. Hivyo, zabuni ya kupata benki itakayosimamia kazi hiyo ilitangazwa Mwezi Februari, 2013 na mshindi amepatikana ambaye ni Benki ya *TIB*. Taratibu za kuhamisha fedha hizo na utoaji wa mikopo zitakamilishwa kabla ya Julai, 2013.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kuwaendeleza wachimbaji wadogo limekabidhiwa kwa *STAMICO*. Katika kutekeleza jukumu hili, Mpango Kazi na Programu ya Mafunzo kwa wachimbaji wadogo iliandaliwa na kuanza kutekelezwa ambapo mafunzo katika baadhi ya maeneo nchini yalitolewa. Mafunzo hayo yalishirikisha Wakufunzi kutoka Wizara ya Nishati na Madini; Wakala wa Jiolojia; Wakala wa Ukaguzi wa Madini; *SIDO*; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; na Chuo cha Madini Dodoma. Jumla ya washiriki 797 walihudhuria mafunzo yaliyoendeshwa katika maeneo ya Geita (Geita na Rwamgasa), Kigoma (Ilagala), Lindi (Ruangwa), Shinyanga (Shinyanga Mjini na Kahama) na Singida (Londoni).

Pia, mafunzo hayo yalishirikisha Viongozi wa Serikali na watoa huduma katika maeneo ya uchimbaji. Mafunzo hayo yalilenga kutoa elimu ya nadharia na kwa vitendo juu ya utafutaji wa madini, uchimbaji, uchenjuaji, elimu ya biashara, ujasiriamali na utunzaji wa mazingira pamoja na masuala mtambuka.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendesha Mkutano wa Pili wa Kitaifa tarehe 6 hadi 7 Desemba, 2012 hapa Dodoma. Mkutano huo ulishirikisha Wawakilishi wa wachimbaji wadogo kutoka Mikoa yote nchini na ulilenga kusikiliza changamoto zinazowakabili wachimbaji wadogo nchini na kuweka mikakati ya kuitatua, pamoja na kuimarisha Vyama vyao vya Kimkoa *(REMAs)* na kitaifa. Jumla ya wachimbaji wadogo 185

waliowawakilisha wenzao kutoka katika Mikoa yote ya Tanzania Bara walihudhuria. Kupitia maazimio ya Mkutano huo, *REMAs* zimeundwa katika Mikoa yote, vyama vya Mikoa vimeundwa nchi nzima; Viongozi wa mpito wa kitaifa wamechaguliwa; Mpango Kazi wa kuwaendeleza wachimbaji wadogo ulijadiliwa na kupitishwa na umeanza kutekelezwa; na takwimu na taarifa muhimu za wachimbaji wadogo zilikusanywa kote nchini kwa lengo la kuwatambua, kubainisha changamoto zinazowakabili na kujenga kanzidata *(database). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukuaji wa kasi wa sekta ndogo ya uchimbaji madini, wachimbaji wadogo wengi hawatunzi kumbukumbu za mapato na matumizi na hawalipi kodi na mrabaha stahiki. Hali hii imekuwa ikiikosesha Serikali kiasi kikubwa cha mapato. Serikali imejipanga kuhakikisha kuwa wachimbaji wadogo wanatunza kumbukumbu sahihi za uchimbaji na mauzo ya madini, pamoja na kulipa kodi na mrabaha stahiki. Aidha, taarifa hizo zitawasaidia wakati wa kuwapa mikopo ili kuboresha shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini imeendelea kukumbwa na migogoro ya mipaka ya leseni za madini. Migogoro hiyo imekuwa ikihusisha wachimbaji wadogo wenyewe kwa wenyewe na kati yao na wachimbaji wakubwa. Wizara imeendelea kusuluhisha migogoro ya aina hiyo kwa mujibu wa Sheria.

Pia, uimarishaji wa Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni umesaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa migogoro ya mipaka ya leseni za madini, kwani leseni zinatolewa kwa kuzingatia kanuni ya aliyewahi kuomba kupatiwa leseni kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010. Wizara yangu imeendelea kuwachukulia hatua watumishi wote wanaosababisha migogoro ya aina hiyo kwa uzembe, kukiuka Sheria na taratibu zilizopo au kupokea rushwa.

Changamoto kubwa inayoikabili Sekta kwa sasa ni uvamizi unaofanywa na wachimbaji wadogo kwenye maeneo yenye leseni za utafiti mkubwa wa madini. Nitumie

fursa hii kuwataka wachimbaji wadogo kuacha tabia hiyo kwani ni ukiukaji wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Wizara yangu kutatua migogoro katika Sekta ya Madini, baadhi ya Wakuu wa Wilaya, Mikoa na Halmashauri wamekuwa wakijihusisha na usuluhishi wa migogoro katika maeneo ya utafutaji na uchimbaji madini, pamoja na kutoa maelekezo mbalimbali yanayohusu usitishwaji ama kuhalalisha uchimbaji unaovunja Sheria wa madini. Hali hii imekuwa ikileta migongano ya kiutendaji na kukuza migogoro husika. Nitoe wito kwa viongozi hao kuepuka utoaji wa maamuzi yanayohusu Sekta ya Madini bila kushirikisha mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, katika kuhamasisha uongezaji thamani madini; Serikali kupitia Wizara yangu iliendeleza ushirikiano na wadau wa madini ili kuboresha mbinu bora za uchenjuaji na uongezaji thamani madini. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2012 hadi Aprili, 2013 jumla ya leseni 32 za uchenjuaji madini ya dhababu zilitolewa ikiwa ni maendeleo ya awali katika kuhawilisha teknolojia *(technology transfer)* ya uchenjuaji madini ya dhahabu kwa wachimbaji wadogo.

Aidha, katika kujenga uwezo wa kuchenjua madini ya shaba hapa nchini, Serikali ilitoa leseni mbili za kuyeyusha madini ghafi ya shaba. Leseni hizo zilitolewa kwa Kampuni ya *Danformation (T) Limited* ya Jijini *Dar es Salaam na TPM (T) Limited* ya Mpanda Mjini. Viwanda hivyo vina uwezo wa kuyeyusha jumla ya tani 48,000 za shaba ghafi kwa mwaka. Maboresho zaidi ya teknolojia yanafanywa na viwanda hivi ili viweze kuchenjua shaba zaidi za madaraja ya chini ya kiwango cha asilimia 18.53

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendea kuimarisha shughuli za uongezaji thamani madini ya vito nchini ambapo madini ya vito yaliyokatwa mwaka 2012/2013 ni Karati 751,415 kati ya tani 1,545 za vito ghafi iliyozalishwa. Hivi sasa, kuna vituo 183 vya ukataji vito hapa nchini, mashine 107 za ukataji vito na wataalamu wa ukataji wapatao 105.

Mheshimiwa Spika, katika kuweka mkazo suala la uongezaji thamani wa madini, hususan madini ya vito, Wizara ilianzisha Kituo cha Uongezaji wa Thamani Madini cha Arusha *(Arusha Gemmological Centre)* mwaka 2009 kwa lengo la kufundisha wachimbaji wadogo namna ya kuongeza thamani madini yao. Katika mwaka 2012/2013, Kampuni ya *OGM Consultants* ya Dar es Salaam ilisaini Mkataba wa kusanifu na kusimamia ukarabati wa Kituo hicho.

Aidha, tarehe 01 Aprili, 2013 Mshauri alipatikana kwa ajili ya kuandaa Mpango Kazi wa Kituo, Mitaala ya Kufundishia, Mahitaji na Sifa za Wakufunzi wanaohitajika ili kuanzisha na kutimiza masharti ya kusajili Kituo.

Pia, Kampuni ya *Wagtech Projects Limited* ya Uingereza imesaini Mkataba wa kuleta mashine za ukataji, usanifu na utengenezaji wa mapambo ya vito katika Kituo hicho. Kazi hiyo itakamilika mwaka 2014/2015 na itagharimu Dola za Marekani milioni mbili sawa na Shilingi bilioni 3.2.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuimarisha Soko la Madini ya Vito, Serikali ilianzisha Maonesho ya Kimataifa ya Vito na Usonara yaliyofanyika kwa mara ya kwanza mwezi Aprili, 2012 mjini Arusha. Maonesho hayo yanatarajiwa kufanyika tena mwezi Oktoba, 2013. Aidha, maandalizi yanaendelea ili kuhakikisha kuwa maonesho hayo yanapanuka zaidi na kufanyika kila mwaka ili kuifanya Tanzania kuwa kituo cha vito Barani Afrika. Lengo ni kukuza biashara na soko la madini ya vito hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Kitengo cha *TANSORT* imeendelea kusimamia biashara ya madini ya almasi na vito hapa nchini kwa kutambua, kuchambua na kuthamini madini hayo. Katika kipindi cha Mwaka 2012/2013, jumla ya Karati 125,940 za almasi zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 31.70, sawa na Shilingi bilioni 50.72 zilichambuliwa na Karati 751,415 za madini ya vito yaliyokatwa na tani 5,392 za madini ghafi ya vito yenye jumla ya Dola za Marekani milioni 28.72, sawa na Shilingi bilioni 45.95 zilithaminishwa na kuuzwa nje ya nchi. Jumla ya mrabaha

uliolipwa Serikalini ni Shilingi bilioni 4.19, sawa na Dola za Marekani milioni 2.62.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Ilani ya Chama Tawala ya Mwaka 2010 – 2015 Ibara ya 56 (e) kuhusu kuimarisha ukaguzi wa migodi katika masuala ya usalama, afya na utunzaji wa mazingira migodini, Wizara iliendelea kufuatilia kwa karibu utendaji wa shughuli za migodi na utafutaji wa madini nchini. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013 migodi sita mikubwa ya dhahabu, migodi ya kati 15, migodi midogo 1,120 na maeneo 229 ya utafiti wa madini yalikaguliwa ambapo taarifa za ukaguzi huo zilitumika kurekebisha masuala ya kiusalama, mazingira na utendaji kwa ujumla. Aidha, katika kipindi hicho, Serikali ilikamilisha ujenzi wa mtaro katika eneo la D'souza lililopo Kitalu B Mirerani ili kuepusha maafa ya mafuriko kwa wachimbaji wadogo katika eneo hilo kama yaliyotokea miaka ya 1998 na 2008.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utunzaji wa mazingira migodini, uchambuzi na upitishaji wa Mipango ya Ufungaji wa Migodi *(Mine Closure Plans)* ulifanyika kwa migodi ya dhahabu ya Bulyanhulu, Buzwagi, *North Mara* na Tulawaka. Migodi yote hiyo pamoja na Mgodi wa *Golden Pride* ambao Mpango wake wa kufunga mgodi ulichambuliwa na kupitishwa hapo awali, itaingia katika hatua ya kusaini mikataba ya kuweka hati fungani *(rehabilitation bond)* ya ukarabati wa mazingira.

Aidha, uchambuzi wa mipango ya ufungaji wa migodi ya Geita (dhahabu), Mwadui (almasi) na *TanzaniteOne (tanzanite)* utakamilika ifikapo Julai, 2013. Kulingana na taarifa za Mipango ya Ufungaji wa Migodi hiyo, gharama za ukarabati wa mazingira ni Bulyanhulu (Dola za Marekani milioni 35.86, sawa na Shilingi bilioni 57.38), Buzwagi (Dola za Marekani milioni 46.92, sawa na Shilingi bilioni 75.07), *Golden Pride* (Dola za Marekani milioni 9.56, sawa na Shilingi bilioni 15.30), *North Mara* (Dola za Marekani milioni 67.46, sawa na Shilingi bilioni 107.94) na Tulawaka (Dola za Marekani milioni 19.98, sawa na Shilingi bilioni 31.97). Aidha, gharama za awali za ufungaji migodi ambayo mipango yake haijaidhinishwa

na Serikali ni Geita (Dola za Marekani milioni 63.36, sawa na Shilingi bilioni 101.38), Mwadui (Dola za Marekani milioni 26.49, sawa na Shilingi bilion42.38), na *TanzaniteOne* (Dola za Marekani milioni 0.13, sawa na Shilingi bilioni 0.21).

Mheshimiwa Spika, Migodi ya *Golden Pride* (Nzega) na Tulawaka (Biharamulo) inatarajiwa kufungwa rasmi ifikapo mwishoni mwa mwaka 2013 na maeneo yake kukabidhiwa Serikalini. Kwa mujibu wa Sheria, mgodi unapofungwa eneo la mgodi husika hurejeshwa Serikalini ili lipangiwe matumizi mengine kadri itakavyoonekana inafaa. Hivyo, Serikali imeamua eneo la Mgodi wa Tulawaka lichukuliwe na *STAMICO* ili iendeleze uchimbaji kwa kiwango cha kati kwa kuwa bado yapo mashapo ambayo yanaweza kuchimbwa kwa faida. Vilevile, eneo la Mgodi wa *Golden Pride*, Nzega litakabidhiwa Chuo cha Madini Dodoma ili litumike kwa ajili ya kutolea mafunzo kwa mafundi mchundo *(technicians).* Siyo kweli kwamba eneo hili wanapewa Magereza. Siyo kweli!

Mheshimiwa Spika, shughuli za uchimbaji madini huendana na matumizi ya baruti. Pamoja na kwamba baruti ni zana muhimu katika uchimbaji, matumizi yake yanahitaji udhibiti madhubuti ili kuhakikisha kuwa hayaleti madhara kwa watumiaji na jamii kwa ujumla. Ili kutimiza azma hiyo, Wizara iliendelea na maandalizi ya Sheria mpya ya Baruti na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha usimamizi wa matumizi ya baruti, Wizara ilitoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo wa madini wapatao 409 katika Mikoa ya Lindi, Shinyanga na Singida. Mafunzo hayo yalihusu utaratibu wa kisheria wa upatikanaji, usafirishaji, utunzaji na utumiaji salama wa baruti. Lengo ni kuwajengea uwezo watumiaji wa baruti katika shughuli za uchimbaji wa madini nchini.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, utekelezaji wa vigezo vitano vilivyokuwa vimesalia kuwezesha Tanzania kupata uanachama kamili wa *Extractive Industries Transparency Initiative - EITI* ifikapo tarehe

15 Februari, 2013 ulikamilika. Bodi ya *EITI* iliitangaza Tanzania kuwa mwanachama kamili wa *EITI (EITI Compliant)* tarehe 12 Desemba, 2012 baada ya kutimiza vigezo vyote. Hatua hii ya uanachama kamili inaonesha kuwa Tanzania sasa inao mfumo thabiti wa utoaji wa taarifa za malipo na mapato kutoka katika kampuni zinazojishughulisha na uchimbaji wa madini, gesi asilia na mafuta, ambao unawezesha wananchi kufahamu na kujadili mchango wa Sekta za Nishati na Madini katika pato la Taifa. Tangazo la Bodi ya *EITI* lilitolewa miezi miwili kabla ya muda tuliokuwa tumejiwekea kutokana na utendaji mzuri wa Wizara na Sekretarieti ya *TEITI* nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Rasimu ya Sheria itakayosimamia shughuli za *TEITI* katika ngazi ya Taifa imekamilika. Rasimu hiyo imezingatia maoni ya Wajumbe wa Kamati Tekelezi na wadau mbalimbali zikiwemo asasi za kiraia na sekta binafsi. Aidha, Rasimu hiyo imewasilishwa kwa nchi wanachama ambazo tayari zina Sheria ya *EITI* kwa ajili ya kupata maoni ya nchi hizo tukikusudia kuboresha Rasimu yetu. Ni matarajio yetu kuwa uandaaji wa Sheria hiyo utakamilika mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuhamasisha wachimbaji wadogo katika utoaji wa takwimu ili kubaini mchango wao kwenye sekta ndogo ya uchimbaji madini, Sekretariati ilitoa elimu juu ya Mpango wa *EITI* kwa viongozi wa Vyama vya Wachimbaji Wadogo vya Mikoa *(Regional Miners Associations)* waliokutana Dodoma tarehe 6 - 7 Desemba, 2012. Katika kikao hicho, viongozi hao walichagua Mwakilishi wa wachimbaji wadogo kwenye Kamati Tekelezi ya *TEITI* kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2013 hadi 2015.

Mheshimiwa Spika, ili kujenga uwezo wa uendeshaji wa *TEITI*, Wajumbe wa Kamati Tekelezi na watumishi wa Sekretariati wameendelea kupatiwa mafunzo na kushiriki katika makongamano yenye lengo la kubadilishana uzoefu kutoka nchi wanachama wa *EITI*. Mwezi Septemba, 2012 Wajumbe wawili wa Kamati Tekelezi na watatu wa Sekretarieti walishiriki warsha juu ya mchango wa *EITI* katika usimamizi

wa rasilimali za madini, gesi asilia, mafuta na misitu iliyofanyika Accra, Ghana. Aidha, Sekretarieti imeshiriki katika programu ya *revenue forecasting* kwa kutumia *models* kwa ajili ya kukadiria mapato ya Serikali kutoka Sekta ya Madini, Gesi Asilia na Mafuta. Programu hii iliendeshwa na Mshauri *M/S Econ – Poyry* kwa ufadhili wa Serikali ya Kifalme ya Norway na ililenga kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi zinazohusika na usimamizi wa mapato ya Serikali, hususan Wizara ya Fedha, *BOT, NBS, TEITI, TMAA, TPDC* na *TRA*.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyobainisha katika hotuba yangu ya mwaka 2012/2013, kuwa njia mojawapo ya kuongeza fungamanisho la Sekta hii na sekta nyingine za jamii na uchumi ni kuhakikisha kwamba Kampuni zinazojishughulisha na madini zinatumia huduma na bidhaa za ndani kadri inavyowezekana. Katika kutekeleza azma hiyo, kanzidata ya mahitaji ya bidhaa na huduma mbalimbali zinazotakiwa migodini iliandaliwa, ambapo takwimu za Kampuni 13 za madini zilionesha kuwa huduma na bidhaa zinazotakiwa ni pamoja na *catering and food services*; *logistics and clearing;* jasi; pozzolana; makaa ya mawe; chokaa; huduma za maabara; huduma za kisheria; huduma za kihandisi; ukandarasi; na usafirishaji. Serikali itaendelea kuhamasisha na kuwasaidia Watanzania kujenga uwezo wa kutoa huduma hizo migodini.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa migodi mikubwa ya dhahabu nchini, kwa mwaka 2012 ilinunua bidhaa na huduma za ndani zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 520.67, sawa na Shilingi bilioni 833.07. Kiasi hiki ni ongezeko la asilimia 61 ikilinganishwa na ununuzi uliyofanyika mwaka 2011 wa Dola za Marekani milioni 379.57, sawa na Shilingi bilioni 607.31. Wizara inaweka mkazo na inawalazimisha Makampuni watumie bidhaa zetu za ndani.  Huo ni uthibitisho. Ununuzi wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa mwaka 2012 ulikuwa Dola za Marekani milioni 829.35, sawa na Shilingi bilioni 1,326.96. Hivyo, ununuzi wa bidhaa na huduma za ndani kwa mwaka 2012 ulikuwa ni asilimia 38.6 ya ununuzi wote wa ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi na uboreshaji wa Ofisi za Madini; katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara ilikamilisha ukarabati wa Ofisi za Madini za Arusha na Shinyanga. Ukarabati huo umegharimu jumla ya Shilingi milioni 274.66 (Arusha Shilingi milioni 193.21 na Shinyanga Shilingi milioni 81.45). Maandalizi ya ujenzi wa ofisi za Dodoma, Mpanda na Mtwara yamekamilika na ujenzi unatarajiwa kuanza mwaka 2013/2014. Lengo la mradi huu ni kuboresha mazingira ya utoaji huduma kwa wananchi katika Ofisi za madini Mikoani.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na juhudi za kutafuta fedha na kiwanja cha kujenga Ofisi za *TMAA* na *TANSORT* ili jengo hilo litumike pia kama Kituo cha Kimataifa cha Biashara ya Madini nchini. Kwa kuzingatia unyeti wa biashara hiyo, inabidi jengo hilo lijengwe kwenye eneo la kibiashara *(strategic business area).* Hivyo, ujenzi wake utaanza kutekelezwa mara kiwanja na fedha vitakapopatikana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu kwa umma kuhusu uchimbaji wa madini ya urani; Serikali iliendelea na jukumu la kutoa elimu kwa kupitia vyombo vya habari na ziara za mafunzo kuhusu faida na changamoto za uchimbaji wa madini ya urani, ili kuondoa hofu kwa umma juu ya madhara ya utafutaji na uchimbaji wa madini hayo. Napenda kutumia nafasi hii kusisitiza kuwa kitaalamu, urani ikiwa katika hali ya muunganiko na oksijeni *(Triuranium Octoxide - U3O8)* kama ilivyo ardhini ama baada ya kuchimbwa na kuchenjuliwa haina madhara kama inavyodaiwa na baadhi ya watu. Uchimbaji wa madini ya urani unatarajiwa kuanza katika eneo la Mkuju Wilayani Namtumbo. Serikali itakuwa na hisa kwenye mgodi huu.

Mheshimiwa Spika, narudia; migodi yote mipya inayoanza sasa hivi, hatukusanyi tu kodi na mirahaba. Tumeanza kuwa na hisa kwenye migodi. Napenda kutumia nafasi hii kusisitiza kuwa urani kitaalamu urani ikiwa katika hali ya muunganiko na *oxygen*, kwa wale wanaojua chemistry, ni atom tatu za uran na nane za oxygen. Kama ilivyo ardhini

ama baada ya kuchimbwa na kuchenjuliwa, haina madhara kama inavyodaiwa na baadhi ya watu. Nawaomba wananchi waondoe hofu kuhusu madhara tarajiwa ya utekelezaji wa mradi huo kwa kuwa Serikali yao ipo makini na itazingatia taratibu zote za kitaifa na kimataifa za kuchimba, kutunza, kusafirisha na kuendeleza madini hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Mkuju unaomilikiwa na Kampuni ya *Mantra Tanzania Ltd* iliyosajiliwa na Msajili wa Kampuni chini ya Sheria za Tanzania uliuzwa mwezi Desemba, 2010 kwa Kampuni ya *ARMZ* ya Urusi baada ya kununua hisa za Kampuni mama iitwayo *Mantra Resources* ya Australia kupitia soko la hisa la Australia kwa bei ya jumla ya Dola za Marekani milioni 1,043.80, sawa na Shilingi bilioni 1,670.08. Kufuatia hatua hiyo, Serikali kupitia *TRA* iliwapatia madai wahusika ya Dola za Marekani milioni 205.80 ambapo Dola za Marekani milioni 196 zilitakiwa kulipwa kama *Capital Gain Tax* na Dola za Marekani milioni 9.8 ni Ushuru wa Stempu. Hata hivyo, Kampuni hiyo ilipinga madai hayo na shauri hilo lilifikishwa Mahakama ya Kodi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko kuwa Serikali imetoa leseni ya uchimbaji kwa Mradi wa Mto Mkuju bila kushirikisha baadhi ya wadau na kuwa malipo stahiki hayajalipwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa umiliki na uendeshaji wa uchimbaji mkubwa wa madini unakamilika kwa mhusika kupata leseni ya uchimbaji. Aidha, leseni ya uchimbaji hutolewa baada ya mwombaji kupatiwa Hati ya Mazingira kutoka kwa mamlaka husika. Hivyo, taratibu za kisheria zimezingatiwa katika kutoa leseni hiyo. Kutolewa kwa leseni hakukufuta kesi iliyokuwepo Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu migodi mipya iliyoanzishwa; Serikali imeendelea na juhudi zake za kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Madini. Kutokana na juhudi hizo, mgodi mpya wa dhahabu wa *New Luika* ulifunguliwa Wilayani

Chunya na kuanza uzalishaji mwezi Septemba, 2012. Gharama za awali za uwekezaji za mradi huo ni Dola za Marekani milioni 136, sawa na Shilingi bilioni 217.60. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2013 mgodi huo ulikuwa umezalisha wakia 26,636.6 za dhahabu, sawa na kilogramu 755.15 za dhahabu zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 31.49 sawa na Shilingi bilioni 50.38 na kuipatia Serikali Dola za Marekani milioni 1.26, sawa na Shilingi bilioni 2.02 kutokana na mrabaha. Anayesema Serikali haikaribishi wawekezaji, huyo ni mchochezi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *RECB Limited* inamiliki leseni Na. ML 237/2006, ML 238/2006 na ML 239/2006 kwa ajili ya kuchimba madini ya *niobium* kwenye mradi wa Pandahill huko Songwe (Mbeya Vijijini). Wamiliki wa mradi huo wanakamilisha taratibu za kuanza ujenzi wa mgodi. Gharama za awali za mradi ni takriban Dola za Marekani milioni 60, sawa na Shilingi bilioni 96.

Miradi mingine ya madini ambayo inakaribia kuanzishwa ni pamoja na Mradi wa *Kabanga Nickel* ulioko Kabanga, Wilayani Ngara unaomilikiwa na *Kabanga Nickel Company Limited* ya Tanzania; Mradi wa Magambazi Wilayani Kilindi, Mkoani Tanga wa kuchimba madini ya dhahabu, unamilikiwa na Kampuni ya *Canaco Resources (T) Limited* ya Canada; Mradi wa Nickel wa Ntaka uliopo Wilayani Nachingwea unaomilikiwa na Kampuni ya *Ngwena (T) Limited,* Kampuni tanzu ya *IMX Resources* ya Australia; na Mradi wa dhahabu wa Nyanzaga uliopo Wilayani Sengerema unaomilikiwa na Kampuni ya *African Barrick Gold* ya Uingereza ambao upo katika hatua za mwisho za upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, shughuli za upembuzi yakinifu kwa ajili ya Mradi wa Nickel wa Kabanga uliopo Wilayani Ngara zimekamilika. Majadiliano ya awali kuhusu Mkataba wa uendelezaji wa mradi huo yameanza kati ya Serikali na *Kabanga Nickel Company Limited*. Ujenzi wa mradi huo unakadiriwa kugharimu Dola za Marekani bilioni 1.2, sawa na Shilingi bilioni 1,920. Aidha, shughuli za tathmini ya

mazingira na fidia kwa wananchi watakaopisha mradi zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake mengine kupitia Taasisi na Mashirika yaliyo chini yake katika Sekta ya Madini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST)* ulikamilisha kukusanya takwimu za jiofizikia kwa kutumia ndege na kutathmini upatikanaji wa madini katika Wilaya za Babati, Bagamoyo, Bahi, Chamwino, Dodoma, Hanang, Handeni, Igunga, Iramba, Kilindi, Kiteto, Kondoa, Manyoni, Mpwapwa, Mvomero, Simanjiro na Singida Vijijini. Kazi hiyo imegharimu takriban Dola za Marekani milioni 13.67, sawa na Shilingi bilioni 21.87.

Aidha, *GST* imekamilisha utafiti wa kijiosayansi kutathmini upatikanaji wa madini katika maeneo ya Wilaya za Chunya, Lindi, Liwale, Manyoni, Mbarali, Nachingwea na Ruangwa, pamoja na kuchora ramani za jiolojia za maeneo hayo. Hatua hii itasaidia kuelewa maeneo yote muhimu kwa ajili ya uwekezaji na kuwawezesha wachimbaji, hususan wachimbaji wadogo nchini kupata maeneo ya kuchimba. Baadhi ya madini yaliyogunduliwa kuwepo kwenye maeneo hayo ni pamoja na *Platinum Group Metals (PGM),* shaba, *graphite*, dhahabu na almasi.

Mheshimiwa Spika, *GST* imeanzisha vituo vitatu vipya vya kisasa vya kupimia matetemeko ya ardhi vyenye uwezo wa kunakili taarifa za matukio ya matetemeko moja kwa moja kwenye kompyuta mara tukio linapotokea. Vituo hivi viko Arusha, Dodoma na Mbeya. Wastani wa kiwango cha matetemeko kama ilivyonakiliwa kwenye vituo hivyo *(average seismic data reading)* ni kuanzia 4.1 hadi 4.8 kwa kipimo cha Richter ikimaanisha kwamba nchi yetu kwa sasa haiko kwenye hatari ya matetemeko ya ardhi *(earth quakes).*

Aidha, ujenzi wa ghala la kuhifadhia sampuli za miamba *(core shed)* huko Dodoma ulikamilika katika mwaka

2012/2013 na umegharimu Shilingi milioni 417.60, sawa na Dola za Marekani 261,000.

Mheshimiwa Spika, kazi za *geological mapping; geochemical survey;* na *ground geophysical survey* zilianza katika maeneo yenye *Quarter Degree Sheet (QDS)* 12 na kujumuisha taarifa za *remote sensing* katika *QDS* mbalimbali. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wakala umefanikiwa kubadilisha ramani za jiolojia, *QDS* 42 kutoka kwenye mfumo wa karatasi na kwenda kwenye mfumo wa digitali kwa gharama ya Shilingi milioni 33.60, sawa na Dola za Marekani 21,000.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2012/2013, Chuo cha Madini – Dodoma (*MRI)* kiliendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya cheti na stashahada kwa jumla ya wanafunzi 351 katika fani mpya za uhandisi na usimamizi wa mazingira migodini na jiolojia ya mafuta na gesi asilia, na katika fani ya jiolojia na utafutaji madini, uhandisi migodi na uhandisi uchenjuaji madini. Mnamo mwezi Juni, 2013 jumla ya wanafunzi 49 wanatarajiwa kuhitimu katika fani za jiolojia na utafutaji madini 28, uhandisi migodi 10 na uhandisi uchenjuaji madini 11.

Mheshimiwa Spika, Chuo pia kiliandaa Mitaala ya ngazi za stashahada katika fani mpya za uhandisi na usimamizi wa mazingira migodini na jiolojia ya mafuta na gesi asilia. Mitaala hiyo iliwasilishwa *NACTE* na kupata uhalali na ithibati *(accreditation).*

Baada ya hatua hiyo, Chuo kilianza kutoa mafunzo katika ngazi ya Cheti na Stashahada katika fani za uhandisi na usimamizi wa mazingira migodini kwa wanafunzi 35, jiolojia ya mafuta na gesi asilia kwa wanafunzi 65. Wizara ya Nishati na Madini inafadhili wanafunzi 15 katika fani ya uhandisi na usimamizi wa mazingira na wanafunzi 15 katika fani ya jiolojia ya mafuta na gesi asilia.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, na Watanzania wote, Wizara yangu imedhamiria kutongoja

Wizara ya Elimu itafute *scholarship* kwa wataalamu wa mafuta na gesi. Tunasomesha kwa kutumia fedha zilizopo pale Wizarani, na hatubagui. Hata sasa hivi Attorney General tuna vijana wake wawili tumewapa *scholarship* wako *Scotland*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango na Bajeti kwa mwaka 2012/2013, Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania - *TMAA* ulitekeleza majukumu yake na kuwezesha kupatikana kwa mafanikio mbalimbali. Katika kipindi hicho, *TMAA* kwa kushirikiana na *TRA* ilifanya ukaguzi wa hesabu za fedha kwa wamiliki wa migodi mikubwa ya kati na kwa wanunuzi wa madini *(mineral dealers).*

Kutokana na ukaguzi huo, katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Machi, 2013, Mgodi wa *Golden Pride* uliopo Nzega unaomilikiwa na Kampuni ya *Resolute Tanzania Limited* umelipa kiasi cha Shilingi bilioni 19.8 kama kodi ya mapato *(Corporate Tax).*

Mheshimiwa Spika, hivyo, jumla ya kodi ya mapato iliyolipwa na mgodi huo hadi sasa (tangu uanzishwe mwaka 2009) ni Shilingi bilioni 90.9. Mgodi wa dhahabu wa Geita uliopo Geita unaomilikiwa na Kampuni ya *AngloGold Ashanti Limited* umelipa jumla ya Shilingi bilioni 108.1 kama kodi ya mapato. Hivyo, jumla ya kodi ya mapato iliyolipwa na mgodi huo kuanzia mwaka 2009 hadi mwezi Machi, 2013 ni Shilingi bilioni 299.4.

Vilevile, Mgodi wa Tulawaka unaomilikiwa na Kampuni ya *African Barrick Gold* umelipa kodi ya mapato mara moja tu ya jumla ya Shilingi bilioni 77.4 kwa mwaka 2012. Migodi mikubwa iliyolipa kodi ya mapato mwaka 2011/2012 ni *Golden Pride* iliyolipa jumla ya Shilingi bilioni 37.18, sawa na Dola za Marekani milioni 23.24 na Mgodi wa Geita uliolipa jumla ya Shilingi bilioni 188.10, sawa na Dola za Marekani milioni 117.55.

Mheshimiwa Spika, Migodi ya Bulyanhulu (Kahama), Buzwagi (Kahama), *El Hillal Minerals* (Mwadui), North Mara

(Tarime) na Williamson Diamond (Mwadui), haijaanza kulipa kodi ya mapato *(corporate tax)* kwa kuwa bado haijaanza kupata faida. Wizara inafuatilia kwa makini uwekezaji kwenye migodi hii ili ianze kulipa kodi ya mapato haraka iwezekanavyo. Malipo ya kodi nyinginezo yaliyofanywa na migodi mikubwa kwa mwaka 2012 ni kodi ya zuio – *Withholding Tax* (jumla ya Shilingi bilioni 67.64), *Pay As You Earn - PAYE* (jumla ya Shilingi bilioni 87.45), *Skills Development Levy* (jumla ya Shilingi bilioni 19.32), *Service Levy* (jumla ya Shilingi bilioni 4 (kama ilivyofafanuliwa katika aya ya 135), kodi na tozo nyinginezo (jumla ya Shilingi bilioni 42.8) na mrabaha (jumla ya Shilingi bilioni 107)- kama ilivyofafanuliwa katika aya ya 142.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TMAA* imeimarisha ukaguzi wa madini ya ujenzi kwa kutumia hati za mauzo ya madini katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Ukaguzi huo umewezesha kiasi cha Shilingi milioni 838.9 kulipwa kama mrabaha katika kipindi cha kuanzia Julai, 2012 hadi Aprili, 2013 ikilinganishwa na wastani wa Shilingi milioni tatu zilizokuwa zikikusanywa kwa mwaka katika Mikoa hiyo kabla ya utaratibu huu kuanza. Utaratibu huu umeanza kutumika pia katika Mikoa ya Arusha, Katavi, Kigoma, Mwanza na Rukwa ambapo jumla ya Shilingi milioni 722 zimekusanywa kama mrabaha katika kipindi cha kuanzia Julai, 2012 hadi Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, ili kujua kiasi na thamani halisi ya madini yaliyozalishwa na kuuzwa na migodi mikubwa nchini, Wakala ulifanya ukaguzi na uhakiki wa madini katika migodi ya Bulyanhulu, Buzwagi, Geita, *Golden Pride,* Mwadui, *New Luika*, *North Mara*, *Tanzanite One* na Tulawaka.

Ukaguzi huo ulifanyika kwa kuweka Wakaguzi kwenye migodi hiyo yote muda wote wa uzalishaji na umewezesha kukusanywa kwa jumla ya Dola za Marekani milioni 61.04, sawa na Shilingi bilioni 97.66 kama mrabaha kutoka kwenye migodi hiyo katika kipindi cha kuanzia Julai, 2012 hadi Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote, Wizara yangu imedhamiria kutongoja Wizara ya Elimu itafute *scholarship* kwa wataalam wa mafuta na gesi. Tunasomesha kwa kutumia fedha zilizopo pale Wizarani na hatubagui, hata sasa hivi *Attorney General* tuna vijana wake wawili tumewapa *scholarship* wako Scotland. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usimamizi wa biashara ya madini nchini, Serikali kupitia Wakala wa Ukaguzi wa Madini *(TMAA)* imeanzisha Madawati Maalum ya kukagua madini yanayosafirishwa nje ya nchi kupitia Viwanja vya Ndege vya Kimataifa vya Mwalimu Julius Nyerere (Dar es Salaam), Kilimanjaro na Mwanza. Madawati hayo yamesaidia katika kubaini na hatimaye kuwakamata watu wasio waaminifu wanaosafirisha madini nje ya nchi kinyume cha sheria. Kwa kipindi cha kuanzia Oktoba, 2012 hadi Aprili, 2013, Waheshimiwa Wabunge, msikilize, kwa kipindi cha miezi sita tu, madini yenye thamani ya takriban shilingi bilioni 13.12 sawa na Dola za Marekani milioni 8.13 yalikamatwa yakisafirishwa nje ya nchi kinyume cha sheria. Wahusika wamechukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wakala kwa kushirikiana na *NEMC* umeendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa shughuli za ukarabati na utunzaji wa mazingira katika maeneo ya migodi mikubwa, ya kati na midogo. Wahusika wamekuwa wakipewa maelekezo yenye lengo la kuboresha hali ya mazingira kwenye maeneo yao. Jumla ya migodi mikubwa 8, ya kati 12 na midogo 123 ilikaguliwa katika kipindi cha kuanzia Julai, 2012 hadi Aprili, 2013. Ukaguzi huo umesaidia kuimarika kwa shughuli za utunzaji wa mazingira katika maeneo ya migodi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Wilaya zinazohusika na migodi mikubwa nchini zimeendelea kulipwa ushuru wa huduma *(Service Levy)* kwa mujibu wa Sheria zilizopo. Mwaka 2012, Mgodi wa Bulyanhulu umelipa Dola za Marekani 200,000 kwa Halmashauri ya Kahama;

Mgodi wa *North Mara* umelipa Dola za Marekani 200,000 kwa Halmashauri ya Tarime; Mgodi wa Tulawaka umelipa Dola za Marekani 200,000 kwa Halmashauri ya Biharamulo; Mgodi wa Buzwagi umelipa Dola za Marekani 200,000 kwa Halmashauri ya Kahama; Mgodi wa Geita umelipa Dola za Marekani 200,000 kwa Halmashauri ya Geita; Mgodi wa *Golden Pride* umelipa Dola za Marekani 1,462,374 kwa Halmashauri ya Nzega; Mgodi wa *TanzaniteOne* umelipa Dola za Marekani 16,432 kwa Halmashauri ya Simanjiro; na Mgodi wa Mwadui umelipa Dola za Marekani 30,300 kwa Halmashauri ya Kishapu. Jumla ya malipo yaliyofanywa na migodi hiyo kwa Halmashauri husika kuanzia Mwaka 2006 hadi 2012 ni Dola za Marekani 9,099,005 sawa na Shilingi bilioni 14.41.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na majadiliano na Kampuni za Madini zenye *MDAs* ili zikubali kuondoa kipengele kinachowaruhusu kulipa Ushuru wa Huduma katika kiwango cha Dola za Marekani 200,000 badala ya kulipa kiasi cha asilimia 0.3 ya mapato halisi kama Sheria inavyotaka. Migodi hiyo ni ile ya Bulyanhulu, Buzwagi, Geita, North Mara na Tulawaka. Aidha, Halmashauri za Wilaya zinatakiwa kudai malipo ya Ushuru wa Huduma kwa Kampuni zinazotoa huduma kwenye migodi. Kampuni hizo zinatakiwa kulipa ushuru huo kwa kiwango cha asilimia 0.3 ya mapato halisi.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa – *STAMICO*. Serikali iliamua kulihuisha Shirika la *STAMICO* ili litekeleze majukumu mahsusi katika Sekta ya Madini kwa maslahi ya Taifa. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa tumeendelea kulijenga upya Shirika hili ikiwa ni pamoja na kulipatia fedha, vifaa vya utafutaji madini na kuongeza idadi ya watumishi. Bodi ya *STAMICO* imeteuliwa rasmi tarehe 14 Aprili, 2013 na kuzinduliwa tarehe 11 Mei, 2013. Hadi Desemba, 2012 Shirika hilo lilikuwa na thamani *(Book Value)* ya Shilingi bilioni 5.47. Katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Aprili, 2013; matumizi ya Shirika yalikuwa Shilingi bilioni 2.35. Vyanzo vya mapato ya Shirika yalikuwa ruzuku kutoka Serikalini Shilingi bilioni 1.02; malipo ya ubia (Shilingi bilioni 1.22); mabadiliko ya thamani ya Shilingi kwa fedha za kigeni (Shilingi milioni

53.40); huduma ya uchorongaji (Shilingi milioni 29.99); na kodi ya pango (Shilingi milioni 29.35).

Mheshimiwa Spika, *STAMICO* ina ubia na Kampuni ya *TANZAM* 2000 katika Mradi wa Uendelezaji upya Mgodi wa *Buckreef*. Katika Mradi huu, *STAMICO* inamiliki hisa asilimia 45 na *TANZAM* 2000, inamiliki asilimia 55. Katika Mwaka 2012/13, kazi zilizofanyika katika mradi huu ni pamoja na uchorongaji miamba, uchunguzi wa sampuli za miamba katika maabara na *resource modelling* kwa ajili ya kutathmini mashapo. Hadi Mwezi Aprili, 2013 kiasi cha dhahabu kilichothibika kuwepo katika mradi wa *Buckreef* na maeneo ya jirani ya Bingwa na *Tembo Mines* ni wakia za dhahabu milioni 2.12.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza azma ya Serikali ya kushiriki katika uwekezaji kwenye Sekta ya Madini, mwezi Januari, 2013, *STAMICO* ilimpata mbia wa kuendeleza upya Mgodi wa Dhahabu wa Buhemba. Mbia aliyepatikana ni Kampuni ya *Manjaro Resources* ya Australia. Mgodi huo una mabaki ya uchimbaji wa zamani *(tailings)* yanayokadiriwa kuwa na thamani ya Dola za Marekani milioni 70, sawa na shilingi bilioni 112. Aidha, eneo hilo linakadiriwa kuwa na mashapo ya dhahabu katika miamba kwa kiwango cha wakia 400,000. Kupitia *STAMICO*, Serikali itamiliki hisa asilimia 40 katika mgodi utakaoanzishwa na kupata gawio la asilimia 30 ya thamani ya dhahabu itakayozalishwa kutokana na mabaki ya uchimbaji wa zamani yaliyopo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sheria ya Madini ya mwaka 2010 inayotaka madini ya vito kuchimbwa na Watanzania kwa umiliki wa hisa zisizopungua asilimia 50, Serikali ilifikia makubaliano kati yake na Kampuni ya *TanzaniteOne* inayochimba madini ya Tanzanite. Kutokana na makubaliano hayo, *STAMICO* kwa sasa ni mmiliki mwenza wa eneo la leseni ya Kitalu C, Mirerani kwa asilimia 50 kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mgodi wa Kiwira, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, mgodi huu umerudishwa rasmi Serikalini baada ya sehemu kubwa ya madai

yaliyokuwepo kulipwa. Hivi sasa, Serikali kupitia *STAMICO* ipo huru kuuendeleza mgodi huo. Malipo yaliyofanyika ili kuurudisha Serikalini mgodi huo ni jumla ya Shilingi bilioni 40 zilizolipwa kwa wadai mbalimbali ikiwa ni pamoja na *CRDB, PSPF* na *NSSF*. Mgodi huo unatarajiwa kuanza tena uzalishaji wa makaa ya mawe ifikapo Mwaka 2015/16. Shughuli zitakazofanyika kabla ya kuanza uzalishaji ni kupanua mgodi wa chini; kujenga mgodi wa wazi (*open - cast*); kujenga mtambo wa kufua umeme wa *MW* 200; na kujenga njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 132 kutoka Kiwira hadi Mbeya. Shughuli hizo zinakadiriwa kugharimu Dola za Marekani milioni 450, sawa na Shilingi bilioni 720.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya madini. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2012 hadi Aprili, 2013, Sekta ya Madini ilipata mafanikio yafuatayo: kulipwa Serikalini kwa kodi ya mapato *(corporate tax)* kutoka Kampuni za Geita *Gold Mining Limited* (Geita) - Shilingi bilioni 108.1, *Resolute Tanzania Limited (Golden Pride)* - Shilingi bilioni 19.8 na *African Barrick Gold* (Tulawaka) - Shilingi bilioni 77.4. Kulipwa kwa Shilingi milioni 838.9 kama mrabaha kutokana na uzalishaji wa madini ya ujenzi kwa Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani; kukusanywa kwa jumla ya Dola za Marekani milioni 61.04, sawa na Shilingi bilioni 97.66 kama mrabaha kufuatia ukaguzi na uhakiki wa madini yaliyozalishwa kwenye migodi ya Bulyanhulu, Buzwagi, Geita, *Golden Pride,* New Luika, North Mara, Mwadui, *TanzaniteOne* na Tulawaka; kuanzishwa kwa madawati kwenye viwanja vya ndege vya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Mwanza kwa ajili ya kudhibiti utoroshaji wa madini kwenda nje ya nchi, ambapo madini yenye thamani ya takriban Shilingi bilioni 13.12 yalikamatwa yakisafirishwa nje ya nchi kinyume cha Sheria; *STAMICO* kupewa Mgodi wa Makaa ya Mawe ya Kiwira na kupata mbia wa kuendeleza upya Mgodi wa dhahabu wa Buhemba; Tanzania kuwa mwanachama kamili wa *EITI (EITI compliant*); na Chuo cha Madini, Dodoma kuanzisha fani mpya katika ngazi ya stashahada za uhandisi na usimamizi wa mazingira migodini na jiolojia ya mafuta na gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kuanzishwa

kwa miradi mipya ya Mkuju – urani (Ruvuma), Pandahill – *niobium* (Mbeya), Ntaka – *nickel* (Lindi) na Dutwa – *nickel* (Simiyu); kuanzishwa kwa vituo vitatu vya kisasa vya kupima matetemeko ya ardhi katika Mikoa ya Arusha, Dodoma na Mbeya; kukamilika kwa ujenzi wa ghala la kuhifadhi sampuli za miamba (*core shed*); kukamilika kwa kazi ya ukusanyaji wa takwimu za jiofizikia na tathmini ya upatikanaji wa madini katika Wilaya 17; kukamilika kwa utafiti wa kijiosayansi na uchoraji wa ramani wa kijiolojia kwa Wilaya za Chunya, Lindi, Liwale, Manyoni, Mbarali, Nachingwea na Ruangwa; kutengwa kwa maeneo 16 yenye ukubwa wa hekta 265,396 kwa ajili ya uchimbaji mdogo wa madini; kukamilika kwa ujenzi wa mtaro wa D'souza katika eneo la Mirerani; kukamilika kwa ukarabati wa ofisi za madini Arusha na Shinyanga; na kuendelea kurasimisha (*formalizing*) wachimbaji wadogo ikiwa ni pamoja na kuanzisha *REMAs*.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mafanikio hayo ya kisekta, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu imepata Hati Safi ya Hesabu za Mwaka 2011/2012. Matokeo hayo yamepatikana baada ya Wizara kusimamia kikamilifu mapato na matumizi yake kwa kufuata taratibu, sheria na kanuni zilizopo. Wizara itaendelea kuboresha zaidi utendaji wake ili kuhakikisha fedha za umma zinatumika kulingana na vipaumbele vilivyowekwa kwa manufaa ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka 2011/2012, pamoja na Hati Safi ya Hesabu, Wizara pia imepata alama za jumla za asilimia 83 kwa kufuata taratibu za ununuzi ipasavyo na kuwa moja kati ya Wizara zenye ufanisi katika masuala yote ya ununuzi. Ufanisi huo ulibainishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (*PPRA*) baada ya kufanyika ukaguzi. Mafanikio hayo ni dalili njema Kiwizara na Kitaifa kwa ujumla katika kuhakikisha kuwa rasilimali za nchi zinatumika kwa uwazi na kwa manufaa ya Watanzania. Kwa hiyo, mwaka jana mlitaka kunionea tu, ukweli huu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazokabili sekta ya

madini. Katika kipindi cha utekelezaji cha mwaka 2012/2013, sekta ya madini ilikabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo upatikanaji wa mitaji kwa wachimbaji wadogo; utengaji wa maeneo ya wachimbaji wadogo; ukuaji kwa kasi wa shughuli za uchimbaji usio rasmi; kuzuia uvamizi wa maeneo yenye leseni za utafutaji na uchimbaji madini unaofanywa na wachimbaji holela; kushamiri kwa biashara isiyo halali ya madini, hususan, madini ya dhahabu na vito; fungamanisho la sekta ya madini na sekta nyingine za uchumi; na usalama, afya na mazingira katika maeneo ya migodi.

Mheshimiwa Spika, ajira na maendeleo ya rasilimali watu. Kufuatia ugunduzi mkubwa wa gesi asilia nchini, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango wa Uendelezaji Rasilimali Watu wa *Marshall Plan on Capacity Building and Development in Oil and Gas Industry* 2012 - 2016 ili kuzalisha wataalamu Watanzania wa kutosha katika fani hizo. Mwaka 2012/2013 kupitia mpango huo, Wizara kwa kushirikiana na *TPDC* imeweza kufadhili vijana wa Kitanzania 122 katika fani ya mafuta na gesi ambapo vijana 30 walipelekwa Chuo cha Madini Dodoma (MRI) kwenye mafunzo ya miaka mitatu (*Full Technician Certificate);* 10 Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM); 64 VETA Lindi na 50 VETA Mtwara (*Certificates*); na taratibu za kuwapeleka vijana 10 nchini Brazil na 20 China kusoma kozi katika ngazi za Uzamili na Uzamivu katika fani za gesi na mafuta zimekamilika. Aidha, Wizara imedhamini watumishi wanne (4), wawili (2) kutoka Wizara yangu na wawili (2) kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenda katika masomo ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Aberdeen nchini Uingereza.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, ni kosa kubwa sana mtu kusema nchi hii haina wataalam kabisa, itakuwa ni sawa mtu akisema wataalam wamepungua. *TPDC* ina Ph.D. tano (5) za *Oil and Gas*. *TPDC* ina *Masters* 34. Kwa hiyo, mtu asije akawaambia kwamba Watanzania hawakusoma, hivi kesho vijana 10 wanakwenda Brazil kusoma *Master,* vijana 20 wanakwenda China kusoma *Master*, Scotland wako sita (6) na sasa hivi Norway tutafikisha

vijana 30 wanaosoma *Masters*. Hiyo ndio *Marshall Plan* ya Wizara na hizo *scholarship* Wizara ndiyo inatafuta, haingoji mtu awatafutie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/13, Wizara iliajiri watumishi 30 kwa kibali cha Mwaka 2011/2012. Aidha, taasisi zilizo chini ya Wizara ziliajiri jumla ya watumishi 22. Kati ya hao *TPDC* (17) na *REA* watano (5).

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza tija na motisha kwa watumishi, katika mwaka 2012/2013 Wizara iliwapandisha vyeo watumishi 56 na kuwathibitisha kazini watumishi 15. Aidha, Wizara iliwapeleka mafunzoni jumla ya watumishi 90 katika fani mbalimbali. Kati ya hao, 26 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na 64 mafunzo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya afya za watumishi, Wizara iliendelea kutekeleza Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 2 wa Mwaka 2006 ambapo watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (VVU) na wenye UKIMWI wanapewa huduma ya lishe, chakula na madawa maalum.

Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2013/2014, umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 – 2015/2016; Malengo ya Taifa ya MKUKUTA II; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 - 2015; Mpango Mkakati wa Wizara ya Nishati na Madini 2011/2012 – 2015/2016; Maagizo ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa kwa Wizara ya Nishati na Madini kwa nyakati tofauti; Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2013/2014; na ushauri uliotolewa na Bunge pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa nyakati tofauti.

Mheshimiwa Spika, pamoja na miongozo hiyo, Wizara pia imeandaa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2013/2014, kwa kuzingatia Mpango Mpya wa Ufuatiliaji na Tathmini wa miradi mikubwa ya Kitaifa ulioanzishwa na Serikali. Mpango huo

unalenga katika kupata matokeo makubwa sasa *"Big Results Now".* Mpango huo unashirikisha sekta sita, ambapo Sekta ya Nishati ni miongoni mwa sekta hizo. Wizara yangu imejipanga na imedhamiria kwa dhati kuhakikisha kuwa inatekeleza miradi yote iliyobainishwa katika Mpango huo, kwa kuacha kufanya kazi kwa mazoea "*business as usual*" na badala yake kufanya kazi kwa ubora, ufanisi na ubunifu wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulingana na matokeo ya Maabara ya Nishati *(Energy Lab)*, iliyofanyika kupitia Mpango huo, jumla ya miradi 28 ilibainishwa, ambapo saba (7) ni ya ufuaji umeme, saba (7) ni ya usafirishaji umeme na 14 ni ya usambazaji umeme. Kati ya hiyo, miradi mitatu (3) itatekelezwa kwa utaratibu wa *Public Private Partnership (PPP*), mmoja utatekelezwa na Kampuni binafsi ya *Kilwa Energy* na miradi iliyobaki itatekelezwa na Serikali. Gharama za kutekeleza miradi hiyo yote zinakadiriwa kuwa Shilingi trilioni 7, ambapo Serikali itachangia Shilingi trilioni 4.85 kwa kipindi cha miaka mitatu 2013/14 – 2015/16 na kiasi kilichobaki kitatolewa na Sekta Binafsi pamoja na Washirika wa Maendeleo. Bajeti hii ni ya kipekee ambapo 90% inaenda kwenye miradi ya maendeleo, ndio maana ya *Big Result Now. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mpango huu unalenga kuleta manufaa makubwa kwa Taifa letu ifikapo Mwaka 2015/2016, hivyo, naamini kuwa Wizara itapata ushirikiano mkubwa katika kutekeleza miradi hiyo kutoka kwa wadau mbalimbali wakiwemo: Waheshimiwa Wabunge, Washirika wa Maendeleo, Wawekezaji wa Ndani na Nje na Wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2013/2014, pamoja na masuala mengine, unalenga kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika; kuongeza wateja wanaotumia umeme hasa vijijini; kuongeza kasi ya kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya; ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia; kusimamia na kudhibiti biashara ya mafuta; kuvutia uwekezaji katika Sekta za Nishati na

Madini; kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali; kujenga uwezo wa usimamizi na ufuatiliaji katika Sekta za Nishati na Madini ili kukuza uchumi na kuharakisha maendeleo ya Taifa letu, kama ilivyoainishwa ndani ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ifikapo Mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Wizara yangu imepanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 220 katika Mwaka 2013/2014. Kiasi hiki ni asilimia 14 zaidi ya lengo lililowekwa kwa mwaka 2012/2013 la kukusanya shilingi bilioni 193.01. Mipango ambayo itatumika kukusanya mapato hayo ya Serikali ni pamoja na: kuboresha na kusimamia mikataba ya utafutaji na uzalishaji katika Sekta za Nishati na Madini; kuboresha Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini *(Mining Cadastral Information Management System – MCIMS);* kuwezeshwa kwa Ofisi za Madini za Kanda kukusanya maduhuli ipasavyo; kuendelea kuimarisha usimamizi wa wachimbaji wadogo, kuwapa wachimbaji wadogo huduma za ugani na elimu juu ya ulipaji kodi na ada mbalimbali ili kuongeza tija katika uzalishaji madini; kudhibiti utoroshaji wa madini na ukwepaji wa kulipa mrabaha; na kuimarisha usimamizi wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Kanuni zake. Kwa hiyo, mnaona kila mwaka Wizara inazidi kuongeza pato kwenye kibuyu cha Serikali.

Mheshimiwa Spika, sekta ya nishati. Kwa mwaka 2013/2014, kazi zilizopangwa kutekelezwa katika Sekta ya Nishati ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa Bomba la Gesi Asilia kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam; kuimarisha njia za kusafirisha na kusambaza umeme; kuongeza ufuaji umeme; kuongeza idadi ya Watanzania wanaotumia umeme majumbani na kwenye shughuli za kiuchumi; kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya 13 na maeneo mengine vijijini; kuboresha usimamizi na udhibiti wa biashara ya mafuta; kuweka misingi ya kisheria ya kusimamia Sekta Ndogo ya Gesi Asilia; kuendeleza vyanzo vya nishati jadidifu; na kupitia na kurekebisha miundo ya Mashirika ya *TANESCO* na *TPDC* kwa lengo la kuyaboresha na kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali imeamua kutekeleza miradi itakayoleta matokeo makubwa na kwa haraka. Sisi sio maneno, miradi itakayoleta matokeo makubwa na kwa haraka. Kutokana na uamuzi huo, Waheshimiwa Wabunge, sikilizeni kwa makini hapa, kiasi cha shilingi bilioni 545.13 kati ya shilingi bilioni 558.35, sawa na asilimia 98 ya Fedha za Ndani za Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka 2013/2014 zimetengwa ili kutekeleza miradi itakayoleta matokeo makubwa na ya haraka *(Big Results Now).* Hii ni bajeti inayoipeleka Tanzania kwenye karne ya 22. Tunaachana na bajeti za porojo na maneno, tunaenda kwa tarakimu hapa, hii ni bajeti ya tarakimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta Ndogo ya Umeme. Kuongeza Uzalishaji wa Umeme Nchini, Miradi ya Kinyerezi I (MW 150) na II (MW 240). Lengo la Serikali ni kuhakikisha mitambo ya kufua umeme kwa kutumia gesi asilia inakamilika sawia na Bomba la Gesi Asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam. Hivyo, Serikali kupitia *TANESCO* itawezesha utekelezaji wa mradi wa uzalishaji umeme wa Kinyerezi I (MW 150) na Kinyerezi II (MW 240) ambapo, kazi za usanifu wa eneo la mradi (*site layout design*) na shughuli za ujenzi zitaanza. Katika Mwaka 2013/2014, jumla ya shilingi bilioni 208, sawa na Dola za Marekani milioni 130 zimetengwa kwa ajili ya Mradi wa Kinyerezi I na Shilingi bilioni 109.9, sawa na Dola za Marekani milioni 68.69 zimetengwa kwa ajili ya Mradi wa Kinyerezi II. Serikali itakamilisha ujenzi wa mitambo, kituo cha kupoozea umeme (*sub-station 220kV*) na njia ya kusafirisha umeme (*kV 220*) kutoka eneo la mradi na kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa eneo la Kimara na njia nyingine (*kV 132*) kwenda kwenye kituo cha Gongo la Mboto kwa ajili ya matumizi ya Mkoa wa Dar es Salaam. Miradi hii iko kwenye michoro, ile michoro lazima mkaichukue imewekwa humo, sisomi hapa tu iko kwenye michoro vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kinyerezi III (*MW 300*) na Kinyerezi IV (*MW 300).* Mradi wa Kinyerezi III unahusisha ujenzi wa mtambo wa kufua umeme wa *MW 300* kwa kutumia gesi asilia. Mradi huu utatekelezwa kwa ubia kati ya Serikali

kupitia *TANESCO* na sekta binafsi. Katika kipindi cha Mwaka 2013/2014, Serikali itakamilisha majadiliano na kampuni ya ubia kwa ajili ya kutekeleza mradi huo. Mradi huo unatarajiwa kukamilika Mwaka 2015/2016. Mradi huu utagharimu takriban Dola za Marekani milioni 389, sawa na shilingi bilioni 662.4.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Kinyerezi IV unahusisha ujenzi wa mtambo wa kufua umeme wa MW 300 kwa kutumia gesi asilia na njia ya kusafirisha umeme ya *kV 400* kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma kupitia Morogoro. Serikali itakamilisha majadiliano na Mbia kutoka sekta binafsi kwa ajili ya kutekeleza mradi huo unaotarajiwa kukamilika mwaka 2015/2016. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 800, sawa na shilingi bilioni 1,280.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wote mnaonisikiliza na Waheshimiwa Wabunge, mnaona kiasi cha fedha kinachohitajika kuwekeza kwenye miradi ya nishati. Yeyote asikupotoshe akasema Serikali inao uwezo wa kufanya hivyo, ni lazima sekta ya watu binafsi itumike na kutumia mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Somanga Fungu MW 320. Huu ni mradi wa mtu binafsi, *Kilwa Energy*. Kazi zitakazofanyika katika mradi huo kwa Mwaka 2013/2014 ni pamoja na kukamilisha mkataba wa utekelezaji, kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi na kuanza ujenzi. Awamu ya kwanza ya mradi huo itaanza na ufuaji wa *MW 230* kwa kutumia gesi asilia. Mradi utakamilika mwaka 2015/2016 na utagharimu jumla ya Dola za Marekani milioni 365, sawa na shilingi bilioni 564. Somanga Fungu iko katika Wilaya ya Lindi. Hiki ni kithibitisho kingine kwamba miradi inafanyika huko.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuzalisha *MW 400* Mkoani Mtwara. Katika kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya umeme katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma, Serikali kupitia *TANESCO* imeingia mkataba na Kampuni ya *Symbion Tanzania Limited* kwa ajili ya kujenga mtambo wa kufua umeme wa *MW 400* Mkoani Mtwara. Hizi taarifa kama watu

wa Mtwara hamtaki kuzikubali, Serikali ya Marekani inazo *White House*. Njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa *kV 400* kuanzia Mtwara hadi Songea itajengwa ikiwa ni sehemu ya mradi huo. Vyote hivi mtavipata kwenye vijitabu. Umeme utakaofuliwa utatumika katika mikoa ya kusini na ziada itaingizwa kwenye Gridi ya Taifa pamoja na kuuzwa Msumbiji na Malawi. Kutekelezwa kwa mradi huu, kutaongeza fursa za ajira kwa wakazi wa mikoa ya kusini kutokana na kuongezeka kwa uwekezaji kwenye sekta za viwanda na kilimo. Maandalizi ya Mradi yameanza kwa Kampuni ya Symbion kuanza kufanya upembuzi yakinifu na baadaye kuandaa gharama ya mradi husika.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Rusumo wa *MW 80*. Katika mwaka 2013/2014, kazi zitakazofanyika ni pamoja na kukamilisha upembuzi yakinifu kwenye eneo ambapo bwawa la kuzalisha umeme litajengwa; kuanzisha chombo cha kusimamia utekelezaji wa mradi (*Special Purpose Vehicle - SPV*); na kuingia mikataba ya kuuziana umeme kati ya *SPV* na mashirika ya umeme katika nchi husika. Mradi huo unatekelezwa kwa ushirikiano baina ya nchi tatu za Burundi, Rwanda na Tanzania ambapo mchango wa Tanzania ni Dola za Marekani milioni 28, sawa na Shilingi bilioni 44. Katika Mwaka 2013/14, Shilingi bilioni 22 sawa na Dola za Marekani milioni 13.75 zimetengwa ikiwa ni mchango wa Tanzania kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Murongo/Kikagati *MW 16*. Katika mwaka 2013/2014, Serikali ya Tanzania na Uganda zitakamilisha mkataba wa ushirikiano (*Bilateral Agreement)* ili kuwezesha mradi huo kuanza kutekelezwa. Mradi huo unagharimu Dola za Marekani milioni 30.46, sawa na shilingi bilioni 48.74. Mradi utatekelezwa na mwekezaji binafsi *Trond Energy* kutoka Norway na umepangwa kukamilika mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, mradi wa ufuaji na usambazaji wa umeme – Biharamulo, Mpanda na Ngara. Kufuatia kukamilika kwa tathmini ya zabuni, ufungaji wa jenereta za kufua umeme wa MW 2.5 na usambazaji wa umeme katika

maeneo ya Biharamulo, Mpanda na Ngara utaanza Mwaka 2013/2014. Mradi huo unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Uholanzi kwa gharama ya Euro milioni 33, sawa na shilingi bilioni 66. Katika mwaka 2013/2014, Serikali imetenga shilingi bilioni 2.1 kwa ajili ya utekelezaji na mradi utakamilika mwaka 2014. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa mitambo katika Vituo vya Kufua Umeme. Katika kuimarisha vituo vya kufua umeme nchini kwa mwaka 2013/2014, mitambo ya kituo cha kuzalisha umeme cha Hale kinachotumia nguvu za maji itakarabatiwa kwa ufadhili wa Serikali za Tanzania na Sweden. Mwaka 2013/2014, kazi zilizopangwa kufanyika ni hizi zifuatazo: kumpata mshauri wa mradi, usanifu wa mradi na kuanza taratibu za kuwapata wazabuni mbalimbali wa mradi. Mradi huo umetengewa shilingi bilioni 8.93 sawa na Dola za Marekani milioni 5.58 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha njia za kusafirisha na kusambaza umeme. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea kuimarisha njia za kusafirisha na kusambaza umeme. Lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika na kupunguza upotevu wa umeme kutoka asilimia 21 ya sasa hadi kufikia asilimia 15 mwaka 2015/16. Kazi hii itafanyika kupitia miradi mbalimbali ikiwemo:

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa huduma za umeme Jijini Dar es Salaam. Katika mwaka 2013/14, Serikali kupitia *TANESCO* itaanza usanifu wa maeneo yatakayohusika na mradi, ununuzi wa vifaa, ujenzi na mafunzo kwa watumishi wa *TANESCO* watakaohusika na mradi huo. Jumla ya shilingi bilioni 19.85 sawa na Dola za Marekani milioni 12.41 zitatolewa na Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Tanzania *Energy Development and Access Expansion Project (TEDAP)* na Serikali ya Finland ili kutekeleza mradi huo. Mradi huo utakamilika mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Makambako – Songea *kV 220*. Kufuatia kukamilika kwa durusu ya kuongeza uwezo

wa njia ya umeme kutoka *kV 132* hadi *kV 220*, katika mwaka 2013/2014, Serikali kupitia *TANESCO* itafanya tathmini ya mali zilizoko ndani ya njia kuu ya kusafirisha umeme kwa mara ya pili; kulipa fidia; kusafisha njia kuu ya umeme yenye umbali wa kilometa 250 pamoja na viwanja vitakapojengwa vituo vya kupozea umeme eneo la Madaba na Songea; na kumpata mkandarasi wa mradi. Katika mwaka 2013/2014, jumla ya shilingi bilioni 12.58, sawa na Dola za Marekani milioni 7.86 zimetengwa ambapo fedha za ndani ni Shilingi bilioni 2, sawa na Dola za Marekani milioni 1.25 na fedha za nje zitakazotolewa na Shirika la Maendeleo la Sweden ni Shilingi bilioni 10.58 sawa na Dola za Marekani milioni 6.61. Mradi huu utakapokamilika, utawezesha Mkoa wa Ruvuma kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa na kuimarisha usambazaji wa umeme katika Miji ya Makambako, Njombe, Songea na Wilaya za Ludewa, Mbinga na Namtumbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi wa Iringa – Shinyanga *kV 400*. Kazi zitakazotekelezwa katika mwaka 2013/2014 ni pamoja na: ukamilishaji wa zabuni za kuwapata wakandarasi wa kujenga njia ya umeme msongo wa *kV 400* katika vipande vitatu (3) vya Iringa – Dodoma, Dodoma – Singida na Singida – Shinyanga; maandalizi ya kuongeza uwezo wa vituo vya kupozea umeme katika Mikoa ya Dodoma, Iringa, Shinyanga na Singida; na kuhamisha miundombinu ya huduma za kijamii. Katika Mwaka 2013/2014, shilingi bilioni 5.44, sawa na Dola za Marekani milioni 3.4 zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo, ambapo Shilingi milioni 440, sawa na Dola za Marekani 275,000 ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 5, sawa na Dola za Marekani milioni 3.13 ni za nje. Mradi huo utakamilika mwaka 2015/16.

Mheshimiwa Spika, mradi wa *North – West* na *North – East Grid kV 400*. Katika mwaka 2013/2014, Serikali kupitia *TANESCO* itasanifu upya mradi huo kutoka *kV 220* kwenda *kV 400*. Shilingi milioni 560, sawa na Dola za Marekani 350,000 zimetengwa kwa ajili ya kudurusu usanifu wa mradi huo. Mradi umeombewa fedha kutoka Serikali ya China kama mradi wa kipaumbele. Ni mradi muhimu ambao utawezesha nchi

yetu kuwa na Gridi kubwa yenye kusafirisha umeme mwingi. Mikoa ya Magharibi mwa nchi yetu itapata umeme mwingi na wa uhakika kupitia Gridi hii.

Mheshimiwa Spika, mradi wa *North – East Grid* unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya Dar es Salaam – Chalinze – Tanga – Same hadi Arusha katika msongo wa *kV 400.* Mradi wa *North –West Grid* utakaohusisha ujenzi wa njia ya *kV 400* kutoka Nyakanazi – Kigoma – Katavi – Rukwa hadi Mbeya. Awamu ya kwanza itahusisha ujenzi wa njia kutoka Mbeya hadi Sumbawanga ambao utagharimu takriban Dola za Marekani milioni 136.25, sawa na Shilingi bilioni 218. Mradi wa North – East Gridi utagharimu Dola za Marekani milioni 770, sawa na Shilingi bilioni 1,232. Hata hivyo, baada ya msongo wa njia za umeme za miradi hiyo ya kubadilisha kutoka *kV 220* hadi *kV 400*, Serikali inapanga kuhuisha Upembuzi Yakinifu uliopo sasa (*updating Feasibility Study*) ili kupata gharama halisi za miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea na juhudi za kutafuta fedha ili kutekeleza miradi ya *North – West* na *North – East Grid*, ambayo ni miongoni mwa miradi ya Kitaifa ya kipaumbele iliyobainishwa kuleta matokeo makubwa na ya haraka (*Big Results Now*). Miradi hiyo imepangwa kukamilika Mwaka 2015/2016. Miradi hii na yenyewe itatekelezwa na tuko kwenye majadiliano na wenzetu wawekezaji na tutawaarifu tutakapofika tamati ya majadiliano yetu.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa njia za kusafirisha umeme kutoka Mtwara - Songea na Mtwara – Lindi – Somanga Fungu *(kV 220).* Ili kuiwezesha Mikoa ya Kusini kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa, Serikali itasimamia ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha umeme kutoka Mtwara hadi Songea na Mtwara hadi Somanga Fungu (Lindi). Hadi sasa, *TANESCO* wameingia makubaliano *(MoU)* na Kampuni ya *M/S Symbion Power LLC.* Miradi hii ikikamilika itaibua fursa mbali mbali za kiuchumi katika mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Singida – Arusha –

Namanga *kV 400.* Katika mwaka 2013/2014, kazi zilizopangwa kufanyika katika mradi huu ni kumpata mshauri kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Mradi huo unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika pamoja na Benki ya Dunia. Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme yenye urefu wa kilomita 414.4 katika msongo wa *kV 400* kuanzia Singida kupitia Babati na Arusha hadi Namanga, pamoja na vituo viwili vya kupozea umeme. Aidha, mradi unahusisha upelekaji umeme katika vijiji vilivyo kando kando ya njia hiyo ya umeme. Gharama ya mradi ni Dola za Marekani milioni 242.09, 93 sawa na Shilingi bilioni 387.34 na lengo ni kuukamilisha ifikapo Mwaka 2017. Mradi huu ni miongoni mwa miradi ya vipaumbele (*Big Results Now).*

Mheshimiwa Spika, mradi wa *Electricity* V. Serikali imekusudia kuendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme nchini. Mradi wa *Electricity V* unakusudia kuongeza usambazaji umeme vijijini pamoja na upanuzi wa vituo vya kupozea umeme katika Mikoa ya Arusha na Dar es Salaam. Serikali imepata mkopo toka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) wa Dola za Marekani milioni 45, sawa na shilingi bilioni 72. Mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili kubwa, (i) ujenzi wa njia za usambazaji umeme vijijini katika Mikoa ya Geita, Mwanza na Simiyu. Wilaya zitakazofaidika na mradi huu ni Bukombe na Mbogwe (Geita), Busega (Simiyu), Kwimba, Magu, Misungwi na Sengerema (Mwanza). Mkandarasi wa ujenzi wa njia hizi ni *M/S Eitel Networks TE AB* kutoka Sweden na ataanza kazi Mwezi Juni, 2013. Gharama za mradi ni Dola za Marekani milioni 19.2, sawa na shilingi bilioni 30.72.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili linahusu upanuzi wa vituo vya kupozea umeme katika Mikoa ya Arusha na Dar es Salaam. Kituo cha Sokoine cha Dar es Salaam kitajengwa upya na pia kituo cha Ilala kitawekewa transfoma mpya yenye uwezo wa *15 MVA*. Aidha, katika Jiji la Arusha kituo cha kupozea umeme cha Njiro kitawekewa transfoma mbili za kupozea umeme zenye ukubwa wa *50 MVA* kila moja na zitawekwa kwenye msongo wa Kilovolti 132/33. Gharama

za mradi huu ni Dola za Marekani milioni 7.3, sawa na Shilingi bilioni 11.68.

Mheshimiwa Spika, kupeleka umeme Makao Mkuu ya Wilaya na Vijijini. Serikali kupitia *REA* itawezesha utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango Kabambe wa kusambaza umeme vijijini. Mpango huo utajumuisha kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya 13 za Buhigwe, Busega, Chemba, Itilima, Kakonko, Kalambo, Kyerwa, Mkalama, Mlele, Momba, Nanyumbu, Nyasa na Uvinza pamoja na maeneo mengine ya vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, shilingi bilioni 150 sawa na Dola za Marekani milioni 93.75 zimetengwa ambapo fedha za ndani ni shilingi bilioni 90, sawa na Dola za Marekani milioni 56.25 na fedha za nje ni shilingi bilioni 60 sawa na Dola za Marekani milioni 37.5. Aidha, *REA* inategemea kupata shilingi bilioni 36, sawa na Dola za Marekani milioni 22.5 kutokana na asilimia tatu (3%) ya tozo ya mauzo ya umeme na asilimia 0.4 ya *TRA pre- destination inspection fee on imported petroleum products*. Aidha, gharama za kutekeleza awamu ya pili ya Mpango Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini ni shilingi bilioni 881, sawa na Dola za Marekani milioni 550.63.95. Mahesabu yetu yanatuambia kwamba kwenye bajeti hii tukipata shilingi bilioni 450, hali itakuwa ni nzuri na wanavijiji wetu wengi watapata umeme.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *REA* pia itaanza kutekeleza mradi wa majaribio wa gharama nafuu za miundombinu ya kusambaza umeme (*Low Cost Design Standards)* katika Mikoa ya Mbeya na Morogoro utakaounganisha jumla ya wateja 15,000 wa awali na idadi ya wateja inategemewa kuongezeka na kufikia zaidi ya 20,000.

Mheshimiwa Spika, *REA* itaendelea kuwezesha utoaji wa mafunzo na usaidizi wa kitalaam kwa wajasiriamali wa nishati na waendelezaji wa vyanzo mbalimbali vya nishati bora. Aidha, Wakala utawezesha utekelezaji wa miradi

inayofadhiliwa na *Global Village Energy Partnership Program (GVEP).* Katika miradi hiyo, vyanzo sita vya kuzalisha umeme wa maporomoko madogo ya maji vitaendelezwa. Vyanzo hivyo ni Darakuta (Babati), Lingatunda (Songea Vijijini), Luswisi (Ileje), Macheke (Ludewa), Mwoga (Kasulu), na Nole-Ihalula (Njombe). Kwa ujumla vyanzo hivi vitakuwa na uwezo wa kuzalisha jumla ya Megawati 9.1 na hivyo kuwezesha kuunganisha jumla ya wateja 27,600. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi hiyo ni Shilingi bilioni 2 sawa na Dola za Marekani milioni 1.25.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Tanzania *Energy Development and Access Expansion Project (TEDAP)* Unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Katika kipindi cha Mwaka 2013/14, Serikali kupitia mradi wa *TEDAP off - grid* itaendelea kusimamia utekelezaji wa mradi huu ikiwemo: kukagua mifumo ya umeme wa jua iliyofungwa; kuhamasisha matumizi ya nishati bora; kufunga mifumo ya umeme jua kwenye vituo vya huduma za jamii Sumbawanga na kuwezesha kuanza utekelezaji katika Mikoa ya Kagera, Kigoma, Ruvuma, Shinyanga na Tabora. Aidha, waendelezaji wa miradi midogo ya kufua umeme wataendelea kukamilisha miradi yao chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia na *Global Environment Facility (GEF)* kupitia ruzuku na mikopo yenye masharti nafuu. Gharama ya sehemu hii ya mradi (*off – grid*) ni Dola za Marekani milioni 22.5, sawa na shilingi bilioni 35.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza mradi wa *TEDAP (on-grid),* ambapo itakamilisha ujenzi wa kituo cha *KIA* cha kupozea umeme wa *kV 132/33* kwa kuongeza transfoma moja yenye uwezo wa M*VA* 20 na upanuzi wa kituo cha Kipawa kwa kuongeza transfoma mbili zenye uwezo wa MVA 90 kila moja. Aidha, ujenzi wa njia za usafirishaji za msongo wa *kV 132* kutoka Ubungo hadi Kurasini, Kurasini hadi Mbagala na Kipawa hadi Gongo la Mboto utaendelea, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa kituo cha kupozea umeme cha Gongo la Mboto kV 132/33, mbili zenye uwezo wa MVA 45. Gharama ya sehemu hii ya mradi (*on – grid*) ni Dola za Marekani milioni 89, sawa na Shilingi bilioni 142.4.

Mheshimiwa Spika, Sekta Ndogo ya Nishati Jadidifu. Usimamizi wa *Bio-energy*. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itawasilisha kwa wadau Rasimu ya Sheria ya *Bio-energy* ili kupata maoni. Aidha, Mshauri wa kuainisha maeneo maalum *(agro-ecological zoning)* ya uendelezaji wa maeneo ya mimea ya *bio-energy* atapatikana ifikapo Mwaka 2013/2014. Serikali pia itajenga uwezo kwa Taasisi zake na Halmashauri za Wilaya, vyombo vya fedha, wakulima, Taasisi zisizo za Kiserikali ili kuweza kusimamia kikamilifu masuala ya *bio-energy*. Katika mwaka 2013/2014, shilingi bilioni moja, sawa na Dola za Marekani 625,000 zitatolewa na *NORAD* (Norway) na Sida (Sweden) kwa ajili ya kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa Tungamotaka *(Biomass).* Serikali itaandaa Mkakati wa Nishati ya Tungamotaka (*Biomass Energy Strategy*) nchini ambao utatoa mwongozo wa upatikanaji, usimamizi na matumizi bora ya tungamotaka. Kazi hii inatekelezwa na mshauri, Kampuni ya *CAMCO (T).* Aidha, Serikali itafanya tathmini ya miradi ya tungamotaka inayotekelezwa na taasisi na kampuni binafsi kama vile Katani Ltd (kW 300), Sao Hill (MW 15), Tanzania *Planting Company - TPC* (MW 20) na *Tanzania Wattle Company – TANWAT (MW* 2.5). Lengo la tathmini hiyo ni kubaini namna bora ya kuendeleza matumizi ya tungamotaka kama chanzo cha nishati. *TANESCO* inanunua umeme kiasi cha MW 12 kutoka Kampuni za *TANWAT* na TPC. Katika mwaka 2013/2014, shilingi milioni 500, sawa na Dola za Marekani 312,500 zitatolewa na Umoja wa Ulaya (EU) kwa ajili ya mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kuendeleza vyanzo vya Nishati Jadidifu. Mradi wa *Low Carbon Efficient Sustainable Energy Access.* Katika mwaka 2013/2014, kazi zilizopangwa kutekelezwa chini ya mradi huu ni pamoja na: kuandaa tathmini ya mahitaji na upatikanaji wa nishati jadidifu; kuanzisha miradi ya nishati jadidifu; na kujenga uelewa kwa Halmashauri za Wilaya 10 zilizochaguliwa kushiriki katika mradi huu ambazo ni Geita, Kahama, Kasulu, Kwimba, Mbinga, Mbulu, Misenyi, Mpanda, Ngorongoro na Urambo. Miradi hiyo ni ya nishati ya umeme utokanao na jua, upepo, maporomoko madogo ya maji na tungamotaka. Jumla ya

Shilingi bilioni 1.6, sawa na Dola za Marekani milioni moja (1) zitatolewa na *UNDP* kwa mwaka 2013/2014 kwa ajili ya mradi huo.

Mheshimiwa Spika, mradi wa *Biogas*. Wizara kwa kushirikiana na Kituo cha uendelezaji wa Zana za Kilimo na Teknolojia za Vijijini *(CAMARTEC)* kilichopo Arusha itaendelea kusimamia utekelezaji wa mradi wa biogas chini ya programu ya uendelezaji biogas ngazi ya kaya *(Tanzania Domestic Biogas Programme*). Mitambo 12,000 inatarajiwa kujengwa katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Manyara, Mbeya, Pwani, Ruvuma, Singida na Tanga. Mradi huu unafadhiliwa na Shirika lisilo la Kiserikali la Uholanzi liitwalo *HIVOS*, na utakamilika Mwaka 2014/15. Gharama za mradi huu ni takribani Shilingi bilioni 30, sawa na Dola za Marekani 18.75.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa Jotoardhi (*Geothermal*) na Mpango wa *Scaling up Renewable Energy (SREP).* Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo wakiwemo *AfDB, BGR, DFID, ICEIDA, IFC JICA, UNEP, USAID* na *WB* wamekubaliana kushiriki katika kuendeleza joto ardhi hapa nchini. Katika Mwaka 2013/14, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kufanya utafiti wa kina wa kijiolojia, kijiokemia na kijiofizikia katika maeneo matano yaliyopo Kisaki (Morogoro), Luhoi (Pwani), Majimoto (Musoma), Ziwa Manyara (Manyara) na Ziwa Natron (Arusha).

Mheshimiwa Spika, matumizi bora ya nishati (*Energy Conservation and Efficiency).* Matumizi bora ya nishati ni muhimu ili kupunguza upotevu wa nishati, kuokoa fedha na kulinda mazingira. Miongoni mwa hatua zitakazochukuliwa kwa ajili ya matumizi bora ya nishati ni kubadili taa zinazotumia umeme mwingi *(Incandescent Bulbs)* na kuweka zinazotumia umeme kidogo *(Compact Florescent Light - CFL).* Kwa kuanzia, zoezi hili litahusisha mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro na Mwanza, ambapo jumla ya taa milioni 3.2 zitabadilishwa kwa gharama ya Shilingi bilioni 24, sawa na Dola za Marekani milioni 15.

Mheshimiwa Spika, Sekta Ndogo za Gesi Asilia na Mafuta. Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Gesi Asilia kutoka Mtwara – Dar es Salaam. Katika mwaka 2013/2014, Serikali kupitia *TPDC* itaendelea kusimamia utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: ujenzi wa mitambo miwili ya kusafisha gesi asilia katika maeneo ya Songo Songo (Lindi) na Mnazi Bay (Mtwara). Kwa hiyo, sio kweli kwamba gesi chafu inasafirishwa, inasafishwa huko huko Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine ni ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka Lindi na Mtwara hadi Dar es Salaam; ujenzi wa vituo vya kupokelea gesi asilia Somanga Fungu, Kinyerezi na Tegeta; ujenzi wa ofisi na kambi za wafanyakazi wa mradi; na ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme kwa ajili ya kuendeshea mitambo ya kusafishia gesi asilia. Katika mwaka 2013/2014, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 63, sawa na Dola za Marekani milioni 39.4 kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo. Fedha hizo zitatumika kulipia sehemu ya mchango wa Serikali katika mkopo wa Bomba la Gesi Asilia.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia itahakikisha kuwa Vijiji vilivyopo kandokando na mkuza wa Bomba la Gesi Asilia vinanufaika na mradi huo. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali kupitia *REA* itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme katika vijiji hivyo kutoka Mtwara hadi Lindi. Kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na kupata Mshauri wa kufanya tathmini na kuvitambua vijiji vitakavyohusika; kutayarisha na kutangaza zabuni za ujenzi; na kuanza ujenzi wa miundombinu. Katika mwaka 2013/2014, kiasi cha shilingi bilioni 20, sawa na Dola za Marekani milioni 12.5 kimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, utafutaji wa Gesi Asilia na Mafuta. Serikali kupitia *TPDC* itaendelea kusimamia shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika maeneo mbalimbali nchini kulingana na mikataba ya makampuni iliyoingia na Serikali. Jumla ya visima 17 vinatarajiwa kuchimbwa katika kipindi cha mwaka 2013/2014. Visima hivyo vitachimbwa na

Kampuni za *Afren, BG, Dodsal, Dominion, Heritage, Hydro Tanz, Maurel & Prom, Ndovu Resource, Ophir, Pan African na Statoil.* Wastani wa gharama za kuchimba kisima kimoja ni kati ya Dola za Marekani milioni 40 na milioni 100 sawa na shilingi bilioni 64 na bilioni 160 sawia.

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu niwakumbushe kwamba Shirika la Mafuta la Petroli lilianzishwa mwaka 1969 na aliyelianzisha ni Mwalimu Nyerere. Sheria ya Mafuta ya mwaka 1900 aliyekuwa Rais anaisimamia ni Mwalimu Nyerere. Kweli alipotoka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza uwekezaji, Serikali ilipanga kutangaza na kunadi maeneo mapya ya utafutaji wa mafuta na gesi nchini Marekani Mwezi Septemba, 2012. Hata hivyo, ili kuhakikisha mikataba mipya yote inafuata Sera na Sheria husika, tuliamua kusitisha hadi tuwe na Sera na Sheria. Kwa mwaka 2013/14, Serikali imeamua kwamba zabuni ya awamu ya nne ya kunadi maeneo mapya ya uwekezaji (*Fourth Off-shore Licensing Round*) katika kina kirefu cha bahari ifanyike hapa nchini tarehe 25 Oktoba, 2013 Jijini Dar es Salaam. Hii itakuwa ni mara ya kwanza kabisa kwa zoezi la kunadi maeneo mapya ya uwekezaji katika utafutaji wa mafuta kufanyika nchini. Pamoja na faida nyinginezo, zoezi hili kufanyika nchini litakuwa ni fursa muhimu kwa sisi wenyewe kuitangaza nchi yetu.

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Bado dakika tano?

**SPIKA:** Ndio una dakika tano tu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Kusimamia na Kudhibiti Biashara ya Mafuta. Katika mwaka 2013/2014, Serikali kupitia *EWURA*, itaendelea kuimarisha udhibiti wa biashara ya mafuta hapa nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, *EWURA* itahakikisha kuwa: miundombinu inayohusiana na biashara ya mafuta inajengwa na kutunzwa kulingana na Sheria ya *EWURA* ya mwaka 2001 na Sheria ya

Mafuta ya Mwaka 2008; mafuta yanaagizwa na kuuzwa nchini kwa kuzingatia mwenendo wa bei katika soko la Dunia; na kuhakikisha usawa wa mazingira ya ushindani (*level playing field*) katika biashara ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, Sera, Mipango na Sheria katika Sekta ya Nishati. Katika Mwaka 2013/2014, Serikali itakusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali ili kuboresha durusu ya Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2003. Vilevile, Serikali itakamilisha Sera ya Petroli ambayo itatoa miongozo kuhusu shughuli za utafutaji na uendelezaji wa Sekta ndogo za Mafuta na Gesi Asilia *(Upstream Petroleum Policy).*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sera ya Gesi Asilia utaanza katika Mwaka 2013/2014, baada ya Serikali kutoa uamuzi. Aidha, Wizara itakamilisha Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia nchini ifikapo Juni, 2014. Katika mwaka 2013/2014, Serikali pia itawasilisha Sheria ya Gesi Asilia katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Taasisi, Mashirika na Kampuni katika Sekta ya Nishati. Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*). Serikali imeamua kupitia upya muundo wa *TANESCO* ili kuongeza ufanisi na kuongeza ushindani katika Sekta Ndogo ya Umeme kwa lengo la kuboresha huduma za umeme nchini. Wizara imepokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali wakiwemo wananchi na inatarajia kupokea mapendekezo ya muundo kutoka Menejimenti na Bodi ya *TANESCO* ifikapo tarehe 31 Mei, 2013.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) imetoa fedha (*Grant*) za kumpata Mshauri ambaye atatoa mapendekezo juu ya Muundo Mpya wa *TANESCO* unaofaa kufikiriwa na Serikali. Benki hiyo pia, imekubali kutoa fedha za kujenga uwezo wa watendaji wa Wizara, *TANESCO* na *TPDC*. Baada ya kupokea mapendekezo kutoka vyanzo mbalimbali, Wizara itaandaa Mwongozo (*Road Map*) wa namna bora ya kubadilisha muundo wa *TANESCO* na Sekta Ndogo ya Umeme. Mwongozo umepangwa kukamilika Mwezi Juni, 2014.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC).* Kutokana na kuongezeka kwa shughuli za utafutaji mafuta na uendelezaji wa matumizi ya gesi asilia, Serikali inapitia upya muundo wa TPDC ili kuongeza ufanisi kwa kuanzisha kampuni tanzu za Shirika hilo. Kampuni tanzu zitahusika na shughuli za usafirishaji na usambazaji wa gesi asilia, na mafuta nchini. Menejimenti na Bodi ya TPDC zimeagizwa kuwasilisha mapendekezo ya muundo mpya wa Shirika hilo ifikapo tarehe 30 Mei, 2013. Aidha, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imetoa fedha (*Grant*) kumpata Mshauri ambaye atatoa mapendekezo juu ya Muundo Mpya wa *TPDC* unaofaa kufikiriwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa Serikali katika Kampuni za *TIPER*, Puma *Energy Ltd* na *TAZAMA.* Katika mwaka 2013/2014, Serikali kupitia Wizara itaendelea kushiriki kikamilifu katika shughuli za uendeshaji wa Kampuni ambazo Serikali ina hisa za Puma *Energy Limited* (hisa za Serikali ni asilimia 50), Tanzania *Zambia Pipeline Limited - TAZAMA* (hisa za Serikali ni asilimia 30) na Tanzania *International Petroleum Reserve - TIPER* (hisa za Serikali ni asilimia 50).

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini. Kwa mwaka 2013/2014, kazi zilizopangwa kutekelezwa katika Sekta ya Madini ni pamoja na kuboresha utoaji na usimamizi wa leseni za madini; kuendeleza uchimbaji mdogo wa madini; kuongeza idadi ya wachimbaji wadogo (ajira); kuendelea kuvutia wawekezaji wakubwa; kuimarisha makusanyo ya maduhuli yatokanayo na madini; kuimarisha usimamizi wa afya, usalama na utunzaji wa mazingira migodini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kuimarisha usimamizi wa biashara ya madini; kuwezesha Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara; na kujenga ofisi za madini Dodoma, Mpanda na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Kuboresha Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini; katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuboresha Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni (*MCIMS*) ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya kuwawezesha waombaji kuwasilisha maombi kwa njia ya mtandao wa

intaneti (*online*). Wizara pia itaendelea kushughulikia maombi ya leseni kwa wakati na itahakikisha kuwa maombi yote yaliyowasilishwa kabla ya tarehe 31 Desemba, 2012 yanashughulikiwa na kujibiwa ifikapo mwishoni mwa Mwezi Septemba, 2013. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kwa kufuta leseni zote zinazokiuka matakwa ya Sheria hiyo ili kutoa nafasi kwa wawekezaji wengine wenye uwezo wa kuyaendeleza.

Mheshimiwa Spika, Kuendeleza Uchimbaji Mdogo wa Madini. Wizara kupitia *STAMICO, GST, MRI, TMAA* na kwa kushirikiana na *SIDO, VETA* na Chuo Kikuu ca Dar es Salaam (UDSM) itaendelea kutekeleza mpango wa mafunzo kwa nadharia na vitendo kwa wachimbaji wadogo. Katika Mwaka 2013/2014, mikopo kwa wachimbaji wadogo itatolewa kupitia Benki ya *TIB* badala ya utaratibu wa awali wa kukopesha na kukodisha vifaa vya uchimbaji katika vituo maalum vilivyoanzishwa. Utaratibu huu utarahisisha ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo na kuongeza idadi ya wakopaji. Vifaa vya uchimbaji vya kukodisha vitasimamiwa na *STAMICO*. Aidha, Wizara itaendelea kutenga maeneo ya uchimbaji kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, Kuongeza Idadi ya Wachimbaji Wadogo (Ajira). Wizara itaendelea kutenga maeneo kwa ajili ya uchimbaji mdogo. Maeneo 10 yanatarajiwa kutengwa katika sehemu mbalimbali nchini kwa ajili ya wachimbaji wadogo kwa Mwaka 2013/2014. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu ya ugani kwa wachimbaji wadogo ili kuwawezesha kufanya shughuli za utafutaji, uchimbaji na uchenjuaji mbale *(ore)* kwa tija na ufanisi zaidi. Juhudi hizo zitaongeza ajira kwa Watanzania na kuinua kipato chao.

Mheshimiwa Spika, Kuimarisha Makusanyo ya Maduhuli yatokanayo na Madini. Wizara itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na madini ambapo kwa Mwaka 2013/2014, lengo ni kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 199.96, ikiwa ni ongezeko la asilimia 15.12 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 173.70 zilizopangwa kukusanywa kwa Mwaka 2012/2013. Lengo hilo litafikiwa kwa kuimarisha ufuatiliaji wa

maduhuli hayo kupitia Ofisi za Madini za Kanda. Pia, shughuli za ukaguzi kupitia *TMAA* zitachangia kwa kiasi kikubwa kufikiwa kwa lengo hilo. Nitoe agizo kwa wamiliki wa leseni za madini kuacha mchezo wa kukwepa kulipa kodi na mrabaha stahiki. Wale watakaobainika, Serikali haitasita kuwachukulia hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kufuta leseni zao.

Mheshimiwa Spika, Kuimarisha Usimamizi wa Afya, Usalama na Utunzaji wa Mazingira Migodini. Wizara itaendelea kusimamia Sheria zinazohusu Afya, Usalama na Utunzaji wa Mazingira migodini kwa kuimarisha ukaguzi katika migodi mikubwa, ya kati na midogo. Aidha, Wizara itakamilisha hatua ya pili ya mipango ya ufungaji migodi *(mine closure plans)* ya Bulyanhulu, Buzwagi, Golden Pride, North Mara na Tulawaka kwa kuhakikisha kuwa migodi hiyo inaweka hatifungani *(Rehabilitation Bond)* kwa ajili ya ukarabati wa mazingira. Vilevile, Wizara itakamilisha mipango ya ufungaji migodi kwa migodi ya Geita *Gold Mine*, *TanzaniteOne* na *Williamson Diamonds Limited*. Aidha, Serikali itasimamia taratibu za eneo la Mgodi wa Golden Pride, Nzega kukabidhiwa kwa Chuo cha Madini, Dodoma na Mgodi wa Tulawaka, Biharamulo kukabidhiwa kwa STAMICO pindi migodi hiyo itakapofungwa rasmi.

Mheshimiwa Spika, Kuendelea Kuvutia Wawekezaji Wakubwa. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea kuvutia mitaji na teknolojia inayohitajika kuendeleza Sekta ya Madini. Kazi hii itafanyika kwa kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji katika Sekta ya Madini, kushiriki kwenye warsha na maonesho ya ndani na nje ya nchi yanayokutanisha wawekezaji katika Sekta ya Madini, kutoa taarifa za kijiolojia kupitia *GST* zinazohitajika katika shughuli za utafutaji wa madini, kutoa leseni za madini kwa wakati kwa waombaji watakaotimiza masharti ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini. Katika kipindi cha Mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za uongezaji thamani madini nchini na kutoa leseni

za uchenjuaji na uyeyushaji wa madini ya metali ikiwemo shaba. Aidha, Wizara itakamilisha Sheria ya Uongezaji Thamani Madini ili kukuza na kusimamia vyema shughuli za uongezaji thamani kwa lengo la kuongeza mapato na ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kukiimarisha Kituo cha Usanifu wa Vito cha Arusha kwa kukamilisha ukarabati wa majengo yake; kukipatia mashine za ukataji, usanifu na utengenezaji mapambo ya vito; kuandaa Mpango Kazi wa Kituo na mitaala ya kufundishia pamoja na kupatikana Wakufunzi wenye sifa stahiki.

Mheshimiwa Spika, Kuimarisha Usimamizi wa Biashara ya Madini. Katika kuimarisha usimamizi wa biashara ya madini nchini, Serikali kupitia Wakala wa Ukaguzi wa Madini (*TMAA*) itaendelea kuimarisha madawati maalum ya kukagua madini yanayosafirishwa nje ya nchi kupitia Viwanja vya Ndege vya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Mwanza. Nitoe wito kwa watendaji wote wa Serikali katika viwanja hivyo kuhakikisha wanatoa ushirikiano kwa *TMAA* katika kuwabaini na kuwakamata wote wanaojihusisha na utoroshaji wa madini. Pia, niwasihi wale wote wanaojihusisha au kufikiria kutorosha madini, kuacha mara moja kufanya hivyo kwani wakipatikana watachukuliwa hatua kali za kisheria bila huruma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea kuboresha Kitengo cha Utambuzi na Ukadiriaji Thamani Almasi na Madini ya Vito (*TANSORT*), ili kiweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo ikiwa ni pamoja na kutoa huduma ya ushauri wa masoko, ukataji na ukadiriaji thamani madini ya vito kwa wachimbaji wadogo na wa kati; kutoa huduma za kijemolojia *(Gemmological Services)* kwa wachimbaji wadogo na wa kati; kusimamia mauzo ya almasi na madini ya vito ndani na nje ya nchi; na kuthaminisha almasi na madini ya vito kwa ajili ya kukokotoa mrabaha. Aidha, Serikali itaendelea kujenga uwezo wa Kitengo hiki ili kiweze kutoa huduma kwa Watanzania wengi

zaidi; kutoa elimu ya kulinda na kukuza soko la ndani na nje la almasi na vito kwa lengo la kuchangia ukuaji wa uchimbaji almasi na vito nchini; na kuendeleza wachimbaji wadogo wa almasi na madini ya vito, hususan katika maeneo ya ukadiriaji thamani madini ya vito.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha *TANSORT* kitaendelea kutumia ofisi yake ndogo iliyoko *Antwerp*, Ubelgiji katika kusimamia mauzo ya almasi ya Mgodi wa Mwadui *(WDL)* ambayo hufanyika huko *Antwerp*. Kupitia ofisi hiyo, *TANSORT* pia itaendelea kufuatilia masoko ya almasi na vito duniani kwa lengo la kupata bei na mwenendo wa masoko hayo. Pia, Serikali itaendelea kutafuta fedha na kiwanja kwa ajili ya kujenga jengo la kudumu la ofisi za *TMAA* na *TANSORT* ili shughuli za biashara ya madini nchini zifanyike sehemu moja na iliyo salama.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sera ya Madini ya mwaka 2009 kuhusu kuimarisha soko la madini ya vito nchini, Wizara kwa kushirikiana na *TAMIDA* itaendelea kusimamia Maonesho ya Kimataifa ya Vito na Usonara ya Arusha. Kwa Mwaka 2013/2014, maonesho hayo yanatarajiwa kufanyika kuanzia tarehe 28 hadi 31 Oktoba, 2013 huko Arusha. Kupitia maonesho hayo, Serikali inatarajia kukusanya mrabaha wa zaidi ya Shilingi milioni 330, sawa na Dola za Marekani 206,250 kutokana na mauzo ya almasi na vito. Maonesho hayo yatajikita katika uhamasishaji na uendelezaji wa mfumo wa masoko ya madini; na uhamasishaji na uwezeshaji katika uongezaji thamani madini ili kuongeza fursa za ajira nchini. Uendelezaji wa maonesho hayo ni hatua ya kuifanya Tanzania kuwa kituo cha biashara ya madini ya vito barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, kujenga Ofisi za Madini - Dodoma, Mpanda na Mtwara. Lengo la mradi ni kujenga na kuimarisha ofisi za Maafisa Madini Wakazi na Kanda kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa wadau wa Sekta ya Madini. Katika Mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea na mpango wake wa ujenzi wa Ofisi za Dodoma, Mpanda na Mtwara. Ili kutekeleza mradi huu, jumla ya shilingi bilioni nne (4), sawa na Dola za Marekani milioni 2.5 zimetengwa kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Matumizi ya Baruti. Wizara itaendelea kusimamia utunzaji na matumizi sahihi ya baruti nchini. Ili kutekeleza jukumu hilo, Wizara itatoa mafunzo juu utunzaji, matumizi sahihi na salama ya baruti. Kwa Mwaka 2013/2014, mafunzo hayo yatatolewa katika Mikoa ya Arusha, Katavi, Mtwara na Mwanza ili kuendelea kuwajengea uwezo watumiaji wa baruti. Aidha, ukaguzi wa mara kwa mara wa maghala ya kuhifadhia baruti utaendelea kufanyika ili kudhibiti matumizi mabaya na hatarishi ya baruti. Katika kuhakikisha kuwa matumizi ya baruti yanasimamiwa ipasavyo, Wizara itakamilisha Sheria mpya ya baruti ifikapo mwishoni mwa Mwaka 2014. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya kazi hiyo ni Shilingi milioni 300, sawa na Dola za Marekani 187,500.

Mheshimiwa Spika, elimu kwa Umma kuhusu Sekta ya Madini. Kumekuwepo na malalamiko mengi yanayoelekezwa kwenye Sekta ya Madini, hususan, kuhusu mchango wa Sekta hii katika uchumi wa Taifa. Malalamiko hayo, pamoja na mambo mengine yametokana na umma kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu Sera na Sheria zinazosimamia Sekta ya Madini. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vipindi vya redio na televisheni za hapa nchini. Maandalizi ya vipindi vya televisheni yamekamilika na vipindi hivyo vitaendelea kurushwa kupitia vyombo vya habari vya ndani kuanzia mwanzoni mwa Mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Taasisi na Mashirika katika Sekta ya Madini Chuo cha Madini – MRI. Katika mwaka 2013/2014, Chuo cha Madini kitaendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya cheti na stashahada katika fani za jiolojia ya utafutaji madini; uhandisi migodi; uhandisi uchenjuaji madini; uhandisi na usimamizi wa mazingira migodini; na jiolojia na uhandisi wa mafuta na gesi asilia. Aidha, kufuatia ongezeko la wanafunzi lililotokana na kuanzishwa kwa mafunzo ya fani mpya za mazingira; na mafuta na gesi asilia, Serikali kwa kushirikiana na wahisani katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia itafadhili ujenzi wa madarasa unaokadiriwa kugharimu Shilingi milioni 513, sawa na Dola za Marekani

320,625. Katika kipindi hicho pia, Chuo kitakamilisha ujenzi wa madarasa mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 140 kila moja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ujenzi wa madarasa, Serikali imepanga kujenga mihadhara nane (8) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi takriban 800, ofisi nane (8) za wakufunzi na ukumbi wa mikutano ambapo michoro ya majengo hayo imekamilika. Kwa Mwaka 2013/14 kiasi cha Shilingi bilioni 1.22, sawa na Dola za Marekani 762,500 kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kukipandisha hadhi Chuo hicho katika kiwango cha “*Polytechnic*”. Hatua hiyo, itawezesha Chuo hicho kutoa mafunzo ya aina mbalimbali na kupanua wigo wa kujiendesha kibiashara. Aidha, Chuo kitafungua campus mpya huko Wilayani Nzega baada ya Mgodi wa *Golden Pride* kufungwa rasmi na Chuo hicho kukabidhiwa majengo na miundombinu ya mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa – *STAMICO*. Katika kuliimarisha Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*) ili liweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, katika Mwaka 2013/14 Shirika litaajiri wafanyakazi wapya 78, kuwajengea uwezo wafanyakazi wapya na kuongeza vitendea kazi vya utafutaji madini ambavyo ni pamoja na magnetometers*, resistivity/IP equipment na Gamma rays spectrometers.* Vifaa hivyo vinakadiriwa kugharimu jumla ya Dola za Marekani 450,000 sawa na shilingi milioni 720.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, *STAMICO* na mbia wake, *TANZAM* 2000 wataendeleza upembuzi yakinifu katika eneo la Mgodi wa *Buckreef* ambao unatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, kufuatia *STAMICO* kupata mbia wa kuendeleza Mgodi wa Buhemba, Kampuni ya *Manjaro Resources*, taratibu za kuunda na kusajili Kampuni ya ubia baina yao zitafanyika katika kipindi cha Mwaka 2013/14. Katika kipindi hicho, mkataba rasmi wa ubia *(Definitive Joint*

*Venture Agreement)* utakamilika. Kazi zitakazotekelezwa baada ya kuingia mkataba ni kufanya tathmini ya mabaki ya zamani ya mgodi; kujenga mtambo wa kuchenjua mabaki hayo; na kufanya utafiti wa dhahabu katika miamba ndani ya eneo la leseni.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kukamilika kwa makubaliano ya *STAMICO* kuwa mmiliki mwenza kwa asilimia 50 na Kampuni ya *TanzaniteOne* kwenye leseni ya eneo la Kitalu C Mirerani, Shirika litaingia mkataba rasmi wa uchimbaji na *TanzaniteOne Mining Limited*. Mkataba huo utaainisha namna uchimbaji utakavyoendeshwa, menejimenti ya mgodi, mgawanyo wa mapato; na wajibu wa wanahisa. Lengo ni kukamilisha mkataba huo ifikapo tarehe 30 Julai, 2013.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (*TMAA*). Serikali itaendelea kuimarisha ukaguzi wa shughuli za uzalishaji na biashara ya madini kwa migodi mikubwa, ya kati na midogo kupitia Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (*TMAA*), ili kuhakikisha kuwa Taifa linanufaika ipasavyo na rasilimali yake ya madini. Wakala utaendelea kuimarisha ukaguzi wa hesabu za fedha na kodi za migodi mikubwa, ya kati na wafanyabiashara wa madini ili kuhakikisha wanalipa kodi na mrabaha stahiki.

Mheshimiwa Spika, pia, Wakala utakamilisha mchakato wa usajili wa Maabara yake katika Shirika la Viwango vya Kimataifa (ISO 17025) ili iweze kujiendesha kibiashara; na kujenga uwezo katika kubainisha maoteo ya mapato ya Serikali kutoka kwenye Sekta ya Madini kwa kutumia mfumo wa kisasa (*revenue forecasting model)* ili kuwa na takwimu za uhakika za mapato ya Serikali kutokana na Sekta ya Madini. Vilevile, Wakala utaendelea kuimarisha ukaguzi wa mazingira katika maeneo ya migodi mikubwa, ya kati na midogo. Fedha zilizotengwa kwa Wakala ni Shilingi bilioni 9.78.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Jiolojia Tanzania – *GST*. Katika kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Madini, Serikali

kupitia Wakala wa Jiolojia Tanzania itaendelea kukusanya taarifa za kijiosayansi na kuchora ramani. Kwa Mwaka 2013/ 2014, Wakala utaendelea kufanya utafiti na kuchora ramani za kijiolojia, kijiokemia na kiojiofizikia. Utafiti huo utafanyika kwenye maeneo ya QDSs 267, 268, 269, 270/271 yaliyoko katika Wilaya za Kilwa, Liwale, Nachingwea na Ruangwa. Utafiti huo umelenga kubaini uwepo wa madini muhimu yakiwemo dhahabu, *Platinum Group Metals (PGM)* na shaba. Vilevile, Wakala utaendelea kuboresha mfumo wa kutunza kumbukumbu za kijiosayansi na kukusanya taarifa za matetemeko ya ardhi katika vituo vilivyopo nchini. Fedha zilizotengwa kwa Wakala ni Shilingi bilioni 7.31.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *GST* itakamilisha kazi ya kutafuta madini ya kiteknolojia *(technology metals)* kwa kushirikiana na Taasisi ya *BRGM* ya Ufaransa. Mradi huu unakadiriwa kugharimu Euro milioni 3.054, sawa na shilingi bilioni 6.48 na utakamilika mwishoni mwa mwaka 2013/2014. Utafiti huu utawezesha kutengeneza ramani mpya inayoonesha mahali yanapopatikana madini ya kiteknolojia. Kuhusu utafiti wa maeneo yenye jotoardhi, Wakala utaendelea na utafiti huo katika maeneo ya Ziwa Ngozi (Mbeya) na Kisaki (Morogoro). *GST* inafanya utafiti huo kwa kushirikiana na *BGR* ambayo ni Taasisi ya Jiolojia ya Ujerumani.

Mheshimiwa Spika, Ajira na Maendeleo ya Rasilimali Watu. Wizara inakabiliwa na uhaba mkubwa wa watumishi. Katika mwaka 2013/2014, Wizara inatarajia kuajiri jumla ya watumishi 589 wa kada mbalimbali. Kati ya hao watumishi 138 ni kwa ajili ya Wizara, *TANESCO 233, TMAA 12, STAMICO 78, GST 53, MRI 32, TPDC 39 na REA 4*. Jitihada mbalimbali zinafanyika kwa kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Sekretarieti ya ajira ili kuweza kupata wataalam hao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, aidha, ili kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa Sekta za Nishati na Madini, Wizara imepanga kuwajengea uwezo jumla ya watumishi 150 kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi, kipaumbele kitatolewa katika maeneo maalumu yakiwemo

mafuta na gesi asilia, *energy economics; oil and gas accounting and auditing; oil and gas legal regime and contract negotiations; energy management; geothermal; uranium; mineral economics;* na *diamond valuation and sorting*.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Rasilimali Watu (*Marshall Plan on Capacity Building and Development in Oil and Gas Industry 2012-2016*) ambao utawezesha Watanzania kati ya 50 hadi 100 kupata elimu katika ngazi ya stashahada, shahada, na shahada za uzamili na uzamivu kwenye fani za mafuta na gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, Ushirikiano wa Kimataifa. Serikali inatambua misaada na ushirikiano kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2012/2013. Kwa niaba ya Serikali napenda kutoa shukrani kwa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China; Serikali za nchi za Brazil, Canada, Finland, Japan, Malaysia, Marekani, Norway, Oman, Qatar, Sweden, Trinidad & Tobago na Ufaransa. Vilevile, natoa shukrani kwa Benki ya *Exim* ya China, Benki ya *BADEA*, Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini (*DBSA*), Benki ya *HSBC*, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Umoja wa Ulaya (*EU*), pamoja na Taasisi na Mashirika ya *AFD* (Ufaransa), *CIDA* (Canada), *ECDF* (Korea Kusini), *FINIDA* (Finland), *JICA* (Japan), *KfW* (Ujerumani), *MCC* (Marekani), *NORAD* (Norway), *OFID* (Saudi Arabia), ORIO (Uholanzi) na Sida (Sweden), *GEF, GVEP, IDA, IFC, UNDP, UNEP, UNIDO, UNICEF* na Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru Ndugu zangu na wadogo zangu Manaibu Mawaziri, Mheshimiwa Boniphace Simbachawene na Mheshimiwa Julius Massele na Katibu Mkuu Bwana Eliakim C. Maswi kwa uchapakazi wake mahiri na ushirikiano mkubwa anaonipa na niwaeleze tu kwamba Mheshimiwa Simbachawene na Mheshimiwa Massele wanaendelea vizuri na *Masters* zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru Makamishna wote, Wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na watumishi wote wa Wizara kwa kutekeleza majukumu yao kwa bidii na maarifa.

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru, Wenyeviti wote wa Bodi za Wakurugenzi, Wakurugenzi Wakuu, Wakurugenzi Watendaji, Watendaji Wakuu, na Watumishi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa jinsi wanavyofanya kazi kwa kushirikiana na Wizara. Taasisi hizo zimefanya kazi kwa karibu sana na mimi, nawaomba muendelee kufanya kazi kwa uadilifu mkubwa na ueledi ili kuhakikisha Wizara yetu inafikia malengo tuliyopewa na Serikali yetu ya kuwatumikia Wananchi wa Taifa hili ambao ndio waajiri wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa vyombo vya habari mbalimbali nchini kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa. Vyombo hivyo vimekuwa vikifuatilia na kutoa taarifa za shughuli zinazohusu Sekta za Nishati na Madini. Ushirikiano huu utaendelezwa na kuimarishwa zaidi kwa manufaa ya Taifa ili kuhakikisha kuwa umma unapata taarifa za kina na za uhakika. Aidha, Wizara yangu itaendeleza mawasiliano mbalimbali ili kuboresha utoaji wa elimu na taarifa kwa umma. Wizara pia itaendelea kutoa taarifa za shughuli zinazotekelezwa na Wizara kupitia vipindi vya Luninga, Redio, Tovuti *(www.mem.go.tz)* pamoja na majarida mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vilevile, natoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wanaoniletea taarifa mbalimbali kwa njia ya maongezi ya simu, ujumbe mfupi *(sms)* barua na barua pepe zikiwemo za hujuma za miundombinu ya umeme, rushwa na wizi ndani ya Wizara na Taasisi zake. Naomba wananchi waendelee kuniletea taarifa na ninawaahidi nitaendelea kuzifanyia kazi kwa uadilifu wa hali juu. Aidha, nawasihi wananchi kwa umoja wetu tuendelee kupambana na hujuma, wizi na rushwa katika Sekta za Nishati na Madini na kulinda miundombinu ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, naomba

nimshukuru sana mke wangu Bertha Muhongo, wanangu Godfrey Chirangi, Dkt. Musuto Chirangi, Dkt. Bwire Chirangi na Rukonge Muhongo pamoja na familia yangu kwa ujumla kwa msaada mkubwa wanaonipa kutekeleza kazi zangu kwa ubora na ubunifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho, bajeti ya Mwaka 2013/14, inalenga: kuboresha upatikanaji wa umeme wa kutosha na wa uhakika; kuongeza watumiaji wa umeme vijijini na mijini; kuimarisha usimamizi wa Sekta za Nishati na Madini na kuongeza mchango wake katika kukuza uchumi wa Taifa; kuongeza ajira; na kupunguza umaskini nchini.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya matumizi ya maendeleo. Mwaka 2013/2014, Wizara yangu ya Nishati na Madini inaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi bilioni 992,212,745,000 sawa na asilimia 90 ya Bajeti yote ya Wizara kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 558,345,745,000 sawa na asilimia 56 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 433,867,000,000 sawa na asilimia 44 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya matumizi ya kawaida kwa mwaka 2013/2014. Katika Mwaka 2013/2014, Wizara ya Nishati na Madini inaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi bilioni 110,216,384,000 sawa na asilimia 10 tu ya Bajeti yote kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo kati ya fedha hizo, shilingi 14,607,640,000 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake ambapo ni sawa na asilimia 1.3 na shilingi 95,608,744,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida *(OC)* ambayo huwa inapigiwa kelele sana ni asilimia 8.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha jumla ya shilingi trilioni 1,102,426,129,000 kwa ajili ya matuizi ya maendeleo na ya kawaida kwa mwaka 2013/2014 kwa Wizara ya Nishati na Madini. Bajeti ya mwaka uliopita ilikuwa ni bilioni 642 sasa tuko kwenye trilioni 1.12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante. Hoja hiyo imeungwa mkono. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Wizara hii ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Mwenyekiti mwenyewe! *(Makofi)*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI – MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, nataka kutangaza *interest* yangu. Mimi na Mheshimiwa Waziri Muhongo tulikuwa wote Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuanzia mwaka 1976. Mwaka 1977 wanafunzi wengi wa Chuo Kikuu tuliandamana tukipinga mishahara ya Wabunge na bahati mbaya sasa sisi wenyewe ni Wabunge tena. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa imani kubwa waliyotupa ya kutuchagua mimi na Makamu wangu. Hakika ni heshima kubwa waliyotupa, ni jukumu zito wametukabidhi ambalo kwa ushirikiano wa pamoja tunaimani tutaweza kuisimamia na kuishauri Serikali na hususan Wizara ya Nishati na Madini ambayo ni sekta nyeti na mhimili katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2013, kwa ridhaa yako, naomba niwasilishe maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2012/2013, utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2012/2013 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Kamati ilipata wasaa wa kupokea taarifa ya utekelezaji wa

maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati iliyayotoa kwenye bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Kamati iliyopita ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo katika maeneo yafuatayo:- Umeme, Umeme Vijijini, Gesi Asili, Biashara ya Mafuta, Utendaji wa Wizara na Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara. Kamati imepitia taarifa ya utekelezaji wa maagizo hayo. Aidha, yapo baadhi ya maeneo hamna utekelezaji wowote uliofanywa hususan katika maeneo yanayoihusu Serikali moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na uamuzi wa Serikali wa kutotekeleza Maazimio ya Bunge yafuatayo ambayo ni ya muhimu sana katika kuhakikisha Wakala wa Umeme Vijijini *(REA)* unafanya kazi yake bila pingamizi.

(a) Tozo ya Shilingi 5/= kwa kila dakika ya maongezi ya simu kwenda *REA.*

(b) Kutenga shilingi bilioni 300 kwa ajili ya matumizi ya miradi ya umeme vijijini kutoka katika shilingi bilioni 600 ambazo ni kiasi kilicho/kinachookolewa kutokana na uamuzi wa Serikali kulinganisha kodi za mafuta ya taa na dizeli.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa masuala hayo uamuzi wake haufanywi na Wizara pekee, tunaiomba Serikali itueleze kwa nini haitaki kutekeleza Maazimio ya Bunge. Narudia tena Serikali itueleze kwa nini haitaki kutekeleza Maazimio ya Bunge tuliyopitisha mwaka 2011/2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 641,269,729,000/= ili kutekeleza majukumu yake. Kati ya Fedha hizo shilingi 110,078,868,000/= zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaidia ambapo shilingi 17,292,347,000/= zilikuwa kwa ajili ya mishahara *(PE)* na Shilingi 92,786,521,000/= zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC).* Aidha, kiasi cha shilingi 531,190,861,000/= kilitengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Maendeleo, kati ya hizo shilingi 431,190,861,000/= ni fedha za ndani na shilingi 100,000,000,000/= ni fedha za nje. Aidha,

Wizara iliongezewa kiasi cha shilingi bilioni 185 kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa umeme na hivyo kufanya jumla ya fedha iliyotengwa kwa Wizara hii kwa mwaka 2012/2013 kuwa shilingi bilioni 826.27.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 15 Mei 2013, jumla ya shilingi bilioni 740.81 zilikuwa zimetolewa na Serikali sawa na asilimia 89 (89.7%) ya bajeti nzima ya Wizara. Aidha, fedha za nje zilizotolewa zilikuwa ni asilimia 10.8 (10.8%) tu.

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyopita pia ililenga katika kutekeleza maeneo muhimu yafuatayo:- Kujenga Bomba la Kusafirisha gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam, Kuimarisha njia za ufuaji umeme na njia za kusafirisha umeme, kuendeleza usambazaji umeme katika Makao Makuu ya Wilaya na Vijiji na Kuendeleza na Kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu (*renewable energy*) na mbadala (*alternative*) ikiwamo nishati jua, upepo na joto ardhi, kuendeleza uchimbaji wa madini wa kati na mdogo, kuwezesha upatikanaji wa vifaa na mikopo pamoja na kuimarisha huduma za ugani, kuimarisha uwezo wa kitaasisi katika kuendeleleza na kusimamia rasilimali za madini.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa kazi zilizopangwa kutekelezwa na Wizara katika mwaka wa fedha 2013/2014. Wizara ya Nishati na Madini ina jukumu la kusimamia Sekta muhimu za uchumi wa Taifa hili ambazo ni Nishati na Madini. Katika mwaka huu wa fedha wa 2013/2014, Wizara inaomba jumla ya Shilingi 1,102,429,129,000/= kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 826.27 kilichotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 ambalo ni ongezeko la asilimia 33.4.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa fedha hizo shilingi 1,102,429,129,000/= ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Kawaida yanaombewa jumla ya shilingi 110,216,384,000/= sawa na asilimia 10 ya bajeti. Kati ya hizo shilingi 14,607,640,000/= ni mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake *(PE)* na Shilingi 95,608,744,000/= ni matumizi mengineyo *(OC).*

Mheshimiwa Spika, awali Wizara ilitengewa shilingi 11,612,542,000/= kwa ajili ya mishahara ya Wizara na Taasisi zake. Kiwango hicho kilikuwa kidogo ikilinganishwa na mahitaji halisi hasa ikizingatiwa kuwa mshahara ni haki ya kila mtumishi. Kamati iliwaita Maafisa wa Bajeti kutoka Hazina na tukakubaliana bajeti ya mishahara iongezwe. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Hazina waliufanyia kazi ushauri wa Kamati na kutoa nyongeza ya shilingi 8,335,294,828/=. Kati ya hizo, shilingi 5,345,296,828/= ni kwa ajili ya Shirika la Maendeleo ya Petroli *(TPDC)* na zimekasimiwa katika Fungu 21 (Hazina). Aidha, kiasi cha shilingi 2,995,098,000/= kinaongezwa kwenye Fungu 58 (Wizara ya Nishati na Madini).

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Maendeleo inaombewa shilingi 992,212,745,000/= sawa na asilimia 90 ya bajeti yote. Kati ya fedha hizo shilingi 558,345,745,000/= ni fedha za ndani na Shilingi 433,867,000,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha shilingi 531,125,745,000/= sawa na asilimia 95.1 ya bajeti yote ya maendeleo inalenga kutekeleza miradi iliyo katika Sekta ya Nishati. Miradi hiyo ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa bomba la gesi, miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi, kupelekea umeme katika Makao Makuu ya Wilaya na maeneo mengine vijijini na kuboresha miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Kamati yangu imechambua na kujadili kwa kina taarifa za Wizara na Taasisi zilizo chini yake hasa za utekelezaji wa shughuli na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Aidha, Kamati imechambua na kujadili taarifa ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Pamoja na ongezeko la bajeti kwa asilimia 58.1 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2012/2013 bado kuna maeneo ambayo Kamati inayatolea ushauri, maoni na mapendekezo kwa ajili ya kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia sekta ya nishati kwa kupitia utendaji wa taasisi zake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*) lina jukumu la kufua/kununua, kusafirisha, kusambaza na kuuza umeme nchini. Hivyo basi, tunapoongelea masuala mazima ya umeme tunaongelea *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu hayo, *TANESCO* ina mlolongo wa matukio ambayo yamefanya ufanisi wake kuwa chini sana:-

(a) Shirika liliwekwa chini ya *PSRC* likiangaliwa kwa lengo la kulibinafsisha kuanzia mwaka 1995 mpaka 2005 ambapo Serikali iliamua kuliondoa huko. Kwa hiyo, kwa kipindi cha takribani miaka 10 hapakuwa na uwekezaji katika sekta hii ili uende sambamba na ukuaji wa uchumi.

(b) Ukame wa mara kwa mara umelifanya Shirika kukodisha mitambo ya kufua umeme kwa gesi na mafuta mazito. Mitambo hiyo ni kama *IPTL*, *AGGREKO, SYMBION* na *SONGAS*. Makampuni haya yamekuwa yakiiuzia umeme *TANESCO* kwa senti za kimarekani 30 mpaka 49 kwa uniti moja wakati yenyewe inauza umeme kwa senti za kimarekani 12 kwa kila hali inayolifanya Shirika kuendeshwa kwa hasara.

(c) Kwa muda mrefu kidogo kumekuwepo na changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara nchini hali ambayo imeleta kero na hofu kwa wananchi. Kamati imefuatilia na kubaini kwamba tatizo la kukatika kwa umeme katika Jiji la Dar es salaam na maeneo mengine nchini linatokana na uchakavu wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme nchini ambayo haikuwahi kufanyiwa marekebisho kwa takribani miaka 40. Kwa sasa *TANESCO* inaendelea na zoezi la kuboresha miundombinu hiyo na hivyo kulazimika kukata umeme ili kuweza kufanya maboresho hayo.

(d) Kamati ina taarifa kuwa hujuma katika miundombinu ya umeme inachangia sana katika kuzorotesha huduma ya upatikanaji wa umeme nchini. Takwimu zinaonyesha kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Januari 2012 hadi Disemba 2012 jumla ya nyaya za umeme zenye urefu wa Kilomita 11.249 zenye thamani ya shilingi milioni 408 ziliibiwa, mafuta ya transfoma kwenye transfoma 190 yenye thamani ya shilingi bilioni 1.32 yaliibiwa na wateja 532 walikamatwa kwa wizi wa umeme wenye thamani ya shilingi bilioni 5.6

(e) Sababu kubwa ya madeni ya Shirika hili pamoja na mambo mengine ni gharama kubwa za manunuzi ya umeme toka vituo binafsi tofauti na bei ya kuuzia umeme. Takwimu zinaonyesha kuwa *TANESCO* huuziwa umeme kati ya dola za kimarekani senti 30 hadi 49 kwa uniti moja sawa na fedha za Kitanzania kati ya shilingi 495/= na shilingi 808/= na kuuza umeme huo kwa dola za kimarekani senti 12 tu sawa na shilingi 198/=za Kitanzania. Shirika limekuwa likiomba kuongeza bei ya kuuzia umeme kwa viwango mbalimbali toka mwaka 2006 kupitia *EWURA* lakini imekuwa haikubaliki kwa kiwango kinachoombwa. Mfano Januari 2012 Shirika liliomba kuongeza bei ya umeme kwa asilimia 155 (155%) lakini bei iliyokubalika ni asilimia 40.29 (40.29%) tu.

Mheshimiwa Spika, hali hii imekuwa ikisababisha Shirika kuwa na hali mbaya kifedha na uendeshaji kuwa mgumu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo yote haya yaliyoorodheshwa, Kamati imeridhika na hatua za awali za Serikali za kuliunda upya Shirika hili na inatoa ushauri ufuatao:-

(a) Kwa kuwa msimamo wa Serikali ambao tunaupongeza ni kuwa bei ya umeme isipande na kwa kuwa *TANESCO* inanunua umeme kwa bei aghali na kuuza kwa bei ndogo, Kamati inashauri Serikali itoe ruzuku stahili kwa Shirika hili ili liweze kujiendesha. *(Makofi)*

(b) Serikali iendelee kuijengea uwezo *TANESCO* kwa kuitengea bajeti ya kutosha ili iweze kuwa na mitambo yake

yenyewe na kuondokana na matumizi ya mitambo ya dharura ambayo ni ya gharama kubwa. *(Makofi)*

(c) Serikali ilenge kuwekeza kwenye ufuaji umeme kwa maji, gesi, makaa ya mawe, upepo, joto ardhi na kadhalika na kushirikisha sekta binafsi katika uwekezaji huo.

(d) Serikali iwekeze kwenye miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme ili kuondoa hasara itokanayo na uchakavu wa miundombinu hiyo.

(e) Katika kuliunda upya Shirika, pamoja na kushirikisha sekta binafsi katika ufuaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme, tunashauri Serikali ihakikishe inadhibiti vyanzo vya kufua umeme vyenye faida ya kiushindani kama gesi, maji na makaa ya mawe.

(f) Serikali ifanye kila liwezekanalo kuondokana na mitambo ya kufua umeme ya kukodi ambayo umeme wake ni aghali sana. Hivyo basi, ujenzi wa bomba la gesi pamoja na ununuzi wa mitambo ya kufua umeme vipewe kipaumbele sana, hii itasaidia Shirika kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 27 kila mwezi ambacho makampuni haya yanalipwa kila mwezi kama ziada (*capacity charges*). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* imeanzishwa kwa lengo la kuongeza kasi ya kupeleka huduma za nishati bora vijijini ili kuchangia kufikia lengo la Taifa la asilimia thelathini (30%) ya wananchi watakaounganishiwa umeme nchini ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo basi, *REA* ndio mkombozi pekee wa taifa hili katika kuhakikisha huduma ya upatikanaji wa umeme katika maeneo ya vijijini ambayo ndiyo wananchi wengi wa Tanzania wapatao asilimia 80 ya Watanzania wote wanaishi.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwake mnamo mwaka 2007, *REA* imefanya kazi nzuri ya kusambaza umeme vijijini. Takwimu zinaonyesha kuwa kaya zinazopata huduma

ya umeme zimeongezeka kutoka asilimia 2.5 mwaka 2007 hadi asilimia 4.6 mwaka 2011. Aidha, kaya zinazopata umeme utokanao na vyanzo vingine ikiwemo umeme wa jua (*solar power*) imefikia asilimia 2.0 na hivyo kufanya jumla ya kaya zinazopata nishati bora vijijini kufikia asilimia 6.6. (Kwa mujibu wa *Baseline Survey on Energy Access and use in Tanzania Mainland* iliyofanyika 2011/2012).

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi kubwa inayofanywa na *REA*, bado inakumbana na changamoto hasa ya ukosefu wa fedha katika kutekeleza miradi yake. Si hivyo tu hata zile fedha ambazo zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu nazo hazitolewi. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, *REA* iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 58,883,000,000/= fedha iliyopokelewa ilikuwa ni shilingi 14,652,000,000/= sawa na asilimia 25 (25%) tu. Aidha, mwaka wa fedha 2011/2012, fedha iliyotolewa ilikuwa ni asilimia 80 (80%) tu. Hali imekuwa mbaya zaidi katika mwaka huu wa fedha wa 2012/2013 kwani kiasi cha fedha kilichoidhinishwa ni shilingi 53,158,000,000/= lakini mpaka tunaandika taarifa hii kiasi kilichotolewa ni shilingi 6,757,000,000/= sawa na asilimia 13 (13%) tu. Kamati imesikitishwa sana na mtiririko huu wa fedha kwani unakwamisha malengo ya kuwafikishia wananchi umeme vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imetafakari kwa kina changamoto ambazo REA inakumbana nazo na inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, bajeti. Kamati inaamini na kutambua kuwa *REA* ndiyo mkombozi na suluhisho la upatikanaji wa umeme katika maeneo ya vijijini. Kwa misingi hiyo basi, Serikali haina budi kuhakikisha kuwa *REA* inatengewa fedha za kutosha na zitolewe zote kwa wakati kama zilivyoidhinishwa na Bunge. Kamati inaamini kuwa kama kweli tunataka kufikia asilimia 30 (30%) ya wananchi wanaopata umeme ifikapo 2015, suluhisho ni kuiwezesha *REA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuongeza bajeti ya REA, Kamati inashauri vyanzo vingine kama vifuatavyo:-

(i) Ruzuku ya Mafuta ya taa kuchangia Mfuko wa Nishati Vijijini. Kuanzia mwaka wa Fedha 2011/2012, Kamati imekuwa ikitoa ushauri ambao Bunge lako Tukufu liliridhia na kulifanya Azimio. Azimio hilo ni lile linalotaka manufaa yaliyotokana na udhibiti wa uchakachuaji ambapo Serikali ilikuwa inapoteza shilingi bilioni 600 kwa mwaka na Bunge likaridhia nusu yake Shilingi bilioni 300 ziende *REA*.

Mheshimiwa Spika, mpaka tunaandika taarifa hii *REA* haijapatiwa fedha hizo na Kamati ilipojaribu kufahamu ni wapi fedha zinaenda, tukafahamishwa kuwa fedha hizo zilifidia punguzo lililotolewa na Serikali kwenye mafuta ya dizeli jambo ambalo ni kinyume na agizo la Bunge kwamba fedha hizi ziende kwenye Mfuko wa Nishati Vijijini (*REA*).

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa agizo hili la Bunge liliongeza gharama za mafuta ya taa hapa nchini jambo ambalo lililalamikiwa sana na wananchi lakini nia ya Bunge ilikuwa ni huduma ya umeme kusambaa kwa kasi vijijini na hivyo kupunguza matumizi ya mafuta ya taa na tatizo la uchakachuaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati kwa mara nyingine inaitaka Serikali kutekeleza agizo la Bunge kama lilivyopitishwa na iache kubadilisha madhumuni ya agizo bila taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwani Kamati inaona huko ni kulidharau Bunge na tunaitaka Serikali kupitia Azimio la Bunge izitoe fedha hizo bilioni 300 kwa makusudi yaliyoadhimiwa. *(Makofi)*

(ii) Huduma za simu kuchangia Mfuko wa Nishati Vijijini. Kamati inaamini kuwa kwa kupeleka huduma za umeme vijijini kunasaidia kuchangia maendeleo ya sekta ya mawasiliano vijijini, kama vile wateja kuchaji simu, kuwezesha vituo vya urushaji wa mawasiliano kupata umeme na maendeleo ya teknohama vijijini. Pamoja na umuhimu huo wa umeme kwenye sekta ya mawasiliano na Azimio la Bunge lililoagiza utaratibu uandaliwe ili kuwe na tozo ya shilingi tano kwa kila dakika ya maongezi ya simu, Kamati inashangaa kuona bado Serikali inakigugumizi kulitekeleza

azimio hili la Bunge hata baada ya kuongelewa na Kamati mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati bado inaendelea kuamini kwa kuongeza mapato kwenye Mfuko wa Nishati Vijijini, itasaidia maendeleo kufika vijijini kwani bila umeme vijijini hakuna maendeleo. Kwa vile hili lilikuwa ni azimio la Bunge, Kamati inashauri Serikali kutekeleza maagizo ya Bunge kama mhimili mwingine wa dola na kama kuna tatizo katika utekelezaji Bunge lijulishwe ili liweze kutoa maamuzi muafaka ya kulisaidia Taifa badala ya kukaa kimya.

(iii) Tozo ya shilingi mia moja (100) kwa kila lita ya Mafuta ya Petroli. Umeme vijijini ni suala la msingi sana katika ukuaji wa uchumi wa nchi. Bila kuiwezesha Wakala wa Nishati Vijiji *(REA)* kupata fedha za kusambaza umeme huo, itachukua muda mrefu sana wananchi kupata maendeleo. Maeneo ambayo umeme umefika, uchumi umeongezeka kwa kasi kwa kuanzisha viwanda vidogovidogo vya kukamua mafuta ya alizeti, kusindika tangawizi, mashine za kusaga nafaka na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu huo mkubwa kwa wananchi wa vijijini kupatiwa umeme, Waziri wa Nishati na Madini amepewa mamlaka na Sheria ya Mafuta ya mwaka 2008, kifungu cha 32 kuanzisha tozo kwenye mafuta ya petroli kwa uendeshaji bora wa sekta hiyo kwa kushauriana na Waziri wa Fedha. Tozo hii ikiridhiwa, kiasi cha shilingi bilioni 250 kinatarajiwa kupatikana kila mwaka na kitapelekwa *REA* kwa ajili ya kusambaza umeme vijijini. Kamati inapendekeza Wizara ya Fedha kuridhia tozo hii kwa manufaa ya Taifa ili iweze kuanza kutumika kuanzia 1 Julai, 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Akaunti ya Nishati (*Energy Account*). Sheria ya Mafuta ya Mwaka 2008 inaelekeza kuanzishwa kwa Akaunti ya Nishati (*Energy Account*) na sehemu ya mapato ya Akaunti hiyo itachangia kwenye Mfuko wa Nishati Vijijini. Kamati ilipotaka kujua maendeleo ya suala hili ilielezwa bado Akaunti hii haijaanzishwa. Kamati inashauri Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na Wizara ya

Fedha ilishughulikie suala hili kwa vile ni takwa la kisheria na lazima Serikali iwe mfano katika kutekeleza sheria kwa vile sasa ni miaka takribani mitano imepita bila takwa hili kutekelezwa. Kamati inatambua umuhimu wa kuanzisha Akaunti hii kwani itasaidia Wakala kuweza kupata fedha zaidi za kusambaza umeme vijijini na kuamsha maendeleo katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Wilaya kuchangia utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme vijijini. Kamati imebaini kuwa zipo baadhi ya Halmashauri zina uwezo wa kuchangia katika miradi ya kusambaza umeme vijijini hasa umeme wa jua (*solar power*) kwenye taasisi mfano Zahanati, Shule na kadhalika. Kamati inashauri *REA* ishirikiane na Halmashauri kuona jinsi ya kushirikiana nazo katika kufikisha umeme katika maeneo ambayo gridi ya Taifa haijapita na hivyo kusaidia kupeleka maendeleo katika maeneo hayo. Aidha, wakati wa kusambaza umeme huu wa jua katika taasisi mfano Shule na Zahanati, ni vyema nyumba za watumishi nazo zikapatiwa umeme huo ili kuwapa morali ya kufanya kazi katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vibali vya kupitisha umeme katika baadhi ya taasisi za Serikali. Kumekuwepo na ucheleweshaji wa miradi katika baadhi ya maeneo kutokana na kuchelewa kutoka kwa vibali vya kupitisha nguzo katika maeneo ya taasisi za Serikali. Kwa mfano, hali hii imejitokeza huko Kintinku katika Wilaya ya Manyoni ambapo mradi umekwama kwa kuwa Mamlaka ya Reli Tanzania haijatoa kibali cha kupitisha nguzo kuvuka reli. Kamati inashauri ili miradi hii iweze kufanikiwa, ushirikiano wa kila Wizara za Serikali ni muhimu sana. Hivyo Kamati inaitaka Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Uchukuzi kulimaliza tatizo hili ili mradi huo uweze kuanza mara moja.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka huu *REA* imepangiwa shilingi bilioni 150 ili kuweza kumudu kutekeleza mradi kabambe wa kupeleka umeme vijijini.Kiasi hiki ni midogo sana kwani *REA* inahitaji shilingi bilioni 880 ili kuweza kutekeleza hili. Kwa shilingi bilioni 150 zilizoombwa *REA*

itatuchukua miaka sita (6) kukamilisha awamu ya pili ya mradi huu kabambe wa kusambaza umeme vijijini hali itakayotufanya tushindwe kufikia lengo la asilimia 30 la mwaka 2015. Kamati inapendekeza kuwa vyanzo vyote vilivyoainishwa hapo juu vitekelezwe ili tuweze kufikia lengo hilo mapema kadri iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo la Petroli Tanzania *(TPDC).* Shirika la Maendeleo la Petroli *(TPDC)* lina jukumu kuu la kusimamia biashara ya mafuta na gesi. Tangu kuanzishwa kwake *TPDC* imepata mafanikio makubwa ikiwemo kuendelea kugundulika kwa gesi nchini. Mpaka sasa kiasi cha gesi kinachokadiriwa kuwepo nchini ni futi za ujazo trilioni 41.7. Kati ya hizo trilioni 8.0 kipo nchi kavu na trilioni 33.7 katika bahari ya kina cha maji kirefu. Aidha, mpaka sasa gesi iliyohakikiwa kuwepo ni futi za ujazo trilioni 1.369 ambayo ipo nchi kavu.

Mheshimiwa Spika, ugunduzi huu wa gesi ni ishara kuwa nchi yetu ina utajiri wa kutosha na kama tukiitumia vyema gesi hii basi Taifa letu litasonga mbele. Mpaka sasa faida za gesi ni kubwa sana. Baadhi ya faida hizo ni pamoja na:-

(i) Kuokolewa kwa fedha za kigeni kiasi cha dola za kimarekani milioni 346 kwa kipindi cha Julai 2012 – Disemba 2012 kulikotokana na kutumia gesi asili katika kuzalisha umeme badala ya mafuta mazito *(HFO)* na Mafuta ya Taa na Ndege *(JET A1).*

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha kuwa Uchumi wetu unakadiriwa kupoteza kiasi cha dola za kimarekani bilioni 1 kwa mwaka kwa kutumia mafuta kuzalisha umeme badala ya gesi.

(ii) Dola za Kimarekani milioni 40.237 ziliokolewa baada ya kutumia gesi asili kiasi cha futi za ujazo bilioni 2.073 katika viwanda na taasisi badala ya kutumia mafuta na *Liquified Petroleum Gas (LPG).*

Mheshimiwa Spika, pamoja na faida hizo za kiuchumi, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo katika sekta hii ya gesi:-

Mheshimiwa Spika, Sera na Sheria ya Gesi. Sera ni nyenzo muhimu katika kuliongoza taifa lolote lile duniani kuhusu namna bora ya uendeshaji na matumizi ya rasilimali zake. Matumizi bora ya gesi hii yanategemea sana uwepo wa miongozo sahihi (Sera na Sheria). Kwa muda mrefu sana Kamati imekuwa ikishauri kuhusu kuletwa kwa Sera na Sheria gesi ili kuhakikisha tunaitumia vyema rasilimali hii muhimu ambayo Mungu ametujalia.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeona umuhimu wa miongozo hii muhimu na tayari imeandaa Rasimu ya Sera ya Gesi na kuwashirikisha wadau wote kama vyuo, wafanyabiashara, mikoa yenye gesi, NGO na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kamati na Wabunge wote kama wadau nao wamepata wasaa wa kuipitia ili kujiridhisha kama imezingatia maslahi ya Taifa kama zilivyo nchi nyingine mfano Norway na Trinidad & Tobago. Serikali izingatie sana ushauri ulitolewa na wadau wote na Wabunge katika kuiboresha Sera na kuandaa Muswada wa Sheria ya Gesi. Aidha, Kamati inapendekeza mara baada ya Sera kukamilika, Serikali ihakikishe inaleta Muswada wa Sheria ya Gesi mapema ili kuweza kuisimamia vyema rasilimali hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kusitisha utoaji wa leseni katika vitalu vya gesi mpaka hapo Sera na Sheria ya gesi zitakapokuwa tayari.

Mheshimiwa Spika, mafunzo kwa Wataalam wa Mafuta na Gesi. Ni ukweli ulio wazi kuwa suala la gesi ni jambo jipya nchini kwetu. Ili kuweza kusimamia vyema rasilimali na kuleta mandeleo kwa Taifa, ni lazima nchi iwe na wataalam wa kutosha. Kamati ilielezwa kuwa Wizara ina Mpango Kabambe wa kuwapata wataalam hao na imekuwa ikifadhili wanafunzi kwa pesa zake yenyewe katika vyuo

mbalimbali hapa nchini na pia kutafuta wafadhili kutoka nje ya nchi lengo likiwa ifikapo mwaka 2015 Tanzania iwe na wataalam wa gesi wasiopungua 200. Kwa sasa Wizara inafadhili wanafunzi 30 katika Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo cha Madini Dodoma. Aidha, inafadhili wanafunzi 64 katika vyuo vya VETA Lindi na Mtwara (wanaotoka maeneo yenye gesi) ili wajifunze ufundi utakaosaidia kufanya kazi ndogondogo mara viwanda vitakavyoanzishwa katika Mikoa yao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa jinsi ilivyotekeleza ushauri wa Kamati na kufanikisha upatikanaji wataalam wetu katika masuala ya gesi na mafuta kwa fedha za ndani na nje ya nchi. Aidha, Kamati inasisitiza Wizara kuangalia utaratibu wa kuwapata wanafunzi watakaofadhiliwa na Wizara wa kutoka kwenye Mikoa yenye gesi kwa kuanzia ngazi ya Vitongoji, Vijiji, Kata, Tarafa, Majimbo na Wilaya na viongozi wote katika ngazi hizi wahusishwe.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati inashauri Wizara kuchangamkia ufadhili unatolewa na nchi ya Trinidad & Tobago kwa vile ni muda mrefu wameonyesha nia ya kufadhili wanafunzi wa Kitanzania lakini kama nchi hatujachukua hatua stahiki wakati wenzetu nchi jirani ya Uganda wameshapeleka wanafunzi wao kusomea masuala haya. Nchi zote zilizoendelea kwenye sekta hii zimetokana na jitihada za kusomesha wataalam wake.

Mheshimiwa Spika, mradi Bomba la Gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam. Itakumbukwa kuwa mnamo mwaka 2004 mradi wa ujenzi wa bomba la gesi kutoka Songo Songo mpaka Dar es Salaam ulianza baada ya kutambua unafuu wa gesi katika kufua umeme nchini. Bomba hilo ambalo linasimamiwa na SONGAS lina uwezo wa kusafirisha gesi kiasi cha futi za ujazo milioni 105 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuendelea kugundulika gesi nchini umuhimu wake hasa unafuu katika kufua umeme, Serikali iliamua kwa dhati kupitia Shirika lake

la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* kutekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha gesi asili hasa baada ya Bomba la awali kutokidhi mahitaji ya sasa, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alivyoeleza katika hotuba yake, Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Jamhuri ya watu wa China na miundombinu hii itamilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja. Mradi utakapokamilika utakuwa na uwezo wa kusafirisha gesi hadi kiasi cha futi za ujazo milioni 784 kwa siku kwenda Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam ambapo itatumika kwenye viwanda, majumbani, mitambo ya kuzalisha umeme pamoja na mahitaji yoyote ya gesi yatakayojitokeza; juhudi zitafanywa kusambaza huduma ya gesi asilia kwenye Mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumekuwa na sintofahamu kuhusiana na mradi huu wa gesi ambao Serikali imepanga kuuanzisha. Nasema sintofahamu kutokana na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikijitokeza.

Mhesimiwa Spika, Kamati inatambua umuhimu wa mradi huu hasa kutokana na faida zake kiuchumi na inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo:-

(i) Elimu juu ya manufaa ya gesi kwa jamii na Taifa itolewe kwa Wenyeviti wa Vitongoji, Vijiji/Mitaa, Madiwani na Wenyeviti wa Halmashauri katika Mikoa ya Mtwara na Lindi itolewe ili waje wawaelimishe wananchi. Elimu hii pia itolewe kwa viongozi wa makundi mbalimbali ya kijamii.

(ii) Viongozi waliotajwa katika namba moja hapo juu wahimizwe ili kwenda kwa wananchi wote na kuwapa elimu juu ya umuhimu na manufaa ya Sekta ya gesi katika jamii yao na taifa kwa ujumla.

(iii) Serikali ianishe miradi yote ya uwekezaji katika Mikoa ya Mtwara na Lindi na usiwepo ucheleweshaji wowote katika utoaji wa vibali. Mfano Viwanda vya saruji, mbolea, chuma na kadhalika.

(iv) Huduma kwa jamii (*Corporate Social Responsibility*) ni za msingi sana kwa jamii. Kamati inashauri ni vyema wananchi wenyewe waamue aina ya huduma wanayotaka kufanyiwa/kupewa badala ya kuamuliwa na hivyo kuleta kutokuelewana.

(v) Serikali ihakikishe kuwa mapato yoyote yanayokwenda kwa jamii kutoka Serikalini au kwa wawekezaji iyasimamie kwa kina ili yawafikie walengwa hii ni pamoja na Huduma kwa jamii (*Corporate Social Responsibility)* na *Service Levy.*

(vi) Kutokana na sekta kuwa ngeni miongoni mwetu, zipo fikra kuwa uzalishaji utaanza mara moja, naomba kuwaambia Watanzania kuwa matunda ya gesi ni kuanzia miaka 8-10.

(vii) Wananchi wengi hutarajia kupata ajira hata kama hawana utaalam wa fani ya gesi. Kamati inashauri Wizara kuwatumia wazawa kwa kazi ambazo hazihitaji utaalamu na kuendelea kutoa elimu kwa umma kwa kutumia njia mbalimbali ili kuongeza uelewa wa wananchi hali itakayosaidia kupunguza migogoro mara gesi itakapogundulika katika maeneo mengine.

(viii) Kamati imejipanga mara baada ya bajeti hii kwenda Mtwara na Lindi kuyasikiliza na kuongea na makundi mbalimbali ya jamii na wananchi ili kuweza kuishauri Serikali namna bora ya kutatua migogoro iliyopo. Kamati inawasihi wananchi wa Mtwara na Lindi watulie na wategemee Kamati itawasikiliza vizuri na kuishauri Serikali kwani hakuna migogoro inayokosa utatuzi.

Mheshimiwa Spika, gesi inayopatikana mpakani kati ya Tanzania na nchi nyingine. Kwa tafiti zinazoendelea inaonyesha kuna uwezekano mkubwa wa kuwa na miamba ambayo inahifadhi matufa na gesi kukatiza mipaka ya nchi mbili. Kamati ilielezwa kitalu 1A na 1B ambavyo viko mpakani na nchi ya Msumbiji kwa upande wa Msumbiji wameshagundua kuna gesi nyingi sana maeneo hayo. Vilevile

kuna dalili za kugundulika gesi kati ya mpaka wa Tanzania na Malawi, Tanzania na Kenya, Tanzania na Jamhuri ya Watu wa Kongo (DRC). Kamati inashauri:-

(i) Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje wachukue hatua za haraka kutumia diplomasia kuzungumzia jinsi ya kuingia mikataba ya kuchimba gesi hiyo kwa pamoja (*Unitization*) kwani kila nchi kuchimba peke yake ndio huwa kuna malalamiko ya kudhulumiana na hivyo kuwa na migogoro isiyoisha. Mikataba kama hii ya pamoja sio migeni ipo pia katika nchi za Thailand na Malyasia.

(ii) Maeneo yote yenye miamba ya gesi inayokatiza nchi mbili na maeneo yote yaliyogundulika gesi, ni vema Wizara ya Nishati na Madini wakaendelea kushirikiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ili ulinzi wa uhakika utolewe kwenye mipaka yetu kwa gharama yoyote ile kwa vile kuna tishio la uharamia Baharini na Ziwa Tanganyika kwa meli za utafutaji.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati inashauri Serikali kupitia Hazina iwaongezee bajeti Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa ajili ya kutekeleza jukumu hili kwa vile sio jukumu lao maalum kwa ulinzi wa utafutaji mafuta, kwa sasa Wizara ya Nishati ndio inasaidia kibajeti ili ulinzi huo ufanyike na hivyo kuongeza gharama za utafutaji wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa Mafuta na Gesi kwenye Hifadhi za Taifa. Kamati ilielezwa kwamba ni nia ya *TPDC* kufanya utafiiti kwenye Hifadhi za Taifa ili kuona kama kuna mafuta au gesi. Shirika limeshindwa kufanya hivyo kutokana na Kanuni za utekelezaji wa shughuli hiyo kutokamilika kwa muda wa miaka mitano sasa ambapo Sheria ilipitishwa toka mwaka 2009. Kamati inashauri Wizara ya Maliasili na Utalii kukamilisha Kanuni hizo ili Shirika liweze kutekeleza shughuli zake za utafiti wa mafuta na gesi katika maeneo hayo kwa maslahi ya Taifa. Aidha, Kamati inashauri Wizara husika kuhakikisha usalama wa rasilimali ya wanyamapori katika hifadhi zetu wakati wa utafiti huo.

Mheshimiwa Spika, *TPDC* kuchimba gesi katika maeneo maalum. *TPDC* iandaliwe kimkakati ili iweze kujihusisha kikamilifu katika shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi. Historia inaonyesha kuwa *TPDC* kwa kutumia wataalam wazalendo imewahi kuhusika katika uchimbaji wa gesi katika kisiwa cha Songo Songo kwa mafanikio makubwa. Kwa kuanzia Kamati inashauri *TPDC* ianze kazi kwa kuchimba katika vitalu 1A na 1B vilivyo mpakani na Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji *(EWURA).* Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) ilianza kazi rasmi mwaka 2006 kwa lengo la kudhibiti huduma za nishati (umeme, bidhaa za petroli na gesi asili) na maji safi na maji taka mjini. Kwa misingi hiyo basi *EWURA* ndiyo mamlaka ya kulinda maslahi ya walaji, kuimarisha ushindani wa haki na kusimamia masuala ya uchumi na ufundi.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo majukumu ya *EWURA* yalivyo ni pamoja na kudhibiti huduma za nishati (umeme, bidhaa za petroli na gesi asili) Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, ubora wa mafuta. Ubora wa mafuta jambo la msingi katika biashara ya mafuta kwani kinyume na hapo ni kuharibika kwa vyombo vinavyotumia mafuta yasiyo na ubora. Pamoja na taarifa zinazotolewa na *EWURA* kuhusu mafanikio ya kudhibiti ubora, lakini tatizo bado lipo katika baadhi ya maeneo. Kamati inashauri:-

(i) Kutokana na gharama kubwa za kupima sampuli za mafuta nje ya nchi na kwa kuzingatia kwamba zipo maabara ndani ya nchi zinazoweza kufanya kazi hiyo, kwa mfano maabara ya *TBS*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mkemia Mkuu wa Serikali, Serikali izijengee uwezo maabara hizi ili ziweze kutoa huduma hii kwa haraka na kwa gharama ndogo.

(ii) Kwa kuwa *EWURA* imepanga kujenga

maabara yake yenyewe ya kupima ubora ili kujiridhisha na ubora wa mafuta na kwa kuwa maabara hiyo inapaswa ijengwe katika eneo la *TPA* ambako mafuta yanashushwa, Wizara ya Uchukuzi isaidie upatikanaji wa eneo haraka kwani Kamati imeelezwa kuwa *TPA* wamekuwa wagumu kutoa eneo la kujenga maabara kwa *EWURA*.

(iii) Kwa kuwa chanzo cha mafuta yachujwayo katika gesi (*condensate*) hutumika kuchakachua mafuta jamii ya petroli (dizeli na mafuta ya taa) ni kisiwani Songosongo na wanunuzi wake wanajulikana, Kamati inashauri *EWURA* ichukue jitihada ya kudhibiti mafuta haya kabla ya kuingia sokoni.

(iv) Kumekuwepo viashiria dhahiri vya makampuni yanayopewa msamaha katika mafuta yanayotumika katika kuchimba madini kuyauza mtaani. Kamati inashauri *TMAA* na EWURA watathmini matumizi na mahitaji halisi ya makampuni hayo ili kudhibiti mafuta yanayotumika kukwepa ushuru.

(v) Kwa kuwa upo umuhimu wa kudhibiti Sekta ya Maji na wakati huohuo limekuwepo ongezeko la uhitaji wa udhibiti wa sekta ya nishati, Kamati inashauri tena ziwepo Mamlaka mbili za Kudhibiti Maji na nyingine ya Nishati.

(vi) Kamati inapendekeza *EWURA* kubuni utaratibu wa kusambaza mafuta mpaka vijijini utakaozuia utaratibu wa sasa ambapo mafuta huuzwa katika chupa za maji au mifuko ya plastiki hali hii inaathiri ubora wa mafuta na hatari kwa usalama wa watumiaji na jamii.

Mheshimiwa Spika, bei ya mafuta. Pamoja na udhibiti wa bei unaofanywa na *EWURA*, bado bei ya mafuta kwa baadhi ya maeneo ipo juu. Kamati inashauri yafuatayo yafanyike ili kupunguza makali ya bei hasa kwa mlaji:-

(i) *EWURA* iendelee kufanya ukaguzi wa kushtukiza katika vituo vya mafuta na ikiwakamata wahalifu adhabu kali itolewe ili iwe fundisho.

(ii) *EWURA* ifuatilie kwa ukaribu mafuta yanayosafirishwa nje ya nchi (*Transit cargo)* kwani mengi yamekuwa yakiishia humuhumu nchini. Aidha, mbinu za kisasa zitumike ikiwa ni pamoja na kufunga *device control* kwenye magari.

(iii) *EWURA* ishirikiane na mamlaka zingine ili kudhibiti mafuta ya aina yoyote yasiingie nchini bila kulipa ushuru.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Wingi (*Bulk Procurement System*). Mfumo wa kuagiza mafuta kwa wingi una manufaa makubwa ukilinganisha na utaratibu wa kuagiza/kununua kiasi kidogo. Tangu kuundwa kwa mfumo huu manufaa kadhaa yamepatikana ikiwemo ni pamoja na kupungua kwa msongomano wa meli bandarini na kupata takwimu sahihi za kiasi cha mafuta kinachoingia nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na faida za mfumo huu zilizotajwa hapo juu, Kamati inashauri:-

(i) Serikali isimamie mfumo huu kwa karibu kwani wakati wa kujenga hoja ya kuingia katika mfumo huu Watanzania waliaminishwa kuwa meli zitakazotumika zingeshusha gharama za usafirishaji *(premium*) mpaka dola 20 – 25 kwa tani yaani kwa kutumia meli za *LR* (*Long Range*) zenye uwezo wa tani 100,000 na zaidi badala ya *MR* (*Medium Range*) zinazobeba tani 35,000 – 40, 000.

(ii) Serikali ihakikishe ucheleweshaji wa meli katika Gati la Kurasini (*Kurasini Oil Jetty)* umepunguzwa mpaka kiasi kinachokubalika.

(iii) Makampuni ya Mafuta yaboreshe haraka sana mfumo wa mabomba ili kukidhi kasi ya kushusha mafuta iliyopangwa awali.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Taifa ya Mafuta *(COPEC).* Kwa miaka mitatu sasa Kamati ya Nishati na Madini

imekuwa ikishauri juu ya umuhimu wa kuunda Kampuni ya Taifa ya Mafuta bila mafanikio. Inasikitisha kuona Taifa kubwa kama hili letu halina Kampuni ya kuendesha biashara ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ikafahamu kuwa wakati umefika sasa Kampuni hii ianzishwe ili nchi iwe na uhakika wa upatikanaji wa mafuta nchini na Serikali isimamie yenyewe biashara hii badala ya kusubiri wafanyabiashara ndiyo waisimamie.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilieleze Bunge kwa nini haitaki kuunda Kampuni hii muhimu kwani ni ukweli ulio wazi kuwa nchi nyingi duniani zimefanikiwa kutokana na kuwa na Kampuni yake ambayo ndiyo imekuwa kiongozi katika kuhakikisha usalama wa mafuta katika nchi.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini. Pamoja na ukweli ulio wazi kuwa nchi yetu imebarikiwa kuwa na madini ya aina mbalimbali, mchango wa sekta hii katika uchumi wa taifa na maendeleo ya jamii unaonekana kutokidhi matarajio ya wananchi ikilinganishwa na sekta nyingine za uchumi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba madini ni sehemu ya maeneo ya kipaumbele kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Kamati haioni dhamira ya dhati katika kutelekeza hili kwani bajeti iliyotengwa katika kuendeleza sekta hii hairidhishi. Kwa mfano, zimetajwa Taasisi za *GST*, Chuo cha Madini, *TMAA* na *TANSORT* kuwa miundombinu yake itaimarishwa lakini fedha zilizotengwa ni kidogo na mara nyingi huwa hazitoki zote. Kamati inashauri:-

(i) Serikali ihakikishe inatenga fedha za kutosha na zitolewe kwa idara na vitengo husika kwa wakati ili sekta hizi ziweze kuchangia katika ukuaji wa Pato la Taifa.

(ii) Kwa kuwa mojawapo ya sababu zinazotajwa kuwa ni chanzo cha Taifa kutopata gawiwo zuri kutokana na sekta hii ni utaratibu wa kutumia Mikataba ya *concession* katika kugawana mapato. Kamati inashauri Serikali,

ihakikishe kuanzia sasa migodi mipya inazingatia njia zenye tija kama ile inayotumia kwenye mafuta na gesi (*Production Sharing Agreement*).

(iii) Kwa kuwa sekta hii ya madini imekosa muingiliano wa moja kwa moja na shughuli za wananchi walio wengi, Kamati inashauri Serikali ichukue hatua za makusudi ili kuwawezesha wananchi ili shughuli zao ziweze kuhusiana na shughuli za sekta ya madini kama ufugaji, kilimo cha mbogamboga na kadhalika. Ni imani yetu kuwa iwapo vyakula na vinywaji vinavyotoka nje ya nchi vitanunuliwa kutokana na mazao yanayozalishwa na wananchi, haraka sana wananchi na Taifa kwa ujumla tutaona faida ya Sekta hii.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ukagzi wa Madini Tanzania *(TMAA).* Lengo la *TMAA* ni kuhakikisha kuwa Serikali inapata mapato stahiki kutoka kwenye biashara ya madini hapa nchini. Tangu kuanzishwa kwake, Wakala umesaidia Serikali kupata jumla ya shilingi bilioni 1.801 kutoka kwa wamiliki wa migodi mikubwa na ya kati kwa kipindi cha kuanzia Julai 2012 hadi Februari, 2013, kuongezeka kwa malipo ya mrabaha yatokanayo na madini ya ujenzi kutoka shilingi milioni mbili kwa mwaka zilizokuwa zinakusanywa kabla ya Wakala kuanzishwa hadi shilingi milioni 731.4 kwa mwaka; kuanza kwa matumizi ya lakiri za kisasa kwa wachimbaji wadogo wanaotumia kemikali ya *cyanid*e katika kudhibiti na kukagua shughuli zao na uanzishwaji wa Madawati Maalum ya kukagua madini kwenye viwanja vya ndege. Pamoja na yote hayo kufanyika ambapo kutokana na kazi ya Wakala mapato ya Serikali yameongezeka jamii haina taarifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri:-

(i) Wakala kujitangaza kwa kutumia vyombo vya habari, mtandao na kutengeneza vijarida mbalimbali ili kuelimisha jamii faida iliyopatikana toka kuanzishwa kwake na jinsi inavyosaidia katika sekta nzima ya madini.

(ii) Wakala uanzishe ofisi zake hadi Mikoani kuliko kuwatumia Maafisa Madini Kanda ambao utendaji wao hulalamikiwa mara kwa mara kuwa sio mzuri.

(iii) Serikali itoe kibali cha ajira cha watu 12 ambacho kimeombwa kwa muda mrefu lakini mpaka sasa hakijatoka. Aidha, UTUMISHI na Serikali kwa ujumla iliangalie upya suala hili la utoaji vibali vya ajira kwa vile kwa sasa limekuwa ni kikwazo katika maeneo mengi ya utumishi nchini. Serikali ilipe kipaumbele cha pekee suala hili la ajira kwani kazi inayofanywa na Wakala ni muhimu sana katika kuongeza mapato.

(iv) Kwa kuwa kazi mojawapo ya Wakala ni kusimamia na kukagua shughuli za ukarabati na utunzaji wa mazingira katika maeneo ya wachimbaji wadogo, wa kati na wakubwa na kwa kuwa kumekuwepo na uharibifu mkubwa wa mazingira unaofanywa na wachimbaji na watafutaji wa madini hasa kwenye vyanzo vya maji. Kamati inashauri Wakala ujizatiti kufanya ukaguzi kwenye maeneo yote yenye uchimbaji wa madini ili kujiridhisha uchimbaji huo unafanyika kwenye maeneo ambayo si vyanzo vya maji na kupelekea kuhatarisha maisha ya watu hasa kwa vile utumiaji wa sumu katika suala la madini ni mkubwa hivyo kuweza kusababisha vifo kwa binadamu na wanyama wa maeneo husika.

(v) Kamati inapendekeza pamoja na majukumu yake, *TMAA* ipitie maeneo yote yaliyochimbwa madini na kutathmini kwa kina madhara yaliyotokana na kuchimba madini. Kutokana na uzoefu wa uchimbaji wa madini katika Mkoa wa Geita, mashimo yaliyoachwa baada ya shughuli hii, yamekuwa madimbwi na mabwawa makubwa ambayo yamekuwa mazalia ya mbu hali iliyopelekea Mkoa wa Geita kuwa Mkoa wenye maambukizi makubwa sana ya ugonjwa wa malaria.

(vi) Moja ya changamoto ya Wakala iliyoelezwa ni kutokuwa na jengo lake la kudumu kwa ajili ya utekelezaji

wa majukumu yake ya kila siku, *TMAA* inatafuta kiwanja cha kujenga jengo ambalo litajulikana kama *Madini House* ambapo huduma zote kuhusiana na madini zitapatikana ndani ya jengo moja ikiwa ni pamoja na shughuli za *TRA*, Benki, *Strong room* ambapo mteja yeyote ataruhusiwa kuhifadhi madini yake kwa kulipia na ikiwezekana hata kuwa na sehemu ya kutua na kurukia helkopta ili kurahisisha usafirishaji wa bidhaa hii. Kamati inashauri Wakala isaidiwe kifedha hasa fedha za maendeleo ili iweze kufanikisha azma hii ambayo inaonekana ni nzuri na itarahisisha biashara ya madini nchini.

(vii) Kamati ilielezwa kwamba kwa mwaka 2011, Wakala kwa kushirikiana na Ofisi ya Madini Kanda ya Mashariki ilibuni mkakati maalum wa kukagua madini ya ujenzi (kokoto na mchanga) katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kwa kutumia Hati ya Mauzo. Katika kipindi hicho hadi Februari, 2013 jumla ya tani 2,578,646 za madini hayo zenye thamani ya shilingi bilioni 24.1 yalizalishwa na wamiliki wa leseni za madini ya ujenzi na mrabaha wa shilingi milioni 723 ulilipwa Serikalini ikiwa ni ongezeko kubwa ikilinganishwa na wastani wa shilingi milioni mbili (2) tu kwa mwaka zilizokuwa zikilipwa Serikalini na wamiliki wa leseni za madini ya ujenzi kabla ya *TMAA* kuanzisha ukaguzi huo. Kamati inapongeza *TMAA* kwa hatua hiyo ambayo imesaidia kuongeza mapato ya Serikali tunashauri ukaguzi huu sasa ufanyike katika Mikoa yote.

(viii) Kamati ilielezwa kwamba *TMAA* imeamua kuanzisha Madawati Maalum ya kukagua madini yanayosafirishwa nje ya nchi kupitia viwanja ya ndege vya Julius Nyerere Dar es Salam, Kilimanjaro na Mwanza. Madawati haya yamesaidia kukamatwa kwa madini yenye thamani ya shilingi bilioni 13 yaliyokuwa yakisafirishwa nje ya nchi kinyume cha sheria na wahusika walichukuliwa hatua za kisheria. Tunapongeza *TMAA* kwa uzalendo wao. Aidha, Kamati inashauri mbali na kuwa na Madawati Maalum katika viwanja vya ndege Madawati hayo yawekwe katika njia zote za kutokea ikiwa ni pamoja na bandari na vivuko vya mpakani.

(ix) Serikali ianze mchakato wa kuifanya *TMAA* kuwa Mamlaka ili ifanye kazi zake kwa ufanisi zaidi. Kwa kufanya hivyo chombo hiki kitapata nguvu kisheria za kuisaidia Serikali kupata mapato zaidi kwenye sekta hii ya madini na utunzaji wa mazingira katika nchi. Ushauri huu ulitolewa pia na Kamati iliyopita wakati wakiwasilisha maoni yao kwenye Mkutano wa Bajeti 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Kuthamini Almasi na Vito *(TANSORT). TANSORT* iliundwa mwaka 1966 na ofisi zake mwanzo zilifunguliwa London nchini Uingereza ili kuchambua na kusimamia mauzo ya almasi za Tanzania. Mwaka 2010 ilihamishiwa nchini Tanzania na kuongezewa majukumu mapya ambayo ni kuthaminisha almasi na madini ya vito kwa ajili ya kukokotoa mrabaha, kutayarisha miongozo ya bei (*price guides*), kutoa huduma za kijemolojia (*Gemmological service*) kwa wachimbaji wadogo na wa kati, kusimamia mauzo ya almasi na madini ya vito ndani na nje ya nchi, kufanya tafiti za masoko na bei za almasi na madini ya vito na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Kitengo kutokana na shughuli za uthamini ilifanikiwa kupata jumla ya dola za kimarekani 651,653 sawa na shilingi bilioni moja na kilitoa huduma za uthamini na uchambuzi wa almasi na vito kwa makampuni 19 tofauti na awali ambapo huduma ilitolewa kwa makampuni mawili tu na ukaguzi ulifanyika maeneo ya uzalishaji wa almasi ya Arusha, Shinyanga, Songea na Tunduru.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo ambayo ni ya kipindi kifupi cha takribani miaka minne tangu Kitengo kihamie Tanzania, zipo changamoto nyingi ambazo Kamati imezibaini na zinahitaji ufumbuzi wa haraka:-

(i) Kutokuwepo kwa kada ya Wajemolojia (*Gemmoligist*) katika muundo wa Kada za Utumishi wa Serikali. *TANSORT* ina uhaba mkubwa wa watumishi wa kada ya Jemolojia (*Gemmoligist*) na imeshindikana kuwaajiri kwa

sababu kada hiyo haimo katika muundo wa Utumishi wa Serikali. Watumishi waliopo wa kada hii wanatambuliwa kwa kada zao za awali ambazo ziko kwenye Muundo wa Utumishi wa Serikali. Kamati inashauri Ofisi ya Rais- Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini ilishughulikie tatizo hili kwa kulipa uzito unaostahili kwani kwa kutowatambua watu wa kada hii inakifanya Kitengo kutopata watumishi wenye utaalam kwa viwango vinavyokubalika kimataifa kwani waliopo hawavutiwi kujiunga kutokana na maslahi kuwa madogo ukilinganisha na maslahi halisi ya kada hii. Kamati inasisitiza muundo huu ufanyiwe kazi haraka ili wataalam wavutike ili kuongeza ufanisi.

(ii) Kutokuwepo kwa Jengo la ofisi. Kamati imebaini Kitengo hiki hakina ofisi yake na hakuna vyumba salama kwa ajili ya kazi ya uthamini. Kamati inashauri kwa vile kazi ya uthamini wa vito na almasi inahitaji usiri na usalama wa hali ya juu ili kumpa mteja amani kwamba yuko kwenye mikono salama, Serikali itenge fedha kwa ajili ya kujenga jengo *(Madini House)* ambalo litaweza kutumiwa na taasisi zote zinazohusika na madini ikiwemo na *TMAA* ili kurahisisha utoaji wa huduma hizi za madini nchini. Aidha, ofisi za Kanda zinazosimamiwa na Kitengo ziwezeshwe kupata vyumba salama na vifaa vya kisasa vya kazi ya uthamini ili watekeleze majukumu yao kama inavyotarajiwa. Aidha, wakati jengo la kudumu linatafutwa Wizara ifanye jitihada za kutafuta jengo la muda.

(iii) Soko la ndani la Almasi na Vito. Kwa sasa hapa nchini hakuna soko au kituo maalum cha kufanyia biashara ya Almasi na vito hali inayowalazimu wafanyabiashara kwenda kuzitafuta kwenye chanzo (migodi), hali hii inasababisha tatizo la kutapeliwa na kudanganywa na Serikali kupoteza mapato. Kamati inashauri Wizara ishirikiane na Mifuko ya Hifadhi za Jamii kama *NSSF, PPF, LAPF* ili kuona uwezekano wa kujenga soko hili kwa *joint venture* na biashara hii ijulikane inafanyika wapi, hii itasaidia

kuongeza mapato ya Serikali na itaondoa udanganyifu na itapunguza kutapeliwa kwani wataenda kuuza sehemu ambayo bei inajulikana na salama.

(iv) *Directory* ya *Licensed Dealers* wa Madini, Vito na Almasi. Kamati imebaini kuwa kwa sasa hakuna *Directory* maalum ya watu ambao wamepatiwa leseni za Madini, Vito na Almasi na hivyo kuchochea suala zima la utapeli na kwa kiwango kikubwa waliopo ni matapeli. Kamati inashauri *Directory* hiyo ianzishwe ili mtu yeyote anayetaka kuuza au kununua bidhaa hizo awe na mahali pa kuwapata wafanyabiashara wenye leseni za uhakika.

(v) Elimu kwa umma. Kitengo hiki kwa asilimia kubwa hakifahamiki kwa Watanzania walio wengi na hata kwa Waheshimiwa Wabunge. Hivyo Kamati inashauri kwamba ni vyema Kitengo kifanye jitahada za kujitangaza kwa jamii kupitia mbinu mbalimbali iwe ni kupitia redio, televisheni, semina, vipeperushi na majarida mbalimbali yanayoelezea nini kitengo kinafanya.

(vi) Kuchakata madini nje ya nchi. Kamati bado inasikitishwa na utaratibu wa kuchakata madini yetu nje ya nchi kwani kwa kufanya hivyo tunapoteza ajira za vijana wetu na pia mabaki ya madini hayo ni mali yana thamani kwa kuwa hutumika kwa shughuli nyingine nyingi. Kamati na Watanzania walio wengi wanaonyesha mashaka makubwa juu ya utaratibu huu wa kupeleka mchanga nje ya nchi. Kamati inashauri Serikali kupitia upya utaratibu huu na kuja na utaratibu ambao utawezesha zoezi hili kufanyika bila kuwa na mashaka miongoni mwa wadau.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO).* Shirika la Madini la Taifa ni miongoni mwa Mashirika yaliyokuwa kwenye orodha ya mashirika ya kufutwa na kampuni zake tanzu kukabidhiwa kwa Msajili wa Hazina (*Treasurer Registrar*). Mwezi Machi, 2009, *STAMICO* iliondolewa kwenye orodha ya kufutwa; *STAMICO* imeanza kujijenga upya na jukumu lake kubwa ni kuwekeza katika utafutaji,

uendelezaji na uchimbaji wa madini, kusimamia hisa za Serikali katika migodi, kutoa huduma za kibiashara katika sekta ya madini kama uchorongaji miamba, utafutaji wa madini na utoaji ushauri katika masuala ya madini na kuratibu uendelezaji wa wachimbaji wadogo nchini. Mpaka sasa Shirika lina leseni 18 za utafutaji madini, 14 ni za utafutaji wa madini ya dhahabu na nne (4) ni za urani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na *STAMICO* kusimama kwa muda mrefu, imekuwa na changamoto kadhaa zikiwemo za uhaba wa watumishi, hisa za *STAMICO* kuwa chini ya Msajili wa Hazina bila ya kujua zinasimamiwaje kwa manufaa ya Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo Kamati inatoa maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo:-

(i) Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilipe suala la ajira kwa *STAMICO* kipaumbele cha kwanza kwani waajiriwa waliopo karibu wote wanastaafu. Utumishi ifanye kila inalowezekana na kwa haraka ili *STAMICO* ipate watumishi inaowahitaji. *(Makofi)*

Aidha, wakati hao watumishi wengine watakapopatikana na kama hawa waliopo muda wao wa kustaafu utakuwa umefika, ni vyema wakapewa mikataba kwa taratibu za kiutumishi ili wawafundishe vijana watakaochukua nafasi zao kwa vile wamekuwepo kwa kipindi kirefu hata shirika lilipotaka kufutwa bado walikuwa wazalendo kulipigania.

(ii) Kamati imebaini kuwa wakati wa kutaka kuifuta *STAMICO*, mali zake zilipelekwa kwa Msajili wa Hazina *(TR)* ili kuzisimamia ikiwa ni pamoja na hisa zake asilimia 25 (25%) katika Kampuni ya *Williamson Diamonds Ltd (WDL).* Kamati inashauri na hisa hizo warudishiwe waweze kuzitumia kwa mujibu na taratibu ili *STAMICO* iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. *(Makofi)*

(iii) Mgodi wa Kiwira ukabidhiwe *STAMICO* na mradi wa kuzalisha umeme *MW 200* kwenye mgodi huo uanze mara moja. Mradi huu ukianza mapema utawezesha *TANESCO* kuachana na mitambo ghali ya kukodi mara moja. Kamati imesikitishwa kuona sehemu ya Mgodi wa Kiwira hasa mlima Kabulo leseni yake yenye namba SML 235/2005 ilihamishwa kinyemela kutoka *Tanpower Resources Ltd* kwenda *Tanzacoal East Africa Mining Ltd* tarehe 06/08/2011. Kamati inashauri Serikali kuinunua leseni hii upya na kuikabidhi *STAMICO* kwa ajili ya kuendeleza mgodi wa Kiwira. *(Makofi)*

(iv) Kutokana na *STAMICO* kufanyiwa marekebisho makubwa ili liendane na majukumu yake mapya na ya kibiashara, Kamati inasisitiza umuhimu wa kujiendesha kibiashara na isitegemee *free carried interest* pekeyake na badala yake Shirika litafute mbinu zingine za kibiashara ikiwepo kujiunga na soko la hisa (*stock market*) kwani njia hii itawapa fursa Watanzania wengi kumiliki rasilimali zao.

(v) Kwa kuwa Bunge lilishawahi kutoa Azimio kuwa *STAMICO* ishiriki katika uchimbaji wa madini ya vito na almasi na *uranium*, ni vyema likawezeshwa kifedha ili liweze kuchukua miradi hiyo kwa maslahi ya Taifa kuliko kuwapa wawekezaji binafsi.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo. Pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali kuongeza bajeti ya wachimbaji wadogo, bado Kamati hairidhishwi kwani wachimbaji wadogo wana matatizo mengi yakiwemo ya ukosefu wa vifaa vya kufanyia kazi, uhaba wa maeneo ya kufanyia kazi na elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Pamoja na taarifa ya Wizara kuwa wameanza taratibu za kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo ambapo maeneo 16 nchini

yametengwa katika Mikoa ya Dodoma, Singida, Tanga, Morogoro, Pwani, Tarime, Mbeya, Tunduru, Kigoma, Mpanda, Simanjiro na Kilimanjaro. Kamati inaitaka Wizara kuharakisha utaratibu huo ili wachimbaji wadogo wapate maeneo hayo mapema. Aidha, Mikoa mingine nchini nayo itengewe maeneo hayo.

(ii) Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza ushauri wa Kamati iliyopita uliotolewa wa kutaka Serikali iwasaidie wachimbaji wadogo kupata mikopo. Kamati imefahamishwa kuwa Serikali imeanzisha Mfuko wa kuwaendeleza wachimbaji wadogo na imeshaamuliwa fedha za mfuko huo zitapitia Benki ya Rasilimali *(TIB).* Kamati inashauri kutokana na ukweli kwamba Benki hii haipo mpaka vijijini walipo wachimbaji wadogo na kwa uzoefu uliopatikana kutokana na Dirisha la Kilimo lililopo *TIB* na Benki ya Wanawake iliyopo Dar es Salaam, ni vyema Mfuko huo ukawekwa kwenye Benki ya *NMB* ambayo ina matawi mpaka ngazi ya chini ili wachimbaji wadogo waweze kufaidika na kutosumbuka kuja mpaka Dar es Salaam kufuatilia mikopo katika Mfuko hiyo.

(iii) Kamati bado haijaridhishwa na kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo hasa ikizingatiwa kuwa changamoto za kifedha walizonazo ni nyingi. Kamati inashauri Serikali kuendelea kuongeza bajeti ili wachimbaji wadogo waweze kunufaika na hivyo kuleta tija katika kazi.

(iv) Kamati inashauri Serikali iendelee kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo ili waweze kufahamu mbinu bora za utafutaji, uchimbaji, uongezaji thamani madini na masoko.

(v) Kamati ina taarifa kuwa kuna ukwepaji wa kodi na tozo za Serikali hasa miongoni mwa wazalishaji na wafanyabiashara wadogo, wa kati na wale wakubwa katika

maeneo mengi ya uchimbaji wa madini ya vito na almasi na madini mengine, wengi wao hawasemi ukweli wa kile wanachozalisha. Kamati inashauri *TRA* washirikiane na Wizara ili kufuatilia na kuwabaini ili waweze kulipa kodi na tozo stahili za Serikali.

(vi) Elimu kwa wachimbaji wadogo itolewe hasa kuhusiana na utunzaji wa mazingira kwani wengi wanachimba sehemu moja na wanapokosa wanahamia sehemu nyingine bila kufukia eneo la awali kitu ambacho ni hatari kwa maisha ya binadamu na wanyama.

(vii) Kamati inachukizwa na utaratibu wa kuwaondoa wachimbaji wadogo mara madini yanapogundulika na kupewa wawekezaji wakubwa au kupewa maeneo ambayo hayaruhusiwi kuchimbwa mfano maeneo ya shule, barabarani na hivyo kuleta usumbufu. Kamati inashauri Wizara iliangalie suala hili kwa umakini ili kuwapatia leseni katika maeneo yasiyo na migogoro ili wafanye kazi zao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Jiolojia. Tanzania ina rasilimali kubwa ya madini na ili kufahamu sehemu yalipo kazi kubwa inabidi ifanyike kwa lengo la kuifahamu nchi kijiolojia na hivyo kuweza kufahamu takwimu sahihi za rasilimali zilizopo ikizingatiwa kuwa yapo maeneo mengi ambayo bado hayajafanyiwa utafiti. Kamati imebaini kuwa Wakala unakabiliwa na tatizo la upungufu wa vifaa vya kisayansi pamoja na programu za komputa za kisasa kwa ajili ya kuchambulia takwimu. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali iiwezeshe kifedha ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona katika mwaka huu wa fedha unaoishia Wakala uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya miradi ya maendeleo, lakini mpaka tunaandika taarifa hii hakuna fedha yoyote iliyotolewa. Ifike mahali tuwe wawazi na kuacha kuwa tunaidhinisha fedha

ambazo hazitoki kwani utaratibu huu unaharibu mipango ya taasisi zetu. Kitengo hiki ni nyeti na muhimu, Serikali itueleze ni kwa nini Kitengo hiki hadi leo hakijapewa fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo?

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Madini Dodoma. Chuo cha Madini ndiyo chuo kikubwa hapa Afrika ya Mashariki lakini inashangaza kuona chuo hiki hakina muundo na hii inatokana na ukweli kwamba kilianzishwa kufuatia agizo la Waziri wa wakati huo. Kwa mara kadhaa Kamati ya Nishati na Madini imeshauri Chuo hiki kitungiwe sheria ili kiwe na Muundo wake na ngazi zake za Mshahara hasa ikizingatiwa ukuaji wa kasi wa Sekta ndogo ya gesi ambayo inategemea Chuo hiki katika kutoa wataalam wa kuisimamia.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa chuo hiki katika sekta ya madini nchini, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo:-

(i) Kamati inarejea ushauri wake iliutoa hapo awali kuwa Wizara ilete sheria ili chuo hiki kiundwe rasmi kwani kiliundwa kwa tu tamko la Waziri wa wakati huo.

(ii) Kamati imefedheheshwa na utaratibu wa Chuo kutumia Walimu wa mikataba kufundisha baadhi ya masomo kutokana na wakufunzi waliopo kutokutosheleza mahitaji. Mheshimiwa Spika, ikumbukwe Chuo hiki ndio tegemeo la nchi katika kutoa elimu ya masuala ya madini. Kwa kuwa sasa hivi chuo kinaandaliwa pia kutoa elimu katika sekta ya gesi ambayo inakua kwa kasi ya juu, Kamati inashauri Serikali ihakikishe Chuo hiki kinapatiwa wakufunzi wa kutosha ili kuweza kutoa elimu inayotakiwa.

(iii) Kamati imebaini kuwa miundombinu ya Chuo cha Madini haiendani na mahitaji halisi. Kwa mfano madarasa yaliyopo ni manne tu (4) wakati idadi ya wanafunzi ni takribani 400. Lengo la Chuo ni kuwa na wanafunzi kati ya 500 na 600 endapo miundombinu muhimu kama madarasa

yatajengwa. Katika mwaka wa fedha uliopita 2012/2013, Chuo kilitengewa jumla ya shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo uboreshaji wa miundombinu. Inasikitisha kuona hadi tunaandika taarifa hii fedha hiyo haijatolewa. Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa Serikali ilieleze Bunge kwanini fedha hizi hazijatolewa mpaka sasa.

(iv) Kamati inarudia ushauri uliotolewa mwaka uliopita kuwa Makampuni ya madini yasaidie kuongeza utoaji wa nafasi za mafunzo maalum ya vitendo kwa wanafunzi kwenye migodi yao ili kuwapa utaalam unaoendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, Tasnia ya Uzinduaji – TEITI. Tasnia ya Uziduaji (*Tanzania Extractive Industries Transaparency Initiative – TEITI)* ni sehemu ya Asasi inayohamasisha Uwazi na Uwajibikaji katika mapato yatokanayo na sekta za madini, gesi asili na mafuta. *TEITI* ni muhimu kwa sababu inaisaidia Serikali na wawekezaji katika kuweka uwazi kwenye mapato yatokanayo na rasilimali za madini na gesi ambapo pande hizo mbili zitatakiwa kuweka wazi mapato yake. Hatua hii itawawezesha wananchi kujua mapato halisi kutoka kwa wawekezaji na kiasi halisi kilichopokelewa na serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wake, lakini chombo hakijaundwa rasmi kisheria, Kamati inashauri Serikali ilete Muswada wa Sheria Bungeni ili chombo hiki kiwepo rasmi kisheria na hivyo kuwa na nguvu zaidi.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Kwa dhati ya moyo wangu, napenda kukushukuru tena kwa nafasi uliyonipa. Aidha, napenda kukupongeza kwa kuliongoza vizuri Bunge letu Tukufu wewe mwenyewe, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, hakika mnafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, napenda

kutumia fursa hiii kwa mara nyingine tena kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kushiriki vyema vikao vya Kamati na kuuliza maswali ya kidadisi ambayo yamefanikisha kuandaa Taarifa hii. Wajumbe wamekuwa wakishiriki vyema vikao vya Kamati na kutoa michango ya kujenga Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Victor Kiliasile Mwambalaswa, Mwenyekiti, Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagulla, Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mheshimiwa Devotha Mkuwa Likokola, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mheshimiwa Mariam Nassor Kisangi, Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Charles John Paul Mwijage, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Riziki Saidi Lulida na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo, Mheshimiwa George Simbachawene, Naibu Waziri anayeshughulikia Nishati pamoja na Mheshimiwa Stephen Maselle, Naibu Waziri anayeshughulikia Madini kwa utendaji kazi wao mzuri na ushirikiano wanaoipa Kamati katika kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba ya Kuisimamia na kuishauri Wizara ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana watendaji wote wa Wizara ya Nishati na Madini na hususan Katibu Mkuu Ndg. Eliakim Maswi kwa kuwa wazi katika utendaji kazi wake na kutoa ushirikinao pale ulipohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D.

Kashilillah, pamoja na Makatibu wa Kamati Ndg. Pamela Pallangyo, Asia Minja na Msaidizi wetu Ndugu Kokuwaisa Gondo, kwa kuratibu vizuri shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa hii iingie kwenye *Hansard* kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini, Fungu 58 kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, jumla ya shilingi 1,102,429,129,000/=.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani aliyehusika na Wizara hii, Mheshimiwa John Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA – MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kabla ya kusoma hotuba yangu, nieleze tu kwamba hotuba hii ina jumla ya kurasa 95. Sasa kwa muda wa nusu saa, ni wazi kwamba nitafanikiwa kusoma kurasa chache sana. Kwa hiyo, kwa ruksa yako, naomba hotuba hii iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kwa ukamilifu wake.

Mheshimiwa Spika, la pili, hotuba hii ya kurasa 95, ina maelezo na vielelezo vya msingi ambavyo ni muhimu Waheshimiwa Wabunge wakavizingatia wakati wa mjadala. Ukurasa wa 15 wa hotuba hii una kielelezo kutoka kwenye Ripoti ya Timu ya Kamati ya Wataalamu wa Ofisi ya Spika, ukurasa wa 15 - 29, ambao imechambua mikataba mibovu

inayolipa mzigo mkubwa *TANESCO* kwenye sekta ya umeme na hivyo kuwaongezea mzigo wa gharama za maisha wananchi. Kwa hiyo, si kwamba tu kuna maelezo, kuna uchambuzi kuhusu mikataba hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kwenye Kitabu hiki cha hotuba, ukurasa wa 2, ukurasa wa 44, Kambi Rasmi ya Upinzani, haijaleta michoro kuhusu masuala ya ujenzi wa Bomba la Gesi, bali imehoji kutaka tuletewe Bungeni hapa mikataba, sio michoro peke yake. Kwa hiyo, hayo yapo kunzia ukurasa wa 44 na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 62 - 65, Kambi Rasmi ya Upinzani, imezungumzia kuhusu mambo yanayoendelea nyuma ya pazia juu ya majadiliano kati ya *TANESCO* na *Symbion Power Africa LLC.* Kambi Rasmi ya Upinzani imetoa maelezo ya kina kuanzia ukurasa wa 62 mpaka ukurasa wa 65 juu ya kinachoitwa Hati ya Makubaliano kwa maana ya *MoU* na Kambi Rasmi ya Upinzani imechambua vifungu vya *MoU* hiyo na baada ya maelezo yote ya ukurasa wa 62 mpaka 65, Kambi Rasmi ya Upinzani, imetaka *MoU* hii na mikataba mingine iletwe Bungeni ili tusije tukaingia tena mkenge kama ilivyokuwa kwenye kashfa ya kashfa ya *Richmond.*

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 65 - 67, Kambi Rasmi ya Upinzani, imeeleza kuhusu Mradi wa Umeme Vijijini. Kambi Rasmi ya Upinzani katika kurasa hizi, imetoa maelezo kwa kurejea takwimu za miaka mbalimbali kwamba tatizo letu kama nchi sio tu kutenga asilimia kubwa ya bajeti kwa maana ya 90% ya bajeti, tatizo letu ni kwamba hata fedha zinazotengwa hazitolewi na imetoa mfano kuhusu miradi ya umeme vijijini ambapo mpaka tunavyozungumza ni 13% tu ya bajeti ya mwaka jana imeweza kupelekwa, hali ambayo kwa vyovyote vile haiwezi kufanikisha miradi ya umeme hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba kusoma hotuba hii, ambayo vilevile kwa urefu wake inapatikana katika mtandao wa *mnyika.blogspot.com.*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri wa Nishati na Madini ilianzishwa kwa mujibu wa kipengele cha 21 cha Nyongeza ya Waraka wa Rais uliochapishwa kama Tangazo la Serikali Na. 494 la tarehe 17 Desemba, 2010. Majukumu ya Ofisi hii yameainishwa katika Tangazo la Ukasimishaji wa Majukumu ya Kiuwaziri la mwaka 2010 *(The Ministers (Assignment of Ministerial Functions) Notice,* 2010) lililochapishwa katika Gazeti la Serikali kama Tangazo la Serikali Na. 494A la tarehe 17 Desemba, 2010.

Mheshimiwa Spika, katika kujadili Mapitio ya Utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2013/2014, naomba tuyatafakari maandiko ya katika muktadha wa uongozi wetu wa leo na hatma ya sekta hizi mbili muhimu za nishati na madini.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere katika kitabu chake cha TUJISAHIHISHE katika ukurasa wa pili tutafakari kwamba, naomba kunukuu: “Ukweli una tabia moja nzuri sana. Haujali mkubwa wala mdogo, haujali adui wala rafiki. Kwake wote ni sawa. Pia ukweli unayo tabia ya kujilipiza kisasi kama ukipuuzwa. Ukiniona nataka kulipiga teke jiwe kwa kuwa nafikiri kuwa ni dongo au mpira, natumaini utanionya. Lakini nikilipuuza onyo lako kwa sababu eti wewe ni mdogo au kwa sababu sikupendi, nitalipiga teke, basi litanivunja dole japo ningekuwa nani. Ukweli haupendi kupuuzwapuuzwa”.

Mheshimiwa Spika, tuendelee kutafakari maandiko ya Nyerere kwamba: “Wakati mwingine, mtu tunayempinga huwa ana makosa kweli, lakini hoja tunazozitoa ni za binafsi na hazihusiani kabisa na hoja zake. Nikisema mbili na tatu ni sita, nakosa. Lakini ni bora kunionesha kwamba pengine nilifikiri tunazidisha kumbe tunajumlisha.

Mheshimiwa Spika, ni kweli mbili mara tatu ni sita; lakini mbili na tatu ni tano, siyo sita. Lakini ukijaribu kuwashawishi wenzetu wakatae mawazo yangu na kukubali yako kwa kusema kuwa meno yangu ni machafu au natoa kamasi daima, utakuwa unatumia hoja ambazo hazina maana, huu

ni mfano wa upuuzi; lakini mara nyingi hoja tunazozitumia kuwashawishi watu wakatae mawazo ya wale tusiowapenda au kukubali mawazo yetu, huwa hazihusiani kabisa na mambo tunayojadili".

Mheshimiwa Spika, tutafakari maandiko ya Mwalimu Nyerere katika kitabu chake cha UONGOZI WETU NA HATIMA YA TANZANIA uk. 50, nanukuu: "Rais Mwinyi ni mtu mwema na mpole, lakini ni kiongozi dhaifu; au upole wake na udhaifu wake unatumiwa na watu ambao wala si wema wala wapole kuhatarisha umoja na amani ya nchi yetu, kipindi chake cha pili kinakaribia kwisha".

Mheshimiwa Spika, tutafakari maandiko mengine ya Mwalimu Nyerere kwamba: "Lakini hatulazimiki kuendelea na uongozi mbovu wa Chama na Serikali. Wala tukiendelea na hali hii, bila kubadili uongozi wa Chama na Serikali, sina hakika kama tutafika huko salama. Masuala muhimu ya nchi yetu hayatashughulikiwa. Viongozi wetu wataendelea na matendo yao ya kuvuruga Muungano. Matatizo ya kweli ya Muungano hayatashughulikiwa, maana hatuna Serikali ya kuyashughulikia na masuala mengine muhimu ya uchumi, huduma za umma, rushwa, chuki za uzawa na ukabila na udini yataachwa yajitatue yenyewe.

Nasema katika hili sina hakika kama tutafika salama; na tukifika salama, tukiwa na uongozi huu huu wa Chama na Serikali, mbele yetu kutakuwa ni giza tupu. Majuto ni mjukuu, huja baadaye. Tunaweza tukafikishwa mahali tukilinganisha uongozi wa Rais Mwinyi na wa Rais wa kesho tukaona kuwa chini ya Ndugu Mwinyi, Pamoja na udhaifu wake wote, tulikuwa peponi!"

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere anaendelea kuandika kwamba: *"Waingereza wana msemo: "Nature abhors vacuum"*, "hulka huchukia ombwe." Hata siasa huchukia ombwe. Kama uongozi ni mbovu, upo kama haupo au upo kwa maslahi ya wenyewe, watatokea watu waujaze uwazi uliopo; hauwezi kuachwa wazi hivi hivi. Lakini uongozi mbovu ni kama mzoga, una tabia ya kukaribisha mafisi na

mainzi. Tusidhani kuwa hulka ya siasa yetu ni tofauti na hulka ya siasa ya watu wengine; kwamba sisi tunaweza kuvumilia uongozi mbovu na tusivune matunda ya hulka ya uongozi mbovu".

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere alikuwa akiandika wakati wa awamu ya Rais Mwinyi kuhusu masuala yanayohusu Muungano, sisi tutafakari maandiko haya katika muktadha wa uongozi wa sasa wa Taifa letu na mustakabali wa sekta nyeti kwa uchumi wa nchi na maisha ya wananchi ya nishati na madini.

Mheshimiwa Spika, masuala mtambuka; mapitio ujumla ya utekelezaji kwa mwaka 2012/2013 na makadirio ya mapitio na matumizi kwa mwaka 2013/2014. Tarehe 27 Julai, 2012 niliwasilisha Bungeni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2011/2012 na makadirio ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Kufuatia maoni hayo, yapo masuala machache ambayo Serikali imeyazingatia kwenye utekelezaji na mengine mengi ambayo Serikali haikuyazingatia pamoja na umuhimu wake kwa maslahi ya nchi na maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ilitaka kiwango cha bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kuongezwa, miongoni mwa masuala ambayo Serikali imetekeleza ni pamoja na kuongeza bajeti ya Wizara hii kwa kupanga kutumia kwa mwaka 2013/2014, jumla ya sh. 1,099,434,031,000/= ikilinganishwa na mwaka 2012/2013 ambako kiasi cha sh. 641,269,729,000/= kilipangwa kutumika.

Aidha, napenda kuikumbusha Serikali kuzingatia vipaumbele vya miradi ya maendeleo ambavyo Kambi Rasmi ya Upinzani ilipendekeza katika Hotuba zake za 2011 na 2012 ili kuweza kuleta maana ya ongezeko hili la bajeti kwa maana ya kuvipatia vipaumbele uzito unaostahili kwa kuwekeza

fedha za kutosha kwenye sekta ya umeme na gesi ili kumaliza kabisa tatizo la nishati ya umeme na kupunguza gharama za maisha kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilishauri kuwepo kwa mfumo thabiti wa kuhakikisha maoni na maazimio yanatekelezwa kwa wakati na kwa ukamilifu. Lakini Serikali imeendelea kupuuza mapendekezo hayo na kutoa ahadi ambazo haikuwa tayari kuzitekeleza, mathalani ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyotoa wakati akiahirisha Bunge la bajeti 2011/2012, ya kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ili kuiongezea pesa Wizara ya Nishati na Madini, lakini tofauti na ahadi yake, Serikali ikaamua kuja na mpango wa kukopa fedha katika taasisi za fedha ili kulinusuru Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)*, ambao nao haujatekelezwa kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali hiyo natambua maoni machache ambayo yalizingatiwa kuhusu gesi asili, ikiwemo kuendelezwa kwa mchakato wa kuwa na Sera na Sheria ya Gesi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA ikaitaka Serikali ieleze hatua ilizochukua juu ya maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambayo hayakuzingatiwa na mengine yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge na michango ya Wabunge kwa nyakati mbalimbali mwaka 2011 na 2012.

Mheshimiwa Spika, aidha, ni kwa bahati mbaya kabisa Serikali haikupenda kufanyia kazi maoni na ushauri iliyopewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Kamati ya Bunge na Wabunge mbalimbali kwa nyakati tofauti na ambayo kama yangezingatiwa kikamilifu yangeweza kuliepusha Taifa na matatizo yaliyotokea katika Mikoa ya Lindi na Mtwara na ambayo bado yanaendelea mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, makadirio ya mapato na matumizi ya kawaida yanaombewa jumla ya sh. 107,221,286,000/= kati ya fedha hizo kiasi cha sh.

11,612,542,000/= ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na taasisi zilizo chini yake na kiasi cha sh. 95,608,744,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengine *(OC)*. Matumizi haya yanaonekana ni pungufu ya kiasi cha sh. 2,857,582,000/= kwenye bajeti ya mwaka jana katika fungu hili la matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, upungufu huu, unaacha maswali, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwaeleza Watanzania sababu za kupungua kwa bajeti ya mishahara ya Wizara na taasisi zilizoko chini yake, ambayo katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara ya Nishati na Madini ilitengewa sh. 17,292,347,000/= na kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014 Serikali inaomba kiasi cha sh. 11,612,542,000/= ikiwa ni pungufu ya sh. 5,679,805,000/=.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka majibu kwa kuwa wakati wafanyakazi wakitarajia kupandishwa madaraja na ongezeko la mishahara kutokana na kupanda kwa gharama za maisha pamoja na mfumko wa bei, bajeti ya mishahara kwa Wizara na taasisi zilizo chini yake inapunguzwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo iwapo punguzo hilo ni kutokana na kubana matumizi au ni udhaifu katika maandalizi ya bajeti na nini athari zake kwenye ufanisi wa Wizara na taasisi zake? Au Wizara imebaini mianya ya ufisadi ambayo ilikuwepo katika bajeti zilizopita kuhusiana na fungu la mishahara?

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya CCM inaonekana kuziba masikio katika kupunguza matumizi yasiyo ya lazima pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, wananchi na wadau wa maendeleo kulipigia kelele suala hili. Jambo hili limejirudia kwa upande wa matumizi ya kawaida, ambapo Serikali iliomba kiasi cha sh. 92,786,521,000/= katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 na mwaka huu wa fedha 2013/2014, Serikali inaomba kiasi cha sh. 95,608,744,000/= ikiwa ni ongezeko la sh. 2,822,223,000/=.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa Wabunge na Bunge kuungana pamoja kabla ya kupitisha matumizi haya makubwa na kuitaka Wizara ya Nishati na Madini kubana matumizi kwa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ili tupate fedha za kuwekeza kwenye nishati.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuonesha udhaifu na uwezo mdogo wa Wizara katika kusimamia sheria za nchi, kwa mujibu wa taarifa ya *CAG* ya Juni 2012 nchi imepoteza kiasi cha dola za Kimarekani 12,634,354.61 sawa na shilingi bilioni 19.71. Hizi ni fedha ambazo hazikukusanywa kutoka kwa Makampuni ya Madini kwa kufuata Sheria mpya ya Madini ya mwaka 2010, kifungu cha 87(1) kuwa mrabaha wa 4% utozwe kabla ya makato na badala yake mrabaha ukawa ni 3% na kutozwa baada ya makato kama Sheria ya zamani ilivyokuwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2011/2012 na 2012/2013, Serikali iliathiriwa kwa kiwango kikubwa na mvutano baina ya Watendaji Waandamizi wa Wizara ya Nishati na Madini na Taasisi zake kwa upande mmoja na baadhi ya Wabunge kwa upande mwingine katika mvutano ambao uliambatana na kutuhumiana hadharani kupitia vyombo vya habari juu ya madai ya ubadhirifu na matumizi mabaya ya madaraka.

Mheshimiwa Spika, baadhi yamejidhihirisha kufuatia chunguzi na ripoti zilizofanyika na kubaini kasoro kubwa za kiutendaji hususan kupitia ukaguzi maalum uliofanywa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* katika Shirika la Umeme *(TANESCO).*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA, inataka Serikali ieleze hatua iliyofikiwa katika uchunguzi juu ya ununuzi wa mafuta mazito kama ambavyo tulipendekeza ufanyike. Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kwamba Mamlaka ya Ununuzi wa Umma *(PPRA)* nayo iliwahi kueleza kwenye vyombo vya habari kuwa imeanza uchunguzi ambao ulipaswa kukamilika mwaka 2012;

hivyo, tunataka taarifa ya uchunguzi iwekwe hadharani na Serikali ieleze hatua ilizochukua dhidi ya madai ya ufisadi na matumizi ya madaraka kupitia mianya ya dharura ya umeme.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maazimio ya Bunge; maazimio kuhusu uhalali wa uchangishaji (Sakata la Jairo); kwa kipindi cha mwaka 2011/2012, Bunge lako Tukufu lilishuhudia mambo kadhaa yaliyokiuka miiko ya uongozi, ambalo yalilazimu Bunge kuunda Kamati Teule kuchunguza uhalali wa uchangishaji uliofanyika katika Wizara ya Nishati na Madini (Sakata la Jairo) na baadhi ya mapendekezo yake ambayo yalipitishwa kuwa maazimio yalikuwa:-

(1) Kamati Teule inapendekeza kwamba Serikali ichukue hatua za kinidhamu kwa Ndugu David Kitundu Jairo kwa matumizi mabaya ya madaraka, kukusanya na kutumia fedha za Serikali kinyume cha Sheria, Kanuni na Taratibu za Fedha za Umma na kuruhusu matumizi mabaya ya fedha za Umma;

(2) Vile vile Serikali iwachukulie hatua za kinidhamu, kwa mujibu wa Sheria, watumishi wote wa Wizara ya Nishati na Madini waliotajwa kwenye Taarifa hii kushiriki kwa namna mbalimbali katika mchakato wa uchangishaji na matumizi ya fedha hizi za umma. Aidha, kwa kuwa kwa mujibu wa Mwongozo wa Baraza la Mawaziri, Waziri ndiye Msimamizi Mkuu wa Wizara, hivyo suala la uchangishaji halikupaswa kufanyika bila yeye kufahamu;

(3) Kamati Teule inapendekeza Serikali ichukue hatua zinazofaa kwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja;

(4) Kamati Teule inapendekeza Serikali ichukue hatua zinazofaa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa upotoshaji huo; na

(5) Kamati Teule inapendekeza Serikali ichukue hatua zinazofaa kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA inahoji ni kwa nini hadi sasa Bunge hili limeshindwa kuhakikisha kwamba, maazimio haya yametekelezwa na Serikali? Hakika huu ni uzembe wa wazi wa Bunge kushindwa kutimiza majukumu yake ya kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hatua za utekelezaji wa maazimio hayo ya Bunge, kwani baadhi ya wahusika bado wapo maofisini wakiendelea na kazi na wengine wakiendelea kuteuliwa kushika nafasi zingine katika uongozi na utumishi wa umma kama vile hakuna lililowahi kutokea.

Mheshimiwa Spika, maazimio ya *Richmond.* Itakumbukwa kwamba, taarifa mbili za Serikali kuhusu utekelezwaji wa maazimio haya ziliwasilishwa Bungeni na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, tarehe 28 Agosti, 2008 na tarehe 11 Februari, 2009.

Mheshimiwa Spika, Taarifa moja ilikabidhiwa na kujadiliwa na Kamati ambazo zililitaarifu Bunge kuwa utekelezaji wa Maazimio 10 kati ya 23 yaliyotolewa na Bunge, yalifanyiwa kazi hadi mwezi Februari, 2009 na Maazimio 13, bado yalikuwa hayajakamilika.

Mheshimiwa Spika, Bunge liliazimia kwamba taarifa za utekelezaji wa maazimio yaliyobaki ziwasilishwe kwa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambayo hata hivyo katika mwaka 2011, 2012 na mpaka mabadiliko ya muundo wa Kamati yalipofanyika, Kamati hiyo haikuwasilisha taarifa yoyote Bungeni ya kueleza kukamilika kwa utekelezaji wa maazimio husika, hali ambayo inahitaji Bunge kuingilia kati kuweza kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Katiba ya Nchi Ibara ya 63 (2) na (3). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hali inayozua maswali kuhusu umakini wa Bunge katika kusimamia maazimio yake mwaka 2011, Mbunge wa Monduli, Mheshimiwa Edward Lowassa, aliyekuwa Waziri Mkuu na kujiuzulu kufuatia kashfa

hiyo ya *Richmond,* alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama iliyopewa dhamana na Bunge kufuatilia utekelezaji wa maazimio kuhusu mkataba kati ya *TANESCO* na *Richmond. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hali hiyo, haishangazi kwamba kwa miaka miwili toka wakati huo, mpaka mabadiliko ya Kamati za Bunge yalipofanyika; Kamati hiyo katika Taarifa zake zote Bungeni, haijawahi kuisimamia Serikali kuhakikisha maazimio husika ya Bunge yanatekelezwa. Huu ndio uwajibikaji, ndani ya Serikali na uongozi wa Bunge; vyote vikiongozwa na CCM. *(Makofi)*

**SPIKA:** Pamoja na wewe na kundi lako lote. *(Kicheko/ Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, sasa inajulikana wazi kuwa Mkataba wa *TANESCO* na *Richmond* ulirithishwa kinyemela kwenda kwa *Dowans* kama inavyoonekana katika nyaraka za Mahakama ambapo *Dowans* na *Richmond* zilidaiana huko Marekani na kuwa hilo lilifanyika bila kuitaarifu *TANESCO,* kinyume na kifungu cha 15:12 cha Mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hukumu ya *Dowans,* ushahidi umepatikana na kuwa mashahidi mbalimbali walioitwa mbele ya Kamati Teule ya Bunge na wakiwa chini ya kiapo walitoa taarifa za uongo kuwa mkataba kati ya Richmond na *TANESCO* ulihamishwa kwenda *Dowans* 23 Disemba, 2006 na hivyo wahusika hao mbalimbali wakiwemo wamiliki wa *Richmond* walidanganya au kuficha ukweli mbele ya Kamati Teule na hivyo kuonesha dharau dhidi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, masuala haya ni muhimu yakajadiliwa sasa ili kupata undani wa wahusika wanaopaswa kubeba mzigo wa fidia kwa kampuni ya *Dowans* badala ya kubebesha mzigo huo *TANESCO* na umma wa Watanzania. Kushindwa kuwashughulikia kwa ukamilifu

mafisadi wa *Richmond* na kukwepa kutumia mianya ya Sheria za Kimataifa kukana mikataba iliyoingiwa kwenye mazingira ya ufisadi kwa mara nyingine tena kunaelekea kuligharimu Taifa, hivyo wakati umefika sasa wa Bunge kuingilia kati kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara ya Nishati na Madini na Serikali kwa ujumla kutoa majibu Bungeni juu ya hatma ya maazimio 10 yaliyobaki: Nambari tatu (3), tano(5), saba(7), nane(8), tisa(9), 10, 11, 13, 14 na 18 ili Bunge liweze kuishauri na kuisimamia Serikali kuhakikisha maazimio husika yanatekelezwa kwa ukamilifu na kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka taarifa ya utekelezwaji wa Maazimio tajwa yaliyotolewa na Bunge juu ya Mkataba baina ya *TANESCO* na Kampuni ya *Richmond Development Company LLC* badala ya kuwasilishwa kwenye Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambayo kwa sasa haipo, sasa iwasilishwe kwenye Bunge zima ili yaweze kujadiliwa na hatima yake iweze kujulikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze kwa nini mpaka sasa haijatekeleza maazimio hayo na Bunge liweke muda wa ukomo wa kutekeleza Maazimio yote ya Bunge yaliyokuwa yamesalia katika sakata hili la *Richmond* ili mara moja na daima sakata hili la *Richmond* limalizwe na kufungwa baada ya maazimio yote kutekelezwa kwa ukamilifu. Ikiwa maazimio ya mwaka 2008 utekelezaji wake haujakamilika mpaka mwaka 2013 kwa miaka mitano, nini kitalihakikishia Taifa kwamba, maazimio mengine mapya yaliyopitishwa 2011 na 2012 yatatekelezwa kwa wakati na kwa ukamilifu?

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. tatu (3), ambalo liliagiza kwamba: "Mkataba kati ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC* uliorithiwa na *Dowans Holdings S.A.* na ile kati ya *TANESCO* na *IPTL, SONGAS*, *AGGREKO* na *Alstom Power Rentals,* ipitiwe upya mapema iwezekanavyo

kama ambavyo Mikataba ya Madini ilivyopitiwa upya na Serikali". Iwapo Azimio hili lingetekelezwa kwa ukamilifu wake, gharama za uzalishaji *TANESCO* na Serikali kwa ujumla zinazotokana na matatizo katika mikataba zingepungua.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. tano (5) Mkataba kati ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC* na sasa *Dowans Holdings S.A* umesheheni makosa mengi ya kisheria yanayoashiria udhaifu mkubwa wa kitaalam katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali au ukosefu wa umakini ama ubinafsi katika kuiwakilisha Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kushindwa kutambua ukosefu wa sifa za kikampuni za *Richmond Development Company LLC;* kushindwa kuishauri Serikali kuifanyia kampuni hiyo ukaguzi wa awali *(due deligence)* au ukaguzi baada ya uteuzi *(post qualification);* kushindwa kutambua tofauti kati ya *consortium agreement* na *proprietary information agreement;* kushindwa kuona dosari kisheria za *proprietary information agreement;* kushindwa kuona tofauti za kisheria kati ya *Richmond Development Company LLC, RDEVCO, RDVECO* na *RDC,* majina ambayo wamiliki wa *Richmond Development Company LLC* walikuwa wanayatumia kwa kubadilisha badilisha *(interchangerbly)* kwa makusudi.

Mheshimiwa Spika, kushindwa kuwashauri Wajumbe wa *GNT* kwamba *business card* si mbadala wa hati mahsusi kisheria; kushindwa kuishauri Serikali kuhakikisha kuwa muhtasari wa majadiliano kati ya Kamati ya Serikali ya Majadiliano *(GNT)* na *Richmond Development Company LLC* ambao ulizingatia baadhi ya maslahi ya nchi, uwe sehemu ya Mkataba kati ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC;* kushindwa kuishauri Serikali kutumia fursa iliyokuwepo wazi ya kuvunja Mkataba baada ya *Richmond Development Company LLC* kushindwa kutekeleza sehemu yake ya Mkataba; kushindwa kuhudhuria idadi kubwa ya vikao muhimu vya majadiliano na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali

ambaye katika majadiliano yake na Kamati Teule alionesha kutokuelewa kabisa kilichokuwa kinatendeka na wasaidizi wake na mwakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Wakili wa Serikali Donald Chidowu, ambaye ushiriki wake katika *GNT* haukuwa na tija yoyote, wawajibishwe na Mamlaka ya juu ya nchi kwa kuchangia kuiingiza nchi katika mkataba wa aibu.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. saba (7) lilikuwa Kamati Teule inapendekeza kuwa, Wajumbe wote wa *GNT* ambao ni Maafisa Waandamizi wa Serikali wawajibishwe mara moja kwa kushindwa kutumia elimu na ujuzi wao kulinda maslahi ya Taifa. Aidha, Azimio namba tisa (9) lilikuwa linataka mabadiliko ya haraka ya uongozi wa taasisi ya TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 13, Kamati Teule inatoa wito kwa Kamati zote za Bunge zihakikishe kuwa zinapitia mikataba mikubwa na ya muda mrefu ya kibiashara chini ya sekta zao ili kuliondolea Taifa mizigo isiyo ya lazima. Pale ambapo upatikanaji wa mikataba hiyo unakwamishwa kwa urasimu usio wa lazima Kamati zitumie utaratibu uliotumiwa na Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara ya kuunda Kamati Teule yenye ufunguo wa mikataba iliyofichika.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 14, Kamati Teule inapendekeza kwamba Waziri wa Nishati na Madini wa wakati huo Mheshimiwa Dokta Ibrahim Msabaha na Katibu Mkuu Ndugu Arthur Mwakapugi wachukuliwe hatua kali za kinidhamu kwa kuliingiza Taifa kwa makusudi kwenye mkataba na kampuni ya mfukoni ambao umesababisha hasara kubwa kwa nchi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamishna wa Nishati Ndugu Bashir Mrindoko naye achukuliwe hatua za kinidhamu kwa kushindwa kumshauri Katibu Mkuu mpya wa Wizara kuhusu udhaifu wa *Richmond Development Company LLC* ambao ulijulikana dhahiri na Wizara toka mwaka 2004 kwenye mkataba wa Bomba la Mafuta. Ndugu Mrindoko ndiye

aliyeiandikia barua kampuni hiyo kusitisha mkataba wake na Serikali mwezi mmoja tu kabla ya mchakato wa zabuni ya umeme wa dharura haujaanza.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Wataalam wa Ofisi ya Spika; mbali na maazimio hayo pia kuna uchambuzi uliofanywa na Kamati ya Wataalam wa Ofisi ya Spika, kuhusiana na makampuni yanayouza umeme kwa *TANESCO* ambayo mikataba yake haipishani na ule wa *RICHMOND,* taarifa hiyo iliwasilishwa Bungeni wakati Mheshimiwa Harrison Mwakyembe akiwasilisha Taarifa yake ya Kamati Teule ya *RICHMOND* ili Waziri atoe ufafanuzi ni kwa kiwango gani mapendekezo yake Serikali imeyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, uhalali kisheria wa Kampuni ya *Aggreko (legal status).* Kwa mujibu wa maelezo yaliyomo kwenye Mkataba, Kampuni ya *Aggreko International Projects Limited* ni Kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria za nchi ya Scotland. Uchambuzi na utafiti wetu haukuweza kuthibitisha kuwa Kampuni hiyo kweli imesajiliwa kisheria huko Scotland ili kubaini kama kulikuwa na udanganyifu kama ule uliofanywa na Kampuni ya *RICHMOND,* yaani kutoa taarifa za uongo kuhusu uhalali kisheria wa Kampuni.

Mheshimiwa Spika, malipo ya kodi; kama ilivyo katika Mkataba wa Kampuni ya *Richmond*, Kifungu cha 3.4 cha Mkataba wa *AGGREKO* kinatamka kwamba, kodi zote na malipo mengine yanayotokana na uingizaji nchini na utoaji wa nchi za nje wa Mitambo ya uzalishaji wa umeme, ikiwa ni pamoja na vipuri na vifaa vingine vinavyohusika na uendeshaji wa Mtambo huo italipwa na *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kifungu hicho kimeweka pia sharti kwamba, pale ambapo bodi au malipo yoyote yatadaiwa na Mamlaka yoyote ya kodi kutoka kwa *AGGREKO*, Kampuni hiyo italijulisha Shirika la *TANESCO* ambalo litalipa kodi au malipo hayo kwa mamlaka husika au litairejeshea *AGGREKO* fedha ambazo itakuwa imelipa kwa Mamlaka hiyo katika kipindi cha siku 14.

Mheshimiwa Spika, malipo; kwa mujibu wa Vifungu vya 4.2 na 4.3 vya Mkataba, Shirika la *TANESCO* lina wajibu wa kuilipa Kampuni ya *Aggreko* malipo yafuatayo:-

*(i)* *Capacity Charge* – Dola za Marekani 35.928 kwa mwezi.

(ii) Malipo ya Umeme *(energy purchase price)* – Dola 4.99 kwa *Kwh*.

Mheshimiwa Spika, fidia kwa ucheleweshaji wa kuzalisha umeme; kwa mujibu wa Kifungu cha 4.4.2 cha Mkataba, *Aggreko* inawajibika kulipa kwa *TANESCO* Dola ya Marekani 0.5 kwa *Kw* kwa siku kwa wiki nne za kwanza za ucheleweshaji na baada ya hapo kama ucheleweshaji wa uzalishaji umeme utaendelea, anawajibika kulipa Dola ya Kimarekani moja kwa *Kw* kwa siku.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, malipo hayo ya fidia *(liquidated damages)* yamewekewa ukomo chini ya Kifungu cha 10.3 (a) na (c) ambapo hayatazidi Dola za Kimarekani 350,000 na kwamba, malipo hayo kwa ujumla wake chini ya Mkataba huo hayatazidi Dola za Kimarekani 500,000. Aidha, Kifungu cha 8.8 cha Mkataba wa *Richmond* kinachoiruhusu *TANESCO* kuendesha Mitambo ya *Richmond* pale ambapo Kampuni hiyo itaitelekeza *(abandon)* mitambo hiyo, kimeondolewa kwenye mkataba wa *AGGREKO*.

Mheshimiwa Spika, Nyongeza ya Mkataba; Mkataba huo una Nyongeza *(Addendum)* au *(Amendment No*. 2) ya Januari, 2007 ambayo imebadilisha *formula* ya kupata *capacity payments*, ambapo muda uliopotezwa na *TANESCO* kutokana na matatizo ya upatikanaji wa gesi na pia kutokana na *TANESCO* kutoomba kupewa umeme kutoka *AGGREKO* umepigiwa hesabu kwa ajili ya *AGGREKO* kulipwa na *TANESCO.* Nyongeza hiyo pia imebadilisha bei ya Umeme unaotolewa na *AGGREKO* ambapo, bei mpya sasa ni Dola za Kimarekani 0.0499 x 1000 kwa kila *Mwh.*

Mheshimiwa Spika, Mkataba Kati ya *TANESCO* na

*Alstom Power Rentals Energy LLC.* Tarehe ya kusainiwa kwa Mkataba, Mkataba huo ulisainiwa tarehe 27 Oktoba, 2006 Mkataba huo ni kwa ajili ya uzalishaji na usambazji wa umeme wa dharura kutoka kwenye kinu cha dizeli cha kuzalisha umeme *(emergency supply of power from a diesel – based generating plant* in Mwanza *with a capacity of 40 Mw*).

Mheshimiwa Spika, Muundo *(form)* wa Mkataba; kama ilivyo kwa Mikataba iliyotangulia, Mkataba huu upo katika muundo wa *Standard Power Off-take Agreement.* Muda wa Mkataba huo ni miezi kumi na mbili (12) kwa mujibu wa Kifungu cha 2.1 cha Mkataba. Kwa mujibu wa maelezo yaliyomo kwenye Mkataba hususan kwenye Kifungu cha 5.1 (a) na (b), Kampuni ya *Alstom Power Rentals Energy LLC* imesajiliwa chini ya Sheria za Florida, Marekani.

Mheshimiwa Spika, malipo ya kodi; Kifungu cha 3.4 cha Mkataba kinatamka kwamba, *TANESCO* itatumia juhudi za kibiashara kuhakikisha kwamba, Serikali ya Tanzania inatoa msamaha kwa *Alstom* wa kutolipa *import duties* na kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)* kuhusiana na Mtambo au utekelezaji wa majukumu ya *Alstom*, chini ya Mkataba huo. Aidha, Kifungu hicho kinatamka pia kuwa, pale ambapo kodi hizo zitadaiwa, *Alstom* itaiomba *TANESCO* ilipe kodi hiyo au kama italipwa na *Alstom, TANESCO* itarejeshea *Alstom* malipo hayo ya kodi.

Mheshimiwa Spika, kutii Sheria za Mazingira; Kifungu cha 3.9 cha Mkataba huu kinamtaka *Alstom* kuhakikisha kwamba, hatafanya kitendo chochote ambacho kitasababisha kuwepo kwa hali ya mazingira ambayo inakiuka Sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, malipo ya umeme; kwa mujibu wa Kifungu cha 4.3 cha Mkataba, *TANESCO* inawajibika kulipa malipo ya *capacity charge* kwa kiasi cha Dola za Marekani 43.8 kwa *Kw* kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, Malipo ya fidia kwa ucheleweshaji

wa kuzalisha umeme; kwa mujibu wa Kifungu cha 4.4 na cha 10.1(a) cha Mkataba, *Alstom* anawajibika kulipa kwa *TANESCO* kiasi cha Dola za Kimarekani 400,000 kama kiwango cha mwisho cha malipo ya fidia *(damages)* kwa ucheleweshaji wa kuzalisha umeme na kiasi cha Dola za Kimarekani 600,000 kama kiwango cha mwisho cha malipo yote ya fidia *(damages).*

Mheshimiwa Spika, dhamana ya malipo kwa *Alstom;* Kifungu cha 4.6 cha Mkataba kinaitaka *TANESCO* kufungua *Letter of Credit* ya kiasi cha Dola za Kimarekani 3,500,000 kwa kipindi chote cha Mkataba, kama dhamana ya malipo kwa *Alstom*. Aidha, Kifungu cha 4.7 cha Mkataba kinaitaka *TANESCO* kufungua *Standby Letter of Credit* ya kiasi cha Dola za Kimarekani 14,000,000 kwa ajili ya malipo ya miezi minane (8) ya Mkataba.

Mheshimiwa Spika, mafuta *(fuel);* Kifungu cha 6 cha Mkataba kinatamka kuwa, *TANESCO* itawajibika kulipia mafuta ya dizeli yatakayotumika kuendeshea mtambo wa *Alstom* wa kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, kutolipa malipo *Capacity Charges* wakati wa majanga. Kwa mujibu wa Kifungu cha 13.1 cha Mkataba, malipo ya *Capacity Charges* yanayotakiwa kulipwa na *TANESCO* yatasitishwa kwa siku 30 iwapo litatokea janga lolote ambalo litasababisha *Alstom* kutelekeza majukumu yake ya kuzalisha na kusambaza umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhamisha *(assign)* majukumu; kwa mujibu wa Kifungu cha 15.12 cha Mkataba, *Alstom* au *TANESCO* inaweza kuhamisha *(assign)* sehemu au majukumu yote yaliyomo kwenye Mkataba kwa Kampuni Tanzu, baada ya kutoa taarifa kwa mhusika wa pili, uhamishaji huo wa majukumu. Hata hivyo, mhusika yeyote anayehamisha majukumu atabaki na wajibu wa kuhakikisha kuwa majukumu hayo yanatekelezwa ipasavyo na yasipotekelezwa, atawajibika.

Mheshimiwa Spika, Mkataba Kati ya *TANESCO* na

*WARTSILA FINLAND OY.* Tarehe ya Kusainiwa kwa Mkataba, *m*kataba huo ulisainiwa tarehe 20 Juni, 2006. Madhumuni ya Mkataba *(Subject Matter),* mkataba huo ni kwa ajili ya uzalishaji na usambazaji wa umeme wa dharura kutoka kwenye kinu cha gesi cha kuzalisha umeme *(Energy Purchase Contract for Procurement of Emergency 100 Mw Gas-based Power Generation Plant a*t Ubungo, Dar es Salaam).

Mheshimiwa Spika, Muundo *(form)* wa Mkataba. Tofauti na Mikataba yote iliyotangulia kufanyiwa uchambuzi hapo juu, Mkataba huo upo katika muundo uliowekwa na Kanuni ya Ununuzi wa Umma *(The Public Procurement (Goods, Works, Non-Consultant Services and Disposal of Public Assets by Tender) Regulations, G.N*. No.97 of 15/4/2005] zilizotungwa chini ya Kifungu cha 88 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya Mwaka 2004 *(The Public Procurement Act*, 2004 (No.21 of 2004).

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 115(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2005; Taarifa ya Serikali Namba 97 ya Mwaka 2005 inaelekeza kama ifuatavyo:-

“Kwa kadri inavyowezekana, kila jitihada itafanywa kutumia miundo ya rasimu za mikataba iliyotayarishwa na Mamlaka ya Ununuzi wa Umma.”

Mheshimiwa Spika, tafsiri na msisitizo ni wetu. Ili kuondoa tatizo la tafsiri, Kanuni hiyo iliyoandikwa kwa lugha ya Kingereza inasomeka kama ifuatavyo:-

“*Every effort shall be made to utilize as for as possible, the sample Standard Contract documents prepared by the Authority.”*

Mheshimiwa Spika, Muda wa Mkataba *(contract period)* ni miezi 21, kwa mujibu wa Kifungu cha *G.C.C* 1.1 (aa) na *GCC* 8.1 *of Contract)*.

Kwa mujibu wa maelezo yaliyomo kwenye Mkataba, Kampuni hiyo imesajiliwa chini ya Sheria za Finland.

Hatukuweza kufanya utafiti wa kina kuthibitisha kuwa maelezo hayo ni sahihi, isipokuwa tumefanya hivyo kwa Kampuni moja tu ya *RICHMOND.*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 2.1 cha Mkataba, *TANESCO* anawajibika kulipa kiasi cha *Euro* 57,550,000/= kama malipo ya huduma ya kupatiwa umeme wa *Megawatt* 100 kutoka kwenye kinu cha kuzalisha umeme cha *WARTSILA.* Kwa mujibu wa Kifungu cha 2.2 cha Mkataba, *TANESCO* anawajibika kufanya malipo ya huduma ya umeme kwa kufungua *Letter of Credit* ya kiasi cha *Euro* 51,795,000/= kwa jina la *WARTSILA.*

Mheshimiwa Spika, dhamana ya utekelezaji *(Performance Bond).* Chini ya Kifungu cha 3.1 cha Mkataba, *WARTSILA* anawajibika kutoa dhamana ya utekelezaji wa kazi *(Performance security/bond)* ya kiasi cha 10% ya malipo anayostahili kulipwa, kabla ya kuanza kazi. Kwa mujibu wa Kifungu cha 14.4 *(GCC),* ukurasa wa 3 wa *Special Conditions of Contract,* kodi zote ambazo *WARTSILA* anapaswa kulipa zitasamehewa *(be exempted)* au zitalipwa na *TANESCO.* Aidha, chini ya Kifungu hicho pia, kodi na malipo yote yanayohusu mishahara ya watumishi wa kigeni wa Kampuni ya *WARTSILA* zinapaswa kulipwa na *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, Chini ya Kifungu cha 6.2.3, taratibu zitakazotumika wakati wa Usuluhishi ni za Mahakama ya Kimataifa ya usuluhishi ya London, chini ya Sheria za Uingereza. Tunadhani kifungu hiki si kwa manufaa na maslahi ya *TANESCO.* Chini ya Kifungu cha 26.3 cha Mkataba ukurasa wa tano wa *SCC* malipo ya *bonus* hayaruhusiwi. Kwa mujibu wa Kifungu cha 27.2 cha Mkataba Ukurasa wa tano wa *SCC*, kipindi cha matengenezo ni miaka miwili (2) baada ya kukamilika kwa ufungaji wa Mtambo. Tunadhani kwamba, Kifungu hiki ni kwa manufaa na maslahi ya *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, Mkataba Kati ya *TANESCO* na *Songas Limited;* Mkataba huo umesainiwa tarehe 11 Oktoba, 2001. Mkataba huo ni kwa ajili ya uzalishaji na usambazaji wa nishati ya umeme kutokana na gesi ya Songosongo

*(Power purchase relating to the Songosongo gas-to-electricity).* Mkataba huo upo katika muundo wa *Standard Power Purchase Agreement.* Kwa mujibu wa Kifungu cha 4.1 cha Mkataba, muda wa Mkataba ni miaka ishirini (20) na unaweza kuongezwa kwa makubaliano kati ya *TANESCO* na *SONGAS.*

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Songas Limited* ni Kampuni ya Kitanzania iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni, Sura 212, Toleo la 2002 *(The Companies Ordience (Cap. 212) of the Laws of Tanzania, R.E,* 2002).

Malipo ya kodi; kwa mujibu wa Kifungu cha 15.1 cha Mkataba, *Songas Limited* inatakiwa kulipa kodi kulingana na masharti yaliyomo kwenye Mkataba wa Utekelezaji *(Implementation Agreement)* ulioingiwa kati yake na Serikali ya Tanzania.

Malipo ya umeme; kwa mujibu wa Kifungu cha 2.1(a)(i) na (ii) cha Mkataba, kikisomwa pamoja na Vifungu 9.2 na 9.5, *TANESCO* anawajibika kulipa malipo yafuatayo kwa *SONGAS:- Capacity Charge* – Dola za Kimarekani 6,638,600 *Energy Charge* kwa kiasi kitakachotokana na formula iliyowekwa na Kifungu cha tano (5) cha Nyongeza (F) ya Mkataba.

Usuluhishi; Kifungu cha 3.10 cha Mkataba kinatamka kwamba, *TANESCO* na *SONGAS* wamekubaliana kutotekeleza masharti na matakwa ya Kifungu cha 20(2) cha Sheria ya Umeme, Sura 131, Toleo la 2002 *(Electricity Act, (Cap.*131) *of the Laws of* Tanzania, *R.E* 2002) na badala yake kusuluhishwa migogoro baina yao kwa kutumia utaratibu uliowekwa na Mkataba. Kwa kuwa kinahusu makubaliano ambayo yanavunja sheria, Kifungu hicho hakina uhalali wowote wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, kuvunjwa kwa *TANESCO*; kwa mujibu wa Kifungu cha 4.3(a) cha Mkataba, kikisomwa pamoja na Kifungu cha 17.12, *TANESCO* haiwezi kuvunjwa kwa Sheria au kuhamisha majukumu yake yaliyoainishwa

kwenye Mkataba, isipokuwa tu kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa na Kifungu cha 8.7 cha Mkataba wa Utekelezaji *(Implementation Agreement).*

Uuzaji wa umeme; kwa mujibu wa Kifungu cha 4.1(b), iwapo *TANESCO* watakataa kuongeza muda wa Mkataba baada ya muda wa awali wa miaka 20 kumalizika, *SONGAS* wataruhusiwa kuingia Mkataba na mtu yoyote anayetaka kuuziwa umeme.

Haki ya kununua mradi; chini ya Kifungu cha 4.8 cha Mkataba, *TANESCO* na *T.P.D.C* wamepewa haki ya kununua Mradi huo wa *SONGAS* iwapo *SONGAS* atakiuka masharti ya Mkataba.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo mengine; pamoja na mapendekezo ya hapo juu, tunashauri na kupendekeza pia kuwa, kuna ulazima kwa Mikataba mikubwa ambayo inahusu maslahi na manufaa ya Taifa kama vile Mkataba wa *IPTL* kuwasilishwa Bungeni, kwa utaratibu wa dhana ya demokrasia ya uwajibikaji *(accountability in a Parliamentary democracy)* kwa ajili ya ushauri wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, tunapendekeza na kushauri vilevile kuwa, pale ambapo kuna ulazima wa kutumia rasimu ya Mkataba ambayo ni tofauti na ile iliyotayarishwa na Mamlaka ya Ununuzi wa Umma, mabadiliko muhimu yafanywe katika rasimu hiyo ili masharti yaliyomo ambayo hayafai yaondolewe na yale ambayo ni kwa manufaa ya Taifa letu yawekwe. Wanasheria watumike katika kulitekeleza jambo hili.

Mheshimiwa Spika, tunashauri na kupendekeza vile vile kuwa, Mikataba yote ya umma ifanywe kwa kuzingatia misingi ya kibiashara na si vinginevyo na kwamba, Taasisi na Mashirika yote ya Umma lazima yatekeleze na kufuata utaratibu, masharti na matakwa yaliyowekwa na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Namba 21 ya mwaka 2004, pamoja na Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, tunapendekeza na kushauri kwamba utoaji Mikataba utumike kama njia au chombo cha kutekeleza Sera za Taifa na malengo ya jamii, badala ya kutumika kama chombo cha kuchota rasilimali za Taifa na kuongeza umaskini wa wananchi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, tunashauri pia kwamba, pale inapotokea ukiukwaji wa masharti ya Mkataba unaofanywa na Mwekezaji basi hatua muafaka zichukuliwe, ikiwa ni pamoja na kudai malipo ya fidia iwapo kuna kifungu cha Mkataba kinachotoa haki hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa Mikataba mibovu kati ya *TANESCO* na Makampuni mbalimbali ambapo Makampuni hayo yanalipiwa kodi yote na *TANESCO* imekuwa ni chanzo cha bei kubwa za umeme katika nchi yetu, na kwa kuzingatia kuwa Mikataba hiyo inasababisha Sera muhimu za Taifa, kama vile, Sera ya Kupiga vita Umaskini, Sera ya Huduma Bora kwa Jamii, Sera ya Taifa ya Nishati inayolenga kusambaza nishati ya bei nafuu vijijini na kadhalika kutotekelezeka, tunashauri kuwa Mikataba hiyo ipitiwe upya ili irekebishwe, kwa maslahi na manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa kuzingatia ukweli kwamba, Mikataba hiyo mibovu, kwa kiasi kikubwa inadidimiza uchumi wa nchi yetu, tunapendekeza Serikali ichukue hatua muafaka zinazofaa ili kuondoa hali hiyo ambayo inalipeleka Taifa letu shimoni.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo ya kuachwa kutekelezwa kwa maazimio ya Bunge la Tisa ya Mwaka 2008, hayahusu tu *Richmond* bali pia juu ya Kashfa ya Mgodi wa Kiwira yaliyomgusa Rais Mstaafu Benjamin Mkapa na baadhi ya Mawaziri kama ambavyo hotuba hii itaeleza kwa ufupi wakati wa kutoa maoni kuhusu sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, Serikali wakati inaendelea kuchukua hatua kuhusu kashfa hii ni muhimu ikarejea maelezo

ya ziada na vielelezo zaidi vilivyotolewa wakati wa kusomwa kwa orodha ya mafisadi *(List of Shame)* Septemba 15 mwaka 2007 katika uwanja wa Mwembe Yanga.

Mheshimiwa Spika, adha, matokeo ya Bunge kuzembea kuisimamia Serikali kukamilisha utekelezaji wa maazimio ya Bunge ya mwaka 2008, yamesababisha udhaifu wa Serikali katika kutekeleza maazimio ya Bunge ya mwaka 2011 kuhusu "Sakata la Jairo" kama nilivyoeleza katika Hotuba hii, lakini pia kuhusu uchunguzi juu ya Sekta Ndogo ya Gesi Asili na Mpango wa Dharura wa Umeme kama nitakavyoeleza wakati nawasilisha maoni kuhusu sekta ya gesi na nishati.

Mheshimiwa Spika, sekta ndogo ya gesi asilia ni sekta ambayo kutokana na ukubwa wa hazina iliyokwishapatikana na inayokisiwa kuwepo itakuwa ni kubwa sana katika shughuli za uchumi kwa nchi yetu. Lakini Sekta ya gesi asilia imegubikwa na utata mwingi ambao kwa njia moja au nyingine unatokana na kutokuwepo kwa sera na sheria mahususi ya gesi. Hivyo kusababisha utendaji wake kutokuwa na mdhibiti *(regulator)* wa kuhakikisha maslahi ya Taifa, mwekezaji na mlaji yanaangaliwa.

Mheshimiwa Spika, utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi *(Upstream)*, shughuli zote za utafutaji wa mafuta na gesi nchini unatawaliwa na Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji Mafuta ya mwaka 1980 *(The Exploration Act,*1980). Shughuli ya usafirishaji na uuzaji *(down stream)* hii hutawaliwa na sheria ya EWURA sura 414 kwa kuwa kwa sasa sheria ya gesi nchini haipo. Hivyo basi, makubaliano katika mkataba baina ya wadau hutakiwa kuwasilishwa *EWURA* kwa mapitio tu, na baada ya kujiridhisha *EWURA* hupanga bei za gesi.

Mheshimiwa Spika, mkataba wa ubia ndiyo mwongozo mkuu wa mahusiano yote yanayohusu uzalishaji na ugawanaji wa mapato ya gesi baina ya *TPDC* na mbia yeyote. Lakini kwa makusudi wabia na *TPDC* wamekuwa hawafuati matakwa yaliyomo kwenye PSA na mfano mzuri ni *Pan African Energy.*

Mheshimiwa Spika, utakumbuka moja ya mapendekezo ya Kamati Ndogo iliyoundwa na Bunge lako Tukufu toka kwenye iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini ilipendekeza na Bunge kukubali, kuwa nanukuuu:

"Ipo haja ya kudurusu Sera ya Nishati, kuandaa Muswada wa gesi asili wenye kutoa majibu ya maswali magumu ya Watanzania wa leo na wa miaka 50 ijayo... Majukumu kati ya asasi moja na asasi nyingine yaainishwe bayana na kutenganishwa kwa lengo la kuleta ufanisi na kuongeza tija. Aidha, mipango mkakati na kabambe iandaliwe ili kuibua miradi ya miundombinu na mahitaji ya rasilimali.

Taifa likichelewa kuweka nyenzo hizi muhimu, likaruhusu majadiliano na mikataba kuchukua nafasi, kipindi si kirefu litashuhudia manun'guniko kuwa nchi imeuzwa na mivutano kati ya wananchi na wawekezaji na ya wananchi na Serikali yao itajitokeza kwa nguvu sana jambo ambalo ni vyema likaepukwa mapema."

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yalitolewa Bungeni Novemba 17, 2011 na kupitishwa kuwa azimio la Bunge. Sasa ni mwaka mzima na miezi sita, hadi tunashuhudia maandamano na malalamiko ya wazi toka maeneo ambapo gesi asili imegunduliwa.

Mheshimiwa Spika, licha ya ukweli kwamba gesi asili ilianza kutafutwa toka mwaka 1952 na iligunduliwa kwa mara ya kwanza nchini mwaka 1974 na baadaye mwaka 1982, wakati wote huo hakuwahi kuwa na sera mahususi ya gesi mpaka mwishoni mwa mwaka 2012 zaidi ya miaka 30 baadaye ndipo Serikali imeanzisha mchakato wa kutunga sera ya Taifa ya gesi asili.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhihirisha udhaifu mkubwa wa kisera na kiutendaji kwa kuzingatia kuwa mikataba kadhaa ya uchimbaji na utafutaji wa gesi imeshatiwa saini kati ya Serikali na wawekezaji bila kuwa na sera wala sheria inayotoa mwongozo juu ya namna Taifa

linavyopaswa kudhibiti rasilimali hii adhimu. Uwepo wa Sera na Sheria ya Gesi Asilia ungetoa mwelekeo juu ya namna gani Serikali ingeshirikiana na wakazi wa maeneo yaliyogunduliwa gesi, pamoja na wadau wengine katika kutafuta, kugundua na kuvuna, kusafirisha, kununua na kutumia gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, Serikali bila uwepo wa sera na sheria hiyo, tayari imefunga mkataba na Kampuni ya *Statoil, Ophir, British Gas, Artumas, Shell, Texaco, Agip, PetroBras* na kadhalika. Ni wazi kwamba mikataba husika imeingiwa bila mwongozo wowote wa kisera wala kisheria mahususi. Aidha, licha ya makosa hayo na wakati mchakato wa sera uko karibu kukamilika Serikali imefunga mkataba mwingine kwa Kampuni nyingine kufanya utafutaji kwenye Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, jambo hili linazidisha wasiwasi kama kweli Serikali ina nia ya dhati ya kuhakikisha sekta hii ya gesi inanufaisha Taifa na watu wake. Kitendo cha Serikali kuendelea kuingia mikataba na makampuni ya kutafuta gesi asilia bila ya kukamilisha kwanza sera na sheria ni sawa na kuweka mkokoteni mbele ya punda.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu akiwa ndiye msimamizi na mdhibiti wa shughuli za kila siku za Serikali ndani na nje ya Bunge, anapaswa kutoa maelezo kuhusu hali inayoendelea hivi sasa katika sekta ndogo *(sub sector)* muhimu kwa nchi yetu ya gesi asili kuhusu mazungumzo yanayoendelea na makampuni mbalimbali ya Kimataifa na mikataba inayozidi kusainiwa huku kukiwa na ombwe la kisera na udhaifu wa kiuongozi katika sekta hizo nyeti hali ambayo itakuwa na athari za muda mrefu sana kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshwaji wa sera na sheria katika sekta ya gesi asilia unachangiwa na Wizara yenyewe kwa watendaji wake kuwa na udhaifu katika kuweka mifumo ya kuifanya sekta hiyo kuwa endelevu na yenye manufaa kwa nchi. Hili linathibitishwa na ukweli kwamba *TPDC* imeshindwa kusimamia kwa ukamilifu sekta hii ya gesi asilia kwani hata mikataba iliyopo inayotaka kampuni inayofanya

utafiti baada ya muda fulani kuchimba kisima kipya, lakini hadi sasa kwa mfano, tangu Kampuni ya *Songas* kuchukua visima vilivyochimbwa na *TPDC* haijawahi kuchimba visima vipya kwa kadiri ya mahitaji.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni kampuni ya *Pan African Energy* Tanzania *(PAT)* kukosa sifa za uaminifu ambapo Kamati ilishauri Mkataba wa *Pan African Energy* Tanzania *(PAT)* usitishwe. Aidha, utekelezaji wa kuvunja mkataba huu ulipaswa kwenda sambamba na kuhakikisha kuwa taratibu za kisheria na za kimkataba zinazingatiwa, uwepo wa usalama wa visima na mitambo na uwepo wa uhakika wa huduma ya upatikanaji wa gesi nchini. Hili lilikuwa ni pendekezo namba 4 la kamati iliyochunguza uendeshwaji wa sekta ndogo ya gesi asilia hapa nchini na baadae kuwa azimio la Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni kwa nini mpaka sasa Serikali haijatekeleza azimio hilo? Aidha, ni lini Bunge litachukua hatua ili kuepusha uzembe kwa upande wa chombo hiki muhimu? Aidha, ni lini mabilioni yote ya mapunjo yenye mwelekeo wa ufisadi yatarejeshwa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu gesi asilia, tarehe 15 Julai, 2011, Kambi Rasmi ya Upinzani ilieleza kuwa, nchi yetu imejaliwa utajiri wa gesi asilia katikati ya lindi la umaskini wa wananchi na kwamba Taifa letu lina fursa ya kuwa nchi kiongozi katika gesi Afrika na kushindana Kimataifa ikiwa tutaweka mstari wa mbele uzalendo, upeo, umakini na uadilifu katika sekta ya nishati kuepusha laana ya rasilimali.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mapitio ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2011/2012, yalionesha Serikali kutochukua hatua thabiti kushughulikia ufisadi na udhaifu wa kiuongozi katika sekta ndogo ya gesi asili. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitaka hatua za haraka kuchukuliwa katika mwaka wa fedha 2012/2013, ili kuepusha rasilimali kuwa chanzo cha migogoro na kuhatarisha pia usalama wa nchi,

lakini kwa sababu ya udhaifu wa Serikali hii kutosikiliza ushauri, kitendo hicho kilisababisha vurugu na uharibifu wa mali kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, ushahidi wa hili unapatikana katika ushauri ambao Serikali ilipewa kwa nyakati mbili tofauti, lakini ikashindwa kuzuia vurugu za Lindi na Mtwara. Tarehe 27 Julai, 2012 nikiwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu mapitio na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini nilishauri:

"Mapitio ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2011/ 2012, yanaonekana bado Serikali haichukui hatua thabiti kushughulikia ufisadi na udhaifu wa kiuongozi katika sekta ndogo ya gesi asili hivyo hatua za haraka zisipochukuliwa katika mwaka 2012/2013 na kuendelea rasilimali inaweza kuwa chanzo cha migogoro na kuhatarisha pia usalama wa nchi".

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na angalizo hili Serikali haikuchukua hatua yoyote na matokeo yake sote tunayafahamu, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji ni nani mpaka sasa amewajibika kutokana na hali hiyo?

Mheshimiwa Spika, wakati wa mchakato wa kutoa maoni juu ya rasimu ya gesi , pamoja na kwamba mchakato huo haukufanyika kwa ufanisi katika maeneo mengine muhimu kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ambacho kina kozi mbalimbali za masuala haya na ambako tungepata ushauri mzuri na wa kitaalam kutokana na wadau hao kutokujua na hivyo kutokujitokeza .

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa wananchi waliojitokeza kutoa maoni ni pamoja na wananchi waliofunga safari kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam kuja kutoa maoni yao juu ya rasimu ya gesi. Miongoni mwa mapendekezo aliyotoa mwananchi huyo (jina linahifadhiwa) mbele ya viongozi wa Serikali alishauri Serikali kujua matatizo yanayotokea katika sekta ya madini ili tuhusianishe na gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mwananchi huyo kuwakilisha mikoa ambayo ndiko hasa nishati hiyo inakopatikana, mwananchi huyo alipendekeza kutengwa kwa asilimia kumi (10%) ya mapato yatokanayo na gesi kwa ajili ya kuboresha maeneo rasilimali hiyo inapopatikana.

Mheshimiwa Spika, akapendekeza kijengwe Chuo Kikuu Mtwara kitakachofundisha Watanzania elimu ya gesi na pia vijengwe viwanda vitatu kwa faida ya wana Mtwara. Mapendekezo ambayo pia yamewahi kutolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA kwa mwaka 2011 na 2012. Katika hali kama hii ya kushindwa kutimiza wajibu na kusababisha migogoro, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ikiri kuwa imeshindwa kuiongoza sekta hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilitoa mapendekezo ya kukamilishwa kwa Sera na Sheria ya Gesi kwa haraka na umakini mkubwa. Kamati pia ilishauri Serikali kuonesha katika sera na sheria hiyo ya gesi asilia jinsi ambavyo mapato yanayotokana na gesi asilia yatakavyosimamiwa, mapendekezo hayo ya Kamati yalizingatia wingi wa upatikanaji wa nishati hii kwa sasa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kushangaza Serikali imeendesha mchakato mzima wa kutengeneza rasimu ya gesi asilia bila kuwa na ushiriki mkubwa wa wananchi kinyume na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, hakukuwa na uhamasishaji wa kutosha kwa wananchi katika kutoa maoni juu ya rasimu ya kwanza ya gesi iliyotolewa na Wizara ya Nishati na Madini na ndio maana mahudhurio katika sehemu ambako mijadala iliendeshwa yalikuwa madogo sana. Kwa mfano, katika ukumbi uliopo Makumbusho ya Mwalimu Nyerere waliohudhuria siku ya kwanza hawakufika hata 25 na siku ya pili hawakuzidi watu 30.

Mheshimiwa Spika, pia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), wanafunzi na wadau wa gesi kutoka taasisi

hiyo muhimu ya elimu ya juu hawakujitokeza kwa sababu ya uhamasishaji hafifu na hivyo kupelekea kuahirishwa kwa zoezi hilo katika suala la msingi linalohusu uchumi wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini pia suala hili kwa wakati huo lilitakiwa liwe ni mjadala wa Kitaifa ndani ya vyuo vikuu vingi nchini na jamii kwa ujumla ikihusisha pia mikoa yote ambako kuna uvunaji au utafutaji wa gesi asilia ili kupanua dhana ya kuwashirikisha wananchi katika masuala yanayohusu rasilimali za Taifa kinyume na uhalisia wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kasoro zilizoanza kubainishwa na Wabunge na wadau mbalimbali katika toleo la tatu la rasimu ya gesi; Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo ni kwa nini haikuzingatia baadhi ya maoni muhimu ya wadau yaliyotolewa mara baada ya kutolewa kwa rasimu ya kwanza ya Sera hiyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA inataka mchakato wa kupitia rasimu ya tatu ya sera hiyo upanue wigo wa ushirikishwaji wa wananchi katika mikoa yote ambayo utafutaji wa gesi asilia umeanza au unatarajiwa kuanza pamoja na mikoa yote itakayofikiwa na miradi ya uendelezaji wa gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba udhaifu wa Serikali katika kuwezesha ushirikishwaji wa wananchi katika mipango na miradi ya maendeleo na matumizi mabaya ya muda mrefu ya rasilimali za nchi, ni kati ya sababu zilizochangia migogoro katika maeneo ambayo uendelezaji wa miradi ya gesi asilia umeanza hususani katika Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwashirikisha wananchi na kutoa taarifa za kutosha na kwa wakati juu ya suala hili la gesi asilia na rasilimali nyingine za Taifa ili kuondoa mkanganyiko unaojitokeza kwa wananchi juu ya mchakato mzima wa uwekezaji kwenye

rasilimali za Taifa, rasimu ya sera haikidhi haja irudishwe upya kwa wananchi ikiwemo kwenye mikoa yote yenye utafutaji unaoendelea na maeneo ya matumizi yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa michango mbalimbali iliyotolewa na Wabunge wakati wa mjadala wa kuchangia bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini 2012/2013, Waheshimiwa Wabunge pia walitaka kujua kama Taifa mipango ambayo Serikali imeweka kufuatia kugundulika kwa kiasi kikubwa cha gesi, kama rasilimali watu kwa maana ya wataalam waliobobea, idadi ya wataalam tunaowaandaa kwenda sambamba na uhalisia wa uhitaji wa wataalam wenyewe katika sekta ya gesi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarudia kuitaka Serikali kufanya maandalizi ya kutosha ya kuwekeza katika suala la rasilimali watu ili kuondoa matatizo yanayoweza kujitokeza hivi karibuni kutokana na uhaba wa wataalam katika fani hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2012/2013, baada ya kupokea ushauri wa Kamati kuhusu kusitisha ugawaji wa vitalu vya utafutaji gesi, Serikali iliahidi kwa kusema kuwa zoezi la kugawa vitalu vipya kwa ajili ya utafutaji wa mafuta umesitishwa mpaka hapo Sera ya Gesi Asilia na Sheria ya Gesi Asilia nchini itakapokamilika na kuanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza ni kwamba, wakati Sera ya Gesi Asilia ipo kwenye rasimu na ndio kwanza Wabunge tumeletewa kutoa maoni, Serikali tayari imetangaza kwa mujibu wa vyombo vya habari na tamko la *TPDC* tarehe 18 Mei, 2013 kuanza mzunguko mwingine wa leseni za utafutaji Mafuta na Gesi kwenye Bahari kuu na Ziwa Tanganyika Kaskazini. Kutoa leseni kwenye kitalu ya utafutaji ni hatua ya kuelekea kutoa mkataba wa uvunaji.

Mheshimiwa Spika, zabuni hii mpya ya leseni za vitalu vya utafutaji imetolewa wakati kuna maamuzi ya Bunge

kuzuia ugawaji huu mpya mpaka Sera ya Gesi Asilia na Sheria ya Gesi vikamilike haraka hii ya Serikali kugawa vitalu bila sera wala Sheria inatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, uharaka huu unaifanya Kambi Rasmi ya Upinzani iwe na mawazo kwamba, Wizara iliidanganya Kamati ya Kudumu ya Bunge, je, ilifanya hivyo kwa maslahi ya nani? Tunamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge sababu za kuidanganya Kamati inayofanya kazi kwa niaba ya Bunge. Wizara ya Nishati na Madini imekuwa ikitoa ufafanuzi potofu kwamba, tangazo la sasa halina athari kwa kuwa maamuzi ya utoaji wa leseni yatafanyika mwaka 2014 baada ya kuwa na sera na sheria.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ufafanuzi huu wa Wizara hauzingatii ukweli kuwa, hata zabuni ya maombi ikiwemo vigezo, utaratibu na masuala mengine ilipaswa kutolewa kwa kuzingatia misingi mipya inayopaswa kuwekwa kupitia mchakato wa katiba mpya na maandalizi ya Sera na Sheria ya Gesi Asili.

Mheshimiwa Spika, katika muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutengua tangazo hilo mpaka baada ya kukamilika kwa mchakato wa Katiba mpya na maandalizi ya sera na sheria mpya sio tu kwenye sekta ndogo ya gesi asilia bali katika sekta nzima ya nishati ikiwemo juu ya masuala yanayohusu mafuta.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo, Watanzania wataamini kwamba, hatua hiyo imefuatia msukumo uliotokea baada ya ziara ya Rais wa China nchini Tanzania; hasa kwa kuzingatia namna ambavyo, pamoja na vitalu vilivyotangazwa kwenye zabuni ili kutolewa kwa ushindani, vipo vitalu ambavyo vimebakishwa mikononi kwa *TPDC* ambavyo mazingira ya mchakato wa utolewaji wake unaacha maswali.

Mheshimiwa Spika, katika hatua ya sasa Wizara ya Nishati na Madini ijielekeze katika kusimamia mikataba ambayo tayari nchi yetu imeingia mpaka sasa kwa maslahi

ya nchi na kupitia upya mikataba mibovu. Aidha, katika kutekeleza azma hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA inaitaka Wizara ya Nishati na Madini kutoa kwa Bunge taarifa ya uchunguzi wa mikataba hiyo iliyokamilika toka mwaka 2012, lakini imeendelea kufanywa kuwa siri mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka pia Serikali kuweka wazi kwa Watanzania wote mikataba hiyo na mingine ambayo Serikali imeisaini inayohusu rasilimali za Taifa hili. Aidha, inatoa mwito kwa wananchi kuhakikisha kwamba, masuala ya uwazi katika mikataba yanapewa kipaumbele katika katiba mpya, sera na sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitendo ambacho Serikali ilikuwa inakifanya kupitia Shirika la Maendeleo ya *Petrol (TPDC)* cha kugawa vitalu vipya nane vya gesi wakati bado Sera na Sheria ya Gesi haijakamilika, ni ushahidi tosha kuwa kuna watu wachache katika Serikali wameanza kulichukulia suala hili la gesi asilia kwa manufaa ya watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini katika bajeti yake ya miaka iliyopita imekuwa ikitenga fedha nyingi kwa ajili ya mishahara na posho kwa Kitengo cha Sheria cha Wizara. Jambo hili la kugawa vitalu vipya nane vya gesi wakati sera na sheria kuhusu gesi havijakamilika, linadhihirisha siyo tu udhaifu katika idara hii ya ushauri wa kisheria bali pia mazingira yanayoashiria mianya ya matumizi mabaya ya rasilimali za umma katika zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalichukulia jambo hili kuwa ni udhaifu ambao hauwezi kuvumilika hata kidogo na tunaitaka Wizara ieleze sababu hasa za kuendesha zoezi hili kinyume na maoni na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere aliwahi kusema kwamba, Chama lege lege huzaa Serikali legelege; udhaifu huu wa Wizara unaweza kutafsiriwa kwamba, unachangiwa

na ushiriki wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kupewa na kukubali hisa toka kwa moja ya makampuni yanayojihusisha na utafutaji wa mafuta na gesi asilia nchini, kampuni ya *Ophir energy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa Rasmi za Bunge za tarehe 8 Novemba, 2012 ni kuwa wakati CCM ikipewa hisa wapo pia baadhi ya Watanzania ambao waligawiwa sehemu ya hisa hizo kwa ajili ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Katibu Mkuu wa CCM Abdurahaman Kinana anatajwa na vyanzo mbalimbali kwamba amewahi kuwa Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya *Artumas* ambayo iliingia mkataba na Serikali wa kuzalisha *Megawatt*- 300 za umeme Mtwara eneo la Mnazi Bay.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huo ulikuwa wa misingi ya mabadilishano ya gesi kwa nishati ya umeme *(gas for power).* Kwamba *Artumas* ingechimba na kuuza gesi asilia na kuilipa Serikali kwa pamoja na mambo mengine kuizalishia umeme wa *300MW*. Baadaye mwaka 2010 *Artumas* baada ya kufaidika vya kutosha kutokana na uvunaji na uuzaji iliacha kuendeleza mradi huo kwa kisingizio cha madai ya mdororo wa uchumi mwaka 2009 na kuuza hisa zake kwa kampuni ya *Wentworth* ya Ufaransa.

Mheshimiwa Spika, ushiriki huu wa viongozi waandamizi wa Chama cha Mapinduzi na chama hicho kwenye shughuli ambazo zinaitia hasara Serikali, unazua mazingira ya kwamba, CCM inasababisha unyonywaji wa Taifa na wananchi na hivyo ni dhahiri si muafaka kuendelea kuongoza nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, CCM na baadhi ya viongozi wake wamekuwa wakifaidika kutokana na ombwe la kisera na kisheria katika sekta hii na nyingine muhimu. Katika hali kama hii, maneno ya Mwalimu Nyerere yanapaswa kuongezewa nukuu mpya kwamba, Chama cha Mafisadi huzaa Serikali ya Mafisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haki ya wananchi kumiliki rasilimali asilia; wakati Katiba yetu inatambua haki ya kumiliki mali na hifadhi ya mali hiyo na inakataza unyang'anyi wa mali kwa lengo la kuitaifisha au kwa malengo mengine, haki za wananchi kumiliki rasilimali zao za asilia kama ardhi, madini, mafuta, gesi asilia, misitu na wanyama pori, uvuvi, na kadhalika, zimekuwa haziheshimiwi na mamlaka za Kiserikali kwa hoja kwamba, rasilimali asilia hizo ni mali ya umma.

Mheshimiwa Spika, dhana ya mali ya umma ni dhana yenye asili yake katika ukoloni. Ni dola ya kikoloni ya Kijerumani ndio ilikuwa ya kwanza kutangaza kwamba mali asilia zote katika koloni lao la Tanganyika ni mali ya Mfalme wa Kijerumani. Baada ya Wajerumani kushindwa Vita ya Kwanza ya Dunia na kunyang'anywa makoloni yao ya Afrika, dola ya kikoloni ya Waingereza iliyokabidhiwa Tanganyika, walitangaza kwamba rasilimali asilia zote ni mali ya umma chini ya mamlaka na udhibiti wa Gavana wa kikoloni.

Mheshimiwa Spika, dhana hii ilipokelewa bila mabadiliko yoyote ya msingi baada ya uhuru na ndio imekuwa msingi mkuu wa sera za rasilimali asilia za nchi yetu kwa muda wote wa uhuru wetu. Jambo hili ni hatari kwani mali ya umma maana yake ni mali isiyokuwa na mwenyewe na ndio maana wenye nguvu wanatumia mwanya huo kupora wasio na nguvu.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyokuwa wakati wa ukoloni, utekelezaji kivitendo wa dhana ya mali ya umma wakati wote wa uhuru umekuwa ni kuwanyang'anya wananchi rasilimali asilia zilizoko kwenye maeneo yao na kuzimilikisha mamlaka za Serikali (wakati wa miaka ya uchumi-dola), au kuzimilikisha kwa wawekezaji wa kigeni katika zama hizi za soko holela kwa kisingizio cha huria.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya mfumo huu ni kwamba, milki na mamlaka ya maamuzi juu ya matumizi ya rasilimali asilia yameondolewa mikononi mwa wananchi na kuhamishiwa kwenye mikono ya warasimu wa Serikali. Sio hiyo tu, wananchi wamejikuta wakiondolewa kwa nguvu kutoka

kwenye maeneo yao ili kuwapisha wamiliki wapya wa rasilimali hizo, yaani wawekezaji wa kigeni au wa ndani. Kwa sababu hiyo, uchumi wa wananchi umeanguka, umaskini umeongezeka na matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu yameongezeka.

Mheshimiwa Spika, dhana ya mali ya umma katika umilikaji wa rasilimali asilia imehakikisha kwamba, maeneo yenye rasilimali asilia hayapati faida na manufaa yanayotokana na uwepo wa rasilimali hizo katika maeneo yao. Mrabaha, kodi na tozo nyingine zinazotokana na matumizi au mapato ya rasilimali hizo yanapelekwa kwenye mamlaka za Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, madhara yanayotokana na matumizi ya rasilimali hizo Kama vile uchafuzi wa mazingira na mabadiliko ya matumizi ya rasilimali husika, yanawaangukia wananchi wa maeneo ziliko rasilimali hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze mtazamo na msimamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA kuhusiana na umiliki pamoja na uendelezaji wa rasilimali zetu asilia ni kwamba, wananchi hawatanyang'anywa rasilimali zao asilia na mamlaka za Serikali kwa ajili ya matumizi na watu au taasisi nyingine bila kwanza wananchi watakaoathiriwa na unyang'anyi au matumizi hayo kutoa ridhaa yao baada ya kupatiwa taarifa zote na kamili zinazohusu matumizi yanayotarajiwa ya rasilimali hizo na athari za matumizi hayo kwa mazingira, kiuchumi na kijamii *(the right of prior informed consent).* Wananchi Kama wamiliki wa msingi wa rasilimali asilia chini ya Serikali itakayoongozwa na CHADEMA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wana haki ya kulipwa mrabaha kwa ajili ya matumizi ya watu au taasisi nyingine ya rasilimali asilia za wananchi, wakati Mamlaka za Serikali za Mitaa, Majimbo na Serikali Kuu zitakuwa na haki ya kutoza kodi mapato yatakayotokana na matumizi ya rasilimali hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bomba la gesi toka Mtwara hadi Dar es Salaam; pamoja na ushauri wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wakati wa kuwasilishwa kwa bajeti ya Wizara 2012/2013, kuitaka Serikali kuwasilisha Bungeni na kuweka wazi kwa umma mkataba wa mradi husika ili Bunge liweze kuishauri na kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 63; kuanzia katika hatua za awali kuhakikisha kwamba maslahi ya Taifa yanalindwa katika hatua zote na pia wananchi wananufaika kutokana na fursa za uwekezaji huo mkubwa, lakini bado Serikali haikutilia maanani ushauri huu.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake siyo tu kusababisha mkanganyiko kwa wakazi wa Lindi na Mtwara, bali pia kuacha maswali mengi kwa Watanzania juu ya nini hasa nia ya Serikali kwa kuficha mikataba inayohusu rasilimali hizi za Taifa kwa wananchi wake na hata kwa chombo cha kuwakilisha wananchi kama Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA inaitaka Serikali isiendelee na ujenzi wa Bomba la Gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam hadi kwanza, iweke wazi kwa Bunge mikataba yote inayohusu uendelezaji wa gesi asilia ikiwemo ya ujenzi wa Bomba hilo. Pili, ikutane na wananchi kuwashirikisha na kuhakikisha manufaa kwa Taifa na kwao.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA imeshangazwa na hatua ya Waziri wa Nishati na Madini Profesa Sospeter Muhongo tangu kuibuka kwa mgogoro huo amejikita zaidi katika kutoa kauli kupitia vyombo vya habari, badala ya kwenda kukutana na wananchi hatua kwa hatua na kuwezesha ufumbuzi kupatikana.

Mheshimiwa Spika, aidha, manufaa kwa wananchi wa Lindi na Mtwara ambayo taarifa yake imechapwa kwenye vyombo vya habari yaletwe kama taarifa rasmi Bungeni ikiwa na ulinganisho baina ya shughuli za kijamii zilizofanywa na makampuni tajwa pamoja na miradi

iliyotekelezwa na Serikali kufuatia mapato katika sekta hii tangu mwaka 2004 na thamani halisi ya mapato ambayo makampuni tajwa na Serikali wamepata.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ujenzi wa mitambo miwili ya kusafishia gesi asili Mnazi Bay na Songo Songo kama sehemu ya mradi huo, Kambi Rasmi ya Upinzani inarudia kuitaka Serikali kueleza ni miradi ipi iliyotengewa fedha inayoambatana na mradi huo ambayo imepangwa kuwanufaisha wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, pia imetengewa kiasi gani cha fedha katika mwaka huu wa fedha 2013/2014, ili kuharakisha msukumo wa maendeleo kwa mikoa hiyo ya Kusini ambayo imesahaulika kwa siku nyingi na hivyo siyo tu kuharakisha maendeleo kwa mikoa ya Kusini bali pia kuhakikisha usalama wa mradi huo mkubwa kwa manufaa mapana ya jamii ya Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, kuanza kwa ujenzi wa mitambo ya kusafisha gesi asilia pamoja na bomba la kusafirisha gesi hiyo hadi Dar es salaam na usambazaji wa umeme katika vijiji 52 vinavyopitiwa na bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Lindi haikidhi wala kujibu kilio cha wananchi wa Mtwara na Lindi cha kutaka ugunduzi wa gesi asilia katika mikoa hiyo uweze kunufaisha mikoa hiyo kimaendeleo kutokana na kuwa nyuma kimaendeleo miaka 52 baada ya uhuru wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri akiwasilisha hotuba ya bajeti ya mwaka 2012/2013 ya Wizara ya Nishati na Madini tarehe 27-07-2012 aliliambia Bunge hili kuwa, kusainiwa kwa mkataba wa mkopo kati ya Tanzania na China kwa ajili ya kusafirisha gesi asili na ujenzi wa Bomba la kusafirishia gesi toka Mnazi *Bay* hadi Dar es Saalam na kusainiwa kwa mikataba mingine mitano (5) na mkataba wa uzalishaji na ugawanyaji wa mapato ya mafuta na Gesi asili kuwa ni miongoni mwa jitihada ambazo Serikali imechukua katika

jitihada za kukabiliana na tatizo sugu la umeme hapa nchini, hata hivyo kama ulivyo utaratibu wa Serikali mikataba hii inaendelea kuwa siri.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali na Wizara ya Nishati na Madini kuainisha miradi hiyo na kuitengea fedha ili wananchi wa Mikoa ya Kusini waweze kunufaika na rasilimali hiyo kwani kwa muda mrefu sana wamekuwa wavumilivu wakisubiria utekelezwaji wa ahadi za kuwapelekea maendeleo kwa miaka mingi bila kuyaona wala kuyapata.

Mheshimiwa Spika, Kambi rasmi ya Upinzani, inaitaka Serikali isitishe ujenzi wa bomba hilo kwanza iende ikajadiliane na wananchi wa mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani na wakubaliane jinsi ya kuendelea na mradi huo ndipo ujenzi wa bomba hilo uweze kuendelea. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeamua kumaliza tatizo la msingi kwani Serikali ikiendelea bila kujali madai ya wananchi hawa na kuamua kutumia mabavu kujenga hakuna atakayekuwa mshindi kati ya Serikali na wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, ni rai yetu kuwa, Serikali itaweza kuiona busara hii ili gesi iweze kuwanufaisha Watanzania wote yaani wa Mtwara na wale wa maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa uagizaji mafuta kwa ufanisi; marekebisho ya Sheria ya *Petrol (Petroleum Supply Act* 2008) kifungu cha 33(1) kinatamka kuwa uagiziaji wa bidhaa za petroli lazima ufanyike kwa ufanisi na kwa kigezo cha unafuu mkubwa wa gharama na kufafanuliwa zaidi na kifungu cha 33(2) ambacho kinaeleza ufanisi wenyewe ikiwa ni pamoja na:-

(i) Uagiziaji wa pamoja wa kushirikiana *(Joint Procurement);*

(ii) Uagiziaji wa ushindani *(Competitive Procurement);*

(iii) Uagiziaji wa shehena kubwa *(Bulk Procurement);* na

(iv) Kwa kutumia fursa ya viwango vya kiuchumi (*Taking advantage of economic Scale).* Pia Sheria imetoa fursa ya kubadili kwenye aina nyingine za uagiziaji utakaoonekana una tija zaidi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati *(EWURA)* Sura ya 414 pamoja na *Petroleum Conservation Act (Cap* 392) zimeongeza majukumu ya kudhibiti na kuratibu uagiziaji mafuta kutoka nje. Pia mfumo wa ununuzi na usafirishaji wa mafuta kwa pamoja umependekeza kuwa na mratibu *(Petroleum Importation Co-ordinator - PIC)* wa kukusanya taarifa za mahitaji na kutayarisha zabuni.

Mheshimiwa Spika, Kampuni hii, iliratibiwa na *EWURA* lakini ilisajiliwa kwa masharti ya Sheria ya Makampuni na hivyo kuifanya kuwa kampuni binafsi inayomilikiwa na Umoja wa Makampuni yanayoagiza na kusafirisha mafuta nchini *(TAOMAC).* Uendeshwaji wa Kampuni hiyo upo chini ya Bodi na Mwenyekiti wa Bodi huteuliwa na mkutano wa wanahisa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikieleza jinsi gani Wizara inavyoshindwa kusimamia mambo ya msingi kwa mujibu wa sheria na kanuni za uwepo wake. Mfano dhahiri, ni kitendo cha Mheshimiwa Waziri kuteua Mwenyekiti wa Bodi ya *PIC* kwa kutumia nafasi yake na mbaya zaidi kumteua Ndugu James Andindile ambaye ni Kamishna Msaidizi, Wizara ya Nishati ni dhahiri kuwa Wizara itashindwa kufanya kazi yake ya usimamizi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge ni kwa vipi ana uwezo wa kuingilia utendaji wa Kampuni Binafsi kwa kuteua Mwenyekiti wa Bodi? Ni mfumo gani umewekwa wa kuhakikisha Wizara inafanya usimamizi?

Mheshimiwa Spika, ili kuepusha Watanzania

kubebeshwa mzigo wa gharama kubwa ya mafuta katika Kikao cha Arobaini na Mbili – Tarehe 9 Agosti, 2011, kulitolewa hoja ya dharura kuhusu uhaba wa mafuta baada ya michango kadhaa ya Waheshimiwa Wabunge na hatimaye Serikali ilitoa kauli yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya mjadala huo Bunge lilifanya uamuzi. Hata hivyo, hakukuwa na ufuatiliaji wa karibu baada ya maazimio. Hali hii ni moja katika kasoro kubwa ambayo kuanzia mwaka huu, Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA ilitaka irekebishwe. Katika Kamati zote zilizopo za sekta hakuna Kamati ambayo inafuatilia maazimio yote ya Bunge ili Serikali kusimamiwa kwa zile ahadi au maazimio tuliyoyapitisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Nishati na Madini ya Bunge la Tisa iliweza kupendekeza kwa Serikali mara nyingi sana kuhusu suala la *TPDC* kupitia kampuni tanzu ya *COPEC* kuanzisha biashara ya mafuta. Kamati ya Nishati ya Bunge la Tisa ikazungumzia pia *Bulk Procurement* pia *Strategic Reserve*. Masuala yote haya yamehojiwa na Kambi Rasmi ya Upinzani mwaka 2011 na 2012.

Mheshimiwa Spika, baada ya kushindwa kuchukua hatua, hatimaye Serikali ikaleta ahadi nyingine, nanukuu: "Leo hii tarehe 9 Agosti, 2011, Serikali kupitia *EWURA* imeipa leseni Kampuni ya *COPEC* ambayo ni Kampuni Tanzu ya Serikali kupitia *TPDC* kuanza kufanya biashara ya mafuta mara moja". Naomba kurudia, leo hii tarehe 9 Agosti, 2011 Serikali kupitia *EWURA* imeipa leseni *COPEC* ambayo ni Kampuni Tanzu ya Serikali kupitia *TPDC* kuanza kufanya biashara ya mafuta mara moja.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ya Nishati na Madini, *COPEC* ilikuwa imepangiwa shilingi milioni 20 tu kwa ajili ya kampuni hiyo kuanza kufanya biashara. Ukweli ni kwamba kampuni hiyo haikuwa na miundombinu yoyote ya kuiwezesha kufanya biashara kama Serikali ilivyoagiza.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge toka ilipopatiwa leseni ya biashara hadi sasa *COPEC* imeongeza tija ipi katika biashara ya mafuta kwa Watanzania?

Mheshimiwa Spika, Waziri aliahidi mbele ya Bunge kuanza kwa mpango wa utekelezaji uingizaji wa mafuta wa pamoja *(Bulk procurement)* mwezi Januari, 2012. Wizara ieleze kuanza kwa utaratibu huu kumeokoa kiasi gani cha pesa kilichokuwa kinapotea kabla ya kuanza kutumika kwa utaratibu huu mpya na sababu za mpango huo kushindwa kushusha bei ya mafuta kinyume na ahadi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme; bado kunaendelea kuwepo na utata kuhusu mgawo wa umeme katika maeneo mengine ya nchi huku Serikali ikikanusha kuhusu mgawo wakati Watanzania wakiendelea kupewa nishati hiyo kwa mgawo kwa nyakati mbalimbali. Aidha Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini akiwasilisha makadirio ya Bajeti ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka 2012/1013, aliliambia Bunge lako Tukufu kuwa hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni, 2012, lengo la kuondoa mgao wa umeme lilifikiwa kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalitaka Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* na Wizara ya Nishati na Madini kuwaambia ukweli Watanzania kuhusu mgawo wa umeme kwa kuzingatia hali mbaya ya Shirika hilo kifedha ambayo imeripotiwa na vyombo vya habari hivi karibuni kwa sehemu ikichangiwa na wingi wa mikataba mibovu ya miaka mingi ya ukodishaji wa mitambo ya umeme na hali ya sasa ya ununuzi wa ziada wa mafuta ya kuendeshea mitambo ya dharura.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kutowaambia wananchi ukweli kuhusu mgawo wa umeme wakati wananchi wakipata nishati hiyo kwa mgawo huku wakipewa sababu ambazo zinaonekana hazina ukweli, kinazidi siyo tu kushusha heshima na hadhi ya Serikali kwa wananchi wake

bali pia kinadhihirisha udhaifu uliopo katika mfumo wa kiutendaji wa Serikali pamoja na mashirika yake likiwemo Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO).*

Mhesimiwa Spika, mradi wa kuboresha mifumo ya umeme katika Jiji la Dar es salaam ambayo imekuwa ndio kisingizio kikubwa cha mgawo wa umeme hali ambayo inazua maswali mengi kwa Watanzania. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kazi hiyo ilianza katika bajeti ya 2011/2012 na mpaka sasa tatizo la kukatika kwa umeme bado linaendelea, kitendo ambacho kinatafsiriwa kuwa kazi hiyo bado haijakamilika miaka miwili tangu kuanza kwa kazi hiyo iliyogharimu shilingi bilioni 120. Watanzania wanapenda kujua ni lini hasa kazi hii itakamilika ili kupunguza kero ya mgawo wa umeme kwa Dar es Salaam na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Serikali kutoa ahadi hewa zisizotekelezeka na kutochukua hatua stahiki dhidi ya watumishi wa Serikali wanaoihujumu *TANESCO* imekuwa ndio chanzo cha kuzorotesha ufanisi wa Shirika hili na kufanya liendelee kuendeshwa kwa hasara.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikishauri mara kadhaa juu ya kufikishwa Mahakamani kwa watumishi wote wa Serikali na mafisadi wote wanaohujumu uchumi wakiwemo wale wa *TANESCO,* Kiwira, Meremeta, *Richmond* na kadhalika, lakini inaonekana kuwa ni utaratibu wa Serikali hii au udhaifu wa Serikali katika kushughulikia watuhumiwa hao wa uhujumu uchumi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na udhaifu wa Serikali ya CCM katika kuchukua hatua, kama ilivyokuwa katika kusamehe baadhi ya wezi wa *EPA* na kuzimwa kwa sakata la *Richmond* lililosababisha hasara ya mabilioni ya fedha. Hali hiyo imechangia kuzaliwa kwa sakata jipya la *DOWANS* linalopelekea *TANESCO* kutakiwa kuilipa kampuni hii ya *DOWANS* ambayo ilirithi mkataba wa kampuni hewa ya *Richmond* zaidi ya sh. 97,000,000,000, kunazidi kulipatia Taifa mzigo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu kodi za wananchi na malipo ya wateja zinazotumika katika kashfa zote hizo na kuwasababishia wavuja jasho wa Taifa hili kuwa na ugumu wa maisha pamoja na kwamba waliahidiwa maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu ikieleza sababu zinazowafanya wasimfikishe Mahakamani aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO Engineer* William Mhando, siyo tu kwa matumizi mabaya ya ofisi yaliyosababisha *TANESCO* hasara ya zaidi ya Sh. 6,000,000,000 kwa kila mwezi baada ya kukatisha mkataba wa ununuzi wa mafuta kwa ajili ya *IPTL* kutoka kwa *BP* waliokuwa wakiuza kwa bei nafuu na kuanza kununua kwa kampuni za *Oryx* na *Camel Oil* ambayo gharama yake ilikuwa juu bali pia kwa kukiuka miiko ya maadili ya viongozi wa umma?

Mheshimiwa Spika, katika mjadala wa bajeti ya mwaka 2012/2013, kulijitokeza pia wasiwasi wa namna *TANESCO* inavyojiendesha. Bunge liliiomba Wizara ya Nishati na Madini ichunguze kwa kina suala la mapato ya *TANESCO* na jinsi yanavyotumika. Ilionekana *TANESCO* kwa mwezi inapata takribani bilioni 60 au bilioni 70. Mishahara ya wafanyakazi wa *TANESCO* peke yake ni takribani bilioni kumi na moja.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* inatumia fedha nyingi sana kununua umeme kutoka makampuni yanayotumia umeme hususani wa dharura na kukodisha mitambo ya kufua umeme wa dharura. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini itoe majibu juu ya uchunguzi unaohusu uendeshaji wa shirika hili.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 18 Julai, 2011, Serikali kupitia Waziri Mkuu Mizengo Pinda iliahidi kupunguza matumizi yasiyo ya msingi ya Serikali ili kupata fedha ambazo zilitegemewa kuliongezea Shirika la Umeme la *TANESCO* ili liweze kutekeleza mpango wa umeme wa dharura na kuliongezea shirika hilo uwezo wa kujiendesha. Hata hivyo,

ahadi hiyo ilichukua sura mpya baada ya Serikali kushindwa kutekeleza tamko lake la kwanza na kutoa ahadi nyingine tena ya kupata fedha kwa kukopa ambayo mpaka sasa utekelezaji wake bado unasuasua.

Mheshimiwa Spika, Mnamo 13 Agosti, 2011 Serikali ilitoa ahadi ya kuisaidia *TANESCO* kuweza kukopa bilioni 408 kutoka kwenye mabenki, lakini mpaka sasa ni jumla ya dola za Marekani milioni 65 ambazo ni sawa na bilioni 104 tu ndizo *TANESCO* imeweza kukopa tena kwa kuchelewa. Hii ni kwa mujibu wa taarifa ya Serikali kama ilivyoainishwa na Wizara katika ripoti yake ya utekelezaji kwa Kamati ya Nishati na Madini, *TANESCO* ilipokea fedha hiyo mwezi Januari mwaka huu (2013).

Mheshimiwa Spika, ahadi hizi zisizotekelezeka zimekuwa kikwazo kikubwa cha maendeleo ya sekta hii muhimu ya umeme, ndiyo maana mpaka sasa ni sehemu ndogo sana ya Watanzania wameunganishwa na huduma hii muhimu ya umeme.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na madini ilitoa mapendekezo kadhaa kwa lengo la kuboresha sekta ya umeme. Mapendekezo hayo ya Kamati pamoja na yale yaliyotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni mengi hayajafanyiwa kazi na Serikali na hata yale ambayo yamefanyiwa kazi utekelezaji wake ni kwa kiwango kidogo. Aidha, mapendekezo ambayo hayajafanyiwa kazi ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuanzishwa kwa Mfuko wa Kuendeleza Nishati ya Umeme nchini kwa lengo la kutumia Mfuko huo kama mtaji *(Equity)* ili fedha zake zitumike katika kuboresha huduma ya upatikanaji wa umeme nchini na pia kukopa kutoka vyombo vingine vya fedha.

(ii) Kamati pia ilishauri Wizara kutenga fedha za kutosha katika uzalishaji, usambazaji na usafirishaji wa umeme kwani vinategemeana. Cha kushangaza katika bajeti ya

Serikali ya mwaka 2013/2014, haijatengwa fedha yoyote ile kwa ajili ya kuboresha njia za usafirishaji umeme mbali ya kuwepo kwa asilimia 22.5 ya upotevu wa umeme unaozalishwa inayosababishwa na miundombinu chakavu ya umeme.

(iii) Kamati baada ya kuona ugumu na gharama ambayo *TANESCO* itapata katika kusafirisha mafuta toka bandarini kwenda Nyakato Mwanza, ilishauri tangu kwenye bajeti ya mwaka 2011/2012 na kurudia ushauri huo katika bajeti 2012/2013, kwamba, mradi huu uhamishiwe sehemu ambayo yatapatikana mafuta ya uhakika na mitambo hiyo itumie mafuta ya dizeli ili kuweza kunusuru gharama ambazo nchi itaingia baadaye na kupelekea ufanisi wa mitambo hiyo kuwa mdogo.

(iv) Pia Kamati iliitaka Serikali kuiwezesha *TANESCO* kumiliki mitambo yake badala ya kutegemea mitambo ya kukodi ambayo inaligharimu Shirika hilo fedha nyingi linazolipa kwa makampuni yanayomiliki kama *capacity charge.*

Mheshimiwa Spika, katika hoja hii Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba, Kamati ilifanya uchunguzi wa suala hili kabla ya kutoa ushauri kwa Serikali. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa mchanganuo wa gharama ambazo *TANESCO* itazipata katika kusafirisha mafuta mazito ya mitambo ya kufua umeme inayojengwa Nyakato Mwanza.

Mheshimiwa Spika, katika hoja hii Serikali imejaribu kueleza jitihada yake ya kujenga mitambo mbalimbali ya kufua umeme wa gesi ikiwemo ile ya Kinyerezi, Ubungo na Mwanza.

Mheshimiwa spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza bayana namna mitambo hii inayojengwa itakavyokuwa mbadala wa mitambo ya kukodi kuliko kuendelea kijisifia inajenga mitambo wakati kuna baadhi ya mitambo imekamilika, lakini bado mitambo ya kukodi haipungui na *TANESCO* inazidi kulipa *capacity charge.*

Mheshimiwa Spika, umeme vijijini, zaidi ya bilioni50 ambazo *REA* imetengewa, kiasi hiki ni kikubwa, hivyo kitendo cha Wizara kutenga fedha kwa ajili ya kupeleka umeme vijijini bila kutaja idadi na majina ya vijiji vitakavyonufaika na miradi ya fedha hizo, linatoa mwanya wa kutumia vibaya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, hali hii imejitokeza pia katika Taarifa za Serikali za mwaka wa fedha 2012/2013 ambapo hakuna vijiji vya kutosha vilivyooneshwa kunufaika na hivyo kuleta mkanganyiko mkubwa katika utekelezaji wa miradi hii vijijini.

Mheshimiwa Spika, pia tunamtaka Waziri aelezee juu ya mradi uliotengewa fedha na Serikali katika bajeti mwaka wa fedha 2011/2012, mradi uliohusu taa za mwanga bora vijijini ambao ulitakiwa kutekelezwa Bukombe, Kahama, Biharamulo na Chato.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe majibu kwa nini mradi huo haukutekelezwa wakati fedha za mradi huo zilitengwa? Pamoja na majibu hayo Kambi Rasmi Bungeni pia inaitaka Wizara kueleza juu ya mradi mwingine ambao ulifahamika kwa jina la Tanzania *Affordable Rural Electrification Plan* ambao ulitakiwa utekelezwe Bukombe na Kibondo, hasa juu ya hatua iliyofikiwa hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, TANESCO imefika hapo ilipo sasa kutokana na kutokuwa makini katika uingiaji wa mikataba mbalimbali na makampuni yanayoiuzia umeme. Kamati ya Wataalam wa Sheria ya Bunge wakati wa sakata la *RICHMOND* ilishauri yafuatayo kuhusiana na mikataba:

“Kuna ulazima kwa Mikataba mikubwa ambayo inahusu maslahi na manufaa ya Taifa kama vile Mkataba wa *IPTL* kuwasilishwa Bungeni, kwa utaratibu wa dhana ya demokrasia ya uwajibikaji *(accountability in a Parliamentary democracy)* kwa ajili ya ushauri wa Bunge kuwasilishwa Bungeni…..

Aidha, kwa kuzingatia kuwa Mikataba mibovu kati ya *TANESCO* na Makampuni mbalimbali ambapo Makampuni hayo yanalipiwa kodi yote na *TANESCO* imekuwa ni chanzo cha bei kubwa za umeme katika nchi yetu na kwa kuzingatia kuwa Mikataba hiyo inasababisha Sera muhimu za Taifa, kama vile, Sera ya Kupiga vita Umaskini, Sera ya Huduma Bora kwa Jamii, Sera ya Taifa ya Nishati inayolenga kusambaza nishati ya bei nafuu vijijini na kadhalika kutotekelezeka, tunashauri kuwa Mikataba hiyo ipitiwe upya ili irekebishwe, kwa maslahi na manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge katika ufanyaji kazi wake ni mikataba mingapi ya uzalishaji wa umeme na kuiuzia *TANESCO*, Madini au Gesi imefungwa bila ya kuzingatia ushauri au mapendekezo yaliyokwishatolewa Bungeni? Kama imefanyika, je, jukumu la Bunge kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 63 lina maana gani?

Mheshimiwa Spika, matumizi mabaya ya rasilimali za umma hayako katika mikataba ya kukodi mitambo ya umeme tu, bali katika ununuzi wa huduma za kisheria. Hivyo, narudia kutoa mwito kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali aeleze ni kiasi cha fedha kilichotumika kwenye kuendesha kesi za *Dowans* na *IPTL* mpaka sasa na hatua zilizochukuliwa dhidi ya Mawakili wa *TANESCO* na makampuni binafsi yanayotuhumiwa kusababisha mzigo mkubwa wa gharama za kesi ambazo Serikali inashindwa kwa nyakati mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, izingatiwe kuwa kwa mwaka wa fedha 2011/2012, pekee jumla ya shilingi bilioni 10 zimetumika kwa ajili ya gharama za kuendesha kesi hizo kwa kuilipa kampuni ya *Rex Attorneys* na Makampuni mengine ambayo kwa nyakati mbalimbali yamekuwa yakiiwakilisha Serikali na *TANESCO* na kushindwa katika Mahakama za Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mfululizo wa *TANESCO* kushindwa Mahakamani huku mabilioni ya walipa kodi na wateja wake yakitumika, Kambi Rasmi ya Upinzani

inayoongozwa na CHADEMA inapendekeza Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali *(NAO)* na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma *(PPRA)* wachunguze tuhuma za ufisadi na ubadhirifu kwa Shirika la Umeme *(TANESCO)* kwenye matumizi ya mabilioni katika idara ya sheria na ununuzi wa huduma za kisheria kutoka makampuni binafsi unaofanywa na *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, ukaguzi na uchunguzi huo ufanywe kuhusu matumizi na ufanisi wa huduma za kisheria ambazo *TANESCO* imekuwa ikizipata kutoka kwenye makampuni binafsi katika kesi kubwa za Kimataifa ikiwemo ya *Dowans* na *IPTL* kwa kurejea pia maoni niliyoyawasilisha Bungeni tarehe 27 Julai, 2012.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Kambi Rasmi Bungeni mwaka jana ilitaka Serikali kutoa maelezo ya kina kuhusu matumizi ya kifungu cha 1005 cha Kitengo cha Sheria ambacho kina kasma ya 229900 ambayo kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kimetengewa kiasi cha Shilingi Bilioni nne kama gharama za utetezi wa Serikali katika kesi ya *IPTL* ikiwemo kwa ajili ya kuilipa kampuni ya *Mkono & Co. Advocates.*

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani iliitaka Serikali kueleza jumla ya fedha zilizotumiwa na Wizara kati ya mwaka 1995 mpaka 2011 kwa ajili ya kulipa makampuni binafsi ya uwakili kwenye kesi kubwa za Kitaifa na za Kimataifa pamoja na kutaja orodha ya makampuni hayo.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali ilitakiwa ieleze mkakati wa kudhibiti ongezeko la gharama za kisheria ambazo ni mzigo mkubwa kwa mashirika ya umma na wananchi walipa kodi kwa kuwa yamekuwepo mazingira ya kesi kuendelezwa kwa muda mrefu na kugeuzwa kuwa vitega uchumi vya watu wachache. Nilitaja Mifano ya kesi zilizodumu kwa muda mrefu ni ya *IPTL* ambayo Serikali inawakilishwa na *Mkono and Co. Advocates* na ile ya *Dowans* ambayo Serikali imekuwa ikiwakilishwa kwa nyakati mbalimbali na *Rex Attorneys.*

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Nishati na Madini na Mwanasheria Mkuu wa Serikali wanapaswa kulieza Bunge sababu za kuacha kutoa majibu kuhusu suala hilo mpaka hivi sasa. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua hatua ambazo Serikali imechukua juu ya matumizi hayo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011 Benki ya *Standard Hong-Kong* ambayo ni mdeni mkuu katika sakata la *IPTL* ilifungua kesi ya madai katika Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi *(ICSID case No. ARB*/10/20) inayodai kiasi cha dola za Kimarekani milioni 225, pamoja na riba katika kuendesha kesi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Uwakili ya Mkono (inayomilikiwa na Nimrod Mkono Mbunge wa CCM) ilipewa zabuni ya kuitetea Serikali katika shauri hilo. Kwa kujiamini iliishauri Serikali kuwa kesi hiyo tutashinda pamoja na wanasheria wengine kuwa na maoni kinzani kuhusu suala hilo.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Mkono imekuwa ikiishauri Serikali isifanye usuluhishi nje ya Mahakama ya *ICSID* wakati wadai kupitia kwa Mfilisi wa Mali na Madeni za *IPTL (RITA)* wanakubali kusuluhishwa nje ya Mahakama. Je, mpaka lini Serikali itaendelea kuingia gharama hizo na ni kiasi gani Serikali imelipa kwa kampuni hiyo na zingine mpaka hivi sasa?

Mheshimiwa Spika, mpango wa umeme wa dharura; itakumbukwa kuwa Bunge lako Tukufu lilipitisha mpango wa umeme katika mkutano wake wa nne. Serikaliililiambia Bunge hili usafirishaji wa gesi kutoka Songosongo hadi, Somanga hadi Dar es salaam ungeongezwa ndani ya miezi kumi na mbili ili majenereta yaliyokuwa yamenunuliwa kutumika katika mfumo wa gesi yafanye kazi ndani ya miezi kumi na mbili.

Mheshimiwa Spika, aidha ilikusudiwa pia kuwa mpango huo ulilenga kushusha gharama za uzalishaji wa umeme hapa nchini. Ikiwa sasa ni mwaka mmoja na zaidi umepita fedha zinazidi kutengwa kwa ajili ya kununulia mafuta mazito ya kuendeshea majenerata, kwa sehemu kubwa ikiwa ni kwa ajili ya mitambo ya kufua umeme.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa kauli kuhusu sababu za ucheleweshaji katika utekelezaji wa mpango wa dharura wa umeme na kushindwa kubadilisha mfumo wa majenereta kutumia gesi badala ya mafuta na kama kweli dharura iliyokuwepo bado ipo au imekwisha?

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa miradi ya dharura iliyotakiwa kuwa imekamilika ni pamoja na mradi wa *Jacobsen* awamu ya pili ambao ulitakiwa kutekelezwa kuanzia mwezi Januari hadi Disemba, 2012 ambao ungezalisha *megawatt* 150 na kuendeshwa na fedha za mkopo.

Mheshimiwa Spika, tunapenda kupata ufafanuzi kuhusu miradi hii ya umeme wa dharura, miradi mingapi imekamilika, kiasi gani cha pesa kimetumika na kama Taifa tunadaiwa kiasi gani cha fedha ambazo hadi sasa zimekopwa kwa ajili ya miradi ya umeme. Hii ni kwa vile ni miongoni mwa maeneo ambayo nchi hii imekuwa ikiingia gharama kubwa, lakini ikishindwa kumaliza tatizo hili na kuchangia katika deni la Taifa ambalo sasa linafika trilioni 22.

Mheshimiwa Spika, aidha, moja ya mambo ambayo Serikali iliahidi kuyafanyia kazi katika mpango wa umeme wa dharura ni kununua mitambo yake, napenda kunukuu maneno ya Mheshimiwa Waziri Mkuu:

"Mheshimiwa Spika, ushauri mlioutoa ni wa msingi sana, moja mmesema Serikali nunueni mitambo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuliambia Bunge hadi sasa tangu kupitishwa kwa mpango wa umeme wa dharura ni mitambo mingapi ya kuzalisha umeme ambayo inenunuliwa na tayari imeshaanza kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali iliambie Bunge lako Tukufu ina mpango gani kuhusu mitambo ambayo tumekuwa tunakodi kwa maana ya mitambo ya *Symbion* miaka miwili,

na mitambo ya *Aggreko* ambayo yote tumekuwa tunalipa *capacity charge*, je, Serikali imeandaa njia gani mbadala zaidi ambayo tumekuwa tukitumia?

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa umeme wa dharura, Mashirika ya Mifuko ya Jamii kama *NSSF* nayo yaliruhusiwa kuwekeza katika sekta hii ya umeme, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata ufafanuzi kuhusu mipango inayoendelea juu ya nia hiyo ya Mifuko ya Jamii kuwekeza katika sekta ya umeme hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, *Symbion Power Africa LLC, TANESCO* na kuanzisha kampuni mpya ya umeme kusini mwa Tanzania (*SECO*); kutokana na andiko la kinadharia *conceptual proposal* la kujenga mtambo wa kufua umeme katika Mji wa Mtwara na usambazaji wake lililoandikwa na kuwasilishwa, Wizara ya Nishati na Madini, *TANESCO* na *TPDC* mnamo tarehe 7 Septemba, 2012 na baada ya andiko hilo kupitiwa kwa kina na *TANESCO* kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 12 Februari, 2013 *Symbion Power Africa LLC* waliandaa/waliwasilisha *MOU* baina yao na *TANESCO* ili iweze kusainiwa kwa ajili ya kuanzisha kampuni ya kuzalisha umeme chini ya kinachoitwa *Special Purpose Company (SPC)*, Kampuni hiyo itajulikana kama *Southern Electric Company (SECO)* ambayo inaanzishwa chini ya utaratibu wa *PPP*.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa mujibu wa *MOU* ni kuwa Kampuni hii itakuwa ni kwa ajili ya kujenga, kumiliki na kuendesha mitambo inayotumia gesi kuzalisha umeme 600 *MW* katika Miji ya Mtwara na Dar es Salaam. Aidha, kampuni hiyo mpya ya *SECO* itajenga, kumiliki na kuendesha mtandao wa usafirishaji na usambazaji wa umeme kutoka kusini mwa Tanzania kwenda kwenye Gridi ya Taifa, Kaskazini mwa Msumbiji na Malawi *( ....and to build, own and operate transmission and distribution networks that will link power plants in the South to the Tanzania grid, Northern Mozambique and Malawi (the project)*.

Mheshimiwa Spika, *MOU* hii iliingiwa baada ya *Symbion* kufanya mazungumzo na Shirika la umeme la Msumbiji *Electricite de Mozambique (EDM)* kwa ajili ya kuwauzia umeme eneo la kaskazini mwa Msumbiji katika maeneo ya Pemba na Nacala. Hii ni baada ya *EDM* kuonesha kuwa watakuwa tayari kununua umeme kutoka *Symbion* Tanzania.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa mujibu wa *MOU* hiyo ni kuwa tayari *Symbion* wameshasaini makubaliano na Wizara ya Nishati ya Malawi kwa ajili ya kuanzisha uchunguzi kuhusiana na mradi huo wa umeme kutoka nje, kipengele *E* cha *MOU* kinasomeka hivi, nanukuu:

*"Symbion has signed an agreement with the Ministry of Energy in Malawi that provides for the investigation of a cross border project."*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa *MOU* kipengele cha 2.1 ni kuwa *Symbion* ndio watakuwa na jukumu la kufanya upembuzi yakinifu kwa gharama zao wenyewe na kuwasilishwa *TIC* kupitia kampuni ya *Special Purpose Company (SPC)* kwa ajili ya kupatiwa hati ya *PPP*. Aidha, kampuni ya *Special Purpose Company (SPC)* itapewa hadhi ya kuwa mwekezaji wa kimkakati *(strategic Investor).*

Mheshimiwa Spika, aidha , kwa mujibu wa kipengele cha 2.2 cha *MOU* ni kuwa upembuzi yakinifu huo utahusisha pia kuhusiana na mtaji unaohitajika kuwekezwa na *SPC* kwa ajili ya mtambo wa kuzalisha *300MW* kwa kutumia gesi pamoja na mtambo wa kuzalisha *300MW* Kinyerezi, Dar es Salam kwa kutumia gesi.

Mheshimiwa Spika, kipengele cha 2.4 cha *MOU* kinasema kuwa, upembuzi yakinifu huo utahusisha pia uwezekano wa kuhamisha mara moja baadhi ya mitambo ya kuzalisha umeme kutoka mtambo wa kuzalisha umeme wa *Symbion* Ubungo na kupelekwa Mtwara, lengo likiwa ni kuongeza ufanisi kwa muda mfupi huko Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 2.5 ni kuwa upembuzi yakinifu huo pia utahusisha utoaji wa mafunzo ya kina kuhusiana na uendeshaji wa mitambo ya kisasa ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini Marekani kwa ajili ya utawala wa baadaye wa *SPC.*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitishwa sana na tabia ya Serikali hii ya CCM kutokana na tabia yake ya kuendelea kupuuza maazimio ya Bunge hili, kwani itakumbukwa kuwa moja ya maazimio ya Bunge kuhusiana na *Richmond* ilikuwa ni kuhusisha Kamati za Bunge katika kuingia mikataba na makampuni ya kuzalisha umeme, sasa hapa sio kuzalisha tu bali ni kuanzisha kampuni nyingine.

Mheshimiwa Spika, aidha, tunataka kujua ni kwa nini Serikali hii ya CCM imeamua kusaini *MOU* ya aina hii bila kuishirikisha Kamati ya Bunge au Bunge, tena huu ni mkataba wa kwenda kuuza umeme nje ya nchi wakati sisi tuna shida kubwa ya umeme. Je, hii haiwezi kwenda kuwa *Richmond* nyingine?

Mheshimiwa Spika, Wakala huyu alianzishwa kwa Sheria Na 8 ya mwaka 2005 na alianza kazi rasmi oktoba mwaka 2007, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2003. Lengo likiwa ni kuwapatia wananchi waishio vijijini nishati bora.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa Wakala huyu, bado Serikali haijaonesha kwa vitendo kuwa ina nia ya kusaidia Wakala huyu ili aweze kutimiza majukumu yake kikamilifu na hasa linapokuja suala la kuupatia fedha kama zinavyoombwa na zinavyopitishwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa Serikali imekuwa haitimizi wajibu wake wa kuipatia *REA,* fedha kama zinavyotengwa na kuidhinishwa na Bunge hili, kwa mfano, mwaka 2008/2009, zilipitishwa shilingi bilioni 20.00 ila zilitolewa shilingi bilioni 12.06 sawa na asilimia 60. Mwaka 2009/2010, zilipitishwa shilingi bilioni 39.55, zilizotolewa ni bilioni 22.14 sawa na asilimia 56. Mwaka 2010/2011, zilipitishwa bilioni 58.883,

zilizotolewa zilikuwa bilioni 14.652 sawa na asilimia 25. Mwaka 2011/2012, zilipitishwa bilioni 71.044, zilitolewa bilioni 56.748 sawa na asilimia 80 na mwaka 2012/2013 zilipitishwa bilioni 53.158, zilitolewa bilioni 6.757 sawa na asilimia 13.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014, Wakala unahitaji kiasi cha shilingi bilioni 366.9 kwa ajili ya kutekeleza miradi sita ya nishati vijijini ambayo ni pamoja na awamu ya pili ya kusambaza umeme vijijini bilioni 200, mradi wa kupunguza gharama za miundombinu na usambazaji wa umeme vijijini bilioni 10, kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya mpya 13 bilioni 70, mradi wa kusambaza umeme kwenye maeneo yaliyopitiwa na njia kuu bilioni 75, mradi wa *Global Village Energy Partinership* bilioni 10.4 na mradi wa kuhamasisha na kuongeza matumizi ya nishati jadidifu bilioni 1.5.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inaitaka Serikali kutenga fedha kama zilivyoombwa na Wakala yaani bilioni 366.9 kwa mwaka huu wa fedha na sio kutenga kiasi cha shilingi bilioni 91 za ndani na bilioni 62 za nje, kama Kifungu 3001, kasma 3113 zinavyoonesha, kwani Wakala huyu asipopewa fedha kulingana na mipango ilivyo atashindwa kufikia lengo la kusambaza umeme kwa asilimia 30 Vijijini.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kujua fedha zilizotengwa kwa ajili ya *REA* 2012/2013, asilimia 87 zimekwenda wapi? Mbona hazikupelekewa *REA* kama Bunge lilivyokuwa limeamua?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA, haikubaliani na pendekezo la Waziri alililoliwasilisha mbele ya Kamati ya Bunge (randama ukurasa 22) la kuongeza tozo ya shilingi 100 kwenye kila lita moja ya mafuta ya petroli kwa ajili ya nishati Vijijini kwani huku ni kumwongezea mwananchi mzigo wa gharama za maisha, badala yake tunaendelea kusisitiza kuwa fedha zilizoongezwa kwenye kila lita moja ya mafuta ya taa mwaka 2011/2012, kwa hoja kwamba, ni kuzuia uchakachuaji shilingi bilioni 600 kwa mwaka zipelekwe zote *REA,* kwani watumiaji

wakuu wa mafuta ya taa wapo vijijini na nusu zipelekwe *TANESCO*. Aidha, makampuni ya madini yalipe kodi na tozo za mafuta wanayosafirisha na wanayotumia.

Mheshimiwa Spika, *thermal power operation* bilioni 273.207; mradi huu ni kwa ajili ya kuhudumia vituo vya uzalishaji umeme ambavyo vimeungwa kwenye Gridi ya Taifa na kununua vipuri vyake wakati kina cha maji kwenye mabwawa ya kufua umeme kitakapopungua kutokana na ukame. Kwa mwaka huu, fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya kununua mafuta ya kuendeshea mitambo ya dharura ya kufua umeme na kununua umeme kutoka kwa wazalishaji hao binafsi.

Mheshimiwa Spika, Mnamo tarehe 28 Julai, 2012, Naibu Waziri wa Nishati na Madini (nishati) Mheshimiwa Simbachawene wakati akiwasilisha maoni juu ya hotuba ya bajeti alisema kuwa tatizo la mgao wa umeme nchini ni la kupangwa mezani, nanukuu *(hansard* ukurasa 488):

"………..lakini kila unapokaa siku mbili unaombwa kukubaliana na mgawo wa umeme na mkizungumza mezani mgawo unatoweka. Kumbe umeme wa Tanzania ni suala la kuzungumza mezani halafu mnakubaliana kuwa unakuwepo mgao au haupo; hii haikubaliki."

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa hata suala la kutenga fedha nyingi kiasi hiki kwa ajili ya mafuta ya kuendeshea mitambo binafsi ya kuzalisha umeme wa mafuta nalo ni jambo la kupangwa mezani, kwani kama tukiamua kuwekeza kwenye vyanzo vingine vya umeme hakika tusingekuwa tunatumia fedha nyingi namna hii kwa ajili ya umeme wa mafuta nchini tena kutoka kwa wazalishaji binafsi.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa Wizara hii ni kutenga mabilioni ya fedha kila mwaka, kwa mfano, mwaka 2011/2012, zilitengwa bilioni 204.643, mwaka jana 2012/2013, tulitenga bilioni 51.3 (lakini Serikali ikatumia kiasi cha shilingi bilioni 242.96 randama ukurasa wa nne) na mwaka huu wa

fedha tunatenga bilioni 273.207 kwa ajili ya kununulia mafuta ya mitambo ya kuzalishia umeme. Yaani kwa miaka mitatu tu Taifa limeunguza fedha kiasi cha shilingi bilioni 720.81 kwa ajili ya kulipa makampuni binafsi, hivi Mchuchuma, Liganga, *Stiglers Gorge,* inahitaji uwekezaji wa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, mradi wa umeme Igunga. Kutokana na mradi wa umeme ambao unaendelea katika Wilaya ya Igunga kumekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wa Vijiji vya Mbutu, Mwamakona, Bukama, Igunga na vijiji vingine ambavyo mradi huu unapita kutokana na kutokuridhishwa na kiwango cha fidia ambacho walilipwa ili kuweza kupisha na kuachia ardhi yao, nyumba zao na mazao yao kwa manufaa ya mradi huo. Wapo waliolipwa shilingi laki sita, milioni moja na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, imepokea malalamiko ya wananchi juu ya viwango vidogo vya fidia na madai yao ya kutoona tathimini iliyofanywa kulingana na mali zao na pia hawakulipwa kwa njia ya hundi pamoja na kutakiwa kufungua akaunti bali walilipwa kwa fedha taslimu. Hivyo, tunataka kujua juu ya yafuatayo:-

(i) Ni lini wananchi hawa watalipwa kiasi halisi kulingana na ardhi na mali zao?

(ii) Ni kwa nini wananchi hawa walilipwa fedha taslimu na sio kwa njia ya hundi kama ulivyo utaratibu wa malipo wa Serikali?

Mheshimiwa Spika, Serikali na madeni ya Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO).* Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaishangaa Serikali hii ya CCM kwa kukosa dira ya kuongoza nchi hii, hali hii inatokana na Serikali yenyewe kuwa sehemu ya kudhoofisha Shirika lake huku ikitaka kuwaaminisha Watanzania kwamba inashughulikia matatizo ya kupatikana kwa umeme nchini.

Mheshimiwa Spika miongoni mwa matatizo yanayokwamisha Shirika la Umeme Tanzania kujiendesha ni

pamoja na madeni ambayo yamekuwa sugu kutoka kwa makampuni mbalimbali, watu binafsi, mashirika, katika hali ya kushangaza Idara za Serikali zikiwemo pia Wizara za Serikali ambayo inajinadi kuweka mpango wa kumaliza tatizo la umeme wakati ikishindwa kulipia hata bili zake za umeme.

Mheshimiwa Spika, Taasisi za Serikali ambazo zinaonekana kuwa ni wadaiwa sugu hadi kufikia mwezi Januari, 2013 ni pamoja na Zanzibar *State Fuel* inayodaiwa kiasi cha sh. 46,136,823,543/=, Jeshi la Wananchi wa Tanzania *(TPDF)* linadaiwa sh. 13,839,849,487/=, Jeshi la Polisi linalodaiwa sh. 8,994,752,654/= Wizara ya Maji inadaiwa sh. 4,997,245,027/= *DAWASA* inadaiwa sh. 4,114,828,175/= na Jeshi la Magereza linalodaiwa sh. 3,530,850,068/=.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mifano hii michache wadai wengine ni pamoja na *Regional Water Engineers,* Muhimbili *Medical Centre,* Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Hospitali za Serikali, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na *Radio* Tanzania. Kwa mujibu wa taarifa rasmi za *TANESCO* zilizopo ni kuwa shirika linadai jumla ya sh. 83,773,824,632/= hadi mwezi Januari 2013 kutoka kwa wadaiwa ambao ni Wizara na Taasisi za Serikali hii ya CCM.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kueleza sababu za kulihujumu Shirika la Umeme Tanzania kwa kutolipa bili za umeme, lakini pia ikumbukwe kuwa kila mwaka Bunge hili Tukufu linapitisha bajeti kwa Wizara husika zenye vifungu vya matumizi mengine *(OC)* ambayo hutumika kufanyia shughuli nyingine zikiwemo kulipia *bill* za umeme na gharama za Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, tunataka wakati wa majumuisho Serikali itoe maelezo kwa nini imeshindwa kulipa hadi sasa, fedha hizo zinafanya kazi gani na lini Serikali italilipa shirika la umeme Tanzania ili kuepukana na matatizo ambayo Serikali inayasababisha yenyewe.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini ni miongoni mwa sekta ambazo kama Serikali ikiamua kutumia vizuri rasilimali

hii ni miongoni mwa rasilimali ambazo kama zikitumika kwa masilahi ya Taifa zinaweza kulitoa Taifa katika lindi hili la umasikini. Hata hivyo, inaonekana kuwa bado sekta hii kama ilivyo kilio cha Watanzania walio wengi na wenye mapenzi mema na Taifa hili bado haijaweza kuchangia pato la Taifa kwa kiwango kinachotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali hazina ya madini iliyothibitika hadi sasa ni pamoja na dhahabu tani 222, *Nikel* tani milioni 209, shaba tani milioni13.65, chuma tani milioni 103, almasi tani milioni 50.9, *Limestone* tani milioni 313, magadi soda tani milioni109, jasi tani milioni tatu, *phosiphate* tani milioni 577, na makaa ya mawe tani milioni 911. Lakini pamoja na kuwepo kwa hazina hii mchango wa sekta hii katika uchumi wa Taifa na maendeleo ya jamii haukidhi matarajio ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, aidha miongoni mwa vitu vinavyofanya sekta hii kutochangia vyema ukuaji wa uchumi ni pamoja na misamaha katika ulipaji wa kodi ya madini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishangaa Serikali hii ya CCM kwa kushindwa kufuta misamaha inayotoa kwa makampuni ya uchimbaji wa madini hapa nchini licha ya kwamba, jambo hili limekuwa linapigiwa kelele na wadau walio wengi. Kama Taifa tunajiuliza na kutaka majibu toka kwa Serikali ni nini nia hasa na siri ya Serikali katika kuendelea kutoa misamaha hii ya kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ripoti ya kodi katika madini iliyotolewa na Shirika la *International Centre for Tax and Development (ICTD)* iliyotolewa mwezi April 2013 inaonesha kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zinapata pato dogo la mapato ya ndani yanayotokana na madini kwa wastani wa 1:1:3 ikilinganishwa na nchi ya Botswana ambayo ina wastani wa 1.32:1 ikifuatiwa na nchi ya Chile.

Aidha ripoti hiyo inaonesha kuwa Tanzania ingeweza kufikia kiwango cha nchi ya Chile kama ingekuwa na viwango vya kutoza kodi kama nchi ya Chile kwa sekta ya

madini na kuchangia kukua kwa pato la Taifa endapo ongezeko ya kodi ya thamani, kodi ya kusafirisha na kodi ya mapato zinazotokana na madini zingechangia kupanda kwa pato la Taifa *(GDP)*.

Mheshimiwa Spika, suala la mrabaha limeonekana kutopatiwa jawabu halisi kwani kiwango cha asilimia nne kinachotozwa kwa sasa baada ya kufanyika marekebisho bado ni kidogo. Pamoja na kwamba, Kamati ya Jaji Mark Bomani kupendekeza kuwa tozo la mrabaha lizingatie ukokotoaji kwa kigezo cha *gross value* badala ya *net back value,* pendelezo hilo halitekelezwi kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuboresha mazingira ya utoaji wa mrabaha pamoja na kodi, ikizingatiwa kuwa baadhi ya makampuni hayafuati Sheria ya mpya ya Madini ya mwaka 2010 inayotaja kiwango kipya cha mrabaha *(Royalty)* na kuchukua hatua nyingine za ziada kwa kuzingatia mapendekezo tuliyotoa 2011 na 2012 hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ieleze kwanza ni makampuni gani ambayo hayajaanza kutumia sheria hii mpya. Pili ni hatua gani imechukuliwa dhidi ya suala hili, lakini pia viwango vya kodi na mrabaha vinavyotozwa vilingane na viwango vinavyotozwa katika nchi nyingine kama Botswana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mchango wa sekta ya madini katika maendeleo na huduma za jamii *(Corporate social responsibility);* Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kuwa sekta ya madini inayo kazi ya kuhakikisha maendeleo na huduma za jamii vinapatikana.

Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha adhima hii, ripoti ya Jaji Mark Bomani ilipendekeza miongoni mwa mambo mengine ni pamoja na wawekezaji kutoa huduma za jamii ili kuimarisha uhusiano na jamii zinazozunguka migodi,

wawekezaji washiriki katika mashauriano ya mashauri ili wajue vipaumbele na mirabaha inayokwenda Halmashauri itumike katika kuboresha huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mapendekezo hayo, lakini hali ya Halmashauri ambako makampuni ya uchimbaji wa madini yanakopatikana, bado ni Wilaya maskini sana. Halmashauri za Kahama, Geita, Tarime hazifanani na thamani ya madini yanayopatikana katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo kuna mkanganyiko katika sheria ya *Local Authority Finance Act* dhidi ya mikataba na kusababisha Halmashauri kukosa haki zake. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza hatua zaidi za makusudi ambazo inachukua kuhakikisha wananchi wa maeneo hayo na Watanzania kwa ujumla wananufaika na rasilimali za nchi hii kwa maeneo hayo ikiwa ni pamoja na kushughulikia mkanganyiko huo wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kunukuu tulichokisema mwaka 2011/2012, kuhusiana na ujanja wa makampuni makubwa ya madini. Ili kuongeza kiwango cha mapato ikiwemo ya kodi kutokana na uchimbaji wa madini; Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutekeleza mikakati ya kupenya kuta za umiliki na mitaji *(capital and ownership structures)* zilizojengwa kwa muda mrefu na Makampuni ya Kimataifa kwa kutumia mianya ya udhaifu wa kisheria na ushawishi wa kifisadi uliosababisha mikataba mibovu katika sekta ya madini nchini.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza bayana hatua ambazo imechukua kufuatia Ripoti ya Tume/Kamati mbalimbali ambazo ziliundwa na Serikali kwa nyakati mbalimbali kwa kutumia fedha nyingi za walipa kodi, lakini mapendekezo yake bado hayajatekelezwa kwa ukamilifu wake.

Mheshimiwa Spika, mathalani ripoti za karibuni za Kamati ya Masha na ile ya Bomani (2008) zilieleza bayana

namna ambavyo makampuni makubwa ya madini yamekuwa yakitumia sehemu kubwa ya uwekezaji wao kama mkopo *(debt financing).*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kwamba, makampuni hayo yamekuwa yakitumia mianya hiyo ya kisheria na kimikataba kuwezesha wamiliki na wanahisa kupata faida mapema kuliko kuweka mtaji kwa kuwa riba ya mikopo huondolewa katika kukokotoa kodi. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali iwaeleze Watanzania ni trilioni ngapi za mapato tumezikosa kati ya mwaka 1995 mpaka 2010 katika kipindi cha miaka 15 ya kuachia mianya ya upotevu wa mapato kwa kuruhusu asilimia kubwa ya mikopo kuwa mitaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, ni hatua gani zimechukuliwa kwa waliohusika kuliingiza Taifa katika mikataba mibovu iliyoruhusu makampuni hayo kujitangazia hasara kila mwaka huku yakipata faida kubwa.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya wachimbaji wadogo wadogo wa madini, kimekuwa ni kilio cha muda mrefu kwa Taifa hili. Kwa mujibu wa mapendekezo ya Kamati ya Jaji Bomani kuhusu namna ya kuboresha mazingira ya wachimbaji wadogo wadogo wa madini, Kamati ilishauri muda wa leseni kuongezwa kufikia miaka 10 ili kuwawezesha wachimbaji hao waweze kupata mikopo kutoka taasisi za fedha.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji kusaidiwa mbinu kwa ajili ya kupata mtaji wa kufanya shughuli za uchimbaji, kuchangia katika Mfuko wa Wachimabji Wadogowadogo, kuwekwa kwa utaratibu wa kisheria kwa ajili ya kuwakatia bima wafanyakazi wao na kuanzisha taasisi za fedha kwa ajili ya mikopo kupitia *SACCOS* zao.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2011/2012, pamoja na makadirio ya mapato na

matumizi kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Kamati ilithibitisha matatizo ya wachimbaji wadogo wadogo kuwa ni pamoja bajeti ndogo inayotengwa kwa wachimbaji, elimu kutotolewa kwa wachimbaji, uhaba wa maeneo ya uchimbaji kwa vile maeneo yao yamechukuliwa na wawekezaji wakubwa, ukosefu wa masoko ya kuuzia bidhaa zao na kodi kubwa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza hatua ilizofanya katika kutekeleza mpango mkakati wake hususan katika matatizo yafuatayo:-

(a) Serikali imeongeza kiasi gani cha fedha kwenye bajeti ya wachimbaji wadogo wadogo, ni utaratibu gani umewekwa ili fedha hizo ziwafikie walengwa?

(b) Kuna mkakati gani wa kuhakikisha wachimbaji hao wanapata mafunzo ya uchimbaji na masuala yanayolenga kuongeza thamani ya madini yao?

(c) Maeneo gani na kanda zipi ambapo wachimbaji hawa wametengewa maeneo kutokana na maeneo yao kuchukuliwa na wawekezaji wakubwa?

(d) Serikali imeweka mfumo gani katika kuhakikisha mchango wa uchimbaji mdogo unajulikana kwenye pato la Taifa?

(e) Ili kuongeza thamani ya madini, kuna mkakati gani wa kuhakikisha kazi hii inafanyika hapa nchini na kuongeza siyo tu thamani bali ajira kwa Watanzania?

(f) Hatua gani zimefanywa na Serikali kuhakikisha soko na bei ya madini inakuwa imara na mikakati gani imewekwa ili kuhakikisha umeme unapatikana katika maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo?

Mheshimiwa Spika, sasa ni takriban miaka sita toka kuwasilishwa kwa ripoti ya Mheshimiwa Jaji Mark Bomani kwa Rais. Baada ya kuwasilishwa pia hapa Bungeni na Kamati

husika na Bunge likaijadili na mapendekezo yake yakawa ni maazimio ya Bunge, lakini hadi sasa maazimio ya Bunge bado hayajatekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo ya Tume ya Jaji Bomani ambayo pia yaliridhiwa na Bunge lako Tukufu na kupitishwa kama Azimio la Bunge ni pamoja na kufutwa misamaha ya kodi, kwa badiliko alilotoa Waziri wa Fedha la kufuta utekelezaji wa *GN* 99 kuanzia Julai 2009 kwa makampuni. Marekebisho haya yanahusu kampuni za madini zilizoingia mkataba na Serikali kuanzia Julai, 2009. Kwa nini ufutaji wa misamaha hii usiyaguse makampuni yaliyokuwepo kabla ya Kamati ya Jaji Bomani haijaanza kazi?

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba, msamaha ambao unaendelea kutolewa hadi sasa kwa makampuni hayo ya mafuta unaukosesha Mfuko wa Barabara mabilioni ya fedha na huko makampuni hayo ndiyo yanaharibu kwa kiasi kikubwa barabara zetu. Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge ni kwa nini maazimio ya Bunge hadi leo hii hayajatekelezwa kikamilifu?

Mheshimiwa Spika, aidha, mapendekezo mengine ya Kamati ya Mheshimiwa Jaji Bomani yalikuwa ni:-

(i) Serikali kumiliki hisa ndogo kama kwa kampuni ya *Williamson Diamonds Limited* ambapo Serikali ina hisa 25%, hali ambayo si sawa kwa umiliki wa kigeni. Upo umuhimu wa ushiriki wa kutosha wa Watanzania katika umiliki wa hisa za kampuni za uchimbaji mkubwa.

(ii) Shughuli zote za uchimbaji wa vito na Kampuni za uchimbaji wa kati wa madini mengine, zimilikiwe ama kwa 100% au kwa kiasi kisichopungua 50% na wananchi wa Tanzania.

(iii) Shughuli zote za wachimbaji wadogo zimilikiwe na kuendeshwa na Watanzania tu.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio ya Kambi Rasmi ya

Upinzani, Serikali itawaeleza Watanzania utekelezwaji wa maazimio hayo ya Kamati ya Mheshimiwa Jaji Bomani ambayo yaliridhiwa na Bunge yametekelezwa kwa kiwango.

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumika katika kuingia mikataba ya uchimbaji wa madini umewekwa wazi katika Sheria ya Madini ya mwaka 2010. Sehemu ya 23 ya Sheria hiyo inaelezea kuhusu kuanzishwa kwa bodi itakayojulikana kama Bodi ya Ushauri ya Sekta ya Madini. Bodi hii inamshauri Waziri anayesimamia madini kuhusu masuala ambayo yako chini ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 ambayo yanatakiwa kufikishwa kwenye Bodi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini imeonesha udhaifu wa kumnyima hata Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kuhakiki mikataba ambayo Serikali imefunga na wachimbaji ili kubainisha taratibu ambazo zinafuatwa na Wizara katika kutekeleza matakwa ya sheria hii kwa vile mikataba hii ya uchimbaji ni ya watu binafsi na ni siri kwa watu wengine wasiokuwa sehemu ya mikataba hiyo. Kutokana na usiri huo, sikupewa haki ya kuipitia mikataba hiyo na hivyo kuzuia wigo wa ukaguzi wangu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaliomba Bunge katika mjadala huu utakaoendelea, kupitisha azimio mahususi kuilazimisha Wizara kuwajibika kwa kuendelea na utekelezaji wa mikataba yote ambayo, kwa njia moja au nyingine imekiuka sheria na pia imekiuka maazimio na ushauri unaotolewa na Bunge. Kwa njia hii tutakuwa tumetimiza wajibu wetu wa Kikatiba wa kuisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, mchango wa sekta ya madini katika pato la Taifa bado ni mdogo mno ukilinganisha na jinsi nchi yetu ilivyojaliwa rasilimali hii na uchimbaji unaoendelea sehemu mbalimbali katika nchi yetu. Kwa ujumla madini tuliyojaliwa hayawafaidishi Watanzania kwa kiwango kilichotegemewa zaidi ya kuwaingiza kwenye matatizo ya uchafuzi wa kimazingira na ugumu wa maisha.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini *(STAMICO)* linaimarishwa upya na Serikali baada ya kuondolewa kutoka kwenye orodha ya Mashirika ya Umma yanayotakiwa kufutwa mwezi Machi, 2009. Hivyo lilipewa majukumu makuu manne, ambayo ni:-

(a) Kuwekeza katika utafutaji, uendelezaji na uchimbaji wa madini;

(b) Kusimamia hisa za Serikali katika migodi;

(c) Kuratibu uendelezaji wa wachimbaji wadogo nchini; na

(d) Kutoa huduma za kibiashara katika sekta ya madini, huduma hizo ni uchorongaji wa miamba, utafutaji wa madini na utoaji ushauri katika masuala ya madini.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya shirika iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Nishati na Madini, inaeleza kuwa Bodi ilimaliza muda wake mwezi Juni, 2012. Hivyo basi, Shirika hilo halina Bodi hai. Kwa mujibu wa taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti ameongelea kitendo cha Mwenyekiti wa Bodi kuingilia moja kwa moja utendaji wa Shirika hilo kiasi kwamba, shirika limekuwa likimlipa posho ya mafuta Mwenyekiti huyo sawa na lita 100 za mafuta kila wiki, asilimia 40 ya posho ya mafuta kama fedha za matengenezo kila wiki na shilingi 500,000/= kwa mwezi kama fedha za mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, msuguano huu wa kiutendaji kati ya Mkurugenzi Mtendaji na Mwenyekiti wa Bodi kwa kiasi kikubwa inadumaza utendaji wa shirika. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwachukulia hatua za kinidhamu Wenyeviti wenye tabia kama hii kwani malipo hayo ni aina nyingine ya matumizi mabaya ya rasilimali za umma ambayo yanapaswa kudhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, *STAMICO* ndiyo yenye dhamana ya uendelezaji wa Mgodi wa Buhemba, kwani tangu mwezi

Julai, 2011, shirika lilipewa leseni ya utafutaji wa madini juu ya eneo la mgodi wa zamani wa dhahabu wa Buhemba, Mkoani Mara kwa kumiliki asilimia 40 za mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli kwamba, mgodi huu wa Buhemba ndio uliokuwa ukimilikiwa na Kampuni ya MEREMETA kampuni ambayo mbali ya kuiingiza nchi kwenye kashfa bali pia iliwaacha wananchi/ wachimbaji wadogo wa eneo la Buhemba wakiwa na malalamiko ya kutokulipwa fidia kwa kutwaliwa maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuelewa, je, *STAMICO* ina mkakati gani wa kwanza kuchukua mali zilizokuwa zinamilikiwa na MEREMETA? Pili, madai ya wananchi wanayalipa vipi kwa pamoja na mbia wake?

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ushauri ulipotolewa na Mkaguzi kuhusu ushiriki wa Sekta ya Umma na Sekta binafsi kugubikwa na upungufu mkubwa ambapo faida inakuwa kwenye upande wa pili zaidi na Serikali. Mfano, ni ubia wa *SONGAS Limited, IPTL Limited,* Kiwira *Coal Mines (Tanpower Limited), TICTS* na kadhalika. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwahakikishie Watanzania ni kwa kiwango gani ubia huo wa *STAMICO* na *Manjaro Resources Pty Limited* kutoka Australia utakuwa na tija kwa Taifa?

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ukaguzi wa Madini *(TMAA)* Wizara ya Nishati na Madini 8 Desemba, 2011 ilitoa taarifa kwa umma kuhusu maendeleo ya sekta ya madini. Mrabaha uliolipwa na migodi mikubwa ya dhahabu katika kipindi hicho cha kuanzia mwaka 1998 hadi 2010 ilikuwa ni Shilingi Bilioni 341.57, wakati hadi kufikia mwaka 2010 kulikuwa na Watanzania 6,129 walioajiriwa rasmi kwenye migodi mikubwa sita ya dhahabu. *PAYE* wanayolipwa ni kati ya asilimia 14 mpaka 30 kutegemea kiwango cha malipo.

Mheshimiwa Spika, ili kufanya ulinganisho ulio sahihi wa kama kweli mchango wa sekta ya madini kwenye kodi unatokana na mrabaha au kodi ya *PAYE* wanayolipa

waajiriwa hao 6,129 ilitakiwa tuambiwe ni kiasi gani, kwani kuna uwezekano mkubwa *PAYE* inazidi kwa mbali fedha inayoingia itokanayo na mrabaha.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania *(TMAA)* ndiye mwenye dhamana katika kudhibiti uzalishaji wa madini na ukusanyaji maduhuli yatokanayo na mrabaha kwa kampuni za uchimbaji madini. Hata hivyo, *TMAA* haina udhibiti wowote katika uzalishaji na uthamanishaji wa madini kwa wachimbaji wadogo na wa kati ambao wameachwa kueleza wenyewe kiasi cha madini wanachozalisha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli huo, ni kwa vipi Wizara inataka kuliaminisha Bunge kuwa takwimu za madini hasa dhahabu zilizozalishwa hapa nchini kuwa ni sahihi?

Mheshimiwa Spika, upungufu haya kwa kiasi kikubwa yanatokana na ukweli kwamba *control mechanism* kwa wachimbaji wadogo wakati wa kutoa leseni umegubikwa na matumizi mabaya na udanganyifu ambapo watu wachache wamehodhi maeneo mengi na kuajiri wachimbaji wadogo na kinachopatikana kutokana na machimbo hayo Serikali inanyimwa taarifa. Pia kushindikana kwa udhibiti ni viwanja vidogo vya ndege vilivyotapakaa hapa nchini ambavyo *TMAA* haina udhibiti navyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa hiyo ni kwamba, Serikali imechukua hatua zingine za kuimarisha usimamizi wa sekta ya madini ni pamoja na:-

(i) Kutenga maeneo maalum ya wachimbaji wadogo;

*(ii)* *TANSORT* kuhamishia rasmi shughuli zake hapa nchini kutoka Uingereza mwezi Agosti, 2010; na

(iii) Upigaji marufuku wa usafirishaji nje ya nchi madini ghafi ya *Tanzanite* yenye ukubwa unaoanzia gramu moja na kuendelea mwezi Aprili, 2010.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge tangu kitengo hicho cha kuchambua almasi kirudishwe hapa nchini toka Uingereza ni kiasi gani cha fedha kimepatikana kutokana na kazi zake hizo?

Mheshimiwa Spika, yamekuwepo madai ya wachimbaji wadogo wadogo ambao ndiyo wazawa kunyimwa leseni katika maeneo yao ya uchimbaji na maeneo yao kugawiwa kwa wanaojiita wawekezaji na wao wakihamishwa hamishwa pasipo kupatiwa maeneo mbadala.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo mengi ya wachimbaji wadogo wadogo katika maeneo ya Kalalani Tanga, Mgusu, Nyarugusu, Mtakuja Geita, Winza, Mtakanini, Mpwapwa, Simangulu, Chamwino, North Mara, Rwamgasa, Kasema, Kilindi, Nyamongo na kadhalika. Hivi karibu ni wachimbaji wapatao 400 wa Kijiji cha Nkongilangi wanaochimba eneo la Machimbo ya Sekenke-Iramba Magharibi, ambao toka mwaka 1982 wamekuwa wakiomba leseni lakini hawapatiwi majibu ya maombi yao.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007 waliomba tena na kuambiwa leseni imetolewa kwa kampuni ya WASEKE. Kwa mshangao mkubwa mwaka 2011, alikuja mtu anayedai kuwa ndiye mmiliki wa eneo hilo la uchimbaji mdogo la Kijiji cha Nkongilangi aitwaye John Bina. Hapo ndipo matatizo na unyanyasaji ulipoanzia na kusababisha uporaji na vifo kutokea.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira kama hayo, wachimbaji wadogo wapatao 3,000 kwa ushirika wao Wilayani Maswa baada ya kulipia ada ya maombi yao imechukua takriban miezi minne baadaye wakajibiwa kuwa eneo hilo tayari lilikuwa na mmiliki toka mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya kuangalia *coordinates* zilizosemwa kwenye barua na zile zilizoko kwenye ramani, ni kwamba leseni *PL* 4233/2007 ambayo mmiliki wake ni *Savannah Expl. Limited* iliyotolewa tarehe 2 Mei, 2007 na eneo lake liko Luguru na Luguru ni kijiji kilicho ndani ya Wilaya ya Bariadi na sio Maswa. Huu ni mkakati unaotumiwa na watendaji wa Idara ya Madini kwa kushirikiana na wenye dhamana katika Serikali kuwanyima haki wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza wachimbaji fedha zilizotengwa kiasi cha shilingi bilioni moja kama kianzio cha Mfuko wa kuendeleza Wachimbaji wadogo nchini, kama hotuba ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda alivyosema Bungeni wakati akiwasilisha mapitio na makadirio ya matumizi ya fedha yake na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2010/2011 zilipewa wachimbaji wadogo wa wapi?

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa mujibu wa maneno ya Mheshimiwa Naibu Waziri Madini wakati akijibu swali tarehe 22 Aprili, 2013 alisema Serikali inatarajia kukamilisha taratibu za Mfuko rasmi wa kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa madini ili kuwawezesha kupata mikopo, ikiwa ni pamoja na kuwapatia mikopo ya vifaa vya kuchimbia kwa kanda zote nane zinazochimba madini nchini.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza Mfuko huo ambao umekwishatengewa fedha na hapa Naibu Waziri anasema inatarajia kukamilisha taratibu rasmi za Mfuko huo, hii maana yake nini? Mfuko huo utaendeleza wachimbaji gani wakati ambapo maeneo mengi wana malalamiko ya leseni na wanafukuzwa ovyo kama mifano ambayo tumeitoa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, kwa wale walio na maeneo ya kuchimba madini wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu kutokana na kuwa na mtaji mdogo unaowafanya washindwe kupata zana bora kwa ajili ya uchimbaji. Aidha, watoto wa walalahoi wamekuwa wakiajiriwa katika migodi

mbalimbali nchini mbali ya kuwa na sheria inayopinga ajira kwa watoto hususan katika maeneo ya migodini.

Mheshimiwa spika, kitendo cha Serikali kupandisha kodi mara kawa mara kwa wachimbaji au wawekezaji wadogo wadogo ni kufanya wawekezaji wadogo wasimudu kushiriki kikamilifu katika kuwekeza ndani ya Sekta ya Madini wakati Serikali inajigamba kuwasaidia wawekezaji hao huku Serikali ikipandisha kodi kutoka 80,000/= hadi 1,000,000/= kwa wachimbaji hao.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ambalo pia lililalamikiwa na Wabunge wengi limeonekana limetafsiriwa kuwa ni mkakati wa makusudi wa kuwafukuza wawekezaji wadogo wadogo katika sekta hii na kutoa mianya kwa wawekezaji wenye pesa zao kuendelea kuwekeza katika sekta hii ya madini.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ieleze kwa kina ni kwa jinsi gani itawasaidia wachimbaji wadogo kama gharama za uendeshaji wa migodi hiyo zinapanda bila kuzingatia hali halisi ya wachimbaji hao. Hii ni hatari sana kwani tunafanya wazawa washindwe kunufaika na sekta hii moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha sekta hii ya madini, Kamati ilishauri mambo yafuatayo yafanyike:-

(i) Serikali kuwawezesha wafanyabiashara wadogo kushiriki katika shughuli za kutoa huduma *(supply)*mbalimbali migodini;

(ii) Sheria ya ajira kwa watoto isimamiwe ipasavyo;

(iii) Migodi mikongwe ilipe kodi *(corporate tax);*

(iv) Kuwepo kwa soko la pamoja la madini;

(v) Kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji

wadogo katika kila kanda na kusimamia vizuri zoezi la ugawaji wa leseni;

(vi) Serikali iwasaidie wachimbaji wadogo ili waweze kupata mikopo ya kuwawezesha kuanzisha viwanda vidogo vitakavyowasaidia kuongeza thamani ya madini yao; na

(vii) Serikali kukomesha biashara haramu ya madini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Serikali haijayafanyia kazi kwa ukamilifu mapendekezo hayo ya Kamati katika mwaka wa fedha 2012/2013 na bado sekta hii inakumbwa na hali ile ile na kuifanya iendelee kutokuwa na mchango mkubwa katika uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa fedha za Serikali ulioishia 30 Juni, 2012 inaonesha kuwa Wizara ya Nishati na Madini imeliingizia Taifa hasara ya zaidi ya sh. 20,000,000,000 katika sekta ya madini. Hasara hiyo kama ilivyooneshwa kwenye taarifa ya *CAG* ilisababishwa na malimbikizo ya maduhuli ambayo hayakuonyeshwa Sh. 1,645,582,899.

Mheshimiwa Spika, taarifa za fedha zilizowasilishwa na Wizara hazikuonesha malimbikizo ya maduhuli yenye jumla ya Sh. 1,645,582,899/= kama ilivyotakiwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashangaa ni kwa sababu gani hasa bado Sheria ya zamani inaendelea kutumika wakati tayari Sheria ya mwaka 2010 imeshaanza kufanya kazi. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara ieleze kwa nini hali hiyo imejitokeza na hatua gani inachukua dhidi ya watendaji waliohusika katika kulipatia hasara hiyo?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani pia inaitaka Serikali kutumia Sheria mpya ya kukusanya mrabaha

katika kampuni za madini na hivyo makampuni yote yaliyolipa mrabaha huo kwa kutumia Sheria ya zamani yalipe sehemu iliyobakia kwa mujibu wa sheria mpya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo tunaitaka Serikali ilitaarifu Bunge lako Tukufu kuhusu malimbikizo ya maduhuli ambayo hayakuoneshwa kwenye taarifa za mahesabu ya Wizara hii, tunataka tujue Serikali ina mpango gani na fedha hizi ambazo ni zaidi ya 1,000,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine yanayosababisha hasara katika sekta ya madini ni pamoja na kutokuwa na udhibiti wa mapato ya wachimbaji wadogo wa madini na kutokuwa na udhibiti katika viwanja vya ndege. Udhibiti mdogo katika sekta hii ya madini kumesababisha kupotea kwa mapato mengi ambayo nchi ingeyapata kutokana na madini yanayosafirisha bila kulipa kodi na biashara haramu ya madini inayoendelea nchini.

Mheshimiwa Spika, pia kwa mujibu wa taarifa ya *CAG* hakuna ushirikiano kati ya Wizara na *TRA* na hivyo kodi nyingi zinashindwa kukusanywa kutokana na *TRA* kukosa taarifa sahihi juu ya vyanzo vya mapato vya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa ahadi nyingine za Waziri wa Nishati na Madini katika bajeti ya 2012/2013; Waziri wa Nishati na Madini katika majumuisho yake aliahidi Bunge kuwa kuna madini ya *VANADIUN* na *PGE* yanayopatikana katika madini ya *Copper* na *Nickel*. Hilo atalifanyia kazi suala la wawekezaji wanaochukua leseni ya *copper* na *nickel* kwani kuna upatikanaji wa madini ya *VANADIUM* na *PGE* ambayo inasemekana kuwa yana thamani kubwa kuliko *copper* na *nickel*.

Mheshimiwa Spika, hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza juu ya utekelezaji wa suala hili kama Mheshimiwa Waziri alivyoahidi Bungeni wakati wa kuhitimisha hotuba ya bajeti ya Wizara yake ya mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, katika suala la mkopo wa bilioni 8.9 kwa wachimbaji wadogo kwamba, ni kwa vipi wachimbaji wadogo wangepewa mikopo hiyo wakati kwa wakati huo leseni nyingi na maeneo yote wamepewa wawekezaji wakubwa, Mheshimiwa Waziri aliliambia Bunge kuwa leseni hizo zinakwisha muda wake na zikiisha muda wake wawekezaji wakubwa wanaacha nusu ya eneo walilokuwa wanamiliki na hivyo maeneo haya wanapewa wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, katika suala hilo hilo la wachimbaji wadogo wadogo ilijitokeza pia hoja kutoka kwa Wabunge, waliomuuliza Waziri wa Nishati na Madini jinsi gani mkopo wa *billion* 8.9 uliopangwa kuwanufaisha wachimbaji wadogo wadogo nchini utagawiwa kwa wachimbaji husika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alijibu wanatakiwa waunde Vyama vyao kila Mkoa na wawe na Chama chao Kitaifa ambako ndiko mkopo huu utaelekezwa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itupe takwimu sahihi mpaka sasa tathmini ikoje juu ya leseni za wawekezaji wakubwa kwisha muda wake na wawekezaji wadogo kupewa maeneo husika na je, mkopo wa bilioni 8.9 umewanufaisha wachimbaji wadogo wadogo wangapi mpaka sasa?

Mheshimiwa Spika, kama wachimbaji wadogo hawajanufaika na mkopo huu Serikali itueleze fedha hizi zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2012/2013, kwa ajili ya kazi hii zimefanyiwa nini?

Mheshimiwa Spika, kuhusu madeni ambayo wawekezaji katika sekta ya madini wanadaiwa na Serikali, Naibu Waziri wa Nishati na Madini wakati wa mjadala wa bajeti ya mwaka 2012/2013, alipokuwa anajibu hoja ya madeni ambayo wawekezaji katika sekta ya madini walikuwa wanadaiwa tangu mwaka 1997 hadi mwaka 2005 aliliahidi Bunge kwamba kampuni ya *BARRICK* ambayo ndiyo kampuni pekee iliyokuwa inakataa kulipa deni lake atalifanyia kazi suala hilo na kuhakikisha wanalipa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ieleze kama madeni yote yamelipwa kwa kuzingatia Sheria mpya ya Madini ambayo pamoja na mambo mengine inataka mirabaha kulipwa kwa asilimia nne (4%) kabla ya makato ya kodi na kama kuna makampuni hayataki kutii sheria hii mpya ya madini, kwa nini Serikali isiyafutie leseni ya kufanya kazi za uchimbaji wa madini nchini? Kwa sababu nchi haiwezi ikavumilia wawekezaji ambao hawatii sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, pia Naibu Waziri alikiri mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa mgodi wa Buzwagi haujalipa kodi ya kampuni yaani *(Corporate tax)* na kuahidi kuwa mgodi wowote mpya utaoanza kuanzia wakati huo Serikali itaanza kuwa na *share* ya 15% kama hisa za kubeba *(free carried interest).*

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu na umma wa Watanzania kwa ujumla wake kama mgodi huo umelipa kodi hiyo na Serikali imejipangaje kumiliki hisa kwenye migodi inayotegemewa kuanzishwa na hii ambayo imeanzishwa kwa ajili ya kuwa na udhibiti wakati kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 ambayo inatoa haki hiyo ya Serikali kuwa na hisa.

Mheshimiwa Spika, uchimbaji madini aina ya urani; kwa kuwa suala la uchimbaji na utafutaji wa madini ya aina yoyote lipo chini ya Wizara ya Nishati na Madini na kwa kuwa suala la uchimbaji wa madini ya aina ya urani kama Taifa tunahitaji kuwa na angalizo kubwa ikiwa ni pamoja na kutochimba madini hayo ya aina ya urani kutokana na uhatari wake kwa maisha ya binadamu.

Pia kwa kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa mara kadhaa ndani ya Bunge hili imekuwa ikitoa maoni yenye nia njema na maisha ya Watanzania na viumbe vingine na kwa kuwa tatizo la Serikali kutokubali kufanya maamuzi ya kubadili mtazamo wa kutegemea uchumi wa urani na kujikita katika uchumi wa rasilimali mbadala ambazo Taifa letu limebarikiwa kuwa nazo.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la mbarang'andu katika Wilaya ya Namtumbo ambapo kampuni ya *Game Frontiers* iliyojipatia kitalu hicho kwa ajili ya uwindaji kwa mujibu wa sheria imeamua kufanya biashara ya kuruhusu utafiti wa uchimbaji madini aina ya urani kinyume na taratibu za uendeshaji wa vitalu vya uwindaji.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili mnamo Tarehe 28 Julai, 2012 zilitolewa taarifa hapa ndani ya Bunge hili kwa vielelezo kutoka kwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu masuala ya ardhi Mheshimiwa Halima Mdee juu ya kampuni ya *Game Frontiers* kukodisha kitalu chake cha uwindaji kwa ajili ya utafutaji wa madini ya urani katika eneo la Mbarang'andu katika Wilaya ya Namtumbo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani alitaka kupata ufafanuzi kwa Waziri juu ya maagizo yaliyotolewa na Naibu Spika wakati wa majumuisho ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Maagizo husika yalitaka Wizara ya Nishati na Madini, wakati wa kupitisha makadirio ya mapato na matumizi itoe maelezo juu ya mkataba ulioingiwa tarehe 23 Machi, 2007 kati ya *Uranium Resources PLC* na *Western Metals Limited* na *Game Frontiers of Tanzania Limited*. Mkataba ambao, pamoja na mambo mengine unaihalalishia *Game Frontiers Limited* kupata malipo toka kwa makampuni yanayofanya utafiti katika kitalu cha uwindaji katika Kijiji cha Mbarang'andu.

Mheshimiwa Spika, majibu ya Waziri yalikuwa kama ifuatavyo nanukuu: "....Mheshimiwa Spika, lingine lililoulizwa na Kambi ya Upinzani hasa Mheshimiwa Mdee, huu mkataba wa siri, kweli tumeufuatilia mkataba wa siri, ule wa uchimbaji wa *uranium...*"

Mheshimiwa Spika, kuonesha Waziri alikiri mbele ya Bunge na kuahidi kulitafutia ufumbuzi suala hilo na kuwa ataleta taarifa kwa mtoa hoja. Kwa mara nyingine tena Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni vipi Wizara

ya Nishati na Madini imeshughulikia suala la kampuni ya uwindaji ya *Game Frontiers* kukodisha kitalu chake cha uwindaji kwa ajili ya utafutaji wa madini ya urani katika eneo la Mbarang'andu, Wilayani Namtumbo, lakini pia Serikali iwaambie Watanzania kwa hatua ilizochukua za kuchimba urani ni vipi itaweza kuwalinda dhidi ya madhara ya uchimbaji wa madini hayo?

Mheshimiwa Spika, mgodi wa Kiwira. Kati ya kashfa ambazo ziliikumba Serikali ya Awamu ya Tatu ya Rais Mkapa ilikuwa ni pamoja na kubinafsishwa kwa mgodi huu wa Kiwira. Kwa mujibu wa kumbukumbu za Bunge lako Tukufu, Bunge lilipitisha maazimio yake juu ya taarifa ya kamati ya Nishati na Madini kuhusu ubinafisishaji wa mgodi wa Kiwira kufuatia mapendekezo yaliyokuwa yameelekezwa Serikalini kwa ajili ya hatua stahiki, miongoni mwa maazimio ya Bunge ambayo hayakufanyiwa kazi na Serikali yalikuwa ni pamoja na:-

(i) Urejeshwaji wa vifaa na mali ambavyo vimeibiwa au kuhamishwa kutoka kwenye miundombinu ya mgodi wa Kiwira;

(ii) Bilioni 17 zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya ukarabati wa miundomninu ya mgodi, Serikali ilitakiwa kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha hizo kupitia kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ili kujua matumizi halisi na halali ya fedha za umma;

(iii) Serikali kufuatilia uchunguzi uliofanywa na TAKUKURU wa shilingi milioni 50 zilizotolewa kutoka Mfuko wa *Consolidated Holdings Corporation;*

(iv) Kuwalipa wafanyakazi wa mgodi wa Kiwira mafao yao na stahiki zao kwa wafanyakazi ambao *CAG* alithibitisha kuwa hawakulipwa;

(v) Serikali kukamilisha haraka zoezi la kukabidhiana mgodi huo; na

(vi) Serikali kueleza kigezo kilichotumika kuwalipa

viongozi waandamizi kiasi cha shilingi milioni 80 wakati wafanyakazi wa kati walilipwa kati ya shilingi milioni nane na wafanyakazi wa chini wakilipwa shilingi milioni moja na nusu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo halijafanyiwa kazi lilikuwa ni hili la malipo yaliyolipwa mara mbili, kwa mujibu wa *Hansard* za Bunge, maoni ya Wabunge yalikuwa ni:

"…niligusie hili la dola milioni nne na laki nane na sitini na tano ambazo ni sawa na bilioni tano na laki sita, Serikali imekiri…imefanya *double payment,* jambo ambalo ni kosa la jinai, … mwenzangu anadai tuachane nayo, haiwezekani", lakini katika hali ya kustaajabisha hadi hivi leo haijulikani hatima ya fedha hizo zilizolipwa mara mbili.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa Serikali ihakikishe maoni yote yanafanyiwa kazi, fedha za walipa kodi haziwezi kupotea hivi hivi kwa wajanja wachache. Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka maelezo ya kina kuhusiana na mambo yafuatayo:-

(i) Fedha za mwaka jana zilitengwa bilioni 40 na zilitumika Bilioni 28 kulipa fidia, je, fedha hizo alilipwa nani na zilikuwa ni kwa ajili gani?

(ii) Mwaka huu tumetenga tena bilioni 20, je, ni kwa ajili ya kuendelea kufidia ufisadi huu au ni kwa ajili ya kazi gani?

Mheshimiwa Spika, Maoni yetu juu ya mapitio ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2012/2013 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2013/2014 yanaonesha kwamba, chanzo cha hali tuliyonayo hivi sasa ni cha muda mrefu. Bunge la Tisa likiongozwa na Spika Samuel Sitta halikuweza kukamilisha kurekebisha hali hiyo, ikiwemo kukwepa kukamilisha kwa wakati maazimio ya Bunge ya mwaka 2010.

Bunge la kumi, likiongozwa na Spika, Mheshimiwa

Anne Makinda katika kipindi chake cha kwanza cha miaka miwili na nusu, halijaweza kukamilisha utekelezaji wa maazimio ya mwaka 2008 na maazimio yake ya mwaka 2011 na 2012. Bunge hili, bado linalo nafasi ya kurekebisha hali hii kuanzia sasa katika kipindi chake cha miaka miwili na nusu iliyobaki.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere katika kitabu chake cha TUJISAHIHISHE ukurasa wa pili (2) aya ya nne (4) kinasema, nanukuu:

"Makosa yetu mengine hutokana na woga; woga unaotuzuia kumlaumu mkubwa japo tunajua kuwa kakosa, au kumtetea mdogo anayelaumiwa na wakubwa japo tunajua kuwa hana makosa na msingi wa woga pia ni unafsi.

Pengine twaweza kuwa hatuna cheo chochote ambacho tunaogopa kupoteza; pengine huwa hatuna wala tamaa yoyote ya kupata cheo fulani. Lakini woga unaweza kutokana na tamaa ya kila binadamu kupendwa na binadamu wenzake.

Sisi wote tunayo tamaa hii au sivyo tusingekuwa binadamu, woga huu huweza ukamfanya mtu kuvumilia maovu, hasa kama maovu yale yanatendwa na walio wengi kwa walio wachache, au yanatendwa na wakubwa kwa wadogo. Kwa kuogopa kuwaudhi wengi tunawaacha watende makosa bila kuwasahihisha, wasije wakatuchukia. Huu ni unafsi mbaya sana.

Ni kweli kwamba, demokrasia haiwezi kudumu ikiwa wachache hawatakubali matakwa ya wengi, lakini matakwa ya wengi hujulikana katika majadiliano au mazungumzo ya wazi wazi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika ukurasa wa tatu (3) aya ya pili, anasema nanukuu: "Kadhalika, matakwa ya wachache hujulikana katika majadiliano na mazungumzo. Bila wale wachache kusema wazi wazi matakwa yao, majadiliano hayana maana. Wakati mwingine, hata baada

ya majadiliano, wachache japo wamekubali kutii uamuzi wa wengi wanaweza kuendelea kuamini kwamba mawazo yao ni sawa na ya walio wengi yamepotoka.

Demokrasi inawapa haki na ukweli unawapa wajibu wa kuendeleza mawazo yao mpaka wengi waone kuwa ni ya kweli. Bila hivyo maendeleo katika mawazo hayawezekani, kwani mara nyingi wazo zuri hutokana na mtu mmoja tu. Mwanzo laweza likapingwa, pengine kwa nguvu kabisa na walio wengi, lakini hatimaye wengi hulikubali. Huu ndio msingi wa maendeleo katika mawazo ya binadamu”.

Mheshimiwa Spika, Katika sekta za Nishati na Madini, kama ilivyo katika sekta nyingi nchini; tumefika hapa tulipo kwa sababu ya udhaifu wa Serikali inayoongozwa na Rais Kikwete, uzembe wa Bunge na ulegelege wa CCM. Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA inataka kama Taifa; tubadilike, tuwajibike, tujisahihishe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Naomba nieleze utaratibu rasmi unaofuatwa ndani ya Bunge. Bunge letu limegawanyika katika Kamati za kisekta na Kamati zote za Kisekta zina wajumbe wa Vyama vyote na *gender* zote. Kamati za Kisekta zinafanya kazi na Wizara siku zote, sasa ukisema kwamba kuna udhaifu wa Bunge, kwa kweli haiwezi kueleweka na hakuna udhaifu wa Bunge isipokuwa udhaifu wa Wabunge wenyewe katika Kamati zenu. Katika Kamati zenu, hakuna Kamati ambayo imefuatilia Wizara yake, ukaona wanashindana, wakaja wakasema tunashindana na Wizara, haipo.

Kwa hiyo, maneno mengine ya kurusha rusha, hayasaidii sana. Naona ni maneno ya kinafiki tu, kwa sababu ni sisi wote tunahusika humu ndani, ni maneno ya kinafiki kwa sababu tunahusika sisi wote pamoja na wanaosema. *(Makofi)*

Halafu kuna Kamati ya Uongozi, Kamati ya Uongozi ni Wenyeviti wote wa Kamati mbalimbali na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ni Mjumbe wa Kamati hiyo.

Pia tuna Kamati ya Nidhamu inayohusisha watu wote. Nadhani *allegation* nyingine hazina msingi na ni vizuri tukajifunza kutokutumia *allegation* zisizokuwa na mantiki baadaye. *(Makofi)*

Unajua tujifunze kutobadilisha ukweli, maana na hilo pia amelisema na yeye amesema vizuri sana, ukweli kila siku unajitenga wenyewe na huo ndiyo kweli na ndiyo ulikuwa ukweli wa Mwalimu Nyerere na siyo ukweli huu wa siku hizi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nitamwita msemaji wa kwanza Dkt. Dalaly P. Kafumu na napenda kumpongeza kwa kurejea tena Bungeni! (*Makofi/Vigelegele*)

Naamini amekuja kwa hali mpya, nguvu mpya na utekelezaji mpya! (*Makofi*)

Atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafuata Mheshimiwa Andrew Chenge, halafu tuangalie itakavyokuwa.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipendelea kuwa wa kwanza, pamoja na kuwa ndiyo nimeingia tena katika Bunge lako kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie dakika mbili kumshukuru Mungu kwa yale ambayo yametokea katika maisha yangu ndani ya kipindi hiki. Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote mlioniombea na mlioshirikiana nami kwa hali na mali ili niweze kurudi Bungeni. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nawashukuru wananchi wa Igunga kwa uvumilivu wao katika kipindi cha mwaka mmoja,

wamekosa Mbunge, lakini wamevumilia. Nawaomba sasa wananchi wa Igunga sasa tujenge Igunga yetu, bila kujali tunatoka chama gani au tuna dini gani au rika. Ahsanteni sana wananchi wa Igunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nakishukuru Chama changu kwa kunisaidia katika kesi iliyokuwa inanikabili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze viongozi wa Wizara ya Nishati na Madini, Mawaziri pamoja na watendaji wao, kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuendeleza sekta hii yenye changamoto nyingi sana duniani. Wanafanya kazi ngumu kwa sababu sekta ya madini duniani kote ina changamoto. Changamoto yake inasababishwa na kuwa ni sekta ya *extractive Industries,* ni sekta ya kuvuna mali kutoka kwenye ardhi.

Mheshimiwa Spika, unapovuna mali kutoka ardhini, unaharibu mazingira, lakini pia unaharibu maisha ya watu. Kwa hiyo, kufanya vizuri ni kazi kubwa. Hivyo nawapongeza sana Mawaziri na Watendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, naomba kutoa mchango kidogo katika hoja hii ya Nishati na Madini. Kwa ajili ya utaalam wangu katika sekta ya madini, nitajikita kidogo katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, Sekta za Nishati na Madini duniani kote ni injini ya uchumi. Ina uwezo wa kukuza uchumi wa nchi ile kiasi kwamba ikaendelea haraka. Kuna mifano mingi Afrika, Mfano *South Africa*, Botswana na Ghana, uchumi wake unatokana na uchimbaji wa madini. Nchi nyingine nje ya Afrika mfano, China, Quatar na nchi za Uarabuni, Sekta ya Nishati imekuwa ni injini kubwa ya uchumi wao. Kitu gani kilifanyika mpaka wakafikia hivyo? Kitu kikubwa ambacho kilifanyika katika nchi hizi ni kualika na kusaidia uwekezaji kutoka nje. Ukienda Dubai leo, uwekezaji wa Dubai kwenye sekta ya madini na nishati ni mkubwa kutoka nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dunia sasa ni kipande kimoja, hatuwezi kuwa nje ya huo utaratibu. Kwa hiyo, sisi Tanzania tunatakiwa kualika uwekezaji kutoka nje na ndani na kuukuza bila ubaguzi, ili uchumi unaotokana na sekta hizi mbili muhimu uweze kuwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bomani wanasema: "Kufungamanishwa na uchumi mpana" maana yake ni nini? Kilimo, maliasili, biashara na viwanda viweze kuwa pamoja na madini badala ya madini na nishati kuwa *enclave* au kitu cha peke yake. Hivyo, tuna changamoto hii kubwa ya kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi nilizozitaja badala ya kufikiria kupambana na wawekezaji zinawakaribisha wawekezaji. Sisi kwetu, ukisikiliza mitandao ya kijamii, ukisikiliza Wabunge, hata viongozi wengine. Mwekezaji ni mwizi, maana yake ni nini? Ina maana hatutaki kukuza uchumi wetu kwa kutumia hizi injinia mbili za nishati na madini. Tuna wajibu mkubwa sana sisi Watanzania leo hii hasa viongozi wa Kambi ya Upinzani na sisi wengine huku, kuwaelimisha wananchi wetu umuhimu wa sekta hizi katika kukuza uchumi wa jumla wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mzee Mkapa alipoingia alitambua hili na akasema ni lazima tukuze sekta ya madini ili ichangie uchumi wetu. Kukuza sekta ya madini ni kitu cha taratibu ambacho kinachukua muda mrefu. Nashukuru sasa hivi tumefika mahali pazuri, watu wengi wanaelewa na tunashiriki vizuri.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwamba, Kambi ya Upinzani katika hotuba yao, kuna mahali pamesemwa sana kuhusu Kamati ya Bomani. Kamati ya Bomani ilikuwa ni kazi nzuri aliyoifanya Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kurekebisha Sekta ya Madini ili iweze kukuza uchumi. Kurekebisha kwa maana ya kuhakikisha wawekezaji tunaendelea kuwalinda, wa ndani na nje. Kuhakikisha kwamba tunafungamanisha sekta hii na sekta kubwa ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba hii kunasemwa sana, kwamba hakuna kilichotekelezwa kwenye Tume ya Bomani. Naomba niseme, nilipokuwa Serikalini, Tume ya Bomani ililetwa Wizarani, mimi kama Kamishna wa Madini wakati ule, tulichambua ripoti ile, tukapendekeza Serikalini mambo ya kubadilisha na kukamilisha na tukabadilisha Sheria ya Madini, tukaleta Sheria ya mwaka 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Kambi ya Upinzani wasiwe wanarudi nyuma, waangalie tumefanya nini, Sheria inasema nini na vitu gani vinatakiwa kutekelezwa. Tunatakiwa tusaidiane katika kutekeleza Sheria ya Madini. Nikinukuu mambo machache kwenye Sheria ile. Kufungamanisha Sekta ya Madini na Sekta ya Uchumi mpana ni lazima kuhakikisha manunuzi ya migodi na makapuni yanafanyika ndani. Wizara inafanya vizuri katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, ni lazima kuhakikisha Watanzania wanashiriki sana, kwenye sekta ya madini. Wizara inafanya vizuri na imetueleza kwenye hotuba yao. Ni lazima kuhakikisha wachimbaji wadogo wanasaidiwa na wanaendelezwa. Ni vizuri kuhakikisha Serikali nayo inakuwa mwekezaji japo kwa mbali na jambo hili linafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amesema hapo, jinsi ambavyo *STAMICO* inavyofanya shughuli hizi ili tuweze kufungamanisha uchumi huu wa madini na uchumi wa jumla, kilimo, maliasili, viwanda na biashara. Kwa hiyo, nasema tena, *Foreign Direct Investment (FDI)* ni kitu muhimu sana kwenye sekta hizi. Tukiwaita wawekezaji wezi, tunafanya makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka kuchangia ni kuhusu Mikataba. Wakati nikiwa Kamishna wa Madini, hii mikataba inakuzwa kweli kweli, mikataba tumeiweka kwa sababu tunataka kualika wawekezaji waje, tuwape *confidence* ya kuja. Jambo kubwa kwenye mikataba ni moja tu, kuhakikisha viwango vya kodi mwekezaji akivikuta atalipa hivyo mpaka mwisho wa mradi wake. *Tax stabilization clause,* ndiyo kitu kikubwa sana kwenye

mikataba hiyo. Mengine kama mambo ya kulipa kodi na mazingira, sheria zinazohusika zinasimamiwa. Sheria ya Kodi, Sheria ya Madini, Sheria ya Ardhi zinasimamia, lakini kwenye mkataba ni hilo tu.

Mheshimiwa Spika, tulifanya hivyo kwa sababu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa John Chenge.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya pili ya kuchangia. Kwanza, naomba kwa moyo wangu wa dhati kabisa, nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Mheshimiwa Masele; Naibu Waziri Mheshimiwa Simbachawene, Katibu Mkuu. Kwa sababu mimi ni mjumbe wa Kamati hii, naomba ku-*declare interest*.

Mheshimiwa Spika, nimekaa na viongozi hawa kwa muda mfupi na wana dhamira ya dhati ya kuleta mabadiliko katika Sekta hii ya Nishati na Madini. Ninachoomba Waheshimiwa Wabunge katika hili tuwaunge mkono Serikali.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri sana, hotuba ile ilijaa *facts*, ilikuwa na *figures* na ilikuwa ya kisayansi. Sisi hapa ndani hatutaki hotuba za porojo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nianze kuchangia kuhusu Umeme Vijijini. Kabla sijaanza kuchangia umeme vijijini, naomba nimnukuu Mzee Nelson Mandela. Alisema kitu kidogo na mimi nitakichukua kidogo: *“overcoming poverty is not a task of charity, it is an act of justice.”* Niendelee

kumnukuu aliyekuwa Rais wa 35 wa Marekani John Kennedy: *"If a free society cannot help the many who are poor, it cannot serve the few who are rich."*

Mheshimiwa Spika, Serikali ielewe kwamba, ni jukumu lake kuondoa umaskini kwa wananchi wa Tanzania. Zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wa Tanzania wanaishi vijijini. Kupata umeme kwa wananchi wa vijijini ni haki siyo hisani na ndiyo maana nimemnukuu Mheshimiwa Nelson Mandela na nimemnukuu na marehemu Rais Kennedy. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umeme vijijini ni haki ya wananchi wa vijijini, bila ya kupeleka umeme vijijini kwa wananchi ambao ni zaidi ya asilimia 80, hatutaondoa umaskini Tanzania. Sasa nami niende kwa Takwimu, kwa sababu na Waziri anasema yeye anakwenda kwa takwimu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007/2008, *REA* ilipoanza kazi ilipewa bajeti yake kwa asilimia 100, *that was good*. Mwaka 2008/2009 wakapewa asilimia 60 tu katika pesa ambazo walitengewa; mwaka 2009/2010 wakapewa asilimia 56; mwaka 2010/2011 wakapewa asilimia 25; mwaka 2011/2012 wakapewa asilimia 80 na mwaka 2012/13 wakapewa asilimia 13.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wao tangu wameanza mpaka leo wamepewa asilimia 49, lakini kosa hili ni la Hazina. Naomba Hazina isikie vizuri kilio cha Wabunge. Leo bajeti iliyosemwa hapa, pesa zilizoombwa hapa kwa ajili ya umeme vijijini, kwa niaba ya Wabunge wote, naiomba Serikali, naisihi tena narudia, izitoe pesa zote kama zilivyo, kabisa ziende kwenye umeme vijijini, bila ya kufanya hivyo, bajeti inayokuja mtaona ambavyo tutapambana na ninyi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye gesi asilia. Huyu ndiyo mkombozi wa Taifa hili. Gesi asilia ambayo imegunduliwa na ambayo hata haijagunduliwa, lakini tuna uhakika ipo, ndiyo itakayotuondoa hapa na kutusogeza kuwa Ulimwengu wa pili, kwani tumechoka kuwa kwenye Ulimwengu wa tatu.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha hivi, ukitumia gesi asilia kufua umeme, gharama ya umeme ni kati senti za Kimarekani sita mpaka nane kwa *unit* moja. Ukitumia mafuta mazito au *Diesel* kufua umeme, gharama ya umeme ni kati ya senti za Kimarekani 30 mpaka 40 kwa *unit* moja. Kuna mengi ambayo yanatofautisha baina ya kutumia gesi asilia na mafuta, siwezi kuyazungumza yote.

Waheshimiwa Wabunge, nawasihi, tuiunge mkono Serikali katika hili suala la gesi asilia. Tuondoe hofu, tusirudishwe nyuma na watu wenye kauli pinzani, tutabaki kuwa ulimwengu wa tatu kama hatutakuwa makini. Waheshimiwa Wabunge naomba muwe mnasoma vitabu vya *organization behavior*.

Mheshimiwa Spika, wakati wowote jambo linalokuja ambalo linaleta mabadiliko, kuna wanao-*resist* mabadiliko yale, wanayapinga mabadiliko pale yatakapofinya maslahi yao. *Always* mabadiliko yote yanapotokea, yanagusa watu wengine kwenye maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya sasa, sisi tunakwenda kusimama imara, kuiunga mkono Serikali twende kwenye gesi, lazima kuna watu ambao tumegusa maslahi yao, hebu na wao waende kwa wakati. Kama ulikuwa una biashara ya *petrol,* badilisha nenda kwenye gesi, siyo lazima ung'ang'anie *petrol* tu! Sisi tunatafuta kuliondoa Taifa hili katika kuwa ulimwengu wa tatu liende ulimwengu wa pili, Serikali endeleeni tutawaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nisogee Mtwara. Mtwara ni sehemu ya Tanzania, msidanganywe. Sasa naomba nizungumze, naichukua Mtwara sawa na Trinidad na Tobago. Ukienda Trinidad na Tobago ni *gas* imewafikisha pale, wana viwanda vingi sana, pale ambapo inapatikana *gas* vitajengwa viwanda vingi sana. Leo Trinidad na Tobago ukienda kwenye *employment rate*.

Nyamaza wewe mtoto! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye *employment rate* ya visiwa hivi viwili ni *minus five.* Ina maana wote wanaoweza kuajirika katika vile visiwa wameajiriwa kwa sababu ya viwanda. Hii asilimia tano wametafutwa watu wa nje, Serikali, Mtwara wote ambao wataajirika, waajiriwe kwanza, isiachwe kuwa anga huru, waajiriwe kwanza wale wanaoajirika, sina maana kila mtu, kama mtu hana sifa ya kuajiriwa, jamani ataajiriwaje, lakini kila anayeajirika Mtwara, aajiriwe kwanza kama ambavyo wenzetu walifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ukimsikia mtoto analia kwa sisi akinamama, mbona huyu mtoto analia sana, mbona huyu mtoto analia, huwa tunakimbilia kuangalia Nepi, labda ana homa, labda ana nini, ni kweli. Mtwara kuna makelele, lakini tusiyapuuze sana yale makelele.

Mheshimiwa Spika, nakusihi, uitume Kamati yako ya Nishati na Madini, inayoongozwa na Mheshimiwa Mwambalaswa, waende wakawasikilize wale wananchi, huenda kuna hoja ya msingi.

Naomba Serikali, Kamati hii ikienda ije iwashauri mkae pamoja ili mtoto anyamaze. Sisi akinamama hatupendi mtoto alie muda mrefu, lazima utafute chanzo cha mtoto kulia, umwangalie kwa nini mtoto analia, utafute jinsi ya kumnyamazisha yule mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii naomba niongee na Watanzania wote kwa ujumla, naomba niongee na Wabunge wote kwa ujumla, nchi yetu kabla ya ugunduzi wa gesi, kabla ya ugunduzi wa *Uranium*, nchi ilikuwa imetulia kimya.

Sasa hivi tangu tumeanza kuonekana na sisi tuna gesi, na sisi tuna *Uranium*, mnaona ambavyo kuna makelele, huku kuna makelele, huku kuna vurugu hii, jamani tusipokuwa makini, wenzetu wanataka tuvurugane, wao wachukue hivi ambavyo vimepatikana sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawasihi, nawasihi, nawasihi Watanzania, nawasihi kwa unyenyekevu, msikubali kuingia kwenye migogoro, migogoro hii inazalishwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Andrew Chenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na niseme naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, rasilimali ya Tanzania iliyopo ardhini, baharini, katika kitanda cha bahari, tangu uhuru wa nchi hii, sera na sheria zote zinazosimamia maeneo haya zinatamka wazi kwamba, rasilimali hii ni mali ya Jamhuri ya Muungano, kwa faida ya Watanzania, kwa kizazi cha sasa na kizazi kijacho kwa faida ya watoto wetu na kwa faida ya watoto wa watoto wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo sheria ya nchi, Sheria ya Madini na Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji wa Petroli ya mwaka 1980. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, najisikia vizuri sana ninapoiona Wizara hii ya Nishati na Madini, Taasisi zake, Viongozi wake, Watendaji wake na Wataalam waliopo pale, kazi iliyofanyika tangu miaka ya 70 hasa kuanzia mwisho, miaka ya 60, 69 ambapo *TPDC* ilianzishwa, imefanyika kazi kubwa sana na yote haya ambayo tunayaona leo, ni msingi wa sera nzuri, sheria nzuri, ambazo zimekuwa zinahuishwa mara kwa mara ili kuweza kuvutia wawekezaji wakubwa.

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka, mara tu baada ya vita vyetu vya kumfukuza Nduli Idd Amini, Marehem Mwalimu

Julius K. Nyerere alisema, watanzania fungeni mikanda kwa kipindi cha miezi 18, alikuwa na maana gani? Alikuwa anamaanisha kwamba, kwa sababu tulikuwa tumeanza zoezi kubwa la kutafuta madini ya Urani, Bahi na kule Selous, eneo la Mkuju, tulikuwa tunajenga mtambo wetu hapa wa *yellow cake*.

Mheshimiwa Spika, lakini bahati mbaya, bei ya Urani iliporomoka na ndiyo maana hatukuendelea na hiyo, lakini tuliendelea kwa upande wa mafuta. Ndiyo maana mwaka 1974 tuligundua Songosongo, 1982 tumeona Mnazi Bay, lakini na maeneo mengine ya Tanzania Rukwa kule, *Lake* Tanganyika, Pwani hii, *Costal Basin* hii imefanyiwa kazi kweli kweli na matokeo haya ndiyo tunayaona.

Tumeelekea bahari kuu, lakini yote haya ni kwa sababu tuna sheria nzuri, Makampuni haya makubwa, yasingeweza kuja Tanzania kama sheria ya Tanzania ingelikuwa haijakaa vizuri. Naipongeza sana Serikali, na tuendelee kuhuisha sheria zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesikia hotuba ya upande wa Upinzani, nawaheshimu sana, lakini kusema kwamba, eti Serikali isitishe *round* ya nne ya kutoa vitalu, Serikali msikubali kabisa ushauri huo, endeleeni mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *round* ya kwanza, ya pili na ya tatu, imefanyika kwa mujibu wa Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji wa Mafuta ya mwaka 1980. Tusiwadanganye watu, *upstream operations* za utafutaji wa gesi asilia na mafuta utaendelea kusimamiwa na sheria iliyopo.

Mheshimiwa Spika, na utoaji unaokuja wa vitalu hivi, ikumbukwe kwamba utafutaji wa mafuta na gesi asilia ni miaka 11 kwa mujibu wa sheria ya Tanzania. Sasa usipoanza sasa, unataka uanze lini? Yote haya ambayo tumeyaona ni kwa sababu tulianza huko nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mikataba hii, ningelipenda sana niwasikilize hawa wataalam wanaosema wanafahamu

mikataba ya kugawana mapato. Nimegundua kitu kimoja, kwa upande wa madini, baadhi yetu kwa sababu tunasoma sehemu moja tu, wamekwenda wakasoma Sheria ya Madini wanakuta kuna kiwango cha *royalty*, wameshindwa kusoma sheria zingine na leo nataka niwaambie waende kwenye *library* ya hapa Bunge. Wakasome Sheria Na. 27 ya mwaka 1997 ambayo itawaeleza ni nini ambacho Serikali inapata kutokana na Sekta ya Madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naelewa baadhi yetu hatuyaelewi sana masuala haya na sishangai sana ninapowasikia kwa sababu *is a dry subject my friend.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nchi hii imeendelea kutumia wataalam wa hali ya juu kuishauri na ndiyo maana hatuogopi mtu anapotoa *constructive criticism*, maana *constructive criticism* inakupeleka mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa niipongeze sana Serikali kwa upande wa *REA*, hiyo ndiyo mkombozi kwa Mtanzania. Mheshimiwa Waziri hongera sana, Serikali ya Jakaya M. Kikwete, hongereni sana kwa sababu, umeme ni uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ya vijijini ambayo umeme huu umefika, unaona *transformation* ya haraka sana, ukiunganisha hilo na ujenzi wa barabara za vijijini, Zahanati, Shule, utaona Tanzania itakavyokwenda kwa kasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, anayeshukuru anaomba tena. Nimepata umeme huo wa *REA* katika baadhi ya vijiji, naomba tena mniangalie katika vijiji vyangu vingine na kule kwa ndugu yangu John Cheyo, kule Itilima na vijiji vya kule Mashariki na wenyewe wapate umeme wa *REA*. Naungana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, lazima Serikali itafute fedha ya ziada kwa *REA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bilioni 153 kwa mahitaji ya bilioni 450 kwa mwaka huu peke yake, iko wapi, haitoshi. Sasa changamoto yetu Waheshimiwa Wabunge, tuzipate wapi?

Hilo pengo tulipate wapi, kama ni kuumia maeneo mengine kwa sababu ya uchungu wa kukuza uchumi hasa vijijini tukubali, kilio hiki ni hapa ndani ya Bunge hili, lakini tunahitaji bilioni 297, kuweza kufika kile kiwango ambacho *REA* kwa mwaka ujao wanahitaji.

Mheshimiwa Spika, nina mengi ya kusema kwa *TPDC,* ushiriki wao katika mikataba ya *PSA* hili ni jambo zuri sana kwa niaba ya Serikali, lakini mpaka sasa hawapewi fedha za kushiriki. Naomba Serikali iliangalie kwa umakini sana, pale *Mnazi bay*, lakini pia katika maeneo ambayo tuna mikataba hiyo 25 sasa hivi ya *PSA*. Bila wao kushiriki, itakuwa ni tatizo kubwa, mengi hayo mazuri mnayosema ambayo yamo ndani ya mikataba hii mizuri, yatakuwa ni bure tu.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho, nimefurahi sana kwa upande wa Serikali angalau *retention* ambayo imeombwa kwa miaka mingi, asilimia 50 ya mauzo ya gesi. Mkiona kwenye vitabu vya Bajeti, mwaka huu mtaona, *retention* asilimia 50 angalau kwa *TPDC*, Serikali imekubali kuanza kulitekeleza hilo. Hongereni sana, hiyo ndiyo itaanza kujenga uwezo wa *TPDC*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zile leseni mbili, zile *blocks* mbili za *TPDC*, hayo ndiyo maendeleo. Naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nami nianze kwa kumsifu sana Mheshimiwa wa Nishati na Madini kwa hotuba yake kama alivyoita mwenyewe kuwa ni hotuba ya takwimu siyo porojo. Laa! Nimeshtuka kweli kweli leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waingereza wana msemo wanasema *once beating twice shy, (*ukitafunwa na nyoka ukiona ung'ongo unashtuka).

Mheshimiwa Spika, gesi au mali yoyote ile inayotokea

kwenye nchi, wananchi huwa wanaitegemea au wanakuwa na matumaini kuwa itawasaidia kwa namna fulani katika maisha yao.

Mheshimiwa Spika, madini kwa mfano, nina hakika madini Mwenyezi Mungu alitupa siku nyingi tu, lakini yalipoanza kuchimbwa, wananchi wakafanya matumaini kuwa labda yatawasaidia katika kujikomboa. Lakini mpaka sasa ukiwaangalia watu wa kawaida au ukimuuliza mtu wa kawaida mtaani, hivi unafaidika nini au unajua nini kuhusu madini? Haelewi na haelewi kwa sababu hatuelimishwi.

Mheshimiwa Spika, maneno yamalizia Bungeni hapa, ukiondoka hakuna kingine, kwenye *TV* sijapata kuona hata siku moja ikioneshwa mikataba ya madini ilikuwa mingapi labda imefanyiwa *review* mingapi, tumefaidika na nini hatuoni vitu kama hivyo. Sasa kama watu hawaelimishwi malalamiko yatakuwa mengi na watasema maneno mengi sana. Lazima muanzishe program ya kuwaelimisha watu juu ya jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulikuja hapa tukaambiwa mikataba inakuwa *reviewed*, hivi leo tukiuliza ni mikataba mingapi imekuwa *reviewed* na katika *review* hiyo, Tanzania au nchi yetu imefaidika vipi katika kufanya *review* ya mikataba hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa kabisa, tumetiliana mkataba na wachimbaji wakubwa wa madini kwa dola 240 kwa wakia moja kwa wakati ule, leo wakia ile ile katika soko la dunia inauzwa kwa dola zaidi ya 1700. Hivi Serikali inafaidika vipi angalau ile *windfall tax* ambayo walipaswa watulipe, Watanzania hawajui na wakisema msichukie kwa sababu hawaelewi, tuelimisheni tuelewe. Huo ndiyo wajibu wenu, kama hamtafanya hivyo yatakuwa matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye gesi, ndiyo nikaanza na ule msemo wa *once beaten twice shy,* watu wa Kusini ambao sasa hivi Mwenyezi Mungu amewajalia gesi inatoka

kwao. Siamini kuwa ni watu wakorofi kiasi hicho, kama labda watu wengine wanavyowahisi, hawa watu wana hofu, hii gesi itawafaidisha vipi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lugha yangu niliyoanzia ya *once beating twice shy,* tokea nasoma shule, Mheshimiwa Rashidi Mfaume Kawawa Mbunge wa zamani wa Liwale, ambaye alishika nafasi nyingi katika nchi hii, ilikuwa yazungumzwa barabara ya Kibiti - Lindi, mpaka juzi tu na mpaka leo barabara ya Kibiti - Lindi haijamalizika yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa watu wa Kusini unapowaambia tutajenga Kiwanda cha Gesi, amesema hapa Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 92, Ibara ya 175, amesema atakayoyafanya, lakini huoni fedha zilizotengwa. Sasa watu hawa wanakuwa na haki ya kulalamika na wanalalamika kwa sababu wao wanachokitaka wala si mambo mengi, wanataka wajengewe mtambo wa kuzalisha umeme angalau *megawatts* 300.

Mheshimiwa Spika, wanataka katika hilo iunganishwe Mikoa yao ya Kusini na *grid* ya Taifa ili vile viwanda kama itatokea *downfall* yoyote ya umeme, waweze kupata, lakini ukisema unawawekea umeme kule hukuunganisha na *grid* ya Taifa, hukuwasaidia na hawa ambao wanakwenda kuwekeza, matokeo yake utawatia hasara tu.

Mheshimiwa Spika, hata hili ni baya wakisema! Sidhani kama hili ni baya, nafikiri tungewasikiliza. Nimeona hicho kitabu na nimekisoma, lakini, ninachosisitiza si kitabu kwa sababu hata hiyo barabara ya Kibiti - Lindi ilisemwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ilisemwa sana tu na ilisemwa Bungeni hapa wala haikusemwa kwingineko, ilisemwa Bungeni, lakini haikujengwa. Sasa hawa wana hofu, watoeni hofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine wao wanalolitaka ni kuwa, yakitokea hayo, maana yake Bandari ya Mtwara

itafunguka, ikifunguka watapata maslahi mengi. Sasa watu walioteseka, watu waliosumbuka, wakiwa na matumaini kama hayo, utawafanyaje?

Mheshimiwa Spika, nataka tuzungumze kidogo kuhusu gesi, kwanza naomba hii sera ya gesi ambayo kwa maoni yangu iko katika hatua za mwisho, ileteni haraka, kwa sababu kama hatuna sera ya gesi tutapata matatizo makubwa baadaye.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wanaochimba gesi wakubwa wa *Norway,* kwa mfano, Norway wanajulikana duniani ni wachimbaji wa mafuta, ni wachimbaji wa gesi wakubwa, wana mambo mengi waliyoyafanya, lakini pamoja na hayo, tunapata kujifunza yafuatayo kutoka Norway:-

Mheshimiwa Spika, watu wenyewe raia wale, wanakuwa na mtazamo wa kuamini kuwa gesi itawasaidia. La pili, wanakuwa na imani na viongozi wao na hapa ikiwa gesi itawasaidia watu wale, watakuwa na imani na viongozi wanaowaongoza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hili suala la malalamiko, la kusemana na kupigana vijembe, wala halitatusaidia sana. Nafikiri tungeandaa mkakati ambao mwisho wa siku, watu wa Kusini watafaidika na gesi yao na Watanzania watafaidika nayo. Ile gesi inachimbwa kwao lakini si ya kwao peke yao, yetu sote na hili ninyi mnalidharau sana, mnaona labda ni kitu kidogo.

Mheshimiwa Spika, napenda leo niwape siri, sisi watu wa Pemba asilimia 80 ya karafuu za Zanzibar zinalimwa Pemba na Wapemba ndiyo wanaochuma Karafuu. Wanaovunjika miguu ni Wapemba, wanao pata ulemavu ni Wapemba, lakini matunda ya karafuu hizo yametuchukua muda mwingi hatuyaoni. Msalaba huu tumeutwika Chama cha Mapinduzi, kwa sababu ndiyo kinachoongoza. Tumeikataa CCM, hivi ninyi hamuogopi watu wa Kusini wakiwakataa baadaye? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, asilimia kubwa ya mafanikio yale yamekwenda upande wa pili, sisi tunaumia, hatuyaoni. Ni juzi tu sasa ndiyo tunaona angalau mambo kidogo kidogo yanabadilika. Sasa mambo kama haya mnayaona ninyi ni madogo. Mnakuja hapa tunapigana pigana vijembe, kila mmoja akajifanya anajua sana kusema kumjibu mwingine. Haya hayatusaidii, tuwasaidieni watu na tuwe *fair*.

Mheshimiwa Spika, muwe *fair* katika kuleta maendeleo, mkiwa *fair* wananchi watawaamini, watawapenda, watawaunga mkono, lakini wakibaini kuwa mnakula njama dhidi yao, wakiamini mnawadanganya danganya, mwisho wa siku mtawalaumu bure, lakini bado itabakia kuwa makosa ni ya viongozi, kwa sababu ninyi ndiyo kwa sasa mnaoshika usukani wa gari hii, madongo yote yatakuja kwenu, jirekebisheni, muwatendee watu haki na muwasaidie.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nizungumzie mafuta, kwa mujibu wa ripoti ya *EWURA* iliyotolewa Oktoba, 2012, inaonesha uagizaji wa mafuta ya taa umeshuka kwa asilimia -30, hiyo ni *significant*, inaonyesha kuwa mafuta ya taa hayatumiki sana, lakini nini maana yake? Maana yake ni kuwa, watu wanatengeneza mkaa kwa wingi na unaleta athari kubwa ya mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kitu hiki lazima mkiangalie sana, msione mafuta hayaagizwi tu mkaona ni jambo la kawaida, watu hawatumii, maana yake ni kuwa, wana nishati nyingine wanayoitumia kwa kupikia na kwa shughuli zao, litatuathiri sana jambo kama hili.

Mheshimiwa Spika, yalikuwa yakitumika kwa kuchakachulia diseli, labda mlipozuia, kwenye diseli imekuwa nafuu kidogo, lakini hata hivyo naamini suala kubwa ni kuwa watu wamepata *officially* wanatumia kuni kwa ajili ya kazi zao za kupikia. Tafadhalini, jambo hili lisimamieni, kwa sababu mwisho wa siku litaweza kutuathiri sana katika suala zima la mazingira.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nashukuru, tutaendelea baadaye Saa kumi na moja. Kwa hiyo, nasitisha shughuli mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge liliahirishwa hadi Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni, Bunge lilirudia)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Nimesema tukae.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, najua tulikuwa na hii Wizara ambayo inabidi kuijadili kwa siku mbili, lakini kuanzia wiki ile taarifa zilipotolewa kwamba Wizara itajadiliwa, tunaambiwa kule Mtwara walijiandaa kufanya matatizo. Kweli toka tumeanza kufanya shughuli yetu ya kusoma Wizara hii, Mtwara kumeanza kuwa na matatizo.

Sasa najua wengi hapa mnataka tujadili suala hili kwa dharura, nakubali suala hili lipo, lakini tutajadili kwa dharura kuhusu nini, ni yale tuliyoona kwenye vyombo vya habari.

Kwa hiyo, naiagiza Serikali kwamba, kwa kesho watoe hali halisi iliyoko kule Mtwara na sasa hivi naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho Saa tatu asubuhi ili Kamati ya Uongozi ya Bunge tukakae sasa hivi, kwa sababu tuna shughuli tuliahirisha kipindi kile nilipotaka kuituma Kamati yangu ya wakati ule, halafu nikawa nimeivunja. Kwa hiyo, twende tukashauriane halafu na sisi pia tutatoa maelezo kesho tumefikiria nini. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naahirisha Kikao hiki mpaka kesho Saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.00 Jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 23 Mei, 2013, Saa 3.00 Asubuhi)*